

**Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

---

**Kikao cha Ishirini na Nne - Tarehe 2 Juni, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 163

**Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya**

**MHE. CHARLES P. MWIJAGE (K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE)** aliuliza:-

Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la Vijana wa Kitanzania kukamatwa nje ya nchi wakiwa na Dawa za Kulevya na vijana wote hao wamekamatwa nje ya nchi wakitokea Tanzania hali inayochafua sifa ya Tanzania nje ya nchi:-

(a) Je, ni Watumishi wangapi wa Vitengo vinavyodhibiti Dawa za Kulevya wamekamatwa au kuhusishwa na biashara hiyo, na ni hatua gani zimechukuliwa dhidi yao?

(b) Je, ni mikakati gani inayochukuliwa na Serikali kukomesha biashara hiyo haramu na yenye madhara makubwa kwa jamii ya Watanzania?

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)**

alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2013, jumla ya watumishi 11 wa vitengo vinavyodhibiti dawa za kulevya wamekamatwa au kuhusishwa na biashara ya dawa za kulevya katika maeneo mbalimbali.

Watumishi hao walisimamishwa kazi na kisha kushtakiwa mahakamani ambapo baada ya kesi zao kusikilizwa mahakamani wapo waliofungwa magerezani na kufukuzwa kazi pia. Baadhi ya Watumishi bado kesi zao zinaendelea mahakamani.

(b) Mheshimiwa Spika, mikakati inayochukuliwa na Serikali ili kukomesha biashara ya dawa za kulevya ni pamoja na:-

(i) Kuundwa kwa kikosi kazi cha kupambana na biashara ya dawa za kulevya mwaka 2006;

(ii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma hususani kwa vijana kuhusu athari zitokanazo na dawa za kulevya;

(iii) Kutoa huduma za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya aina ya *heroin* hasa wanaojidunga;

(iv) Kuongeza uangalizi wa karibu katika maeneo ya mipaka yanayotumiwa kuingiza dawa za kulevya kama vile Viwanja vya ndege, bandari, mipaka ya nchi kavu; na

(v) Kutunga sheria mpya ya kupambana na kuzuia biashara ya dawa za kulevya itakayoanzisha chombo kipya chenye mamlaka ya kukamata, kuchunguza na kupeleleza masuala yanayohusiana na udhibiti wa dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati iliyopo na jitihada zinazofanyika hivi sasa changamoto za kupambana na biashara hii ni nyingi. Hivyo natoa wito kwa wananchi wote nchini Tanzania kutoa ushirikiano katika mapambano haya kwa kuwafichua wahalifu na kuwapeleka waathirika wa dawa za kulevya katika vituo vya ushauri nasaha, matibabu na huduma zingine. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali yanazungumzia zaidi kutibu ugonjwa badala ya kuuzia, napenda kuiuliza Serikali.

Je, hamwoni kuwa Vijana wengi wanashawishika kuingia katika mchezo huu ni kwa sababu ya kukosa shughuli zenye kipato na kuweza kuwashughulisha, hali inayowafanya wawe chambo kirahisi kuvutwa na wale wenye biashara hii na kutumiwa?

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuweza kuwapa shughuli a kuchangamsha uchumi wao vijana ili waepuke kurubuniwa kirahisi na hawa magwiji wanaoendesha biashara hii mbaya?

### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wapo vijana ambao wanaendelea kujishughulisha na madawa ya kulevyo, lakini jibu la msingi nimeeleza namna ambavyo Serikali inaendesha jitihada mbalimbali za kudhibiti tatizo la kuongezeka kwa idadi ya vijana kushiriki kwenye Madawa ya Kulevyo.

Lakini nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Mwijage kwamba Serikali inao mkakati wa kuwafanya vijana kwenye maeneo yetu mbalimbali kujiingiza kwenye shughuli za kiuchumi zaidi badala ya kushiriki kwenye masuala ya kushawishika na Madawa ya Kulevyo.

Halmashauri zetu kote nchini, zimepewa uwezo wa kuwakusanya vijana kwenye maeneo yao kuwaanzishia vikundi mbalimbali vya ujasiriamali ili kila mmoja apate kujishughulisha waingie kwenye vikundi vile wafanye kazi za kuongeza uchumi wao badala ya kujishughulisha na masuala mengine.

Mheshimiwa Spika, tumeona mifano ya Waheshimiwa Wabunge mkiwa mnahamasisha, hata vijana wa bodaboda wanakaa pamoja kuanzisha SACCOS, vilevile vijana wengine wote kuwaanzishia masuala ya kilimo na tumeona maeneo mengi yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa vijana wote nchini kujiunga kwenye makundi mbalimbali ya kujiongeza uchumi, waachane na kujiingiza kwenye makundi ambayo yatawaletea madhara baadaye. Wito huu utakuwa ni wito wenye tija kwa vijana wote nchini. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri. Je, kuna mkakati gani sasa wa kuondoa tatizo hilo kwa vijana ambao hasa katika maeneo yetu ya Dar es Salaam vijana wengi wanaathirika na madawa hayo?

### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**

Mheshimiwa Spika, mikakati ipo ya kuhakikisha kwamba vijana wengi hawajihusishi na hasa katika kulinda kuingia kwa madawa haya kwa kuimarisha ulinzi kwenye mipaka, kwa kuimarisha mitambo yenye uwezo wa kubaini kwenye maeneo yetu ya bandari na viwanja vya ndege.

Lakini pia kwa kupitia Tume ambayo sasa inakamilika na ambayo itaingia kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuhakikisha tunaunda ile Tume itakayoongeza udhibiti wa uingiaji wa madawa nchini ndiyo utakuwa muafaka wa kuwaondolea vijana hawa kupata dawa hizi na kuendelea kuwa wateja kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msingi hapa ni sheria kwa sababu tumeshaona mara kadhaa vyombo vya habari vinaonesha watu wanakamatwa na madawa, tunazungumzia watu wanafanya biashara ya madawa, lakini ndani ya nchi yetu mpaka sasa hapajawa na sheria kali ambayo inaweza kudhibiti vitendo hivi.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Je, ni lini Serikali sasa itaona kuwa Taifa linaangamia na wanapaswa kuleta sheria kali ya kudhibiti mambo haya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, ambalo ametaka kuona Serikali imejikita vipi kuimarisha sheria tuliyonayo sasa.

Lakini kungeza baadhi ya vipengele ambavyo vitazidi kuwabana vijana hawa ili kuweza kuondokana na hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie kwamba kupitia chombo ambacho sasa kinaundwa ambacho kitaendelea kudhibiti hata mianya ya kuingiza dawa zenyewe ni pamoja na sheria ya kuwabana waletaji, wateja waliopo ndani, lakini pia wafadhili wanaofadhili uletaji wa dawa hizi. Sheria hiyo ikikamilika tutakuwa tumeshamaliza jambo hili na kuleta unafuu kwa vijana wetu kuingia kwenye shughuli mbalimbali.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Modestus Kilufi.

Na. 164

### **Posho kwa ajili ya Viongozi wa Serikali za Mitaa.**

**MHE. MODESTUS D. KILUFI** aliuliza:-

Viongozi wa Serikali za Mitaa, Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa wanafanya kazi kubwa ya kuhudumia wananchi.

(a) Je, Serikali itaandaa lini utaratibu wa kuwalipa posho au kifuta jasho?

(b) Je, kama utaratibu wa kuwalipa upo kwa nini hawalipwi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri zote nchini imeweka utaratibu wa kuwalipa posho Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani na fidia za vyanzo vilivyofutwa inayorejeshwa kwenye vijiji ambayo ni asilimia 20.

Mgawanyo wa fedha hizi ni kwamba asilimia tatu hutumika kwa ajili ya maendeleo na asilimia 17 hutumika kwa ajili ya utawala ikiwemo kulipa posho za Viongozi ambao nimewataja.

Hata hivyo Viongozi wa kulipwa posho hizo hutofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine kulingana na makusanyo, mapato ya ndani katika vyanzo vilivyopo.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014 Serikali imetenga katika mamlaka ya Serikali za Mitaa shilingi bilioni 63.5 kwa ajili ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ilitengewa shilingi milioni 439.4 na hadi Aprili, 2014 zimepokelewa shilingi milioni 198.4 kati ya hizo zilizorejeshwa ngazi ya vijiji ni shilingi milioni 12.1 kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi za vijiji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014/2015 Halmashauri ya Mbarali inatarajia kukusanya fedha jumla ya shilingi bilioni 2.9 kutokana na mapato ya ndani. Pia inatarajia kutoa fedha za ruzuku kiasi cha shilingi milioni 459.4 katika fedha hizo Halmashauri imetenga jumla ya shilingi milioni 13 kwa ajili ya utawala ikiwemo na kulipa posho za Viongozi wa Vijiji. *(Makofi)*

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri. Nataka kujua kwa sababu Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa kazi zao siyo za msimu ni za muda wote. Lakini ruzuku mpaka ikusanywe, ipatikane na vyanzo vya mapato na ile inayorejea kutoka Serikali Kuu inachukua muda mrefu sana na hawa viongozi wakiwa wanafanyakazi bila malipo yeyote akiwemo Mtendaji wa Kijiji pale anapokea mshahara lakini Mwenyekiti wake hapati chochote.

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuachana na mfumo huu na kutengeneza mfumo mzuri zaidi wa kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ili waweze kufanyakazi zetu kwa moyo mweupe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba zipo baadhi ya Halmashauri nchini hazijatekeleza jambo hili kikamilifu, lakini nina hakika kama Halmashauri imejipanga vizuri kupitia robo ya mwishoni mwa mwaka wa fedha inaweza kulipa pia kwa mtiririko wa mwaka wafedha unaoanza kupitia mapato yale na baadaye wanapokusanya na kama Halmashauri imejiweka vizuri kwa kukusanya vizuri vyanzo vya ndani jambo hili linaweza kuwa endelevu. Kwa sababu umeshauri vizuri kwamba tuandae utaratibu mpya ambao unawezesha Halmashauri na Viongozi wetu hawa wa ngazi za vijiji kupata mafao yao kwa mtiririko ulio mzuri. Jambo hilo tunalichukua na tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASA:** Mheshimiwa Spika, Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala zima la malipo kwa Wenyeviti wa Vijiji limekuwa halifanyiki katika sehemu nyingi na baadhi imepelekea kutenda kazi chini ya kiwango au kutokuwa na utendaji mzuri wa kazi. Mfano sasa hivi wanaboresha daftari la Makazi na baadhi ya watu hawaandikwi na hivyo kuleta sintonfahamu kati ya wananchi.

Je, Serikali kwa nini isitoe tamko kwamba sasa watu hawa wapewe malipo kila mwisho wa mwezi, kwa maana ya kwamba watengewe mishahara ieleweke?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi, maana ni swali linazunguka hapo hapo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama ambavyo nimeeleza kwenye majibu yangu ya awali kwamba inatokea maeneo mengine uhakika wa malipo ya fedha ule mtiririko siyo mzuri sana.

Jambo hili kama Wakurugenzi wamejipanga vizuri, kuhakikisha na kutambua umuhimu wa watendaji wetu wa Kada za chini, wanaweza ku-*maintain* kutoa malipo haya kwa mtiririko ili kuwawezesha kufanya kazi zote muhimu kama ambavyo wanatakiwa wazifanye.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa pia bado jambo hili kama nilivyoeleza kama ambavyo Mheshimiwa Kilufi ameshauri bado tunachukua hiyo kama jukumu letu. Tutaliweka vizuri kwa lengo la kuboresha utendaji wa kazi kwenye ngazi hizi za mamlaka ya Serikali za mitaa na hasa Watendaji wetu wa ngazi za Vijiji waweze kufanya kazi kwa mtiririko unaotakiwa.

Pia hata ule uandikishaji, uhamasishaji, na usimamizi uweze kwenda vizuri kwenye shughuli zetu za maendeleo kwa ujumla. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Vitongoji mpaka hivi sasa bado wanaendelea kuchapa kazi ya kusaidiana na Viongozi mbalimbali wa Serikali ili kuhakikisha wanasukuma maendeleo ya nchi yetu.

Je, Serikali haioni kwa kuendelea kutegemea vipato vya ndani kuwalipa viongozi hawa ni sawa na kutegemea sadaka ambayo haijulikani itatoka ama haitatoka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni swali linazunguka hapo hapo, hivyo jibu tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu yote ya awali mawili yaliweza kabisa kufafanua suala alilolieleza Mheshimiwa Nchambi kwamba Serikali tunaandaa sasa utaratibu mzuri wa kulipa kwa mtiririko malipo haya, mbali ya kwamba tunalipa fedha kwa kipindi ambacho hakina uhakika sana. Lengo sasa ni kuboresha ulipaji wa mafao haya.

Jambo hili litakapokamilika litaleta mtiririko, lakini kwa sasa bado Halmashauri kupitia Baraza la Madiwani linaweza kuweka mfumo mzuri kwa Watendaji wetu kukusanya na kuziweka kwenye pool ili ziwe zinaweza kulipa kwa mtiririko kuleta ufanisi wa kazi kwenye maeneo yetu ya Halmashauri.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu atauliza swali hilo.

Na. 165

### **Matumizi ya Bidhaa Zifokanazo na Mmea wa Aloevera.**

**MHE. WARIDE BAKARI JABU** aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni bidhaa zinazotokana na mmea wa Aloevera zimezagaa sana kwa matumizi mbalimbali zikiwemo sabuni, mafuta ya kujipaka, dawa za meno na kadhalika.

Je, Serikali imeshafanya utafiti juu ya ufanisi wa bidhaa hizo kama inavyotangazwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembesamaki, kama ifuatavyo:-

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi imefanya tathmini mbalimbali kuhusu matumizi yam mea wa *Aloevera* (Mshubiri) kutumika kama mojawapo ya kiambato salama katika bidhaa za vipodozi. Hii hufanyika katika kipindi cha usajili ambapo viambato vyote vinavyoorodheshwa katika kila kipodozi hufanyiwa tathmini ya kina kuona kama matumizi yaliyotajwa na mtengenezaji ni sahihi kwa aina ya kipodozi anachotarajia kuweka sokoni ikiwemo viambato vyake.

Mheshimiwa Spika, Mmea wa *AloeVera* una viambato takribani 126 vikiwemo *vitamins, enzymes-(vimeng'enyoy), minarals, sugars, lignis, saponins, Salicylic Acid, Amino Acids, Athraquinones na Fatty Acids*. Viambato hivyo vina manufaa mengi katika mwili wabinadamu ambapo vikitumika katika vipodozi husaidia kulainisha, kung'arisha ngozi na kuondoa mpauko wa ngozi na pia kujikinga na mionzi ya jua (*UV na Gamma*).

Hutumika pia katika kurutubisha nywele na kuzifanya ziwe imara na kulinda kinywa na meno inapotumika kwenye dawa za meno.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hakuna tafiti za kina zilizofanyika duniani kuhusu matumizi ya mmea wa *Aloevera* (Mshubiri) ila umekuwa ukitumika katika matumizi mbalimbali tangu miaka ya 2000 iliyopita (*Ancient Egypt*) na kuonesha manufaa makubwa katika matumizi haya. Nawataarifu kuwa matumizi ya mmea huo ni salama katika utengenezaji wa vipodozi na ndiyo maana mamlaka ya chakula, dawa na vipodozi hadi sasa imeshasajili na kuruhusu kuwepo sokoni bidhaa za vipodozi vyenye viambato vya mmea wa *Aloevera*.

Vipodozi hivyo vilivyosajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa na Vipodozi (*TFDA*) ni takribani 70 zikiwemo sabuni, dawa za meno, mafuta ya kujipaka, mafuta ya kuoshea nywele na vipodozi vya kupaka usoni.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa swali langu la msingi lilikuwa ni utafiti na Naibu Waziri amekiri kuwa hakuna utafiti wowote uliofanyika wa mmea huo wa *Aloevera*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitumia *cost age* katika kufanya utafiti wa kina katika mmea huu wa *Aloevera*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kuwa mmea wa *Aloevera* umethibitishwa kuwa na viambato vingi muhimu kwa afya ya binadamu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kilimo cha *Aloevera* kama zao la biashara ili kukuzwa uchumi wa wananchi? Ahsante sana Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe pongezi kwa hali ya juu kwa Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa suala la msingi la kuhusu mshubiri. Ushauri ambao ameutoa Mheshimiwa Spika ni ushauri nzuri kwa manufaa ya nchi yetu na kwa maendeleo ya nchi yetu na hasa usalama wa Tanzania.

Maswali yake yote mawili naomba kuyajibu kwa pamoja kwa ushauri huu kwa sababu kwa mazingira yalivyo ni suala ambalo ni mtambuka hasa ukishirikisha Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili kwa maana kujielekeza katika mimea na Wizara ya Afya kwa maana ya usalama wa dawa na vipodozi. Ushauri huo tunauchukua tutasaidiana na Wizara zingine kama Serikali kuona uwezekano wa utekelezaji wake.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa bidhaa hii imeenea katika nchi yetu na kwa kuwa bidhaa hii hutoka nchi mbalimbali ambazo zinaingiza hizo bidhaa hapa nchini Tanzania.

Je, kuna njia gani za kuzuia bidhaa ambazo siyo nzuri zinazotokana na *Aloevera* zinazotoka katika baadhi ya nchi ambao ni wadanganyifu huwa hawaweki viambata ambavyo vimetangazwa katika box au sehemu ambayo inayo hii *Aloevera*?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu ambao nchi tunaweza kuzuia bidhaa ambazo hazikidhi ubora kulingana na viwango kwa Tanzania tunayo Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi ambayo katika maeneo yote ya mipakani ikiwemo Bandarini ikiwemo Uwanja wa Ndege, katika mipaka yetu kama Kagera pale Mara, Arusha na kule Zambia mipaka yote pamoja na Malawi.

Tunao wataalam wetu ambao wanahusika na ukaguzi wa bidhaa mbalimbali ambayo Watanzania tumeshuhudia bidhaa mbalimbali ambazo Watanzania tumeshuhudia bidhaa ambazo hazikidhi ubora chini ya Mamlaka hii huwa zinaondoshwa, kuzuiwa na kuharibiwa pale ambapo hazikidhi ubora.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea na swali linalofuata, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Mendrad Kigola atauliza swali linalofuata.

Na. 166

### **Mbolea ya Ruzuku kwa Wakulima wa Mufindi Kusini**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** alliluliza:-

Jimbo la Mufindi Kusini lipo kwenye ukanda wa mvua nyingi sana na wananchi wake ni wakulima wazuri japo wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa mbolea ya ruzuku ambayo hugawiwa mwezi wa kumi na moja tu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea mbolea ya ruzuku kwa kipindi cha mwezi wa nne na wa sita ili wakulima wa kilimo cha umwagiliaji nao wafaidike?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima kwa utaratibu wa vocha kwa lengo la kujenga tamaduni ya matumizi ya pembejeo za kisasa miongoni mwa wakulima wa nchi yetu na kuwezesha uzalishaji wa chakula cha kutosha nchini na hivyo kuondokana na upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo hayo ya kujitosheleza kwa upatikanaji wa mahindi na kuongeza uzalishaji wa mazao mengine ya chakula na biashara, mpango wa matokeo makubwa sasa umejielekeza sana kwenye Wilaya ya Mufindi miongoni mwa Wilaya za kimkakati. Aidha, waraka wa utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo pamoja na mambo mengine umeelekeza kwa Kamati za Vocha kuyapa kipaumbele maeneo yenye fursa za kilimo cha umwagiliaji kwa kuwa yana fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji.



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika utoaji wa ruzuku ya pembejeo ikiwemo ufynywa wa Bajeti na usimamizi hafifu wa utaratibu wa utoaji wa ruzuku katika ngazi ya Serikali za Mitaa ambayo imechangia pembejeo za ruzuku Kushindwa kuwafikia wakulima kwa wakati.

Kutokana na changamoto hizo Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima ikiwemo mpango wa kutoa ruzuku kupitia vikundi vya wakulima kwa njia ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, kupitia utaratibu wa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa njia mikopo, vikundi vya wakulima nchini wakiwemo wa maeneo ya umwagiliaji katika Wilaya ya Mufindi watapata fursa ya kupata pembejeo kwa wakati wote wa mwaka na hivyo kuongeza uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo.

Aidha, utaratibu huu ukitekelezwa na kusimamiwa vizuri utapunguza ubadhirifu wa fedha za umma na utakuwa ni suluhisho endelevu wa utaratibu wa kutoa ruzuku kwa wakulima nchini. Hivyo basi, namsihi Mheshimiwa Mbunge aendelee kuhamasisha vikundi vya uzalishaji ili visajiliwe na viweze kukopesheka wakati wote wa msimu wa kilimo.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kwa kunipa nafasi niulize mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri mwaka jana katika Jimbo la Mufindi Kusini, kuna Kata 3 ambazo zilikuwa na vikundi vilivyosajiliwa na viliambiwa kwamba wachache asilimia 20 wale wananchi na Serikali itatoa asilimia 80. Wananchi walitekeleza hilo, walichanga asilimia 80. Matokeo yake hawakuweza kupata mbolea na fedha ile ilichukuliwa na Serikali na Kata hizo zilileta maisha magumu sana kwa viongozi wa vijiji pale. Kwa mfano Kata ya Luhunga na Kasanga pamoja na Mtambula.

Je, Serikali inasemaje kuhusu hii hela iliyochukuliwa ya wananchi na Serikali haikutimiza ahadi yake?

Swali la pili, katika Wilaya ya Mufindi kuna vikundi vingi sana ambavyo vimesajiliwa na kuna vikundi vingine vinalima chai. Si unajua Wilaya ya Mufindi inalima sana chai. Mara nyingi wakulima wa chai walikuwa hapati mikopo.

Sasa je, wakulima wa chai wale unawathibitishia kwamba mwaka huu mgao huu wa mbolea ya ruzuku wanaweza kupata?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mwaka jana kulikuwa kumejitokeza matato kwa sababu Serikali ilikuwa imeahidi wananchi kupitia vikundi vyao wangeweza kupata pembejeo. Lakini pia Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wakumbuke kwamba mwaka tulikuwa na mipango miwili. Tulikuwa na utaratibu wa mbolea chini ya utaratibu Tuliozoea wa vocha.

Lakini utaratibu ule ulikuwa unakwisha kwenye msimu wa mazao ambayo yako shambani sasa. Kwa maana hiyo, pamoja na kwamba vile vikundi vingine ambavyo vililhamasishwa vianzishwe na kwamba Serikali ingeweza kupeleka pesa hazikupeleka. Lakini bado Wilaya zote ziliweza kufaidika kwa utaratibu ule wa vocha za kawaida.

Hata hivyo, Mheshimiwa Mbunge anaposema kuna vikundi vitatu vilitoa ile asilimia 20 na kwamba Serikali iliahidi kutoa asilimia 80. Ni kweli, lakini si kweli kwamba zile asilimia 20 zilizochangwa zilichukuliwa na Serikali kwa sababu zile pesa zilikuwa ni za vikundi na vikundi kwa sababu havikupata asilimia 80 ya Serikali bado zile hela ni za vikundi wala Serikali haikuchukua.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Kama Serikali ilichukua hilo siyo la Wizara. Lakini nataka nimhakikishie kabisa Serikali haikuchukua pesa za wakulima.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba wakulima wa chai wamekuwa hawafaidiki. Tumetenga pesa kwenye Bajeti yetu na kama tulivyoisoma tumetenga karibu shilingi bilioni 89 ambazo zitakuwa chini ya utaratibu wa kupeleka mbolea kwenye vikundi, kupeleka mikopo kwenye vikundi hivyo ili viweze kufaidika na mikopo hiyo.

Kwa hiyo, na wakulima wa chai kama watakuwa wamejinga kwenye vikundi vya Saccos na amcos wakiwa na sifa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba na wenyewe pia wanaweza wakapata mikopo hiyo. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii nichangie swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Njombe ina wakulima wengi wanaozalisha sana zao la chakula na kwa kuwa ruzuku hutolewa kwenye kilimo cha mahindi na Njombe ni wakulima wakubwa wa zao la viazi.

Je, Serikali imejipangaje na kwa sababu kilimo cha viazi kindimwa wakati wote wa mwaka. Serikali imejipangaje kuwasaidia wakulima wa zao la viazi kupata ruzuku ya mbolea? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao tunakwenda nao sasa kwa maana ya kupatia mikopo vikundi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama wakulima wa viazi watajiunga kwenye vikundi vya kuweka na kukopa wakiwa na ushirika ulio nzuri wata-qualify kupata mikopo na jambo zuri Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mikopo hii imekuwa inaelekezwa kwenye zao la mahindi, mpunga na mengine ni kwamba sasa hivi tuna utaratibu wa vikundi na tunazungumza na mabenki.

Kama mabenki yakikubali na Serikail ikiwa tayari kuweka pesa kwenye mabenki basi vikundi vingi vinavyojishughulisha na shughuli za kilimo vitaweza kupata mikopo kwa urahisi zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

Na. 167

### **Mkataba wa Umoja wa Afrika Kuhusu Demokrasia**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI (K.n.y. MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Mkataba wa Umoja wa Afrika juu ya demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora unazitaka nchi wanachama kuendesha nchi zao kwa kuzingatia demokrasia na utawala bora ili kusababisha uwepo wa amani na utulivu nchini:-

Je, kwa nini hadi leo nchi yetu haijaridhia mkataba huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni sahihi kabisa kuwa nchi ambazo ni wanachama wa Umoja wa Afrika tumekubaliana kuzingatia demokrasia na utawala bora ili kusababisha uwepo wa amani

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

na utulivu katika nchi zetu na maendeleo pia. Kwa sasa Mheshimiwa Spika, Tanzania haijaridhia mkataba huu kwa sababu una vifungu ambavyo vinapingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyopo sasa pamoja na Sheria zetu za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu itaendelea na mchakato wa kuridhia mkataba huu ikiwa ni pamoja na kukamilisha mchakato wa Katiba Mpya. Mheshimiwa Spika, kutokana na swali hili zuri la Mheshimiwa Benadertha Mushashu, mwakilishi wetu aliyetuletea sifa nzuri na kubwa katika Bunge la Afrika na jibu nililolitoa ni dhahiri kwamba Rasimu ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba ina maeneo mengi na sura nyingi na vifungu vingi vyenye manufaa kwa nchi yetu na wananchi.

Sasa na kwa miaka mingi ijayo, zaidi ya muundo wa Serikali. Ni matumaini ya Serikali kwamba Bunge Maalum litakutana kama ilivyopangwa na Wajumbe wote watahiriki kikamilifu.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, asante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ambayo amenipatia. Lakini nataka kuhoji Mheshimiwa Spika, kwamba je, Mheshimiwa Waziri anaweza kunieleza sasa ni Kamati zipi za ufuatiliaji zinazoshughulikia suala hili na Kamati hiyo inaweza kunipa tathmini ya suala hili zima kwa ujumla?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nilishiriki kwenye majadiliano ya Mkataba huu Brazzaville na kote ambako tulikutana. Jambo ambalo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri tathmini inayofanywa ni katika Sheria zetu za Uchaguzi na hasa kwenye suala la Matokeo ya Urais.

Sasa kama mnavyofahamu kwamba katika Sheria yetu Katiba yetu ya sasa hairuhusu Uchaguzi wa Urais kuhojiwa na ile *treaty* ya Afrika inasema ni lazima mtu yoyote ambaye hakuridhika na mwenendo wa uchaguzi anaweza kufanya kuhoji Mahamani na kutokana na mchakato tulio nao sasa umeshaona vifungu ambavyo vinataka hilo lifanyike. Nafikiri itakuwa inakwenda sambamba na yale matashi ya wa Mkataba huo.

Lakini nani anafanya Ofisi yangu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, tunaona ni maeneo gani ambayo yanaweza kurekebisha kusudi tuweze kuridhia na nafikiri yamebaki machache eneo kubwa lililobaki ni hilo la utaratibu wetu wa uchaguzi pamoja na kuruhusu wagombea binafsi. Kwa sababu ile mkataba unasema ni lazima mtu yoyote ambaye anataka kugombea agombea.

Sasa kama tukikubaliana hivyo itakuwa. Kama hatutakubaliana hivyo ina maana kwamba huwezi kuingia kwenye mkataba ule.

Lakini la pili ni kwamba hakuna utaratibu kwenye mkataba ule wa kuweka *reservation* kwamba uwe mwanachama lakini mambo mengine usitekeleze. Nafikiri Serikali ya Zimbabwe ilijaribu, Waziri wa Sheria wa Zimbabwe alijaribu kuwashawishi Wajumbe waliokuwa wana-*negotiate*. Lakini ikakataliwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, huo ndiyo utaratibu wa sasa na ikifika wakati tutaridhia. Kwa sababu tulikuwa tunaongoza kwenye majadiliano ya Mkataba huo.

Na. 168

**Bwawa la Maji la Mwanjoro (Meatu)**

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. DKT. ANTHONY MBASSA (K.n.y. MHE. MESHACK J. OPULUKWA)** aliuliza:-

Je, Bwawa la Mwanjoro lililoko Wilayani Meatu limefikia hatua gani ya utekelezaji na ni fedha kiasi gani kimekwishatumika hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bwawa la maji la Mwanjoro lipo katika kijiji cha Dinamo Wilaya ya Meatu. Bwawa hilo linalenga kuwapatia maji wananchi wapatao 7,420 na mifugo ipatayo 42,526. Hadi sasa shilingi milioni 819.1 zimetumika kutekeleza kazi zifuatazo:-

Ujenzi wa tuta la kuzuia maji, uchimbaji na ujenzi wa utoro wa maji pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kutolea maji kwenye bwawa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ujenzi wa bwawa umesimama baada ya mkarandasi wa mradi kuondoka eneo la kazi bila ruhusa ya mwajiri. Wizara kupitia Wataalam wake imefanya ukaguzi na upimaji wa kazi zilizofanyika na zinazohitajika kufanyika ili kukamilisha ujenzi wa bwawa hilo. Kwa sasa wataalam hao wako katika hatua za mwisho kukamilisha taarifa ya ukaguzi huo.

Aidha, Wizara iko katika mchakato wa kumpata mkandarasi mwingine wa kuendeleza ujenzi wa bwawa hilo. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 shilingi milioni 428 zimetengwa ili kuendelea na ujenzi wa bwawa hilo. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ANTHONY MBASSA:** Asante sana Mheshimiwa Spika. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa mradi huu wa maji ni mkubwa sana na huyu mkandarasi ametoroka kazini kwa muda mrefu sana.

Je, Wizara ina mpango gani wa kumfuatilia na kumchukulia hatua za kinidhamu?

Swali la pili, kwa kuwa miradi mingi ya maji inagharimu fedha nyingi na watu wamekuwa wakichukua kandarasi hizi aidha watu ambao hawana uwezo, hawana vifaa na utaalamu duni, *I mean* utaalamu wa kutosha. Wizara ina mpango gani wa kuwatambua wandarasi kama hawa pindi wanapooomba kazi ili kusudi wasipewe, wapewe watu wenye uwezo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba kweli ujenzi wa Bwawa hili umechelewa na wiki moja iliyopita nilikuwa pale nimekagua lile bwawa, na kwamba hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa juu ya mkandarasi huyu ambaye amesababisha hasara kwa Serikali. Sasa hivi tunashauriana na Wanasheria na Kitengo chetu cha Manunuzi kuwaandikia Bodi ya Usajili wa Wakandarasi wamnyime kazi zozote ndani na nje ya nchi hii. *(Makofi)*

Lakini la pili ni kwamba, Serikali baada ya kasoro zilizojitokeza juu ya watu wasiokuwa na uwezo, kwa sasa tutachukua hatua za kuona kwamba, tunawapata wakandarasi wenye uwezo na kujiridhisha na uwezo wa kifedha na vitendea kazi.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. ROSEMERY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa, mabwawa yote nchini yanayosimiwa na Wizara imeonekana ufanisi wake au utekeleaji wake kuwa hafifu na Wakandarasi wote wametoroka nchini.

Mheshimiwa Spika, je, huyu Mkandarasi aliyekuwa anajenga Bwawa la Mwanjolo, ambaye amelipwa zaidi ya 95% ya malipo ya gharama za mradi na bado hajakamilisha kazi na sasa Waziri anasema Serikali imetenga milioni 400 ambazo hazitoshi kabisa.

Je, Waziri yuko tayari kuji-commit hapa atenge bilioni moja nyingine ambayo ni sawasawa na gharama ya mradi, ili kuweza kukamilisha bwawa lile?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rose Kirigini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkuu wa Wilaya hii, Rose Kirigini, kwa kazi nzuri anayoifanya. Amefuatilia sana bwawa hili na amenishawishi mimi na Waziri na Waziri akaniagiza kwenda na nimejionea hali iliyopo hapo Mwanjolo na kijiji cha Dinamu kwa hiyo, nampongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niliwaahidi Viongozi wa Wilaya wakiwemo Wajumbe wa Kamati ya Siasa kwamba, Serikali itakamilisha Bwawa hili Mwaka huu wa Fedha. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba, pamoja na hatua za kinidhamu tutakazochukua juu ya Mkandarasi huyu ambazo tayari nimeshazisema kwamba, tutampiga marufuku asipewe kazi ndani na nje ya nchi hii, lakini la pili ni kwamba, fedha zitatengwa kuhakikisha bwawa hili linakamilika.

Mheshimiwa Spika, taarifa nimeshaipokea. Tutamtafuta Mkandarasi ndani ya miezi mitatu na kasi baada ya hapo itakamilika katika miezi mitatu. *(Makofi)*

Na. 169

### **AHADI YA KUUPATIA MJI WA LUSHOTO MAJI**

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

Serikali kupitia Mawaziri/Manaiibu, Waziri wa Wizara ya Maji alitoa ahadi ya kuboresha upatikanaji wa maji katika Mji wa Lushoto, ikiwa pia ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2010.

Serikali ilikubali kuunganisha maji kutoka chanzo cha Kibohelo hadi kwenye matanki ya Kwembago na ujenzi wa tanki kubwa pale *Magamba Coast* kama hatua za dharura za kuupatia mji huo maji wakati tukisubiri mpango wa kusambaza maji kwa mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

(b) Serikali iliahidi kulipia gharama mradi uliobuniwa na wananchi uitwao *Mtumbi Water Supply Project*. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, lenye Vipengele (a) na (b), kama ifwatavyo:-

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kushughulikia suala la kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Lushoto. Wataalamu wa Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Lushoto walifanya tathmini ya gharama halisi ya mradi huu. Tathmini hiyo ilibaini kuwa, jumla ya shilingi milioni 260.2 zinahitajika kwa ajili ya kuweka mtandao wa bomba kutoka chanzo cha Kibohele kupitia Magamba hadi Tenki la Maguzoni, lenye ujazo wa Lita 225,000. Kutoka Maguzoni mtandao huo utapeleka maji Lushoto.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetuma shilingi milioni 150 mwezi Disemba 2013 kupitia Mamlaka ya Maji Safi na Mazingira Mjini Tanga, ambao wanasimamia utekelezaji wa Mradi huo. Hadi sasa kazi zilizofanyika ni upimaji wa njia ya bomba likakopita, usanifu pamoja na kuagiza na kulipia mabomba yanayohitajika. Kazi ya ulazaji wa mabomba itanza mwezi Juni 2014 mara baada ya mabomba hayo kuwasili eneo la mradi, fedha zilizobaki zitatolewa katika Mwaka huu wa Fedha, 2013/2014.

(b) Mheshimiwa Spika, wananchi katika Vijiji vya Kwekanga, Mziragembeyi, Malimbwi na Hemtoye walibuni Mradi wa Maji uitwao *Mtumbi Water Supply Project*. Serikali kwa kuthamini juhudi za wananchi hao itatekeleza mradi huo katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na kuagiza na kulipa mabomba yanayohitajika. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Na nianze kwa kumshukuru Profesa Maghembe na aliyekuwa Naibu, Mheshimiwa Mahenge, kwa kuonesha dalili za kutaka kutatua tatizo hili la maji Mji wa Lushoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Swali langu la Msingi niliuliza na nikasema kwamba, hizi ni hatua za dharura. Na katika hatua hizo, ilikuwa lijengwe Tenki la maji pale *Magamba Coast*, lakini halikutajwa humu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itamke kwa sababu, mradi huu ulikuwa usaidiwe na wanaoita *Water Sector Reform Program*, ili kutatua tatizo la maji Mji wa Lushoto, Waziri hajataja lolote ni hatua gani zinachukuliwa katika mradi huu ili tatizo la maji mji wa Lushoto litoweke.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu vijiji vya kata za Kwekamga, malimbwi, Kilole, kupata maji kwa juhudi zao walizoonyesha Serikali katika mkutano wa tatu wa Bunge lako hili iliahidi kutoa fedha kusaidia wananchi hawa milioni kumi na tatu mpaka leo fedha hizo hazijatolewa.

Je, ni wathibitishieje wananchi hawa kwamba sasa mradi wao utajengwa kama walivyoahidi katika jibu lao la pili kwamba utajengwa 2014/2015? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la Mheshimiwa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu zuri. Katika jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri Serikali imepeleka shilingi 150 milioni kwa ajili ya kuanza kazi hiyo. Kabla mwaka huu wa fedha haujakamilika tunatarajia kuukamilisha mradi huo fedha hizo ambazo zilipelekwa awali zilikuwa hazitoshi kazi zilizotajwa pamoja na kujenga tenki katika eneo la *Magamba Coast*. Hivi sasa kazi ya kujenga tenki hilo itakamilika na mradi huo utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, pili kwa wananchi wa vijiji vilivyotajwa vya mradi huu uliobuniwa na kijiji tumetenga fedha katika Bajeti itakayoanza Julai moja mwaka huu kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. *(Makofi)*

Na. 170

**Ahadi ya Kupeleka Umeme Ndagalu**

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kutekeleza ahadi yake ya kupeleka umeme katika Tarafa ya Ndagalu kutoka Magu Mjini kupitia Vijiji vya Lumeji, Ng'haya, Nkuhungulu na Mwashepi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGA KITWANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia wakala wa Nishati vijijini REA inatekeleza mradi wa kupeleka umeme katika tarafa ya Ndagalu chini ya mpango kabambe wa umeme vijijini awamu ya pili. Mradi huu unahusisha vijiji vya Lumeji, Ng'aya, Nkungulu na Mwashepi ulianza kutekelezwa mwezi Aprili mwaka 2014 na mkandarasi aitwaye CHIKO.

Kazi zilizokamilishwa mpaka sasa ni upimaji wa maeneo yatakayopatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme kwenye tarafa hii itajumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 28, ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 15, ufunguji wa transfoma nane na kuwaunganisha umeme wateja wa awali wapatao 412. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2015 na utagharimu shilingi bilioni 1.36.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze sana Serikali kwa kuitikia kilio cha wana Ndagalu ambayo tarafa nzima yenye tarafa nne haina umeme hata kidogo nashukuru sana Serikali kwa hilo na ninaishukuru kwamba imetenga kiasi hicho cha fedha bilioni 1.36 na kuteua mkandarasi tayari.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza kwa kuwa ahadi ya Serikali ya awali ilikuwa kwamba hadi kufikia Juni mwaka huu umeme utakuwa umeshaanza kufungwa lakini sasa hivi inasema sasa utakamilika mwezi Juni mwakani miezi mitatu kabla ya uchaguzi. Swali langu ni kwamba ni sababu gani zimesababisha mradi huo kuchelewa kuanza na wakati awali Serikali ilisema utakamilika mwezi Juni mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mkandarasi CHIKO ambaye amepewa tenda hii inasemekana ana eneo kubwa sana mpaka Tabora, mpaka maeneo mengi. Kwa kuwa, ana maeneo makubwa uwezekano wa yeye kumaliza mradi huu mwaka kesho Juni ni mdogo. Je, kwa nini Wizara isimsaidie huyu Mkandarasi na kumtaka agawanye huu mradi kwa Makandarasi wengine wadogo na ikasimamia, ili kuhakikisha kwamba, kweli Mradi huu unakamilika Juni mwaka kesho, ili wananchi wa Tarafa ya Ndagalu wakipe kura zote Chama cha Mapinduzi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA (MHE. CHARLES MUHANGA KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dokta Limbu, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kwamba, Mradi ulikuwa ukamilike mwezi Juni mwaka huu, lakini Wakandarasi kwa mara ya kwanza walipo-*tender* hakuweza kupatikana Mkandarasi ambaye alikuwa anakidhi viwango mwezi Novemba mwaka jana. Kwa hivyo, *tender* hiyo ilirudiwa na iliporudiwa ndipo Mkandarasi huyu akapatikana na alisaini Mkataba mwezi Machi na hiyo ndiyo iliyokuwa sababu kubwa ya kuchelewa Mkandarasi huyu.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu swali lake la pili kwamba, Mkandarasi huyu ana eneo kubwa sana, sisi tunaenda kwa Mkataba. Mkandarasi huyu ana Mkataba na sisi na amethibitisha kwamba, yeye ana uwezo na tunamsimamia kwa karibu sana. Kwa hivyo, sisi tutahakikisha kwamba, amekamilisha kazi hii kulingana na Mkataba aliowekeana na Serikali.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mkandarasi Chiko ndiye aliyeko katika Jimbo pia la Sumve; Wilaya ya Magu pamoja na Wilaya ya Kwimba ni Wilaya majirani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, imesemwa miradi hii itakamilika Juni mwaka 2015. Naomnba nimuulize Mheshimiwa Waziri, kama atakamilisha Juni 2015 ni lini ataanza kazi ambayo ameipanga?

**SPIKA:** Naomba Mheshimiwa Badwel, naomba urudi ulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI (MHE. CHARLES MUHANGA KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndassa, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi huyu anafanya kazi katika Mkoa wote wa Mwanza. Tuna uhakika kabisa mpaka sasa hivi kazi ambazo ameshafanya ni kuhakikisha kwamba, amefanya *survey*, amechora michoro ya *design* na sasa hivi ameagiza vifaa, ili kuanza kuweka nguzo, kuweka nyaya na kuhakikisha kwamba, wateja wanaunganishwa. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Ndassa kwamba, atatekeleza kulingana na Mkataba tuliowekeana naye.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Mradi wa Serikali wa Kupeleka Umeme Vijijini kupitia Wakala wake wa REA ni mradi mzuri, lakini wananchi wengi wanaoishi vijijini bado wanaishi katika nyumba za matope na zilizoezekwa kwa nyasi; jambo ambalo hawataweza kufaidika na umeme hata kama nguzo zinzipita katika mashamba yao. Je, Serikali iko tayari kuangalia kwamba, vifaa vya ujenzi vinashushwa bei, ili na wananchi wa Vijijini wafaidike na umeme huu na mradi wa REA?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGA KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishti na Madini, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi ni suala mtambuka, maana unapozungumzia kushusha bei, unazungumzia gharama za uzalishaji kutoka viwandani. Sasa sina uhakika kama kwamba, Serikali itoe ruzuku au iweje. Lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba,



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Serikali siku zote imekuwa ikidhibiti na ikihakikisha kwamba, vifaa vya ujenzi vinakuwa katika hali ya nafuu. Kwa hivyo, nimhakikishie tu viwango vilivyopo sasa hivi ndivyo hivyo vitakavyowawezesha wananchi. Tutakachotakiwa kufanya ni kuongeza uzalishaji, kupata mapato zaidi, ili tuweze kujihakikishia kwamba, tunajenga nyumba zilizo bora.

Na. 171

### **Faida za Uchimbaji Madini Nchini**

**MHE. MARIAM N. KISANGI (K.n.y. MHE. RITA L. MLAKI)** aliuliza:-

Nchi yetu ni nchi ya tatu katika Afrika kwa kuwa na madini mengi ya dhahabu.

(a) Je, Tanzania imefaidika vipi na madini hayo tangu yameanza kuchimbwa?

(b) Je, ni mgawanyo wa asilimia ngapi kwa migodi iliyopo na tunapata fedha kiasi gani kwa mwaka?

(c) Je, kwa nini nchi isikope fedha kwa ajili ya kuendesha migodi kupitia STAMICO kuliko kuwapa wageni rasilimali yetu yote?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGA KITWANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louis Mlaki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania imefaidika na Migodi ya Dhahabu kwa kupata mapato, ajira na fursa za kibiashara kwa makampuni ya ndani. Kwa mfano, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 mpaka 2013 Serikali imepata kiasi cha shilingi trilioni 2.07 kama kodi na mrahaba kutoka kwa wamiliki wa migodi mikubwa ya dhahabu nchini, sawa na 9.3% ya mapato yote ya migodi katika kipindi husika. Aidha, takribani Watanzania wapatao 8,800 wamepata ajira za kudumu kwenye migodi hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa wastani Serikali inapata kati ya 6% hadi 12% ya mapato kutoka Sekta ya Madini, ambayo ni takribani shilingi bilioni 380 kwa mwaka kutokana na malipo ya kodi mbalimbali na mrahaba kutoka kwa Wawekezaji katika Sekta ya Madini.

(c) Mheshimiwa Spika, Aya ya 5.5 ya Sera ya Madini ya Mwaka 2009 inaelezea nia ya Serikali kuwekeza mikakati katika shughuli za madini. Kwa msingi huo Serikali iliamua kulifufua Shirika lake la Madini la Taifa (STAMICO), ili pamoja na majukumu mengine lishiriki katika kuanzisha na kuendesha migodi mikubwa nchini. Uamuzi huo umeanza kutekelezwa kama Bunge lako Tukufu lilivyoelezwa kupitia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya Mwaka 2013/2014. Shirika hilo linaendelea kuimarishwa kulingana na upatikanaji wa fedha, ili liweze kushiriki ipasavyo kwenye shughuli za madini kwa niaba ya Watanzania wote.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninalo swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, mpaka sasa kuna watu mbalimbali wanakamatwa kwenye Viwanja vya Ndege wakiwa wanatorosha madini kutoka katika nchi yetu, hali ambayo kwa upande wangu inanionesha wazi kwamba, pamoja na faida tunayoipata pia, kuna hasara kubwa ndani yake.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kudhibiti wezi hawa wa madini katika mipaka yote ya nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGA KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimia Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa TMAA, imejipanga vizuri kwa kuhakikisha kwamba, inaweka Wataalamu katika maeneo yote ya Viwanja vya Ndege na sehemu ambapo uzalishaji wa dhahabu unafanyika. Kama siku zote tumekuwa tukisema sasa hivi umepungua sana na kukamatwa kwa watu hao ambao wanatorosha madini ni ishara tosha kuonesha kwamba, Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba, utoroshaji wa madini haufanyiki.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri tafiti zinaonyesha duniani kote ambako madini yanachimbwa wakazi wa maeneo hayo wengi wamekuwa *traumatized, wounded, stressed* kutokana na vitendo ambavyo wamefanyiwa na makampuni makubwa na Serikali husika zimekuwa zikitetea makampuni ya kigeni.

Je, ni taratibu gani na mipango gani mizuri ambayo imewekwa kwa ajili ya maeneo mbalimbali ambayo yanaendelea kugunduliwa katika nchi hii yenye madini ambayo Watanzania hawatapata tena maswahiba kama hayo ambayo yamepatwa katika maeneo mengine kama kule Nyamongo na maeneo mengine?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msigwa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji au makampuni yanayochimba madini katika nchi yetu yanaongozwa na Sheria na katika maeneo hayo tumehakikisha kwamba kunakuwepo na hali ya amani kwa kuhakikisha kwamba migodi pamoja na wananchi wanapoishi pale wanakuwa na mahusiano mazuri ikiwa ni pamoja na kuyaomba na kuyataka makampuni haya yatoe huduma za kijamii kwa wananchi wanaoishi na kuzunguka migodi hiyo.

Tumeona namna ambavyo kule Nyamongo kwa sasa hivi ambapo shule zinajengwa na makampuni haya. Tumeona kule Geita *Gold Mine* ambako wameweza kusaidia kuhakikisha kwamba wananchi wa Geita wanapata maji hayo ni mahusiano mazuri na hatujapata taarifa inayoonyesha kwamba wananchi katika maeneo hayo wanakuwa *traumatized* kama ulivyosema. *(Makofi)*

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba na mimi nimwulize swali dogo Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sehemu ya migodi, kuna viwanja vya ndege ambavyo viko katikati ya migodi.

Je, Serikali inadhibitije viwanja hivi vya ndege ili visipate kutorosha madini yetu na kwenda nchi za nje?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msabaha kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza ni kwamba katika migodi hii kwanza tuna watu wetu wa TRA, halafu tuna watu wetu kutoka TMAA ambao wanakuwepo pale kuhakikisha kwamba uzalishaji wa dhahabu au almasi unapotokea wanahakiki na kuona kwamba kodi na tozo zote ambazo zinastahili zinalipwa. Kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba utoroshaji haufanyiki na mapato ya Serikali yanapatikana kwa Sheria zilizopo.

**MHE. RIZIKI. S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia hii hoja. Kwa kuwa sasa hivi katika TMAA baada ya kubaini kuweka udhibiti mkubwa katika Airport tumeona ndugu zetu kutoka China. Katika watu waliokamatwa watu 18 ni kutoka China, ina maana asilimia karibu 90 ya watu wanaoiba madini ya Tanzania ni Wachina.

Je, Serikali ina mpango gani na kushirikiana na Ubalizi wa China hapa nchini na kuwaambia wenzetu wa China waje kutuhakikishia usalama wetu wa madini yetu kuwa katika hali ya usalama? Naomba Mheshimiwa Waziri atoe majibu haya.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lulida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwizi wa madini ni mwizi tu awe Mchina, awe Mswahili, awe Mkenya ni mwizi na Serikali itaendelea kuwakamata wote ambao wanajaribu kuiba madini yetu. Kuhusu kuwa na mahusiano ya moja kwa moja na Ubalizi wa China au Nchi ya China nimweleze tu kwamba sidhani kama Serikali ya China inawatuma hawa watu waje watu bie madini yetu. Hawa ni watu binafsi kwa hiyo watashughulikiwa kulingana na Sheria na hata kama utakuwa unatoka Lindi umeiba utashughulikiwa tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naona muda umekwisha sana naomba kwanza niwatambue wageni waliopo. Kwanza kabisa nina wageni wa Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, Waziri wa Maji, ambao ni familia yake. Nilitangaza jana ikiongozwa na mke wake Mrs. Kudra Maghembe kama yupo tena asimame lakini tulitangaza jana. Wageni wengine wa Profesa Maghembe nilisema jana wanaongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Mheshimiwa Engineer Bashir Mlindoko na Naibu Katibu Mkuu Engineer Mbogo Mfutakamba kwa maana hiyo nasema ikiongozwa kwa sababu leo ni siku yao. Kwa hiyo, ni timu yote ipo hapa, ziko Taasisi na Bodi na kila kitu.

Halafu nina wageni 23 wa Mheshimiwa Amos Makala Naibu Waziri wa Maji kutoka Jimbo la Mvomero. Naomba wale wa Mvomero wote wasimame waliopo kama wapo aah mbona ishirini na tatu. Okay wengine wako huku ahsante sana. Sasa hapa kuna Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Mvomero wakiongozwa na Ndugu Abdallah Mtiga mwenyekiti ahsante, Sekretarieti ya Wilaya ya Mvomero wakiongozwa na Kaptaini Bakari Bindo, Katibu Msaidizi wa Wilaya ahsante sana. Makatibu wa Mheshimiwa Mbunge wakiongozwa na Ndugu Abdallah Mgaya, Ndugu Farida Zafarani, Ndugu yake Naibu Waziri amekuja kwa niaba ya mke wake maana mke wake anauguliwa na mzazi wao. Wageni wa Mheshimiwa Godfrey Wenston Zambzi, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika nao tunapenda kuwakaribisha. Watu wakiwa wametajwa halafu tujue ni watu gani hawa sasa ni majina tu naomba wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, wasimame ahsante sana. *(Makofi)*

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Wageni wa Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, ambao ni Ndugu Issa Njonjo, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ruangwa naomba ahsante sana, Mheshimiwa Essau Bernard, Katibu CCM Wilaya ya Ruangwa, yuko pia Ndugu Kasembe Hokororo, Katibu wa Ofisi ya Mbunge wa Ruangwa, ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, ambaye ni Engineer Oscar Abeid, kutoka Kilindi sijui kama naye yupo hapa ahsante sana. Tuna wageni wa Mheshimiwa Deo Sanga, ambao ni Katibu mwenezi wa CCM Mkoa wa Njombe Honoratus Pilimin Mgaya ahsante sana, kuna Katibu mwenezi wa CCM Wilaya ya Njombe Ndugu Hitler Benjamin Msolla, ahsante sana. Halafu tuna wageni 19 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bahi wakiongozwa na Ndugu Rahel Chuwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, naomba wasimame hawa kumi na tisa nadhani hawajafika. *(Makofi)*

Kuna wageni waliokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wako wanafunzi 90 kutoka Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam (DSA) naomba wasimame wanafunzi hao ahsanteni sana, na someni kwa bidii na mimi nilisomea maeneo hayo ya Uhasibu. Someni kwa bidii kabisa. Tuna wanafunzi 67 kutoka Shule ya Sekondari Kisiwani, naomba wasimame wanafunzi hao naona hawajaingia na Ndugu Hassan Msingi kwa ajili ya kutembea naye pia anakuja kuliangalia Bunge lakini sijamwona.

Matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Luhaga Mpina, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba kutakuwa na kikao chao leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo napenda niwatangazie kwa masikitiko kuhusu misiba ambayo tumeipata. Mheshimiwa Zitto Kabwe amefiwa na Mama yake Mzazi tarehe 1 Juni, 2014 huko Dar es Salaam alikokuwa anatibiwa katika Hospitali ya AMI. Mwili wa Marehemu ulisafirishwa jana kwenda Kigoma kwa mazishi ambayo yatafanyika leo saa saba mchana.

Halafu wakati huo huo jana hiyo hiyo tumepata pia msiba wa Baba yake Mzazi Mheshimiwa Martha Mlata, ambaye amefia katika Hospitali ya KCMC Moshi, Kilimanjaro alikokuwa anatibiwa. Mwili wake umeshasafirishwa jana kwenda Singida kwa mazishi ambayo yatafanyika kesho tarehe 3 Juni, 2014 huko huko Singida saa sita mchana. Kwa hiyo ilikuwa weekend siyo nzuri, Wazazi wa wenzetu wamefariki na kama mtakumbuka siku Martha Mlata alipokuwa anachangia aliwaomba wazazi wote wawili hivyo mwenyezi Mungu alifanya alivyofanya. Roho za hawa Marehemu ziweze kupumzika kwa amani, amina.

Baada ya kusema haya Waheshimiwa Wabunge mimi nina kazi Ofisini. Kwa hiyo, nitamwomba Mwenyekiti Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan. anipokee. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Kamati zinazohusika na Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani walimaliza shughuli zote Jumamosi. Kwa hiyo, tutakwenda kwenye uchangiaji na tutakuwa na orodha kubwa kutokana na umuhimu wa Wizara yenyewe. Nafikiri nafasi tunayo ya kuweza kuwamaliza wote. Kwa hiyo, mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, ajiandae Mheshimiwa Kiumbwa.

**MHE. ABDUL-AZIZ MOHAMED ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa wa kwanza kuchangia leo katika Wizara hii ya Maji. Pili napenda

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri inayoendelea katika kuendeleza miradi ya maji. Pia napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yake kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro Mjini kuna tatizo kubwa sana la maji. Tunashukuru tumepewa mradi wa maji wa MCC toka mwaka 2011 ulianza ukarabati vyanzo vya maji katika mji huu wa Morogoro lakini hadi leo ni mwaka wa tatu bado hawajamaliza wakandarasi wanasuasua inasababisha adha kubwa kwa wananchi wa Morogoro kutopata maji na maji kwa sasa wanavyoendelea kukarabati kidogo kidogo maji yanatoka machafu, yana rangi ya kijani, ni mabaya kwa afya za wana Morogoro.

Lakini sehemu kubwa ya Morogoro ina tatizo hili la maji, kuna sehemu ya Kihonda, Kihonda yote ni tatizo la maji, Mkundi tatizo la maji, Lukobe tatizo la maji, Kihegea tatizo la Maji, Nguru wa Ndege tatizo la maji, Tubuyu tatizo la maji, Misongeni tatizo la maji, Tungi yote tatizo la maji, Nanenane tatizo la maji, Area Six tatizo la maji, Area five tatizo la maji na Kata ya Mindu yote ni tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huu mradi tunata tujue huu mradi utawanufaisha wote hawa wana Morogoro maana umekaa miaka mitatu na wananchi wa Morogoro wanasubiria tu, hali imekuwa mbaya ya maji na maji mpaka sasa wanayopata mjini sasa yanatoka kidogo kidogo na hawapati maji lakini cha kushangaza bado. Pale Morowasa maji yanatoka na magari yanajazwa manteki kwa manteki haya maji yanatoka wapi? Kitu ambacho kinashangaza sana. Nilitaka kujua vile vile huu mradi huu wa MCC utawanufaisha wananchi wa Morogoro wote au wataongezewa wale waliokuwa nacho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri kwako sidhani kama kuna tatizo la maji sasa na wewe mimi naamini ni mkazi wa Morogoro ukiwa na mdogo wangu pale Makalla mnajua tatizo la Morogoro wote ni wakazi pale kwangu.

Lakini mpaka sasa bado. Tumeambiwa kuna miundombinu inayotakiwa kwenda kutoka kwenye tanki la maji Tumbaku kwenda Kihonda huko mabomba yameoza kuna mradi unaotakiwa upite pale mpaka leo mwaka wa pili hakuna ni maneno tu na mimi ningependa ile Morowasa pale Mheshimiwa Waziri uisafishe, umebadilisha Mkurugenzi lakini bado hata bodi inachaguliwa kirafiki, tuchague watu wapo wa kufanya kazi wa kuweza kuishauri na kuweza tukafanikiwa. Mheshimiwa Waziri ulikuja Morogoro na ulituhidi utatupa pesa bilioni mbili kwa ajili ya kusambaza mabomba lakini mpaka leo mwaka wa tatu sasa huu neema ya 2015 Mheshimiwa Waziri tunahitaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia tena wananchi wanahunua maji sasa kwa shilingi elfu moja, shilingi mia nane kwa ndoo kwa mtu wa kawaida wa hali ya chini ataweza kumudu kimaisha, hata mfanyakazi wa Serikali atapata mshahara wa shilingi ngapi ili aweze kuweza kukidhi mahitaji yake ya maji. Tunachimba visima lakini havitoshelezi bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine kero nyingine ya bili za maji na mita za maji. Wananchi wanachajiwa maji mita za maji zinaonyesha mwisho wa mwezi mtu hajatumia miezi mitatu mita inamuandikia bili alipe mwisho wa mwezi na kuna mita hizi mpya zilizofungwa sasa hivi ndiyo zinawaumiza wananchi analetewa bili hajaona hata tone moja la maji kwa kweli hii hali si nzuri. Mheshimiwa Waziri ninaomba chonde chonde ukija Morogoro uje uone hali halisi nikutembeze maeneo yote ili uone tatizo kubwa hili la maji. Kuna tatizo lingine ambalo lipo pale mgao wa maji.

BGT020514AM05LP

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, namshukuru Mwenyezi Mungu Subahhan Wataallah, kunipa afya, uzima na salama ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Profesa Maghembe na Naibu Waziri pale kwa kazi nzuri wanayofanya. Hii timu ya Profesa na mtani wangu pale Mheshimiwa Makala, ni timu nzuri ambayo kwa kweli wanaweza wakafanya kazi nzuri sana katika mambo yetu ya maji.

Tatizo ni kwamba hatuwapi pesa za kutosha, mimi naamini kama Profesa kama angepewa fedha za kutosha kama ambavyo tunajua umuhimu wa maji, akisaidiwa na Ndugu Makala, pale, tatizo la maji linaweza likapata ufumbuzi mkubwa sana. Msiendelee kumlaumu bila kumwezesha tumwezeshe ashindwe ili tupate nafasi ya kumlaumu. Kwa hiyo, nimwombe sana sana, Serikali imsaidie kutatua tatizo la maji na ipo Wizara hii iko ndani ya BRN, huo ni umuhimu wa kuwa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niseme kwamba mimi ni miongoni mwa watu ambao nimelalamika sana habari ya mradi wa Benki ya Dunia kwa kweli mradi huu haufahi. Jina kubwa mradi wa Benki ya Dunia, lakini vitu vinavyofanyika na mradi huu ni kwamba hamna kitu kabisa, ni aibu hata kuita mradi wa Benki ya Dunia, afadhali hata ungeitwa mradi wa Benki ya Singida, au wa Benki ya Lushoto au ya wapi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umeanza mwaka 2007, mimi katika jimbo langu mpaka sasa ni vijiji vitatu tu, vijiji vitatu moja, mbili, tatu. Ni vijiji vitatu tu toka mradi umeanza mwaka 2007 takriban miaka minane. Sasa mradi gani na sisi hatuna mradi mwingine zaidi ya mradi wa Benki ya Dunia? Ukiuliza Singida ukiuliza Ikungi, unaambiwa kwamba ninyi mnao mradi wa Benki ya Dunia. Sasa vijiji vitatu katika miaka minane na wananchi walipoambiwa kwamba ninyi mna mradi wa Benki ya Dunia waliweka matumaini makubwa kwa sababu ya kujua Benki ya Dunia inayo fedha. Ni Benki kubwa, jina kubwa, *repetition* kubwa lakini yanayofanyika na hali halisi kwa kweli mradi huu haufai kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe basi Serikali itutafutie mradi mwingine. Mbona mikoa mingine, wilaya zingine wana miradi zaidi ya miwili, mitatu, kwanini Singida tutegeme mradi mmoja tu wa Benki ya Dunia ambao siyo *effective*? Niombe sana, naomba tutoe mradi mwingine kwa sababu huu wa Benki ya Dunia unaonekana umefeli. Inatia kichefuchefu, vijiji vitatu tena katika vijiji vitatu vyenye hivyo viwili ndiyo vimepata maji, kimoja hakijapata maji mpaka leo, sasa hiyo ni asilimia ngapi ya kati ya vijiji tulivyonavyo. Niombe sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili najua ana uwezo fedha atapewa lakini Singida atuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ufumbuzi wa maji, mimi nadhani kwamba tufuate uzoefu ambao tumeuonyesha, tumejenga barabara nzuri kwa sababu ya mfuko wa barabara. Sasa tunafanya vizuri kwenye umeme kwa sababu REA, tunafanya vizuri katika simu za mkononi kwa sababu UCAF. Huu ni uzoefu wa kutosha kuonyesha kwamba pale ambapo Serikali imedhamiria na ikaweka mfuko maalum tumefanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa *it is high time* tuanzishe mfuko rasmi wa maji. Nimeona katika ukurasa wa 100 kana kwamba kuna kiashiria cha kuanzisha, kwa kutenga seed money Bajeti iliyopita ya shilingi milioni 100. Sasa mwaka huu sijaona popote pale kama zimetengwa kiasi gani. Kama kweli tunataka tutatue tatizo la maji, ambalo ni muhimu.

Mpinzani mmoja aliniuliza sawa mmefanya vizuri kwenye umeme, mmefanya vizuri habari ya simu, lakini sisi tutawapiga bao kwa sababu vijijini hakuna maji. Nikamwambia

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

tunaenda kwa awamu, ikifika 2015 nina hakika kila kijiji kitakuwa kimepata maji. Sasa mnisaidie nisije nikasutwa, nikaonekana nimesema neno ambalo siyo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema kama kweli tunataka tufanikiwe katika maji, tufanye kama tulivyofanya kwenye barabara kuwa na mfuko, tufanye kama kwenye umeme kuwa na REA na tufanye kama tunavyofanya sasa UCAF kwa suala la simu za mkononi kwa kuwa na UCAF. Tuanzishe mfuko wa maji upatiwe fedha kama inavyostahili nina hakika tunaweza tukafanikiwa. Ifikapo 2015, nina hakika tutakuwa tunasema sasa vijana wetu hawana sababu ya kukimbilia kuja mijini kwa sababu umeme uko vijijini, maji yako vijijini pamoja na mawasiliano ya simu yako vijijini na mambo mengine kadhaa wa kadha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la mradi mbadala nasikia kuna kitu kinaitwa *quick win projects*, mbona Singida hakuna hizi kwa maana hiyo *quick win*, kama kweli kuna *quick win* basi ningetazamia kwamba na Singida nayo tupate. Kuna vijiji ambavyo nimemwambia Mheshimiwa Waziri mara nyingi tu kuna kijiji kinaitwa Makuruchanga katika Kata ya Elisia, kuna Kipunda, kuna Masweya, ni vijiji ambavyo kwa muda mrefu vimekuwa vikililia maji, maji hamna, sasa hivyo Mbunge unakwenda pale miaka kumi unasema tutashughulikia miaka kumi utakwenda kusema nini yaani unafika wakati unashindwa hata kwenda kuwasalimia wale wananchi utakwenda kuulizwa habari ya maji na maji hakuna.

Mwisho, ni hii habari ya kuwa mkandarasi anayekwenda kutafuta maji, au kuangalia maji yapo mwingine anayekuja kuchimba hilo ni tatizo. Mimi ningedhani Serikali au Wizara ya Maji ibadilishe utaratibu, mkandarasi anayefanikiwa kwenda kutafuta kwenye utafiti kama maji yapo, huyo huyo awe na uwezo wa kwenda kuchimba.

Kwa sababu uzoefu umeonyesha kwamba hao wanaokwenda kutafuta maji wanasema yapo, huyu anayekuja kuchimba anasema maji hakuna na mnajua kwamba wananchi wanachangia *five percent* katika miradi ya maji fedha inapotea. Kama ni filimbi ya kwanza eeh! Mimi nadhani ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nasema ili kuondoa tatizo hili la wananchi kutokulalamika kwa ajili ya hela zao zinazopotea *five percent* ile ni afadhali tubadilishe utaratibu mkandarasi anayefanya utafiti wa maji ndiyo huyo huyo mkandarasi anakwenda kuchimba hili tatizo halitaonekana. Kwa hiyo, mimi nimalizie hayo sitaki kupigiwa kengele ya pili. (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Tayari ilishapigwa.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Katika jimbo langu la Kibaha Mjini, tumepata maji Vikawe tunashukuru lakini bado tunachangamoto kubwa sana katika mitaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na mikongeni, Kidenge, Karabaka, Kidugalo, Sofu, Viziwaziwa, Sagale na Muheza. Miradi hii kimsingi imeanza lakini inasuasua sana kwa sababu fedha zinapatikana kidogo kidogo. Niombe Serikali iweze kupeleka fedha za kutosha hii miradi iweze kukamilika na wananchi waondokane na tatizo kubwa la maji katika Kibaha Mji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi, bado tunaamini tatizo kubwa la upatikanaji wa maji litakuwepo kama ule mradi wa bomba kubwa kutoka Ruvu hadi Kimara hautakamilika. Nimekuwa nikiufuatilia na kuulizia mara kwa mara lakini majibu ni kwamba mradi umekwishanza, mradi umekwishanza utakamilika mapema, hadi leo hatuna uhakika kamili kwamba mradi huu utakamilika lini. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri atupe majibu hapa

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

kwamba mradi wa bomba kubwa kutoka Ruvu ambalo litaihudumia Kibaha unaoanzia Mlandizi litakamilika lini ili wananchi waweze kufahamu na waweze kujipanga ili kunufaika na maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni wazi kwamba mradi huu unaenda sambamba na ujengaji wa bwawa la Kidunda ili tuweze kuwa na maji ya kutosha, naiomba Serikali vilevile ihakikishe hili linafanyika ili wananchi waweze kupata maji katika kipindi chote na kusiwe na msimu wa kutokupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizi jitihada, sasa hivi bado kuna changamoto kubwa sana wananchi wa Kibaha wamekuwa wakilinda bomba la kupeleka maji Dar es Salaam na hata tunapojaribu kupata maji kutoka katika bomba lenye maji muda wote wananchi wangu wanakatiwa maji na wanaelekezwa kwenye bomba ambalo maji hutoka mara chache katika mwezi. Mfano mzuri katika kipindi cha takriban wiki tatu zilizopita Kibaha wananchi wote walikuwa hawana maji, ni simu mihangaiko hawana maji kabisa lakini wenzetu wa Dar es Salaam maji wanayo na maji yanbapita Kibaha kuelekea Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waziri ajitahidi kuhakikisha kwamba miundombinu hii inayotengenezwa ya maji basi na sisi tunatapa maji katika lile bomba ambalo lina maji muda wote na wananchi wa Kibaha waweze kufaidika na maji hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna kero nyingine katika suala la maji, wananchi wamekuwa wanapata *bill* ambazo hakika hawajazifanyia kazi. Mfano mzuri ni pamoja na Kibaha Vijiji na Kibaha Mjini wananchi wamekuwa na malalamiko makubwa lakini bado ufumbuzi muafaka haujapatikana. Hata kama hawajapata maji bado wanapewa *bill* na kama hawalipi basi hatua mbalimbali zinachukuliwa dhidi yao. Tunaiomba Serikali itambue kwamba huduma ya maji kwa wananchi ni muhimu, lakini vilevile Mamlaka husika inaendesha shughuli ile kwa maana ya kwamba mtu analipia huduma aliyoipata. Kwa hiyo, tunaomba uhakiki uwepo na mwananchi aweze kulipa kile alichotumia na kama hajapata basi asilipe na hakuna sababu ya kulipa huduma ambayo hakika hajaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ili kuweza kuboresha huduma hii na kuondoa malalamiko makubwa mimi ningeliomba tuwe na mamlaka ambayo inaweza ikahudumia Kibaha Mjini na hata Kibaha vijijini, ninafahamu kigezo ni pamoja na kuwa na chanzo cha maji. Lakini mimi naamini mto Ruvu unapita katika majimbo haya mawili. Kwa hiyo, mimi ningeliomba ili tuwe na ufanisi mzuri, basi kuwe na utaratibu wa kutenganisha ili kuwe na mamlaka ya maji ambayo itaweza kuhudumia wananchi wetu na tuweze kuisimamia vizuri na ili iweze kutoa huduma iliyo bora ya maji ili wananchi wasiwe na malalamiko katika huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache, haya niliyotaka kuzungumzia kuhusu utaratibu wa maji. Niipongeze Serikali kwa kazi kubwa, lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Maji anipe majibu muafaka na hususan hili bomba kubwa ni lini mradi huu utakamilika. Bila hivyo kuna hatari wananchi wa Kibaha Mjini wakang'ang'ania shilingi ya mshahara wake punde tunapokamilisha hoja hii ya Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE TABITHA CHAGULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu sana Wizara ya Maji. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa leo nikiwa mzima wa afya ya kutosha. *(Makofi)*



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kutoa masikitiko yangu kuhusu tatizo la maji katika mkoa wa Geita. Mkoa wa Geita wakazi wake ni wakulima na wafugaji. Wadau wakubwa wa kilimo ni kinamama na nguvu ya kazi ya Taifa hili ni kina mama lakini bahati mbaya sana kinamama hawa wamekuwa wakishindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli zao za kilimo kutokana na kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinamama hawa wanaamka saa kumi na moja mpaka saa tatu, saa nne, wakitafuta maji tu, kwa hiyo, inapelekea kutoshiriki vizuri katika shughuli zao za kilimo. Niombe basi Serikali iweze kuliona hili wakinamama hawa wapate maji, ili waweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa lao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, kuna suala la wafugaji, wafugaji hawa pia hawana maji ya kuweza kulisha mifugo, mifugo yao inakuwa hamna malambo, hamna maji kwa maana hiyo wafugaji hawa wanakuwa wakizunguka nchi nzima Wasukuma walikuwa wakizungukazunguka kutafuta maji siyo kwamba wanapenda kuzunguka lakini hawana maji ndiyo maana wanafanya hivyo. Niombe sana Serikali iweze kuliona hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo katika hospitali zetu, katika *dispensary* zetu hamna maji, vituo vya afya hatuna maji, lakini pia katika hospitali za wilaya maji ni tatizo. Huwezi kuamini kuna kinamama wanaenda kujifungua katika vituo vya afya, wanaambiwa waende na maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo sawa, unapomwambia mtu aende na maji, ataenda na maji kiasi gani. Niombe sana Wizara pamoja Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) iweze kuliangalia hili. Katika vituo vya afya, Zahanati na hospitali za wilaya maji iwe ni kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Nyang'hwale kulikuwa na mradi mkubwa sana wa maji ambao uliweza ku-supply maji katika eneo lote lile, lakini mradi huu uliweza kutekelezwa kwa sababu mitambo ya mradi huu ipo mizima kabisa ila tatizo ni ukarabati. Nimwombe Waziri, sisi hatuhitaji mradi mwingine ila aweze basi kukarabati mradi ule wananchi wa Wilaya ya Nyang'hwale waweze kupata maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru naunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. DKT. DAVID M. MALOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii uliyonipatia, awali ya kwanza naomba uniwie radhi niweze kutoa pole nyingi sana kwa wananchi wote wa Jimbo la Dodoma Mjini, kwa kuweza kuondokewa na mpendwa wetu Mama Hadija Jambo, ambaye ni mhasisi wa TANU na mwana jamili Manzi na mtu aliyeshiriki katika kupandisha bendera ya kwanza ya uhuru wa Tanganyika. Nasema pole sana kwa wananchi wote wa Jimbo la Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Maji, Prof. Jumanne Maghembe, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Amos Makalla na Wizara yake yote kwa kazi nzuri ya maji ambayo wameifanya katika jimbo letu la Dodoma Mjini.

Mpaka dakika hii asilimia 87 ya maji inapatikana katika jimbo la Dodoma Mjini na mikakati imeshawekwa na Wizara hiyo kuhakikisha kwamba hadi kufikia mwakani kutakuwa na asilimia 90 ambayo itakuwa imeshapatikana ya maji katika jimbo letu. Nasema ahsante sana na hongereni sana kwa kazi hii nzuri.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inaendelea vizuri mpaka wakati huu wananchi wa jimbo la Dodoma Mjini hasa wale ambao mko katikati ya mji mnaweza kuzunguka kidogo kwenda maeneo ya *Airport* pale kwenye *round about* mtaona mabomba mengi sana ya maji ambayo yamemwagwa pale kuelekea Mzakwe ambako ndiyo chanzo cha maji katika jimbo letu la Dodoma Mjini.

Mabomba hayo yana lengo la kuweza kubadilisha mabomba ya mkoloni ya zamani yaliyokuwa yanavuja na mabomba mapya yawekwe ili maji yaweze kuendelea kupatikana kwa wingi. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa sana za Waziri wetu Prof. Maghembe na Naibu wake Mheshimiwa Amos Makalla na Wizara yake yote, bado ziko sehemu chache kidogo ambazo hata wakati wa wiki la maji nilikuwa nimewaomba na wakanipa ahadi kwamba watafuatilia.

Yako maeneo ya vijiji vya Mapinduzi, Ng'ong'ona, Matumbulu, Ulabi, Mbabala na Bihawana wana matatizo makubwa sana ya maji. Lakini kwa sababu ahadi imewekwa kwamba hadi kufikia mwakani mtakua mmekamilisha, basi ningeomba muwe karibu kujaribu kuangalia maeneo hayo na yenyewe yaweze kupata maji ya kutosha. *(Makofi)*

Jimbo la Dodoma Mjini mtu akisikia habari ya Dodoma Mjini anaweza kufikiri kwamba eneo lote ni mji tu, kitu kinachoitwa Dodoma Mjini, sawa ni Jimbo la Dodoma Mjini, lakini ni Kata chache sana ambazo ziko katikati ya mji. Ni wastani wa kama Kata tano katika Kata 37 zaidi ya 32 ziko vijijini, ambako watu wanajishughulisha na kilimo pamoja na mifugo.

Yapo mabwawa mengi sana ya asili katika jimbo la Dodoma Mjini, kila upande, upande wa Kusini, Mashariki, Magharibi na Kaskazini, ninaomba Wizara yako, Mheshimiwa Prof. Maghembe, Waziri wetu pamoja na Naibu wetu Mheshimiwa Makalla.

Mkajaribu kuyaangalia upya mabwawa haya na kuweza kuona angalau bwawa moja moja kila upande wa mji likaweza kupanuliwa kusudi wakulima na wafugaji waweze kupunguziwa adha ya kupata maji. Upande wa Kusini kuna mabwawa kama ya Mbabala, Ulabi na Mkalama, upande wa Mashariki kuna mabwawa ya vikonje, upande wa Kaskazini kuna Makotopora na Hombolo. Hombolo bado lina maji lakini tangu lichimbwe na mkoloni mwaka 1959 sasa hivi limeshaanza kujaa tope na maji yanazidi kupungua.

Kama lingeweza kupanuliwa kiasi fulani, lingeweza bado likawa la msaada mkubwa sana kwa Wananchi wa sehemu hizo za Hombolo.

Upande wa Magharibi kuna Mabwawa ya Chigongwe na Mbarawala, yanahitaji kutazamwa lipi linaweza likapanuliwa. Najua kwamba, nchi ni kubwa na wana majukumu makubwa, lakini kuweza kuangalia angalau mara moja moja kwamba hata mabawa nayo yakaweza kushughulikiwa kwa sababu tuna wakulima na wafugaji wengi.

Katikati ya Mji kama maeneo ya Nyika za Zuzu, kama zingepanuliwa zingeweza siyo kubadilisha tu hali ya hewa na mji ukachangamka, Wazungu wanasema *ecology*, lakini ingeweza kuwa ni sehemu ya ajira kwa watu ambao wanakaa katikati ya mji kwa ajili ya kuweza kuendesha shughuli za uvuvi wa samaki.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kidogo tu kwa kusema kwamba, siasa ni watu na watu ni siasa. Wakati wa kipindi cha Wiki ya Maji hapa Dodoma, Wananchi wa Dodoma kwa jadi yao wanavyopenda kuishukuru Serikali yao ya CCM, wengi walimwagika na ngoma wakacheza sana. Mimi waliniomba nikawanunulia ngoma kwa wingi pamoja na vitenge Jimbo zima, lakini bado sikuweza kufauru kutoa mipira kwa timu za mpira. *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii kuwatangazia sasa kwamba, vijiji vyote 40, nitagawa mipira miwili miwili kupitia Waheshimiwa Madiwani wetu. Endeleeni kuipongeza Serikali yetu kwa kazi nzuri iliyofanya. Vijiji vichache ambavyo maji hayajafika, sasa maji yatafika, mtapata bila wasiwasi wowote. Endeleeni kuendesha mashindano hayo, mshindi wa kwanza katika Jimbo nitampatia shilingi 1,000,000, pair mbili za jezi, pamoja na mipira mitano. Mshindi wa pili, nitampatia shilingi 500,000, pair mbili za jezi na mipira mitano.

Mshindi wa tatu nitampatia jezi mbili za mpira pamoja na mipira mitano na shilingi 250,000. Hii ni katika kuishukuru Serikali yetu ya CCM kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya na wanataka kuendelea kushukuru kila kitu, zikiwemo barabara, umeme na kila kitu ambacho kinafanyika katika Jimbo hili. Nawashukuruni sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuruni sana. Wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini ninawapenda sana kama mnavyonipenda mimi. Niko pamoja nanyi, ahsanteni na ninaunga mkono bajeti hii ya maji ipite ili Wananchi wote wa Dodoma Mjini na Vijiji vyote viweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Agripina Buyogera, ajjandae Mheshimiwa Riziki Lulida!

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwa niaba ya Wananchi wa Kasulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, kwanza, naomba nitoe pole sana, kwa kijana wangu Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa kufiwa na mama yake.

Pili, naomba niwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutimiza majukumu yangu. Ni juzi tu nilikuwa kwenye ziara huko, wamenipa ushirikiano wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamheshimu sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, lakini leo kwa mara ya kwanza naomba nitangaze mapema kabisa kwamba, siungi mkono bajeti hii. Kwa utangulizi wa masikitiko makubwa sana, ninaomba Serikali iangalie upya Miradi yote iliyopitishwa ya Maji katika Jimbo la Kasulu Vijijini hakuna Mradi hata mmoja ambao umekamilika.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Ni jambo la kusikitisha sana, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa na ziara Mkoa wa Kigoma, mimi nilizunguka naye kila Wilaya na nikaishukuru Serikali kwa kutupa Miradi miwili mikubwa ya Kasangezi na Nyarugusu ya *Wold Bank*, ambayo tulitegemea ikamilike mwezi Desemba, 2013.

Lakini mpaka leo hii hakuna kitu ambacho kimeshafanyika. Tarehe 17 na tarehe 18 mwezi huu, nilikuwa na ziara na Wataalam, kwenda kuhakiki maendeleo ya miradi hiyo. Mradi wa Kasangezi nimekuta Mkandarasi ndiyo anafyeka barabara kwa panga. Hakuna kitu chochote ambacho kimefanyika zaidi ya kufyeka nyasi. Ni jambo la kusikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, Mradi wa Maji Kijiji cha Ahsante Nyerere, ambao kisima kilishakamilika, maji yametoka, tatizo kusambaza mabomba kuweza kuwafikisha maji Wananchi, ambao *Engineer* aliniahidi kwamba, Mradi ule utapeleka maji mpaka Kijiji cha Sogeeni. Mpaka leo bila sababu yoyote ya uhakika maji hayajafika kwenye vijiji hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nina masikitiko makubwa. Ukienda Shunguliba hali kadhalika, kisima kimechimbwa pale lakini maji Wananchi hawapati. Mbaya zaidi, Kijiji cha Titye, Sekondari, wameahidiwa maji tangu shule imeanza mpaka leo. Juzi nimeenda kutembelea kule na wataalam, watoto wamenishika gauni wanasema Mheshimiwa Mbunge tumeahidiwa tutaletewa maji.

Mwenyekiti wa Halmashauri alienda kwenye sherehe zao za kumaliza shule, akaahidi kwamba, mpaka mwezi Januari mwaka huu maji yatakuwa yametoka pale shuleni. Walimu wamekwenda pale ni wageni, wanasubiri wachotewe maji na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali hii ilianganalie kwa kina. Ninayaongea haya kwa msikitiko, zipo taarifa ambazo siyo sahihi, nimeambiwa na Wananchi, sina uhakika nazo, inawezekana ni sahihi au siyo sahihi. Nimeambiwa kwenye mikutano kule na Wananchi kwamba, kuna hila za makusudi za kuhakikisha Miradi inayopelekwa kwenye Majimbo ya Wapinzani hamuikamilishi eti ili mwaka kesho wasirudi. Ninashukuru kama haitakuwa kweli, lakini nina vielelezo, zipo taarifa ninazipata halafu ninapata mashaka. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ni wa kutoka CCM na ni Diwani kutoka kwenye Jimbo langu, ndiye anayesaini mikataba yote ya wakandarasi hawa. Kama anatoka kwenye Jimbo langu, ni kwa nini Miradi inayopelekwa kwenye Majimbo mengine akiwa ndiyo Mwenyekiti, ikamilike halafu Miradi ya kwenye Jimbo lake isikamilike?

Bado Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kasulu ni Diwani kwenye Jimbo langu, anashindwaje kutetea na kuchochea shughuli za maendeleo zinazofanywa kwenye Jimbo la Kasulu Vijijini akiwa Mwenyekiti wa Chama Tawala chenye Serikali?

Ndugu zangu, yapo mazingira ambayo yanaleta ukakasi, mtu anaposema, mimi huwa sina unafiki wa kumchukia mtu bila sababu, lakini naongea haya kwa masikitiko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, mtakapofanya majumuisho, mtuambie Wananchi wa Kasulu Vijijini ni lini Miradi hii itakamilika. Haiwezekani leo unampa Mkandarasi unasema hana uwezo. Anakaa unabadilisha unaweka Mkandarasi mwingine na yeye akifika miezi mitano anasema mlimpa Mkandarasi ambaye hana uwezo. Hivi ni vitu gani?

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Ofisi ya Ugavi imekuwa ni dalali? Afisa Ugavi juzi namwita kwenye majumuisho, tueleze hii Miradi kuna tatizo gani? Afisa Ugavi ananiambia wala hata mkataba siwezi kukuonesha na wala sijui ukawaulize Serikali huko. Hivi kweli Afisa Ugavi ni cheo unaweza ukamjibu Mbunge namna hiyo na wakati mimi ni mwakilishi wa Wananchi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tunayaongea hapa Bungeni, lazima Bunge lisimame kuhakikisha linaisimamia Serikali kutenda haki bila kujali itikadi za vyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ujumbe umefika. Ahsante sana, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki Lulida, ajiandae Mheshimiwa Ngwilizi!

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napebda kutoa shukrani za dhati kwa Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kunipa afya njema nami niweze kuchangia hoja hii iliyoko mezani.

Nipende kutoa shukrani na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Maji, kwa kazi kubwa wanayofanya kuzunguka Tanzania nzima kuhakikisha maji yanapatikana. Napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kutoka Nachingwea, leo hii Waziri Chikawe yuko Nachingwea, maji yamefika kutoka vyanzo vya maji vya Mto Mbwinji. Leo Nachingwea wanasherehekea maji. Tunategemea Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais, kwenda kuzindua Mradi wa Maji wa Nachingwea; kwa kweli ilikuwa ni kero ya muda mrefu na sasa hivi wanasema ahsante Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ruangwa wana matatizo ya maji kiasi fulani, kwa vile maji ya Nachingwea yamekuwa ya kutosha, tungeomba mambomba yafanyiwe tathmini ili kupeleka mabomba Ruangwa tutatue tatizo la maji.

Nina imani kwa hili, liko ndani ya uwezo wa Waziri na atalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja Lindi Mjini, amefanya kazi kubwa sana ya kusimamia maji Lindi, lakini kuna maeneo madogo madogo kama Muhimbili bado kidogo kuna matatizo ya maji. Kero kubwa iko Lindi Vijijini, kuna matatizo ya maji. Kwa mfano, katika Jimbo la Mchinga, walipata Mradi wa *World Bank*, visima vyote havifanyi kazi na maji hakuna na palipopatikana maji ni mabaya machungu. Namwomba Mwenyezi Mungu, ampe nafasi alisaidie Jimbo la Mchinga, hasa vijiji vya Mihambwe, Kilolambwani na Mvuleni, kote huko kuna matatizo makubwa sana ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la maji. Maji ni uhai, bila maji hakuna uhai. Palifanyika fujo kubwa sana ya ukataji wa magogo katika nchi hii na hayo magogo yalipelekwa katika nchi za Asia hasa China, nazungumza tena. Sing'ating'ati meno na wala sipepesi macho, nitasema ukweli kuwa magogo yamefanya hii nchi kuwa jangwa. Yamekatwa magogo kupelekwa China, ukiingia katika *Google Earth*, Tanzania iko katika jangwa. Unaona Kongo iko katika *green*, lakini Tanzania tuko katika jangwa kubwa sana. Kama mikakati ya makusudi haifanyiki, basi tegemea hii kero ya maji itakuwa kubwa Tanzania nzima. Mfano, katika miaka ya nyuma, Mto Mbwemkuru ulikuwa mkubwa sana sasa hivi umekauka. Mto Rufiji ulikuwa miongoni mwa mito mitatu mikubwa Tanzania, hivi sasa umekauka. Mto Matandu umekauka. Mto Lukuledi unakauka. Je, watu hawa watategemea vyanzo maji kupatikana wapi kama watu wataendelea kukata magogo? Ni matumaini yangu, Waziri ni mtaalam wa mambo ya misitu, hilo analiona. Magogo sasa hivi yanasafirishwa katika njia za panya na hivyo kuifanya nchi kuwa jangwa ambalo halisemekani. *(Makofi)*

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Tukiachia mbali ufugaji wa kutembea hovy hovy huku na huku na kuharibu vyanzo vya maji, tusimamie suala la kupeleka magogo nje, ni hatari katika nchi yetu. Nilipata nafasi ya kuembelea China, nilikwenda Shanghai na Guangzhou, wale wanatunza misitu. Kwa nini magogo yao hawakati huko kwao wanategemea magogo kutoka Afrika? Hii ni fujo! Ninakuomba Waziri na wewe vilevile kama nilivyomwambia Waziri wa Nishati na Madini, amwite Balizi, amwambie suala la kero ya kukata magogo kupeleka China imekuwa ni vurugu. Wanatuletea shilingi mbili, sisi wanatumia rasilimali ya 200. Hii ni hasara kubwa katika nchi yetu. Leo hii magogo wamekata, tembo wanapita wapi?

Leo hii wanyama wanategemea misitu, misitu imekatwa na magogo yamekatwa. Tutamaliza hata utalii wetu nchi hii kutakuwa tena hakuna utalii. Wanyama watapita wapi, hawana maji na mito itakauka? Watu watakuwa wanahangaika, wafugaji wanahangaika, tutakuwa katika kero kubwa. Mheshimiwa Waziri, fanya kazi ya ziada, hali hii ya vyanzo vya maji kukatika itakuwa ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la maji Dar es Salaam; umefanya kazi kubwa sana Jimbo la Ubungo. Wezi wa kuiba maji umewadhibiti na sasa hivi Ubungo maji yatapatikana. Nimeona juhudi zako kubwa ulizozifanya. Mabomba ninayaona Kelege yote, Bunju yote, mabomba makubwa ambayo Jiji la Dar es Salaam litakuwa linapata maji. Kazi unayoifanya ni kubwa, lazima upongezwe, lakini usisahau Mihambwe kutupelekea vijiji vyangu vitano. Nilikuletea barua kukuomba Mihambwe, Mvuleni, wana kero Wananchi, wanakaa katika sehemu ambazo zina wanyama wanyama, usiku kucha wanatafuta maji. Ninamwomba Mwenyezi Mungu, akujalie upeleke maji Mihambwe, Mvuleni, Kilolambwani, kote tunataka maji mpaka Kitomungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngwilizi, ajiandae Mheshimiwa Herbert James Mntangi.

**MHE. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja asilimia 100. Sababu yangu ya kuunga hoja hiyo ni kwamba, ninatambua uchapakazi wa Mawaziri waliopo katika Wizara hii, ila tatizo ni fedha, hawawezeshwi. Sasa kama hawakuwezesha watafanya kitu gani? Tunaweza tukakaa hapa tukawakaanga, tukafanya kila kitu, lakini kama fedha hazitoki, hawana ambacho wanaweza kufanya.

Ninataka kutumia mfano tu katika Hotuba ya Waziri, ile Ibara ya 235, ambayo ukiangalia fedha zilizotengwa mwaka jana na tulifanya kazi kubwa sana kuzitenga fedha hizo, zilikuwa shilingi bilioni 312, lakini zimetoka shilingi bilioni 88, asilimia 74 haikutoka. Hivi tunategemea Wizara hii ifanye kitu gani?

Ndiyo maana sasa hivi najiuliza Waziri anaomba hapa tumpitishie bajeti ya shilingi bilioni 520; bilioni 30 kwa ajili ya matumizi ya kawaida (OC) na shilingi bilioni 490 kwa ajili ya maendeleo. Hizi za mwaka jana zimeshindikana, mwaka unaokuja zitawezekana? Kwa hiyo, hiyo kidogo inanipa matatizo, lakini suala hilo naamini Kamati yetu ya Bajeti inaliangalia na ninaamini kwamba, tukiingia kwenye Wizara ya Fedha, tutajua mbivu na mbichi ni zipi.

Sasa nije kwenye Jimbo la Mlalo, ndugu zangu Jimbo la Mlalo liko kwenye Milima ya Usambara, kule hatuzungumzii visima, tuna maji yanatiririka, kinachohitajika ni kutegwa.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Wananchi wameitikia wito wamechangia, Serikali imekubali kuingiza Bonde la Mto Mlalo kuwa mojawapo ya Vijiji Kumi. Vile siyo Vijiji Kumi, Bonde la Mlalo lina Kata sita na Mradi ule unatakiwa usambaze maji katika Bonde lile. Vilevile kuna Kata nyingine za Shume, Manoro, ambazo nazo ziko kwenye Mradi.

Wilaya ya Lushoto, fedha zilizopelekwa mpaka sasa hivi ni shilingi milioni 300, wakati fedha ambazo zingeweza kuwapatia hawa Wananchi maji zilitakiwa shilingi bilioni 4.9. Sasa milioni 300 kutoka shilingi bilioni nne ni chini ya asilimia kumi. Ndugu zangu suala la maji ni uhai. Pamoja na kwamba, umeme umefika Mlalo, bado tuko Tarafa ya Mtae, pamoja na kwamba, barabara zinapitika, lakini maji ni kero kubwa sana kwa Wananchi.

Serikali ilipoweka Mradi ule Wananchi waliona kwamba, ukombozi umefika. Sasa ukombozi ule unaonekana bado uko katika machaka. Hili ningependa kwa kweli, Mheshimiwa Waziri, najua Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia kwamba, zimepatikana bilioni kadhaa kabla ya wiki hii, lakini ningeomba zile bioni 4.9 zipelekwe kwenye Wilaya ya Lushoto ili tukamilishe ile kazi. Mabomba yapo, kilichobaki ni kukamilisha ujenzi wa matenki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo, nipende kuishukuru Serikali kwamba, maji katika Vijiji vya Kikumbi, Mkundi ya Mbaru na Mkundi ya Mtahe, sasa hakuna matatizo kule. Kitu ninachowaombeni, kamilisheni Mradi ule wa Bonde la Mlalo ili waweze kwenda Shume halafu wateremke maeneo ya Kivingo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, kama nilivyosema, sina ugomvi na Wizara hii, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Herbert Mntangi, ajiandae Mheshimiwa Zedi na Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Sekta hii ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, aliyekuwepo na aliyepo sasa, lakini pia na Watendaji, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, ambao wamefanya kazi kubwa kusaidia Mpango Maalum wa Dharura wa Maji katika Wilaya ya Muheza. Zaidi ya shilingi 350 milioni wamezileta na nataka nimthibitishie Mheshimiwa Waziri kwamba, tumezifanyia kazi vizuri. Tumefufua na kuweka Mradi mzuri sana wa maji ya pampu ya solar katika kisima cha Polisi pale Genge. Vilevile tumechimba zaidi ya visima vingine kumi; kati ya hivyo vitatu tumeshaanza kuvifanyia kazi na tutaendelea kuboresha upatikanaji wa maji kupitia tanki lililoko eneo la *National Housing*, ambalo pia litasaidia kupunguza matatizo ya maji katika maeneo ya Majengo, Muheza Mjini Kati na eneo la Michungwani. Nawashukuru na ninasema tutaendelea kuzitumia vizuri fedha hizo na kuboresha visima vile vingine saba vilivyobaki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nasema tena kwamba, bado kuna matatizo ya maji. Nishukuru pia kwamba, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Machi, 2014, alikuwepo Muheza na alishiriki katika kuzindua Mradi mmoja wa Maji, ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maji Vijijini, *World Bank* na huu Mradi ni wa Maji Mtiririko katika eneo la Ubembe Komhosi.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mwezi Machi, 2014, Mheshimiwa Rais alirudia tena kwa kauli yake ya mpango wake wa ahadi yake ya kuhakikisha kwamba, Mji wa Muheza unapata maji kutoka katika chanzo cha Mto Zigi. Ni miezi miwili tu imepita na siku hiyo ya mkutano, Mheshimiwa Naibu Waziri, ndugu yangu, rafiki yangu, Mheshimiwa Mrindoko, alikuwepo katika mkutano wa hadhara. Matarajio yangu ni kwamba, Mradi huu na ahadi hii ya Mheshimiwa Rais, itapewa heshima inayostahili na itatekelezwa. Mheshimiwa Rais alisema, itatekelezwa mwaka huu wa 2014/2015 na akaahidi kwamba, utendaji huo utakuwa umekamilika kabla hajaondoka madarakani. Kikatiba ni mwaka 2015 utakuwa umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu jitihada ambazo Mheshimiwa Waziri anazifanya. Naelewa kwamba, wako wataalam na nchi ya Uturuki ambayo imejitolea kujaribu kusaidia Mradi huo. Waturuki walifika hapa, lakini kwa bahati mbaya walichelewa, isipokuwa nina uhakika wiki iliyopita wamefika na majadiliano yalikuwa yanaendelea. Wananchi wa Muheza wanataka kujua; je, wataalam hawa wameridhia kusaidia kutoa fedha ya utekelezaji wa Mpango huo ili ahadi ya Mheshimiwa Rais ipate heshima inayostahili? Natarajia tutapata majibu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine kubwa, Mheshimiwa Waziri katika Mpango wake wa sasa hivi, ameeleza Mpango wa maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Pili. Mpango huu unalenga kuhakikisha maji yanafika katika maeneo ya Miji Mikubwa, pamoja na Miji Midogo katika Mikoa na katika Halmashauri. Swali langu; nimeambiwa na ninafahamu kwamba, Kitabu cha Programu hiyo kipo tayari. Sisi Waheshimiwa Wabunge, hatujapewa nakala ya kitabu hicho, kwa hiyo, hatujui ni Wilaya zipi na Miji ipi imeingizwa katika Programu hiyo ya Pili. Je, tunaweza tukapata vitabu hivyo? Swali langu kubwa, je na Muheza ipo ndani ya Awamu hiyo ya Pili katika Kitabu hicho, katika Programu hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafurahi Waheshimiwa Wabunge tukipata uhakika na mimi niweze kupata uhakika kwamba, Wilaya ya Muheza na Mji wa Muheza utakuwepo ndani ya Programu hiyo. Nimalizie kwa kusema, Mheshimiwa Waziri, alikuja Muheza, alialikwa na Mamlaka ya Maji ya Mkoa wa Tanga. Alifika Muheza kwa sababu kulikuwa na chama kimeandaliwa na wenzetu wa Tanga, ili kulinda chanzo cha maji kinachopeleka maji katika Jiji la Tanga. Chanzo cha maji hiki kipo Muheza. Muheza hawana maji, chanzo cha maji kimepeleka maji Tanga. Hatuna matatizo kwa sababu Tanga nimajirani zetu, lakini utaalam umethibitisha kwamba, hata Muheza wakichukua maji kutoka kwenye chanzo hicho, maana vipo vyanzo vingi, hata tukienda palepale Zigi, Tanga haitaathirika hata kidogo kwa Mradi wake ule wa Maji.

Sasa waliopeleka maji Tanga, walikuwa wakati huo ni GTZ, leo wanaitwa GIZ. Mimi binafsi nimewafuata na waliniambia na kunishauri kwamba, niombe Wizara yako ya Maji iwaandikie na nilifanya hivyo na nilifika Ofisini kwako, pamoja nakwamba sikukukuta wewe Mheshimiwa Waziri, lakini nilifika na kukutana na pia na Naibu Katibu Mkuu. Nina imani, GTZ, GIZ, ambao pia waliambiwa wakaangalie hali ya maji ilivyo katika Wilaya ya Muheza na walifika; wamethibitisha kwamba, kweli hali ya maji Muheza ni mbaya. Ninaomba pia, pamoja na tijihada za Wizara, kuendelea kufanya majadiliano na Uturuki, mwendelee vilevile kuwasiliana na GIZ, ambao walinihakikishia, wanaweza wakasaidia, kama wataombwa rasmi na Wizara ya Maji.

Sasa ninaomba GIZ pia mwendelee nao, kwa sababu hali ya maji katika Wilaya ya Muheza ni mbaya sana. Ninaomba vilevile mwendelee na niwakumbushe ahadi ya Mheshimiwa Rais, mwezi Machi, 2014, ameirudia tena, katika mkutano wa hadhara, mbele ya



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Wananchi wale wa Muheza. Leo ukitazama huku kwenye programu ya utekelezaji wa bajeti 2014/2015, sioni programu maalumu iliyopo pale ya utekelezaji huo. Maana yake nini? Maana yake tunawategema wahisani, lakini kweli tuweke nguvu zote zote kwa kuwategemea tu wahisani na kusahau ahadi ya Mheshimiwa Rais!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zedi, ajiandae Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa Moza Abeid Saidy!

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili na mimi kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Bukene, niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu sana, Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuchukua fursa hii, niipongeze Serikali na Wizara ya Maji, kwa kutekeleza Miradi Kumi, ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia ndani ya Wilaya ya Nzega. Katika Miradi hii, Miradi tisa katika vijiji tisa, iko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Katika hii Miradi tisa hii, Miradi sita iko ndani ya Jimbo langu la Bukene. Mradi wa Nawa, uko katika hatua za mwisho kukamilika. Mradi wa Mahene, mkandarasi wa kwanza alijenga akafikia hatua fulani, kazi ikamshinda, lakini Halmashauri ya wilaya ya Nzega, nafahamu iko katika hatua za kutafuta mkandarasi mwingine amalizie kazi hii. Matumaini yangu ni kuwa kazi hii itamalizika ili Wananchi wa Mahene wapate maji. Mradi wa Ikindwa uko katika hatua nzuri, naweza kusema karibu asilimia 80 ili ukamilike. *(Makofi)*

Mradi wa Itobo, juzi nilikuwa na Katibu Mkuu wangu wa CCM, tuliukagua pale unakwenda vizuri na ni matumaini yangu kwamba, muda siyo mrefu utakamilika kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mradi wa Sigili, pale maji hayakupatikana mengi, lakini uamuzi ulifanyika ikafungwa pampu ya mkono na watu wameanza kutumia. Kwa hiyo, Miradi sita hii, niipongeze Serikali kwamba, imetekelezwa na iko katika hatua za mwisho kabisa, ili Wananchi wangu waanze kutumia maji. Miradi hii itakapokamilika, zaidi ya Wananchi 17,000 ndani ya Jimbo la Bukene ambao walikuwa hawana maji, sasa watakuwa na uhakika wa maji safi na salama. Kwa hiyo, kwa hatua hiyo naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la maji kutoka Ziwa Victoria, sitaki kuliongelea sana kwa sababu nafahamu hatua za utekelezaji. Nilifanya mawasiliano ya karibu na Naibu Waziri, Mheshimiwa Makalla. Nafahamu kwamba Serikali ime-engage kampuni ambayo inafanya uchambuzi wa kina na ndani ya miezi 12 kazi hiyo itakuwa imekamilika na vijiji ambavyo vitafaidika vitajulikana. Nilimwomba Mheshimiwa Naibu Waziri, mwezi wa saba huu akipata nafasi tufanye ziara kule ili Wananchi wakaelezwe mpango mzima ulivyo, wawe na matumaini.

Nisisitize hii Sera ya kwamba, mahala ambako bomba kuu la Ziwa Victoria litapita, basi vijiji vilivyo ndani ambavyo havizidi umbali wa kilomita 12, vitanufaika vitapata maji. Sera hii ni nzuri sana, naiunga mkono asilimia 100, kwa sababu hili likitendeka, nina uhakika ndani ya Jimbo la Bukene, zaidi ya vijiji 30 vitapata maji mara tu Mradi huu mkubwa wa Ziwa Victoria utakapokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa nilikuwa nina ombi maalum kwa Serikali na Wizara ya Maji; kwa sababu Sera ya Vijiji vilivyo umbali usiozidi kilomita 12 kutoka bomba kuu, vipate maji, maana yake ni kwamba, bomba kuu la maji kutoka Ziwa Victoria, likipita pale Itobo, kuna Kijiji cha Kabanga, ambacho kiko ndani ya kilomita 12, kitastahili kupata maji hayo. Kutoka

## ***Nakala ya Mtandao (Online Document)***

Kabanga mpaka Bukene, ambako Makao Makuu ya Jimbo na ambako ni mji ambao tunauandaa sasa kuwa Makao Makuu ya Wilaya na Halmashauri mpya ya Bukene, ni umbali wa kilomita nane tu. Kwa hiyo, naiomba Wizara na Serikali ifikirie, ombi maalum, pamoja na kwamba, Sera inasema vijiji visivyozidi kilomita 12, lakini kutoka Kabanga mpaka Bukene ni kilomita nane tu.

Kwa hiyo, kuwe na *consideration* maalum ili bomba litakapofika Kabanga, liongezwe kilomita nane lifike Bukene mjini, mji ambao unaoua sana, una idadi ya watu wengi ili Wananchi hao waweze kunufaika na maji ya uhakika kutoka Ziwa Victoria. Hivi sasa wote tunafahamu kwamba, tunauandaa Mji wa Bukene kuwa Makao Makuu ya Wilaya mpya na Halmashauri ya Bukene. Bado kwa ujumla wake maji bado ni tatizo. Nafahamu kutokana Sera ya Maji, maeneo ya vijijini, watu hawatakiwi kupata maji zaidi ya umbali wa kilomita 400, lakini bado kwenye Kata zangu nyingi sana ndani ya Jimbo la Bukene, maji bado ni shida sana. Kata ya Semembela maji bado ni shida, Kata ya Mambali maji bado ni shida, Mogwa maji ni shida, Isagenhe maji bado ni shida, Karitu, Mwangohe, Kamahalanga, bado kote huko maji ni shida sana. *(Makofi)*

Nilikuwa nafahamu kwamba, kuna shida kubwa sana ya bajeti ndani ya Wizara hii ya Maji, kwa hiyo, rai yangu kwa Serikali ni kwamba, kama ambavyo tumekuwa tukitia mkazo kwenye mambo muhimu kama ya umeme vijiji, naiomba Serikali na suala la maji pia tulipe umuhimu huo huo na uzito huo huo, kwa sababu maji ni uhai. Maji ni jambo ambalo kwa kweli linapokuwa halipatikani, basi Wananchi wetu wanapoteza muda mrefu sana ambao wangeutumia kufanya kazi, kwenda kutafuta maji.

Sisi pale kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Mhandisi wa Maji, Dada Mariam alijitahidi sana kuja na mpango mzuri sana wa kuboresha maji ndani ya Wilaya ya Nzega. Tulitenga bajeti kwa kushirikiana na Madiwani, karibu bilioni mbili, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, bajeti hiyo imepunguzwa mpaka karibu milioni 400. Sasa unaweza kuangalia kutoka kwenye bilioni mbili, kushuka mpaka kwenye milioni 400, maana yake ni kwamba, Miradi mingi ya Maji haitatekelezwa kwa kiwango ambacho tulikuwa tunatarajia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niungane na Mheshimiwa Ngwilizi, ambaye amesisitiza kwamba, ili Wizara ya Maji iweze kutekeleza majukumu yake na kuwapatia maji Wananchi, ni lazima ipate fedha za kutosha. Hatuwezi tukategemea Wizara au Halmashauri zetu ziwapatie Wananchi huduma za maji wakati zinapewa bajeti ndogo sana. Kwa hiyo, ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnyika, ajiandae Mheshimiwa Moza na Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya tote, nitumie fursa hii kutoa pole kwa Wana-CHADEMA nchi nzima, kwa kifo cha Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama, Mama Shida Salum. Chama kimepoteza Mjumbe wa Kamati Kuu. Zaidi nitoe pole kwa familia, kwa kupoteza mzazi, kwa kupoteza mama.

Salamu hizi za pole zifike kwa Mheshimiwa Zitto Kabwe, nilishamtumia salamu, lakini nitume salamu vilevile kwa njia hii na zaidi zifike kwa Chama cha Walemavu (CHAWATA), ambacho Mama Shida Salum alikuwa Mwenyekiti wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii vilevile, kwa sababu Wizara hii ya Maji inasimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (*EWURA*), kumwomba Waziri wa Maji, katika majumuisho ya majibu ya Wizara hii, atoe kauli ya Serikali, juu ya taarifa ambazo zilifika kwenye

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Vyombo vya Habari, ambavyo viliandika Meneja wa EWURA ajiua hotelini baada ya kuhojiwa na Bunge. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema marehemu, lakini tungeomba kauli ya Serikali, ni nini hasa chanzo cha kifo cha Meneja huyo wa EWURA? Kwa sababu Wizara hii ndiyo yenye dhamana ya kuisimamia Taasisi ya EWURA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, nijielekeze kwenye mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015. Mimi ninashangazwa na jambo moja; Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnasema bajeti ya Wizara hii ni ndogo, mnasema bajeti ya Wizara hii fedha hazitoki, lakini kinachonishangaza ni hatua ya mwisho mnaunga mkono bajeti hii ipite kwa asilimia mia kwa mia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona jambo hili ni mkanganyiko wa hali ya juu. Kwa kufanya hivi, tusidhani kwamba tunamsaidia Mheshimiwa Waziri Maghembe, ambaye Chama chake cha CCM, kimemwita kwamba ni Waziri mzigo, kwa sababu ya matatizo katika Wizara hii. Tusidhani kwamba, tunamsaidia Mheshimiwa Waziri, kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia 100, huku tunajua kwamba, fedha zilizotengwa mwaka jana, kwa kelele nyingi, kwa nguvu kubwa ya Wabunge, fedha hizi hazijatolewa. Huku tukijua wazi kwamba, fedha tunazotaka kuzitenga mwaka huu ni wazi kwamba, hazitatoka kwa kiwango cha kuwezesha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini, namna bora zaidi ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri, ili Viongozi wa CCM, Katibu Mkuu Kinana na Viongozi wengine wa CCM, wasiendelee kupita nje ya Bunge wakimwita Mheshimiwa Maghembe kwamba ni Waziri mzigo, ni kuikataa bajeti hii. Tukiikataa bajeti hii tafsiri yake ni nini? Serikali italazimika kurudi mezani kujuliza ni kwa nini Wabunge wameikataa bajeti hii!

Mjadala wa bajeti hii ukisogezwa mbele, kauli ya Waziri Mkuu, ambayo aliitoa Jumamosi, Waziri Mkuu alisema hapa, Kamati ilisema tarehe 31, ambayo imekwishapita, Serikali iwe imekwishatoa bilioni 80 kwa ajili ya Wizara hii. Waziri Mkuu akasimama akasema, msiwe na wasiwasi, wiki ijayo, fedha hizi zitatoka. Leo ndiyo tunahitimisha mjadala, maana yake ni nini? Bajeti hii ikipita, tutauziwa mbuzi kwenye gunia. Kwa mara nyingine tena, fedha hazitatoka, matatizo ya maji kwa Wananchi yataendelea. Tukiambia Serikali kama ambavyo iliitokea kwa bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, kwamba, mjadala huu usiendelee kwa muda kwanza, Serikali mtekeleze *commitment* yenu ya kutoa fedha, halafu tutaendelea na mjadala, ili tuone kweli tumedhamiria kwa dhati kuondoa matatizo ya maji. Jambo hili nategemea Wabunge wenzangu wataliunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayazungumza haya kwa sababu vilevile ya shida kubwa ya maji Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alitoa kauli, siku chache zilizopita, juu ya matatizo ya maji kwenye maeneo yanayohudumiwa na Mtambo wa Ruvu Juu. Pamoja na kauli ya Mheshimiwa Waziri, kuahidi kwamba, tatizo limemalizika, Wananchi wa Dar es Salaam, kuanzia Kibamba, Kwembe, Kimara, Msigani, Saranga na maeneo mengine, wana matatizo makubwa sasa hivi tunavyozungumza, tofauti na ahadi na kauli ya Waziri aliyoitoa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda ni mdogo sana, nakusudia kuleta hoja juu ya kauli ambayo si ya kweli iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni ili jambo hili lijadiliwe hatua za maana ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile Mheshimiwa Waziri arejee kwenye Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuanzia ukurasa wa 39 mpaka ukurasa wa 47, ambapo imeeleza

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

mambo ya msingi ambayo namuunga mkono Mheshimiwa Sakaya, juu ya hatua ambazo zikichukuliwa zitaweza kuhakikisha ufumbuzi unapatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, naelewa huu mzigo umekuzidi uzito, ndiyo maana wenzako wanakuita Waziri mzigo. Katika majumuisho ya Bajeti ya Wizara hii, iwapo hakutatoka kauli ya maana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, juu ya matatizo ya ufumbuzi wa maji; masuala haya ya maji yana ahadi za Mheshimiwa Rais. Nina vitabu viwili hapa, Kitabu cha Tumaini lililorejea na Kitabu cha Ahadi za Wakati wa Kampeni, Ahadi za Siku 90 za Kwanza, ahadi za kila mahali. Ufumbuzi usipopatikana kwenye mjadala wa Wizara hii, tutawajibika sasa kuzielekeza nguvu kwenye kumbana Mheshimiwa Rais, maana mwisho wa siku kama mnamwita Mheshimiwa Maghembe ni mzigo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, utam-address Waziri kwa cheo chake na jina lake tafadhali.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninachokisema, kama Serikali hii ya CCM itaendelea kuacha uwajibikaji wa pamoja na kumbebesha mzigo Waziri wa Maji, katika Mpango wa Maji Dar es Salaam uliopitishwa na Baraza la Mawaziri, sisi na mimi na wenzangu, tutazielekeza nguvu katika kumbana Mheshimiwa Rais, kwa kutoa ahadi zisizokuwa za kweli. Aliahidi kwamba, tungekutana Ikulu kujadili kuhusu matatizo ya maji Dar es Salaam, mpaka sasa ahadi ile haijatekelezwa na kuna matatizo ambayo kama Mheshimiwa Rais, Msimamizi wa Mawaziri, akiingilia kati kuondoa udhaifu uliopo, ni wazi kuna hatua ambazo zitaweza kuchukuliwa kwa haraka. Ninachotaka kusisitiza ni nini hapa?

Jambo hili la matatizo ya maji Dar es Salaam, Pwani, Bagamoyo na maeneo mengine yanayohudumiwa na DAWASA; jambo hili la matatizo ya programu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja zako muhimu, lakini muda umekwisha. Sasa Mheshimiwa Moza, ajiandae Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. MOZA ABEID SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia suala lililopo mbele yetu kuhusu maji.

Mimi ninukuu tu katika ukurasa wa mpango wa maji uliozungumzia mpango maalum kutekeleza sasa kwa matokeo makubwa. Lengo la mpango huu ni kufikia asilimia 74 hapo Mwezi Juni, 2016. Mpango huu unaangalia maeneo makuu manne ya utekelezaji. Ujenzi wa Miradi mipya, ukarabati wa Miradi chakavu, uendeshaji na matengenezo. Lengo la Serikali kuwapatia huduma ya maji Wananchi milioni ishirini na mbili waishio vijijini ifikapo mwezi Juni, 2014, ambayo ndiyo leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeeleza kuwa vijiji ambavyo sasa vina maji, ambavyo vitapata maji leo Juni hii, mwezi huu wa sita ni Igunga, Itolwa, Mapango, Chandama, Jenjeluse, Goima, Mtakuja, Mlongia na maeneo mengine, Hakuna dalili zozote za kuhusiana na suala la maji katika Wilaya ya Chemba. Waishio kule ni wanadamu kama tulivyo sisi, huduma zote zinastahili, kupata maji salama na yaliyokuwa safi. Kitu kinachonishangaza, wanawake wananyanyasika sana kuhusiana na suala la maji; wanakwenda kuchota maji kwenye visima virefu ambavyo si sala na wengine walishawahi kutumbukia miaka iliyopita na kufia kwenye visima hivyo.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Waziri hana dhamira iliyokuwa njema kabisa kwa upande wa wanawake, kwa kuwa wanawake ni muhimu zaidi kuwandanganya nyakati hizi za kipindi kinachokuja cha Bunge, sasa mtaanza kuwadanganya kwamba tayari utekelezaji unaanza. Unaanza utekelezaji ambapo mwezi huu mnasema watapata maji wakati hakuna hata tone la maji kule wanakunywa maji ambayo si salama. Ukienda Mrijo sasa hivi, Mheshimiwa Waziri aende akanywe maji ya chumvi kule. Aende kule Kikengwa, kulikuwa hakuna maji, kile kisima kimekufa, Wananchi wanaenda kuchota maji maeneo ya mbali kabisa ili wapate maji salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hivi kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi ina dhamira iliyokuwa njema au ina dhamira ya mtego wa mamba wa kufikia saa hizi kumtega mtu na kupata kula nyama? Haiwezekani hata kidogo na siungi mkono hoja yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ya Kondoa Mjini hayajui ni lini yatapata hata hivyo visima vya maji, huko Hondomairo, Changaa na Sawi. Pale Mbelo Mjini tu, kilometa kumi kutoka Kondoa Mjini, hakuna maji. Maji watu wakachote kule, kindoo kile cha lita kumi akibebe aende akatoe huduma zote nyumbani kwake. Maji hakuna, tusileteane ujanja wa kudanganyana, naomba maji yapatikane kule. Mimi kawaida yangu, nitakuja kusimama hapa Mheshimiwa Waziri, kama ulivyokuwa umeshazungumza katika Kata moja kule, ukasema sisi wengine tunasimama tu kuja kupiga kelele kwa ajili ya kuomba maji. Kama tunapiga kelele kuja kuomba maji hapa, sasa nasema nitawahamasisha Wananchi wa Wilaya ya Kondoa wakatae kupiga kura, wasiwapigie kura Chama cha Mapinduzi, kwa sababu hawawatendei haki. Akina mama wanakwenda na maji hospitalini wanapokwenda kujifungua na huduma ya maji ni muhimu zaidi katika hospitali. Tuone katika Wilaya ya Kondoa, katika Mamlaka ya Mji wa Kondoa Mjini, inategemea maji mzunguko mzima wa chemchemi.

Sasa hivi wingu la watu limezidi kuwa kubwa, maji yale hayatoshi. Mheshimiwa Waziri, naomba nikuulize swali, wewe na Serikali yako; mna mpango gani wa kuwatekelezea Mradi wa Maji Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kwa kipindi kijacho ili waweze kupata maji ya kutosha?

Sasa hivi mnawalipisha bili hewa, wanalipa bili na maji hakuna; je, mnawatendea haki Wananchi wale? Naomba maji yale yawepo kule Mheshimiwa Waziri. Nakupenda kweli mtani wangu, lakini maji hunifikishii kule, unanidanganya. Siwezi kujisifu kidigo niseme kwamba, nitatembea kifua mbele Kondoa ina maji. Kondoa ina wingi wa maji, lakini haina usimamizi wa vyanzo vya maji. Watu wanapewa hela za maji pale katika Halmashauri ili waweze kununua vifaa vipya, wanakarabati vilevile na vinapigwa rangi. Je, una usimamizi gani katika Mamlaka ya Maji kule?

Naomba Wananchi wale wapatiwe maji, sina jinsi ya kuzungumza hapa, ni suala zima la maji na muwaonee huruma wanawake wale wa Wilaya ya Kondoa na ndiyo wapiga kura wakuu wa Chama cha Mapinduzi. Wanapata adha kubwa ya maji, wanajitwisha maji na ule mfereji sasa hivi haupitishi maji. Twende hata sasa hivi Mheshimiwa Waziri, mfereji ule unatakiwa ukarabatiwe na kama mpango wa maji hauko kule kwenye mabomba, basi hata ule mfereji upitishie maji ili wale akina mama wawe wanachota maji hata pale. Kwa nini mnasababisha akina mama wanaenda kuchota maji na maji mengine siyo salama kama pale hospitalini wanaenda kuchimba shimo. Mmoja anafua kule juu, mwingine anachimba shimo pale, yale maji kweli ni salama?

## ***Nakala ya Mtandao (Online Document)***

Anapofua nguo zile ambazo si salama kule, hazijulikani utaratibu wake, mwingine anaenda kuinga maji kule, ndiyo maji yale anapelekewa mwenzake kule hospitalini. Sikubaliani na suala kama hilo. Naomba maji yaelekezwe katika sekta maalum zinazostahili na kila mtu aweze kuyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije pia katika Mkoa huu wa Dodoma. Maji yapo katika maeneo tofauti tofauti. Hapa tulipo ni wakati wa Bunge, maji yapo yanatiririka kweli kweli na Mheshimiwa mwenzangu kasema maji yapo na sasa hivi yanaanza kutengenezwa huko; ndiyo nakubaliana naye lakini maji hayatoki kwa wakati. Wabunge tukishaondoka hapa na maji yameondoka. Kama vile kesho kutwa Mwenge unakwenda Kondoa, Mwenge ukishaingia pale Kondoa utaona maji utaona mengi tu, lakini ukiondoka na maji yameondoka. Desturi hii inatoka wapi? Mheshimiwa Waziri utakapokuja kwenye majumuisho yako utuambie. *(Makofi)*

Sitakuwa na mengi zaidi, ila namwomba Mheshimiwa Waziri, huu ni wakati mwafaka sasa, kwa kuwa tayari kipindi kilichopita cha mwaka wa jana tulipigia kelele, kama alivyokwisha sema Mheshimiwa Mnyika, tukaomba maji Wizara hii kwa kuililia na kuibembelezea kwa hali na mali ili Wananchi wapate huduma iliyokuwa muhimu. Hakuna suala lingine lolote, hakuna elimu itakayopatikana bila ya maji, hakuna afya itakayopatikana bila ya maji. Sasa suala la maji; ni nini tatizo nchi nzima sasa hivi ya Tanzania haina maji?

Serikali inajiendaaje? Tuna mito, tuna mabonde, tuna chemchemi, tuna maziwa, tuna kila kitu; nini tatizo? Naomba Mheshimiwa Waziri, ukija kwenye majumuisho yako sasa utufikishie taarifa hizi, unauambiaje Umma wa Watanzania, kwamba, suala la maji linafikia lini? Siyo kutuambia, mwaka wa jana ulisema Dar es Salaam litakuwa ndilo suala sasa la hadithi, lakini bado tatizo la maji liko pale pale!

Mheshimiwa Waziri tusidanganyane, tuambizane ukweli, tuiambie Serikali ikusaidie wewe kama Waziri, ihakikishe kwamba, inatoa hela zilizokuwa za uhakika na inasimamia Miradi yote ya Maji na inawafikia Wananchi. Kwanza suala la maji, vinginevyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tundu Lissu, ajiandae Mheshimiwa Rweikiza na Mheshimiwa Kirigini.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba nichangie hoja hii muhimu ya maji kwa ajili ya Wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Jimbo la Singida Mashariki katika Wilaya ya Ikungi ya Mkoa wa Singida. Mkoa wa singida ni moja ya mikoa yenye ukame sana katika nchi hii, ni moja ya mikoa ambayo haina vyanzo vya kudumu vya maji na kwa hiyo, hali ya maji kwa Wananchi wetu ni mbaya sana kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwa mwaka huu wa fedha unaokwisha, Wilaya yangu ya Ikungi imetengewa shilingi milioni 332.987 kwa ajili ya maji. Jimboni kwangu ambako hali ya maji ni mbaya sana, nimeona angalau mwaka huu kuna Miradi imeanza kutekelezwa ya Maji katika Mji Mdogo wa Ikungi na Mji Mdogo wa Makyungu; Miji ambayo imekabiliwa na tatizo la maji kwa muda mrefu sana.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimbo langu hilo lina Kata 12. Kutekeleza Miradi ya Maji katika Kata mbili tu za Ikungi na Mungaa uliko Mji wa Makyungu, hakutoshelezi kabisa. Pengine itakuwa vizuri kwa Wizara ya Maji kuangalia kama sehemu ya utatuzi wa matatizo makubwa ya maji yanayowakabili watu wetu, kukarabati visima vingi vya mkono vya maji ambavyo vilijengwa miaka ya nyuma na *Tanzania Christian Refugees Services (TCRS)*.

Kuna vijiji vingi ambavyo vilikuwa na maji miaka ya nyuma, ambavyo Miradi ya Maji ambayo imekufa, inahitaji gharama si kubwa sana kukarabatiwa ili Wananchi wetu waweze kupatiwa maji katika muda mfupi. Vilevile ni wazi kabisa kwamba, Wilaya kame kama hii na maeneo mengine, yanahitaji Miradi mikubwa zaidi ya Maji. Tutoe maji kwa wingi nje ya mkoa kama inawezekana ili kuweza kutatua tatizo la maji katika maeneo haya.

Nimeona mwaka wa fedha unaokuja tumetengewa shilingi milioni 899, hazitatoshia na hii ndiyo hoja yangu kubwa ninayotaka kuizungumzia. Kuna tatizo kubwa la muda mrefu la mgawanyo usiokuwa wa haki wa fedha za Miradi ya Maji kati ya mikoa yenye matatizo makubwa ya maji na mikoa ambayo ina nafuu.

Kati ya mikoa yenye ukame sana na mikoa ambayo hali yake ya mvua na hali yake ya maji si mbaya sana. Kuna upendeleo mkubwa sana na ninataka nitumie takwimu ambazo amezileta Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake kuthibitisha hili.

Nimesema moja ya mikoa ambayo ina ukame sana ni mkoa wangu wa Singida, lakini kuna Dodoma, kuna Shinyanga na kuna Simiyu. Sasa hii mikoa ambayo ina ukame sana, kwa mwaka huu unaoisha wa fedha, imetengewa fedha kiasi hiki kifuatacho kwa mujibu wa takwimu za Mheshimiwa Waziri. Mkoa wa Dodoma, shilingi 7,236,000,000 Mkoa wa Singida shilingi 3,304,000,000, Mkoa wa Shinyanga shilingi bilioni 3.296 na Mkoa wa Simiyu shilingi bilioni 2.864. Hii ni mikoa ambayo inaongoza kwa ukame na upungufu wa maji katika nchi yetu. Sasa linganisha na mikoa ambayo ina hali nzuri ya maji. Mkoa wa Tanga umetengewa, kwa mwaka huu unaokwisha shilingi 10,791,000,000, Mkoa wa Kilimanjaro shilingi 6,322,000,000, Mkoa wa Mbeya shilingi 9,293,000,000 na Mkoa wa Mtwara shilingi 7,571,000,000. Wale ambao hawana kabisa ndiyo wametengewa kiasi kidogo zaidi cha fedha, wale walio nacho wameongezewa. Kwa taarifa tu, hii mikoa ambayo inapata kidogo zaidi, ndiyo inayotoa kura nyingi zaidi kwa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upendeleo wa aina hii haufai. Upendeleo wa aina hii utaleta matatizo, upendeleo wa aina hii si haki. Kuna Wilaya moja tu ya Makete, kwa sababu Naibu Waziri wa Maji alikuwa Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Makete imetengewa shilingi bilioni moja milioni mia tisa na ushee. Wilaya ya Mwangi ya Mheshimiwa Waziri Maghembe, 1,400,000,000, halafu Wilaya moja ya Singida huko sijui Mkalama sijui kitu gani, shilingi milioni mia moja na tisini na ngapi. Huu upendeleo wa wazi huu haufai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Waziri atakapokuwa anajibu hoja hizi atueleze ni kwa nini mikoa ambayo ina matatizo makubwa ya maji kama hiyo niliyoitaja, isiyokuwa na *surface water* kabisa, haina mito ya kudumu, haina mabwawa yoyote ya maana, kwa nini mikoa hii ndiyo inayotengewa *budgetary allocations* ndogo zaidi ukilinganisha na ile ambayo ina mito ya kudumu na ina mifumo mizuri ya upatikanaji wa maji?

Kwa nini fedha nyingi zaidi zinakwenda Mwangi kwa Waziri au Makete kwa Naibu Waziri halafu fedha kidogo kabisa zinakwenda katika maeneo ambayo hakuna Mawaziri? Ina maana Mawaziri hao wanatumia mamlaka yao kujipendelea? Huu ndiyo utaratibu wa Serikali hii ya CCM? *(Makofi)*

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie na nikushukuru tena kwa kunipa fursa ya kuzungumza. Naomba Mheshimiwa Waziri, tafadhali, utakapokuwa unafanya majumuisho utueleze, kama utaratibu wa migawanyo ya fedha ndiyo huu, sisi ambao tunatoka katika maeneo makame lini tutapata maji kwa utaraibu huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kirigini, ajiandae Mheshimiwa Rweikiza!

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Hotuba hii muhimu. Nianze kwa kusema kwamba, ni ukweli usiopingika kwamba, maeneo yetu mengi hasa ya vijijini ni makame. Nikiri pia katika Wilaya yangu ya Meatu, ambako mimi ni Mkuu wa Wilaya, Wilaya ile ni kame sana. Upatikanaji wa mvua kwa eneo kubwa la Wilaya ni milimita mia tatu mpaka mia nne kwa mwaka. Vilevile niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuyaaisha maeneo haya ambayo ni kame na kuja na Mkakati Kabambe wa Ujenzi wa Mabwawa. *(Makofi)*

Niseme sasa kuna tatizo kubwa kwenye mkakati huu na mimi kama Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, naweza kusema Mkakati huu Kabambe wa Chama cha Mapinduzi unahujumiwa na Wizara yenyewe. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alikalia Kiti*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asema hivyo kwa sababu ukiangalia kuanzia ukurasa wa 58, umezungumzia ujenzi wa mabwawa. Mabawa yale hayajakamilika, mengine tangu tunazaliwa mpaka leo hii tuko humu bungeni, mabwawa hayajakamilika, na yale yaliyokamilika, basi miundombinu yake ya maji kwa maana ya utandazaji wa mabomba haujafanyika au mbovu na wakandarasi wametoroka na matatizo kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, natambua mna uwezo mkubwa. Naomba muangalie, kwa jicho la huruma kitengo hiki pale wizarani kinachosimamia ujenzi wa mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Bwawa la Mwanjolo, lililoko kwenye Wilaya ya Meatu. Bwawa hili lilianza kujengwa mwaka 2008. Bwawa hili limekuwa na mkanganyiko usioeleweka. Hapa nina vitabu vya bajeti tangu mwaka 2009. Bwawa hii linarekodiwa limekamilika kwa 80%. Bajeti ya Waziri Mkuu, bwawa hili limeripotiwa limekamilika kwa asilimia 75%. Leo kwenye hotuba ya Waziri, bwawa hili linatajwa kukamilika, kwa asilimia 78%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 16 Mei, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri, nilimpelekea kilio changu. Mimi na yeye tuliandamana mguu, kwa mguu hadi lilipo Bwawa la Mwanjolo, tumekuta hakuna Bwawa kule. Ukamilishaji ni uchimbaji chimbaji tu, na wataalam wamesema kazi ile ni 40%. Leo katika swali la msingi limeulizwa hapa na Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mechack Opolukwa, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema, Serikali imetenga kiasi cha shilingi 400,000,000/=. Hivi hii ni sahihi, bwawa ambalo lilikuwa linatakiwa kukamilika ndani ya miezi sita tangu 2008, mpaka leo hii halijakamilika?

Pesa zimelipwa tayari 95% ya gharama za malipo za bwawa. Gharama za Mradi, ni bilioni 1.03. Tayari Mkandarasi amelipwa na Wizara shilingi 985,000,000/= sawa sawa na 95%.

Leo hii bwawa limekamilika kwa 40%. Naungana kabisa na Mheshimiwa Tundu Lissu, hivi haya maeneo ambayo, hii Mikoa ambayo haina Maziwa, hizi Wilaya ambazo ni kame kama ilivyo Wilaya ya Meatu, takribani milimita 300 mpaka 400 za mvua tu kwa mwaka. Unatenga



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

shilingi milioni 400 eti ziende kwenye bwawa ambalo lilikuwa likamilike miaka takriban saba nyuma, hii ni sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana. Namuomba Waziri achukue hatua, na auchukue hatua kuanzia pale Wizarani kwake, malipo yalifanyikaje, kwenye Bwawa la Mwanjolo wakati bwawa halipo? Mkandarasi Nyakilang'anyi *Construction* aliwezaje kulipwa shiingi milioni 985 wakati bwawa halijakamilika? Lakini niishauri Serikali, sisi wananchi wa Wilaya ya Meatu kwa kiasi hicho cha mvua tunahitaji bwana hili haraka haraka iwezekanavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri, nina mpango wa kushika shilingi yako kwa mara ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Rwekiza, jandae Mheshimiwa Mwaiposa.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Mimi naunga mkono mkono hoja, lakini niseme kwamba tatizo la maji ni kubwa. Ukisikiliza kilio cha Wabunge sisi wote humu ndani, tatizo la maji ni kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nitoe shukrani kwamba katika maeneo yangu kuna sehemu ambako tumepata maji katika ile miradi ya vijiji 10, ni chache tu; Kyamuraire, Mibwera ni sehemu chache. Sehemu nyingine, bado kabisa kazi haijaanza kama Kata ya Katoma, Kata ya Rubafu, Miradi haijaanza, tunapiga kelele humu ndani, tunalalamika maji hakuna nchi nzima shida ni ilile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa tulilionalo tunategemea wafadhili, maana hata Waziri alivyosema hela nyingi ya wafadhili kutoka India, kutoka *World Bank*, kutoka wapi...Sasa hii kidogo haiwezi kutusaidia sana. Kwa hiyo, kwa sababu muda ni mfupi, niseme haraka kwamba mimi leo nina pendekezo maalum na naomba niunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanzishe Mfuko wa Maji. Tuanzishe Mfuko Maalum wa Maji kama ilivyo Mfuko wa Umeme *REA* (Wakala wa Umeme Vijijini), Kama ulivyo Mfuko wa Baabara (*Road Fund*) kwenye *road toll* na nini. Tunajenga umeme vijiji vyote sasa hivi, miaka kumi/mitano au sita tutakuwa na umeme karibu nchi nzima kwa sababu ya *REA*. Miaka kumi ijayo au mitano, tutakuwa na barabara zote za lami nchi nzima kwa sababu tuna mifuko ambayo ni makini. Tuanzishe Mfuko wa Maji Vijijini. Hili ni jambo jepesi wala halina ugumu wowote. Tuwape majukumu. Jukumu la kwanza ni hilo, kupeleka maji vijijini. Waainishe vijiji ambavyo vina shida kubwa kama wanavyosema Wabunge, tupeleke maji kule.

Jukumu la pili, watafute pesa kama ilivyo *REA* kwenye umeme, watafute pesa kwa wafadhili, waombe misaada huko, kwenye bajeti. Watafute pesa, wakae wapige vichwa vyao watafute pesa. Ukisema kwamba kwa mfano kwenye bia, maana yake bia inatokana na maji, wanywaji wa bia ni wengi, kila bia senti hamsini au soda senti ishiniri, kwa siku utapata mamilioni ya pesa. Au maji ya chupa haya wale wanaokunywa maji ya chupa wa mijini wale senti senti kumi tu kwa chupa moja ya nusu lita. Kwa siku utakuwa na mamilioni ya pesa, hizo hela ziende vijijini, tusaidie watu wa vijijini, kwa kweli hali ya maji kule vijijini ni mbaya sana.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ifanye kazi hii kwa makini ilete sheria. Nilikuwa naongea na Waziri mmoja ambaye zamani alikuwa Waziri wa Maji, alisema jambo hili walishaliongea. Walishaliongea, wakalijadili kwa kirefu, wakaamua kwamba Mfuko huu uanze miaka mingi iliyopita. Lakini mpaka leo haujaanza.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, leta sheria hapa Mwezi Novemba tupitisha sheria. Na mimi niseme usipoleta sheria hiyo, mimi nitaiteta, nitaiandika mimi hiyo Sheria ya Maji Vijijini. Mimi ni Mwanasheria, nitaiandika hiyo *Private Member's Bill*, nitaiteta humu ndani, tuijadili tuiptishe, ili mfuko huo uanze. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumze kwamba, wakati tuna miradi hii tunayo mikubwa, midogo, vijiji kumi (10) hivi, ambayo haianzi, tuna miradi mingine ya zamani ambayo ipo lakini haikarabatiwi. Sasa inashangaza, unanza mradi mpya, wa zamani unauacha unazidi kuharibika, una maana gani, huu hausaidi watu?

Pale kwangu nina Kata Mbili, Kata ya Maruku na Kata ya Kanyangele, tuna mradi wa maji wa miaka mingi ulikuwepo mzuri, lakini umechakaa baada ya muda mrefu kupita, maji hayafiki kwa wananchi. Lakini miundombinu ipo, matanki yapo, matanki manne makubwa sana, yakosafi, yako *intact*. Mabomba yako chini ya ardhi kule. Ubovu ni mdogo tu pale kwenye chanzo, sijui *pump* imeharibika basi. Ukarabati ule ni shilingi 100,000,000/= au 200,000,000/= unahudumia vijiji saba. Shilingi 200,000,000/= itahudumia vijiji saba huku kwenye miradi 10 ya vijiji kila mradi shilingi 800,000,000/= kila kijiji, hela nyingi. Huu wa shilingi 200,000,000/= vijiji saba vinapata maji mengi mazuri na salama. Kwa nini haikarabatiwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, TANROAD wana sheria, ni marufuku kujenga barabara mpya kama ya zamani ni mbovu. Lazima kwanza ya zamani ikarabatiwe ndiyo muanze barabara mpya. Kwa nini maji haifanyiki hivyo? Mradi ya Maruku naomnba utengenezwe. Niliishaongea na Waziri na Naibu Waziri mara kadhaa, mkaniahidi mwaka jana, mwaka juzi, mpaka leo hakuna kilichofanyia. Huu mradi ukarabatiwe, hela kidogo, mradi uanze, tupate maji pale Maruku na Kanyangele wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tu kusema kwamba hata kama nimeunga mkono hoja, lakini shida ya maji ni kubwa nchini. Tujizatiti, tukianzisha huu Mfuko wa Maji, ukasimamiwa vizuri, ukawa makini. Wakala wa Maji au Mfuko wa Maji, vyovyote vile utakavyoitwa ili mradi uwepo, tutapata ufumbuzi wa matatizo ya maji, itatusaidia sana katika kuleta maji vijijini. Na wenye shida ni vijijini, mijini kuna maji. Miji yote karibu ina maji. Kwa hiyo wa mijini wachangie kidogo kusaidia wa vijijini kama ilivyo umeme, wanatoa kidogo kwenye *bill* ya umeme ile kila mwisho wa mwezi, inawekwa kwenye Mfuko wa Umeme Vijijini, na wa maji iwe ni hivyo hivyo, tupate pesa ya kwenda kuhudumia wananchi walioko vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Mwaiposa, jiandae Mheshimiwa Obama na ajiandae Mheshimiwa Lusinde!

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Lakini nianze tu kwa utangulizi kwa kusema kwamba, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2015 ilikuwa na maelengo ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama, hasa wa mijini kwa asilimia mia. Lakini hata katika Dira ya MKUKUTA Namba II, imelenga pia kuwapatia wananchi maji karibu na makazi yao, kwa asilimia 75.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nizungumzie tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam kwa ujumla na kwenye Jimbo la Ukonga. Tatizo la Maji kwa Dar es Salaam ni kubwa mno. Na Wabunge wa Dar es Salaam kila mmoja anapokuwa anasimama anaongelea tatizo lililoko katika Jimbo lake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina wasiwasi tu kidogo na DAWASA, ambayo ndiyo yenye dhamana ya kushugulika na maji katika Jiji la Dar es Salaam, Pwani na maeneo mengine.

Tatizo kubwa hasa lililoko katika Jimbo la Ukonga nahisi hata kwenye majimbo mengine, nilikuwa naongea pia na Mheshimiwa Mnyika, naye tatizo liko hivyo hivo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo visima vingi sana ambavyo vimechimbwa na DAWASA, lakini vimefetelekezwa. Katika Jimbo la Ukonga viko visima saba ambavyo vimechimbwa kuanzia mwaka 2011, 2012. Visima hivi vilichimbwa wakati tukiwa kwenye bajeti. Lakini baada ya bajeti tu, visima sita ambavyo vilikuwa vimekwisha kuchimbwa, viliachwa. Lakini vile ambavyo walikuwa wameamza kufanya utafiti wa kutafuta maji navyo pia viliachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama fedha ni kidogo, hivi njia nzuri ya utekelezaji ni kuchimba visima hapa na pale hapa na pale bila kumaliza? Ni kwa nini fedha hizo ndogo za wananchi, walipakodi zisitumike kuchimba visima vichache, lakini vikakamilika? Visima vinachimbwa vingi, lakini hakuna hata kimoja kinachokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo note ambayo ameniletea Mheshimiwa Waziri hapa. Viko visima saba katika Jimbo la Ukonga, lakini ni kisima kimoja tu kimekamilika, miaka mitano yote. Na kisima hiki kilichokamilika ni hiki ambacho kimetengenezwa kwa nguvu za *UN Habitat*, vingine vyote viko nusu nusu.

Mheshimiwa Waziri, pamoja na kukutembelelea mara kwa mara ofisini kwako pamoja na Mkurugenzi wako, pamoja na barua zangu zote ambazo nakukuletea. Ni kitu gani kinafanya visima hivi visikamilike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida katika taasisi hii ya DAWASA. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, hebu jaribu kufuatilia kwa karibu zaidi. Kwenye ki-note chako uliniambia kwamba Wakandarasi wako kwenye miradi, mpaka hivi ninavyoongea, ni mkakandaasi mmoja tu wa kisima cha Kivule Nyang'andu ndiye yuko site, maeneo mengine yote hakuna wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutaziacha hizi fedha za walipa kodi zikiwa zinateketea kwa visima ambavyo haviendelezwi, mpaka lini, hata kama hiyo bajeti ni ndogo? Kwa hiyo niombe sana ufutiliaji wa visima ambavyo vimekwisha kuchimbwa viweze kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko visima vingine ambavyo vimechimbwa katika Jimbo la Ukonga kwenye eneo la Msongola, Mvuti pale pamoja na Mbondole. Lakini hata kwa Mheshimiwa Mnyika, vimeonekana visima vile vina maji mengi, lakini yale maji yana chumvi.

Ni kwa nini Mheshimiwa Waziri, tusifanye utaratibu wa kuya-treat yale maji kwa sababu kuna njia ya kupunguza ile chumvi ili wananchi waweze kuendelea kupata yale maji na kuyatumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kupitia kwako, Mheshimiwa Waziri hebu aje na kauli ambayo ni ya kiukweli kabisa kwamba ni namna gani anajipanga kumaliza...

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Obama! Jiandae Mheshimiwa Lusinde! (Makofi)

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii.

Kwanza kabisa naunga mkono hoja. Lakini la pili, naomba nimpongeze kabisa Mheshimiwa Prof. Maghembe kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Naibu wake na Naibu mwingine aliyetoka aliyekuwepo wakati ule Mheshimiwa Dkt. Mahenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inazo changamoto, maji ni tatizo la nchi, ndiyo maana mwaka jana tuliamua kwamba iweze kupewa bajeti ya kutosha. Lakini ninaomba ku-register masikitiko yangu kwamba Serikali haijaweza kuiwezesha Wizara hii fedha za kutosha ili waweze kukamilisha mipango mizuri waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze Waziri Mkuu baada ya juzi kusema kwamba anai-commit Wizara ya Fedha ili iweze kumalizia fedha za kipindi kilichopita. Tunaomba Agizo la Waziri Mkuu liweze kutekelezwa ili mambo yaweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, mimi nina tatizo moja, ninayo Miradi yangu ya BRN ambayo tuliiweka kwenye bajeti ya 2012/2013. Ambayo tulikuwa na mradi wa Mnanila - Manyovu, ambao ule unategemea kulisha vijiji visivyopungua vitano. Nashukuru tumepata shilingi milioni 10 kwa ajili ya upembuzi, na ile kazi inaendelea chini ya Engineer mzuri kabisa ambaye yuko pale Wilaya ya Kasulu. Kwa hiyo, tunaomba fedha nyingine, ambazo Waziri Mkuu alipokuja Manyovu, alitamka mbele ya wananchi kwamba kuna milioni 800 ambazo ziko tayari ambazo wamezitenga na wananchi wale unategemea sasa hizo fedha ziwezekwenda. Kwa hiyo ni mategemeo yetu kwamba hizo fedha utazipeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi mwingine wa Mugeru, Namigongo ambao nao ulikisiwa kwenye BRN kutumia milioni 700. Kwa hiyo ni mategemeo yangu kwamba nayo hiyo fedha utatupatia. Lakini wa mwisho kwenye BRN ni mradi wa Kibandwe - Bweranka ambao nao ulikisiwa milioni 800. Hii ni miradi ambayo nina imani kwamba kwa kuamua unaweza ukanisaidia kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nipongeze vile vile, katika utekelezaji wa vile vijiji kumi), vijiji sita vinatekelezwa ndani ya Jimbo langu. Na niishukuru Serikali, niombe ikamilishe fedha ili waweze kukabidhi miradi hii kama inavyotekelezwa katika kijiji cha Munzeze, Kigogwe, Kirungu, Mbanga, Nyamugali na Bulimanyi. Kwa hiyo tunashukuru sana, tunaomba uweze kututekeleza hayo. *(Makofi)*

Jimbo letu linakuomba na linakualika wewe Waziri wa Maji ufike, utembele miradi hii, mingine katika vijiji sita umeishafanya kazi nzuri, ili uweze kuona hii miradi ambayo iko kwenye BRN ambayo umesema utatupatia fedha.

Kwa hiyo mimi sina mengi. Lakini naomba tu ni-support alilolisema kaka yangu Mwanasheria Mheshimiwa Rweikiza kwamba ni lazima tuweze kuwa na Agency, bila kuwa na Agency huwezi kukimbizana wewe Wizara moja kwa moja na wananchi, lazima uwe na Agency ili tuweze kuwa na tozo, ili tuweze kuweka fedha pale ili na wewe uweze kwenda vizuri. Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Waziri, kazi unayo, hao wanokuita ni mzigo bado hawajaelewa umakini wa kazi yako, mzigo watakuwa wao, wewe chapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Lusinde, jandae Mheshimiwa Silinde, ajiande na Mheshimiwa Mkiwa.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kupata nafasi hii ili nami nichangie katika Wizara hii muhimu sana, Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema, nitoe pole sana kwa familia ya Marehemu George Tyson, aliyefariki kwa ajali ya gari, walikuwa wanatoka jimboni kwetu, katika Kijiji cha Mvumi Makulu na kipindi chao cha *Mboni Show*, walikwenda kukabidhi pale madawati 50 kwenye Shule ya Msingi ya Chalula. Kwa hiyo mimi kama Mbunge wa Jimbo lile nalazimika kutoa pole sana kwa familia nzima na kwa wote ambao walipata majeruhi, niwatakie moyo wa subira na Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema roho ya Marehemu George Tyson, amina!

Vilevile, nimkumbuke na Mama yetu Mama Zitto, Mungu amlaze mahali pema peponi, amina!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara muhimu sana kwa nchi yetu, na niseme kwamba mimi nampongeza Prof. Maghembe pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri. Kwa sababu gani?

Kumlaumu sana Profesa, mimi kunanikumbusha akili ya mchungu ng'ombe. Kuna baadhi ya wachunga ng'ombe wanachekesha kidogo, anataka ng'ombe watembee kwa *speed*, lakini anamtandika ng'ombe wa nyuma wakati anayechelewesha safari ni ng'ombe aliyetangulia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa kwamba Wizara hii haipelekewi fedha wanazoomba na Wizara ya Fedha. Sasa kumpiga Mheshimiwa Maghembe haina tofauti na mchungu ng'ombe, kwa sababu tunafahamu na hata ukitaka kuangalia kwenye mjadala huu unaoendelea, hakuna Waziri yeyote wala Naibu Waziri wa Fedha ambao ndiyo tungewaambia watoe fedha. Ah, unajua Rais wetu anateua Mawaziri na Manaibu Waziri, lakini wanakuwa na kazi nyingi halafu hawapatikani kwenye Bunge, ni kichekezo kikubwa sana. Najua huko waliko akina Mheshimia Saada na Mheshimiwa Mwigulu watakuwa wanakuja mbio hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme kwamba Wizara hii ipewe fedha za kutosha ili wananchi waweze kupata maji, kwa sababu hata zile tulizowaombea mwaka jana hawajapewa! Hivi huyu Mheshimiwa Maghembe atakuwa anaenda kuchimba visima vya maji yeye na mke wake? Haiwezekani! Lazima awezeshwe ili hayo maji yaweze kupatikana.

Kwa hiyo, nataka niseme kwamba Wizara hii wanafanya kazi kubwa lakini kazi yao ngumu kwa sababu fedha zinazoombwa hazipatikani. Tuiombe Wizara ya Fedha itoe fedha kwa Wizara ya Maji, fedha wanazoomba wapewe zote ili tupate nafasi ya kumlaumu Mheshimiwa Prof. Maghembe pamoja na Mheshimiwa Makalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo makubwa sana kwenye vijiji, tunaambiwa hapa na ndiyo maana nikapendekeza kwamba wanapokuja Mawaziri kwenye ziara tusiwanunulie maji ya chupa, tuwape maji wanayokunywa wananchi. Tukifanya hivyo mara mbili mara tatu hawa wataona umuhimu wake.

Na nikasema hata akija Mheshimiwa Waziri Mkuu anakuta maji ya kisima mmemwekea pale mbele, akija juu Mkuu wa Mkoa, alete maji eneo lile! Kwa hiyo, wananchi mnielewe tunapotafuta maji ya chupa ya Kilimanjaro tunajifanya kwamba vijiji vyetu vina maji ndiyo maana hawawatilii umuhimu. Akija Waziri wa Fedha ziara maji ya kisima, tukifanya namna hii watatuonea huruma.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, msemu wa maji ni uhai uimejidhihirisha hapa, tunapozungumza maji ni uhai zipo shule za msingi ngapi zina maji? Watoto badala ya kusoma wanabeba madumu ya maji, huku wana madaftari, huku wana dumu la maji, huku wana kuni. Hivi huo muda wa kusoma anaupata saa ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapozungumza maji ni uhai, tunazungumzia vitu vingi sana. Njoo katika Jimbo la Mtera, kuna vijiji, kuna vichekesho vikubwa sana, nenda kuna kijiji kinaitwa Chinoje, anakuja *Surveyor* anapima anasema maji yako umbali fulani, wanakwenda wanachimba wanakuta maji hamna, halafu yule *Surveyor* analipwa, analipwa kwa sababu gani wakati amesema uongo? Yeye kaja kupima kasema maji yapo futi mia, unachimba 150 maji hakuna, unamlipa kwa sababu gani? Kwa hiyo, tupitische utaratibu kwamba anayepima maji achimbe huyo huyo ili yasipokutwa asilipwe! Hii tabia ya kuja kupima mtu mwingine, anachimba mtu mwingine inatuletea wizi mtupu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa! Tumezungumza hapa, kuna mabwawa yamechimbwa na Mwalimu Nyerere. Juzi juzi hapa lipo bwawa moja linaitwa la Bwawa la Mlowa Bwawani, tumekwenda na Mheshimiwa Chiza pale. Tangu ameahidi Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Shein alipokuwa Makamu wa Rais, mpaka leo lile bwawa halijafukuliwa wala kuchimbwa. Kama tunajua hatuna uwezo, tunaahidi ya nini? Si unyamaze? Unakwenda pale, mtu mkubwa anaahidi maji hapa yatachimbuliwa, bwawa litapatikana, matokeo yake bwawa hakuna na huduma ya maji hakuna.

Kila ukienda pale vikundi vya ngoma vinaimba tu, tunakukumbusha ahadi ya Dkt. Shein. Sasa Dkt. Shein kaondoka lakini ofisi ipo! Kwa nini Mheshimiwa Makamu wa Rais aliyepo Dkt. Bilal asinisikie akaja kuondoa ile aibu ambayo ameichacha Makamu wa Rais pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kengele ya kwanza nafuatilia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vijiji vya Loje, vijiji vya Kata ya Nindi, vijiji vya Naheleze na vijiji vya Igandu vipewe maji na tuhakikishe kwamba wananchi wanapata maji ya kunywa safi na salama ili watumie muda mwingine kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa sababu moja tu kwamba tusipounga mkono hata hicho kidogo kilichopangwa hakitapatikana, kwa hiyo tutakosa kabisa. Ndiyo busara ya kuwashawishi wenzangu tumuunge mkono huyu bwana apate hiyo fedha kidogo afanyie kazi walau wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa anakuja Mheshimiwa Silinde, ajiandae Mheshimiwa Christina kwa sababu ana Kamati halafu atakuja Mheshimiwa Mkiwa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii. Lakini mimi napenda nianze tu kwa kum-*quote King Leopold II* ambaye alikuwa ndiye Mfalme wa Ubelgiji wakati ule anatuma *delegation* yake kwenda Congo alikokuwa anatawala.

Aliwaambia hivi, ili tuweze kuendelea kuwatawala Wacongo, "*teach them how to read and not to reason*". Wafundishe kusoma na wala siyo kufikiri ama kutafuta tafsiri ya jambo, utawatawala vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu tuna uwezo wa kusoma, lakini hatutafsiri. Mambo mengi yaliyopo kwenye bajeti zetu, tunasoma tu, lakini hatutafsiri na hilo ndiyo tatizo.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tundu Lissu yeye alikuwa anasoma takwimu ambazo na mimi nilikuwa nimeshaziandika, lakini mimi nitakwenda kwenye *content* yaani kwa maana ya Wilaya tu (katika ngazi za Wilaya).

Mwanga kiasi kilichotolewa ni *1.4 billion*, idadi ya watu wa Mwanga ni 130,000, kiasi kinachopangwa kupelekwa mwaka unaofuatia wa fedha ni *1.7 billion*. Momba, Halmashauri yangu fedha iliyotolewa ni milioni 400, idadi ya watu ni 350,000, fedha zinazotarajiwa kwenda mwakani ni milioni 900. *This is shame!*

Hatuwezi kuendelea kujadili hivi! Watu wachache fedha nyingi! Kwenye maeneo yenye watu wengi fedha kidogo na ndiyo kuna shida zaidi ya maji. Ni kama ilivyo Makete, fedha iliyopekwa mwaka uliopita ni *1.9 billion* watu hawafiki hata 150,000, fedha zinazotarajiwa kupelekwa tena ni *1.1 billion*. Ni *shame!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunduma peke yake ina watu zaidi ya 150,000 kila mmoja anajua. Hakuna mpaka wenye mapato mengi nchi hii kama Tunduma. Mwaka mzima Wizara imepeleka milioni 26! Milioni 26 unapeleka Tunduma hata Mwanga ama Halmashauri yoyote haina uwezo wa kuingiza mapato kama ilivyo Tunduma pale na fedha zenyewe zote za Tunduma haziwi kwa ajili ya maslahi ya watu wa Tunduma, *TRA* ndiyo wanachukua zinakwenda kwenye mgawanyo wa maeneo mengine. *This is unfair!* Hii ndiyo inaitwa *teach them how to read and not to reason!* Yaani tumekuwa siku zote tu, ee tumekutengea milioni 900, *then what for?* Unatenga milioni 900 ambazo haziendi!

Mwaka jana mkatuletea miradi mingi ya *BRN*, zile *story* zimeishia wapi? Kwenye maji Halmashauri yangu ya Momba kwenye miradi ya *BRN* imetenga bilioni 9.3, hata senti moja haijaenda, mimi niunge mkono hii hoja? *The same story!*

Mheshimiwa Rais Mkapa alikuja Tunduma akaahidi maji *in five years, 1995* bila, akaja mwaka 2000 maji hakuna! Akaja Kikwete mwaka 2005 maji hakuna, mwaka 2010 maji hakuna na wanapata kura! *This is unfair!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za wenzetu, nilikuwa napitia hapa kwenye *internet* nikawa natafakari, hivi sisi wenye *surface water* (maji yanaoonekana) yanayopaswa kutumika kwa wananchi, tungekuwa jangwani ingekuwaje? Maana yake sisi leo tuna bahati, tuna Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, tuna siji...kila mmoja anajua tumekuwa tukiyaimba, tuna maji yanayopaswa kutumika. Jukumu letu, *we have waters, our duty is just to channel them*, yaani kazi yetu sisi ni kutengeneza miundombinu iwafikie, hatuna kazi ya kutafuta vyanzo vya maji, vyanzo vyetu ni vya uhakika. Tunajenga taifa au tunabomoa? *We will speak the same story* kila siku! Hii yote tunasema jamani tusipende kubeba mambo ambayo hatuwezi kuyananii...maana unaunga tu mkono, unaunga mkono, watu wanapata matatizo yaleyale, inatisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia kitabu cha Mheshimiwa Waziri, takwimu zinaonyesha hapa, anasema 57% ya Watanzania wanapata maji safi na salama. *This is wrong*, yaani *completely wrong* kwa sababu ukipitia *Order Paper* (shughuli za Bunge za kila siku) huwezi kukosa swali la maji, kila Mbunge hapa ameuliza swali la maji jimboni kwake. 57% maana yake unahitaji Watanzania milioni 27 wamepata maji safi na salama, ni kweli? Yaani tuwe wakweli! *Sometimes you should feel shame!*

Wenzetu Marekani na maeneo mengine, wao Rais anapogombea hajadili tena maji kwa sababu ni wajibu wa Serikali kupeleka maji, ndiyo wajibu wetu! Sasa Bakhresa anaweza kusambaza maji nchi nzima, *Bonite Bottlers* wanaweza kusambaza maji nchi nzima na ndiyo maana yananutuliwa vijijini. Serikali inashindwa kutoa maji safi na salama, tutawaelewaje?

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Watu wa Kamsamba hawana maji, Msangano hawana maji, Shitete hawana maji, Mpapa, Ivuno, Kapele, Msangano, Ngalambwe na maeneo yote, kila mahali, halafu mnasema hamjachoka, why! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie, unajua kwenye maisha kuna ku-achieve na ku-succeed, *these are two different things*, ku-achieve ni kwamba unaweza kupewa milioni moja, mwisho wa mwaka ukaleta milioni moja na elfu tano, ume-achieve. Lakini ku-succeed ni kufikia malengo uliyojipangia, unapewa milioni moja unaleta milioni tatu. Tunataka viongozi wa namna hiyo. Lakini siyo unakaa unachimba kisima kimoja, mbwembwe nyingi, matangazo makubwa, *you have just achieved; you have never succeeded in this country*, hamjafikia hayo malengo na ndiyo maana tumekuwa tukiwaambia kila siku, tunataka mfikie malengo tuliyojipangia, siyo kila mwaka tu hela hazitoshi, kisungura!

Tumetenga bilioni 226, hamjapeleka fedha. Sasa mnategemea nini? Ile miradi yote maana yake imelala. Sasa nani alaumiwe? Waziri hataki, Wabunge hawataki, sasa nani abebe lawama na sisi ndiyo wenye jukumu kama taifa. *This is shame on you!* Lazima mbadilike na ni lazima mtafakari. Mheshimiwa Waziri ukirudi uende uka-reverse hizi hela, Momba tuna shida zaidi ya maji kuliko Mwanga, kajimbo kako kadogo mno, lakini mahela mengi. Ubinafsi muache, *selfishness!* Ndiyo maana mlibeba hata viwanja vyote baada ya vyama vingi mwaka 1992, *selfishness!* Watanzania wote tuna haki sawa ya kupata maji!

Mheshimiwa Maghembe na Naibu, mwaka juzi wewe ulipata milioni 600, mwaka huu naona umeingia tu na wewe *1.3 billion. Take care!* Morogoro na wewe kajimbo kako ni kadogo tu, *selfishness!* Hatuwezi kuendelea na huu utaratibu. Nimeona hizi zote zipo kwenye takwimu, milioni 660 ulipata zipo humu ndani na mwaka huu umepata hiyo *1.3 billion*, unajitengea! Hatuwezi kuendelea na huu utaratibu na hiyo imekuwa karibu kila mahali. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wewe uwe unatoa fedha! Ee lazima tumwambie awe anatoa fedha! Na mwambie na Waziri Mkuu, mambo ya msingi kama ya maji lazima Watanzania wafikishiwe. Lakini hatuwezi kuendelea kukaa kila siku tunaunga mkono mambo yasiyokuwa na msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo,...

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimia Christina! Ajjandae Mheshimiwa Mkiwa na ajjandae Mheshimiwa Mwanjale!

**MHE. MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoa mchango wangu katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza, na mimi nitoe pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliofiwa na wazazi wao, Mheshimiwa Zitto Kabwe amefiwa na Mama yake ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, natoa pole sana kwa familia na chama. Na pia natoa pole kwa familia ya Martha Mlata, Mbunge mwenzangu wa Mkoa wa Singida kwa kufiwa na Baba yake mzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo za rambirambi, nianze mawazo yangu katika hotuba hii kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni kilio nchi nzima, maji ni janga la Taifa. Lakini janga hili inaonekana wanaopaswa kulia hawalii, wanaopaswa kutatua janga hili wala hawalioni kama ni janga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niulize Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, hivi suala la maji ni kipaumbele cha ngapi katika Serikali ya CCM? Kwa sababu kama inaipa maji kipaumbele cha juu basi tatizo hili lisingekuwa kilio nchi nzima kama ambavyo tunashuhudia.



## Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Bunge lako Tukufu lililia baada ya kuona kwamba maji yametengewa bajeti isiyotosha. Baada ya kilio cha Bunge Serikali iliji-*commit* iliongeza bilioni 184.5 katika bajeti ya maji na hivyo kufanya jumla ya bajeti ya maji kwa mwaka unaoisha ikawa bilioni 312.1. Cha kushangaza ni kwamba ilipofika Aprili mwaka huu na mwaka unaelekea kuisha Serikali ilikuwa imepeleka 27% tu ya miradi ya maji nchi nzima, 27%! Maji ni kipaumbele cha ngapi katika Serikali hii ya CCM?

Baada ya kuona kwamba huu ni mzaha katika suala la muhimu kama maji, Kamati ya kisekta ililia na Kamati ya Bajeti ililia na Wizara imeahidi kuongeza shilingi bilioni 100 kabla mwaka huu haujaisha, ni wiki chache zijazo. Pamoja na nyongeza hiyo, bado bajeti nzima ya maji itakuwa ni 47% tu, ndiyo kusema kwamba mwaka unaoisha maji hayajafikia hata 50% ya utekelezaji wake na hiyo ni kama hiyo ahadi ya nyongeza ya Serikali itatekelezwa na mimi nina shaka kama itatekelezwa. Wizara hii mwaka huu inaomba bilioni 490. Sasa mimi naona ajabu, kama mwaka unaoisha asilimia itatekelezwa kwa takribani 46%, leo wanakuja na mahitaji ya bilioni 490, hivi ni kweli inatekelezeka au ni namba tu tunazileta ili Bunge lijifurahishe kwamba maji yametengewa bajeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kushangaza vilevile, bajeti hii mpya haijaonyesha deni ambalo halitafikiwa kwa mwaka huu, kama Serikali ikitoa bilioni 100 ya nyongeza Wizara ya Maji itafunga mwaka ikiwa na *deficit* ya bilioni 165.5 na zenyewe hazijaoneshwa zitatumikaje katika mwaka unaofuata. Ina maana kwamba kwa bajeti ya mwaka huu bilioni 490, ukitoa pungufu ya mwaka huu ambayo haitafikiwa, basi bajeti halisi ya Wizara ya Maji itakuwa ni bilioni 324 na siyo bilioni 490.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ukiniuliza kwamba Waziri ambaye ni mzigo katika Serikali hii ni nani, mimi ningekwambia kwamba Waziri anayepaswa kuitwa mzigo ni Waziri wa Fedha kwa sababu miradi mingi haijapelekewa fedha. Tunafunga mwaka miradi mingi ya maendeleo ikiwa haijafikisha 50% ya bajeti yake na kwa hiyo tunaiomba Hazina waache kuwa mzigo kwenye miradi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiyasema hayo, tunajua kwamba miradi mingi ya maendeleo haijapelekwa fedha na hususani Wizara ya Fedha na wakati huohuo tunajua kwamba makusanyo ya *TRA* yamekuwa karibia 90% na tunajua kwamba yatafika 90% mwaka unapoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo makusanyo ya *TRA*, 90% hawajafika malengo, lakini vilevile siyo mbaya sana, mbona makusanyo hayo hayalingani kiuhalisia na fedha zilizopelekwa kwenye maendeleo? Hii ni kusema kwamba kuna matumizi ya fedha ambayo yanakwenda kinyume na bajeti ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida kama walivyoeleza Wabunge waliotangulia ni moja ya Mikoa kame katika nchi yetu, lakini kama kawaida Serikali yetu huwa haipeleki fedha au miradi ya kipaumbele kwenye Mikoa ambayo iko nyuma na safari hii tunashuhudia Mkoa wa Singida ukitengewa bajeti ndogo kabisa ya maji pamoja na kwamba huu ni Mkoa kame.

Mheshimiwa Waziri wa Maji anasema kwamba miradi ya visima 10 imetekelezwa katika Mkoa wa Singida, lakini saba tu ndiyo vina maji na visima vitatu havitoi maji.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Sasa mimi nauliza kwamba kama mradi ulikuwa na upembuzi yakinifu halafu watu wanatekelea mradi visima vitatu tunaambiwa havina maji, hivi huo upembuzi yakinifu ulifanyika namna gani? Ina maana watu walikula hela, wakasema hapa kuna maji kisima kikachimbwa halafu tunaambiwa hatuna maji na sijui hatua gani zitachukuliwa kwa wapembuzi yakinifu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi na vijiji vyake inatatizo kubwa la maji. Pale Ikungi Mjini kuna visima ambavyo vinaitwa vya Wajapani, Wajapani walichimba maji pale, lakini hivyo visima havijawahi kutoa maji...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mkiwa! Ajjandae Mheshimiwa Mwanjale na Mheshimiwa Shekifu.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kupaswa kushukuriwa kwa kunipa afya nami nikasimama mbele ya Bunge lako kuweza kuchangia kidogo Wizara hii Maji. Pia ningependa kuwapa pole wale wote waliondokewa na wapendwa wao, Mwenyezi Mungu awape subira katika wakati huu mgumu ili waweze kurudi katika hali ya kawaida na tuweze kushiriki nao tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumwambia Mheshimiwa Kibajaji kwamba wafugaji wana akili sana na ndiyo maana wafugaji hupiga ng'ombe wa nyuma ili wa mbele asogee, kwa sababu ukimpiga ng'ombe wa nyuma atawapiga wenzie pembe na wale wa mbele watakaza mwendo. Tuna kila sababu ya kumwambia Mheshimiwa Maghembe nini Watanzania wanapata shida na dhiki ya maji ili na yeye atakapoenda kwenye *Cabinet* aweze kuwaambia wenziwe Watanzania wana shida ya maji. Kwa hiyo yeye ni ng'ombe wa nyuma ndiye tutakayempiga ili awapige pembe ng'ombe wa mbele safari isonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongelea suala moja; miradi ya maji ni muhimu ikatekelezwa kwa haraka, fedha ikatoka wananchi wakapata maji kwa uhakika na wakaweza kujijendesha kimaisha. Kama Watanzania watapata maji safi na salama, Wizara ya Afya itapunguza wagonjwa wengi ambao wanapata magonjwa kutokana na kunywa maji yasiyokidhi viwango, wananchi wengi wanakunywa maji machafu. Ili kuondokana na tatizo hili ni lazima Wizara ya Maji ifanye kazi na kazi ya kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningefurahi zaidi kama wangeweza kunung'unika wananchi wanaotoka katika maeneo ya ukame. Lakini nasikitika sana wananchi wanaotoka maeneo ya maji, maji aliyoyashusha Mwenyezi Mungu bila ya gharama yoyote nasi tukisimama hapa tunalalamika masuala ya maji. Watu tunaotoka Kanda ya Ziwa tunahitaji maji Mheshimiwa Maghembe.

Waziri anapaswa kupeleka fedha katika ile miradi mikubwa ya Kanda ya Ziwa ili iweze kuisha kwa haraka. Mradi ulioko Mwanza upate fedha ya kumaliza ule mradi ili wananchi wa Kata ya Esangabuya waweze kupata maji. Mradi unaosuasua ulioko katika Wilaya ya Sengerema uweze kupewa fedha ya kutosha ili wananchi wa Sengerema waweze kupata maji. Mradi unaoendelea katika Wilaya ya Ukerewe upelekewe fedha ya kutosha, hatuna shida ya maji, shida yetu ni upatikanaji wa maji, tutayatoaje katika Ziwa Victoria na kuwafikia wananchi waweze kunywa maji salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niweze kumshukuru sana Mkurugenzi wa MWAMUWASA, anajitahidi kiasi kwamba anazungukia Mkoa wa Mwanza wote akitaka kuhakiki kabisa kwamba Mwanza inapata maji safi na salama. Lakini napenda kumwambia

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Waziri, fedha anazokusanya inaweza kukusanya MWAMUWASA haiwezi ikaendesha miradi ya maji katika Mkoa kwa Mwanza au katika Jiji la Mwanza. Ni vyema sasa wamuangalie maombi anayotoa, mikopo anayohitaji waweze kumuidhinishia na kuweza kumaliza tatizo la maji katika Kanda ya Ziwa hasa katika Mkoa wa Mwanza na Jiji la Mwanza kwa ujumla ikiwemo Wilaya ya Ilemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi uko katika Kata Bugogwa tangu Jimbo hilo likiwa na Mheshimiwa Diallo umewekwa mradi wa maji pale ambao mpaka sasa wamejenga vibanda, siyo vioski, wamejenga vibanda karibu ya Ziwa kabisa wameshaweka mitambo ndani ya Ziwa, lakini mpaka leo ule mradi haujulikani. Nimeshamchukua Mkurugenzi wa MWAMUWASA nimeenda kumwonesha. Tunaomba mumphe hela amalizie ule mradi, la sivyo vile vitu vitadondoka pale, yale majengo hayana maana kukaa pale bila ya kufanyiwa kazi. Wananchi wa Kata ya Bugogwa wanahitaji maji hawawezi kuyaona maji, hawawezi kulinda Ziwa Victoria, lakini maji yanakwenda Shinyanga na Tabora, hatukatai ni ndugu zetu, ni wenzetu, lakini anayepika sharti ale kwanza, aonje hata mchuzi una chumvi au hauna chumvi.

Ili wananchi wa Mwanza waondokane na dhima hiyo kama ninyi Wizara ya Maji mtakuwa kweli mnawatendea haki ni kwamba muende mkawamalizie ile miradi yote iliyokwama ili angalau na wao wajisikie kwamba wanalinda Ziwa Victoria na wao wana haki ya kunywa maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu, aibu maji yako pale unayaangalia kama jua ni aibu. Aibu unakunywa maji ya kisima ukipiga hatua 15 unakutana na Ziwa Victoria, ni aibu. Ili kuondokana na aibu hii namwomba Mheshimiwa Waziri, hasa Naibu Waziri, ninakuomba Mheshimiwa Naibu Waziri uje Mwanza tufanye kazi tushirikiane na wewe kwa sababu ni Waziri mpya katika Wizara hii na Naibu Waziri aliyepita hapo alishirikiana na sisi vizuri tuliweza kuvuka tulipotoka kwa sababu Waziri wako kidogo nahisi matatizo yapo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 nikiwa kwenye kampeni nilipita Kata moja katika Mkoa wa Lindi inaitwa Kata ya Chikonje, pale nilipata kuona machungu mpaka machozi yalinitoka. Haiwezekani Kata ya Chikonje, Kijiji cha Chikonje ni eneo kama hili, lakini kila mtu amechimba kisima chake, kila mmoja amechimba kisima ambacho akiingia yeye anaishia mabegani na kila mmoja ana kisima chake na eneo ni hilo moja. Kama kunatokea uadui wa kifamilia mtu kumwondoa mtu ni rahisi kabisa. Lakini mpaka leo hali ni ile ile.

Lindi mmeshasema kwamba maji ya Lindi ni mengi, tunawaomba sasa yale maji mfikirie ile Kata ya Chikonje, ilikuwa katika Jimbo la Mchinga, lakini sasa Kata ya Chikonje imerudishwa Jimbo la Lindi Mjini. Limetoka kule kwa yule na ndiyo maana watu wanasema hapa kuna u-CCM, CCM achene. Ile Kata ilikuwa Jimbo la Mchinga, mmeirudisha huku kwenye Jimbo la Lindi Mjini ambalo linaongozwa na Mheshimiwa Barwany. Tunawaomba muende Chikonje mkaangalie madhara wanayopata watu wa Chikonje na ikiwezekana muwagharimie kuwapiwa afya zao, nina mashaka na afya zao. Kwa sababu haiwezekani mtu anachimba kisima cha kuingia ameishia mabegani, halafu akaweza kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuongelea kidogo kuhusiana na mradi wa maji ambao unataka kuanzishwa katika eneo la Nyasaka. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri na ninamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri aje tutembelee hilo eneo na kama kuna maombi yoyote Wizarani kwenu muweze kuyapitisha ili wananchi wa Mwanza hasa Jimbo la Ilemela jamani wapate maji kwa urahisi. Kuna 9, Kata 6 zote zinaguswa na Ziwa Victoria. Eneo la Kirumba, eneo la Ibanda tupande na Mheshimiwa Waziri ukajione.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanjale! Jiandae Mheshimiwa Shekifu.

**MBUNGE FULANI:** Ah, mimi nimekosa leo!

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia pia katika hoja hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati Waziri wa Maji anawasilisha hotuba yake hapa alikuwa ametugawia vitabu vidogo ambavyo vilikuwa vimebainisha vijiji ambavyo vitapewa maji, lakini mwaka huu naona vijiji hivyo havipo. Pamoja na kwamba vijiji hivyo bado havijakamilisha kazi yake lakini ingelikuwa ni muhimu pia kwa bajeti hii ambayo inaendelea tupewe, tujue ni vijiji vipi ambavyo vinaingia katika mpango wa kutekelezwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mwaka jana tumekuwa tulipewa orodha ya miji midogo ambayo ingepewa iboreshewe maji na hotuba ya mwaka huu sijaona, nimeona Wilaya ziko pale chache, lakini Wilaya ya kwangu ambayo ilikuwa ni miongoni mwa Wilaya ambazo zilikuwa zimepangiwa ziboreshewe maji haipo kama Mbalizi. Mbalizi ni mji mdogo ambao kwa kweli miundombinu ya maji ni ya mwaka 1970 na kitu na mpaka leo inatumika hiyo hiyo, nilikuwa naomba labda Waziri anapomalizia aniambie je, mji huu itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maji inayopangwa ni ndogo sana na nilifikiri kwamba labda hii Wizara ingeangaliwa vizuri zaidi kama ambavyo Wizara zingine zinaangaliwa; miundombinu, usafirishaji. Maji ni uhai hii ilikuwa ni kaulimbiu ambayo ilitokea nyuma huko hasa uongozi wa Mwalimu Nyerere na kwa kweli walijitahidi sana baada ya kaulimbiu hiyo, Serikali ilijitahidi kusambaza maji kwa vijiji vingi na vijiji vingi vilipata maji.

Nafikiri ni muhimu tuweze kuirudia kaulimbiu hiyo kwa sababu kwa kweli maji ni uhai ndiyo yameshika uhai wa binadamu. Mtu akinywa maji mabaya, machafu ambayo hayana kiwango, atapata magonjwa na mwisho anaenda kutibiwa, fedha nyingi sana zitatumika, Serikali itaagiza dawa nyingi kwa ajili ya kuhakikisha inawahudumia watu wake. Kwa hiyo nilikuwa nafikiria kwamba huu ndiyo wakati muafaka ambao Serikali ijaribu kufikiria namna gani iboreshwe fedha au kutenga fedha kwa wingi kwa ajili ya Wizara hii, maana hata mwaka jana pia tulikuwa tumeangalia ile bajeti iliyopangwa, lakini bajeti tuliona kwamba ni ndogo na baadaye tukaiomba Serikali itafute vyanzo vingine, njia nyingine ya kupata fedha zaidi na zikatengwa shilingi bilioni 184.5 ili zisaidie kusambaza maji katika maeneo mbalimbali, lakini fedha hizo pia hazikutolewa. Nilikuwa naomba jamani fedha za maji zikiamuliwa kwamba zitengwe, fedha za maji ziwepo kwa sababu maji huko vijijini ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati ndugu yangu wa Upinzani Mheshimiwa Sakaya pale anawasilisha hoja hii ya maji, alijaribu kuvitaja baadhi ya vijiji vyangu vingine, ukiangalia katika kitabu chake Ilota pale watu wanapata tabu kweli kweli ya kupata maji. Unaenda kule Mjere ambako Rais alipopita wale watu walisimamisha gari wakamlilia wakasema Mheshimiwa hapa sisi tunakufa kwa maji, lakini Mjere mpaka leo na Rais anamaliza miaka yake maji hayapo. Nilikuwa naomba Wizara iangalie vijiji hivyo, wale watu wanapata tabu sana. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri unaweza kusema baadaye kitu gani ambacho utafanya, kwa sababu kwa kweli maji vijijini ni tabu na shida na nafikiri wakati mwingine pengine unaona Serikali haiko *serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niipongeze Serikali kwa upande mwingine maana siwezi kulaumu tu. Kuna miradi ambayo mingine ya fedha za Benki ya Dunia inatekelezwa, lakini fedha zake bado hazijafika, zinaletwa kidogo kidogo sana. Nilikuwa nafikiria, maana miradi hiyo inatakiwa iishe mwezi Juni mwaka huu yaani mwezi huu ili mwaka kesho tuanze na vijiji vingine.

Sasa hivi vijiji ambavyo tunashukuru Waziri Mkuu juzi alisema kwamba zitengwe fedha haraka sana kwa ajili ya kutekeleza vijiji hivyo. Sasa nilikuwa naomba hizo fedha zingefika haraka kwa sababu wale watu, makandarasi wanadai fedha wanataka kuishitaki Serikali au

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Halmashauri kwa sababu ilichelewesha kuwalipa na wengine wameshafikia 80%, 60%, 20%, 10% na wengine wametoroka kwa sababu Serikali haitoi fedha kwa wakati wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri unapohitimisha basi tuweze kuona kwamba hiyo fedha itaingia lini na nafikiri kwamba ni muhimu ingeenda mapema kabla ya miradi mingine au vijiji vingine havijapewa tena fedha.

Nilikuwa naomba vijiji hivi vingine utekelezaji wa mwaka unaokuja tungepewa vijiji hivyo ni vijiji vipi ambavyo mradi wa maji kwa fedha ambazo mnatenga utatekelezwa na sina hakika kama fedha iliyopo kwa kweli itatosha kutekeleza katika vijiji ambavyo viko *phase* ya pili ya Benki ya Dunia. Nilikuwa naomba sana hiyo iangaliwe kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa nashangaa kwa upotevu wa maji, pale Mbeya walisema asilimia 36.16 maji yanapotea bure wakati watu wengine huko vijijini wanahangaika na maji. Hivi hakuna mpango wowote wa kuweza kudhibiti hali hiyo? Nilikuwa naiomba Serikali iangalie namna gani maji kiasi hicho yanapotea yaweze kudhibitiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Shekifu! Jiandae Mheshimiwa Hussein Nassoro!

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kukushukuru, lakini pia nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wote ambao wamefiwa na ndugu zao na nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Maji. Ninajua hali anayofanya kazi ni ngumu lakini Waswahili wanasema ukiona mchungwa unapopolewa, basi machungwa yake matamu. Kwa hiyo unavyoona tunakusukuma hivi ni kweli kwamba unahitajika utusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nije katika kuchangia. Asubuhi Waziri alipokuwa anajibu swali langu, nimshukuru kwanza kwa yeye mwenyewe kuamka na kunjibu. Nihakikishe kwamba ilikuwa nishike shilingi, lakini kwa majibu ya matumaini ambayo Waziri ametoa sina nia na sina shabaha.

Nianze kwa kuizungumzia miradi hii ili Waziri aielewe vizuri na nianze kwa kusema hivi, mabadiliko ya tabianchi yameleta majanga hata katika maeneo mengine ambayo hatukuzoea majanga hayo. Tunaotoka milimani hatukuzoea sana uhaba wa maji kwa sababu maji yanaporomoka kutoka milimani. Lakini kwa sasa tunayo matatizo na ndiyo maana tumeshituka sana.

Sasa nikushuru wewe Mheshimiwa Waziri kwa ahadi yako kwa kutoa ufumbuzi wa maji mji wa Lushoto. Nieleze tu kwamba bila ya kujenga lile tanki kubwa ambalo liko kule Magamba Coast, bado tatizo la mradi wa Lushoto na kuondoa tatizo la maji mji wa Lushoto litakuwepo. Tunaomba sana kama ulivyoahidi asubuhi ulizingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tunahitaji taarifa ambayo inahusu upatikanaji wa maji kwa kuondoa tatizo la maji mjini Lushoto kwa kudumu kupitia mradi huu wa *Water Sector Programme* ambao unalipiwa na *World Bank*. Tunataka tujue hivi huu mradi umefikia wapi? Ni lini tatizo la maji mji wa Lushoto litamalizika? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika eneo lingine ambalo kwa sababu nakwenda kwa haraka haraka, naomba nichangie ule mradi wa pili niliuzungumza.

Wananchi walichanga na baada ya kuchanga ndiyo wakaanzisha mradi ambao wameuita na kama ulivyosema *Mtumbi Water Project*. Mradi ule unakwenda katika maeneo muhimu sana katika jimbo la Lushoto. Mradi huu utakwenda katika Kata ya Malibwi, vijiji vya Malibwi, Mbwei, Muhezi, Tambwe mpaka Kwemashai, siyo Kwemashai kuna msitu ambao upo

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

karibu na Tambwe. Lakini mradi huo pia utakwenda vijiji kata ya Kwekanga, vijiji vya Kwekanga yenyewe, Mziragembei, Mshangai, Kaubombo, Kamgogolo na Mateo.

Tunaomba pia tupate maji katika kata ya Makanya. Tatizo ni kubwa katika Kata hili. Hatujajiombea rasmi, lakini naomba mradi huu ukishatekelezwa uhakikishe kwamba mradi wa Kata ya Makanya unachukuliwa hatua. Kata ya Makanya ni Kata ambayo iko nyuma sana katika Jimbo langu na kweli Kata hii ina matatizo makubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia kwa urefu kidogo, ninalo pia tatizo katika Tarafa ya Lushoto. Kuna mradi wa Ngulwi ambao mradi huo ulianzishwa lakini mpaka leo haufanyi kazi, wananchi wanahangaika.

Mwisho, nasikia kengele imelia, nizungumzie mambo ambayo ningeishauri Serikali. Kwanza wenzangu waliunga mkono, suala la kuundwa Mamlaka kama REA itapewa fedha na waendeshe miradi ya vijijini ni jambo muhimu sana. Uvunaji wa maji hata kule milimani Lushoto kama tukiwezesha kujenga mabwawa madogo madogo, inawezekana kabisa tukapunguza tatizo la maji.

Lakini pia vilevile suala la Serikali kuweka utaratibu ambao kwa kweli utasaidia kuvuna maji hata maji yanayotolewa kwenye mabati katika maeneo ambayo miradi hii ikibuniwa na najua kule kwako Mwanga mna utaratibu wa mradi huu ambao unavuna maji kwenye maeneo kutokana na mapaa ya nyumba na maji haya yanasaidia, Serikali isaidie kuwasaidia wananchi kujenga matanki madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyazungumza maneno haya, mimi niombe Serikali na nakuomba sana Mheshimiwa Waziri ahadi yako ya leo kwa maji mji wa Lushoto, maji ya...

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Hussein Nassoro! Jiandae Mheshimiwa Mchuchuli, tunamalizia na Mheshimiwa Lembeli.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Lakini Waziri huyu kwa kweli tunamlalamikia, tujaribu kuangalia tatizo linaanzia wapi. Fedha zinapangwa na hazipelekwi, tutabaki kumlalamikia. Serikali ishushie fedha huko na baada ya fedha kuingia Wizarani ana haki ya kulalamikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana uliniahidi ukasema Jimbo la Nyang'wale kuhusu ule mradi wa kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria eneo la Nyamtukuza, pesa hiyo itapelekwa na maji hayo yatapatikana. Mwaka huo umeisha, mwaka wa fedha huo wa mwaka jana umeisha, sasa hivi tumeingia kwenye Bajeti ya 2014/2015, nimeona hapa pia tena umetupa shilingi milioni 780 na..., lakini pesa ya mwaka jana tulitengewa milioni 500 hatujuai ni kiasi gani cha pesa ambacho kimeishapelekwa.

Kwa hiyo, tatizo hili la maji kwa wananchi wa Nyang'wale ni tatizo kubwa. Nina Kata 12, hakuna hata Kata moja ambayo ina unafuu wa maji. Suala hili la maji tangu niingie bungeni leo nina mwaka wa nne kila mwaka ninazungumzia na na ninaahidiwa kwamba tatizo hili litaondoshwa. Tatizo hili halijapunguzwa na sitarajii kama litaondoshwa kwa mtindo huu.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Kama alivyomaliza kuchangia mchangiaji wa mwisho pale, alisema kuwa maji tunayo lakini namna ya kutafikisha pale inakuwa ni ngumu. Ziwa Victoria mimi ninalo ni kama nusu Kilomita, lakini cha ajabu kuanzia kijiji cha Mwanzo kutoka pale hakina maji. Nina vijiji 54 vyote havina maji.

Kwa nini Serikali isiweke mkakati na kuweza kusukuma fedha kwa haraka kuweza kuufufua ule mtambo wa kutoka Nyamtukuza ili kuweza kumaliza tatizo hili la maji? Mtambo huu ulikuwepo toka mwaka 1975, tatizo ni kufufua tu, lakini mashine ipo, mabomba yapo. Kwa nini Serikali isiende kufufua mtambo huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu, kuna mkandarasi ambaye amekuja hapo leo ana takribani miezi minane amejenga eneo la kuhifadhi vifaa vyake, lakini mpaka leo hii kazi hajaanza. Nimejaribu kumfuatilia Muhandisi wa maji anipe taarifa ya kwamba nini kinaendelea kuhusu huyo Mkandarasi, lakini cha ajabu Muhandisi huyo amenikwepa na wala hanielezi.

Sisi Wabunge kazi yetu ni kufuatilia na kuja kuishauri Serikali, Wahandisi wetu kama wanakataa kutupa taarifa tutashughulikia vipi haya masuala? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninakuomba baada ya bajeti hii uweze kutembelea, twende pamoja ukaangalie tatizo la maji lililo katika Jimbo langu. Kwa kweli tatizo ni kubwa na safari hii ninaunga mkono hoja ili uweze angalau basi kutushughulikia hili suala la maji tuweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliweza kunyahidi kwamba nitaweza kuchimbiwa takribani visima kumi. Lakini cha ajabu Wilaya yote, Jimbo langu langu hata kisima kimoja hakijachimbwa. Naomba sasa utakapokuja kujumuisha hapa uniambie, ni lini Serikali itatekeleza ahadi zake, kwa sababu hakuna hata kisima kimoja.

Leo hii kama alivyosema Mheshimiwa Lusinde, mnapokuja ninyi viongozi kule mnawekewa maji ya chupa pale, hamjui matatizo yaliyoko kule. Safari hii Mheshimiwa Maghembe utakapokuja kutembelea kule ama kiongozi yeyote wa Serikali tutakuja kumpa maji ambayo tunakunywa sisi wenyewe kule ili muelewe uchungu kwamba wananchi wanakunywa maji ambayo siyo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, mimi leo yangu ni kilio tu cha kwamba wananchi wa Jimbo la Nyang'wale wamenituma niunge mkono hoja ili labda inawezekana bajeti hii tukaweza kufikiriwa.

Mwaka jana nilisema kwamba siungi mkono hoja labda ndiyo adhabu hii ambayo nimepewa, safari hii nasema kwamba naunga mkono hoja ili angalau uweze kunifikiria Mheshimiwa Maghembe. Baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mchuchuli! Jiandae Mheshimiwa Lembeli!

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu ya kusimama hapa nikiwa salama. Lakini kipekee natoa pole kwa kaka yangu Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe kwa msiba mzito wa mama yake mzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina vyanzo vingi sana vya maji tuna maziwa, tuna mito, tuna mabwawa makubwa sana, lakini tatizo namba moja katika nchi yetu ukimuuliza kila mwananchi huko chini atakawambia ni tatizo la ukosefu wa maji safi na salama.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naishauri Serikali, kila siku wanatuambia maji, maji, maji, BRN kwenye maji, lakini hakuna kinachoendelea. Lakini pia hata *research* mbalimbali zinaonesha kwamba ni kwa jinsi gani tatizo la maji lilivyo kubwa katika nchi yetu. Kwa mfano *research* ya CINOVET ya mwaka 2009 imetuonyesha tatizo la maji katika nchi yetu.

Lakini Serikali kwa kweli bado haijakuwa na nia ya dhati ya kutatua tatizo la maji katikam nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya CAG inayoishia Juni 2013, CAG alihoji miradi ya maji ambayo ilikuwa bado haijatekelezwa kwa kipindi cha nyuma pesa takribani bilioni 57 zilikuwa zinahitajika kukamilisha miradi ya nyuma, lakini mpaka sasa hivi hakuna hoja iliyojibiwa wala hakuna hoja iliyotekelezwa. Kwa hiyo, tatizo la maji ni kubwa lakini Serikali haioneshi nia ya dhati ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji, Mheshimiwa Waziri mimi ninaomba hawa mnaoita wakandarasi washauri wawe basi wanawasikiliza wazawa wa maeneo husika wanapokwenda kufanya ile kazi za kuchimba maji. Kwa mfano kule kwangu mimi Mutete, Rufiji walipokwenda kuchimba maji kule watu waliwashauri wachukue maji kutoka Mto Rufiji, mto uko pale pembeni kabisa, lakini wakakataa wakaenda wakachimba kisima, kisima ambacho kina maji ya chumvi kupita kiasi. Sasa wananchi wa Rufiji, wananchi wa Utete wanashindwa kunywa yale maji, ukiyachota na kuweka kwenye ndoo yanakuwa kama vile yana kutu. Sasa nini maana ya kuwa na hao washauri? Wawe wanasikiliza maana kwa sababu sasa inaonekana wao wanajali sana maslahi yao, hawaangalii chanzo kipi kinaweza kikawafanya watu wakapata maji mazuri ila wao wanaangalia wao watabaki na nini mifukoni mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea kuwa na wakandarasi wa namna hii ambao wanaangalia nini kinabaki kwenye mifuko yao na siyo tija kwa watu ambao wanaenda kuwatekelezea mradi, hatutaweza kufanikiwa katika miradi yote ya maji. Kwa hiyo, mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri uangalie tusirudi nyuma kwenye miradi kama ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna tatizo wakati miradi ya maji inapokamilika ule mkataba baina ya mkandarasi na Serikali inakuwa haipo wazi kwa wale watu ambao wanakabidhiwa miradi, watu wa Kamati zile za maji.

Sasa unakuta mfano, mkandarasi alitakiwa kwenye mradi wa maji labda atengeneze pampu mbili aweke *generator*, lakini mradi unakuwa hauna hivyo vitu. Kwa mfano mradi wa maji wa Ukwiriri, ulitakiwa ufungiwe pampu mbili na jenereta kule kwenye *source* ya maji, lakini sasa huu mradi unakwenda kukabidhiwa hivi karibuni kwenye ile Kamati ya Maji, lakini ukienda kwenye kile chanzo hakuna hizo pampu mbili, hakuna hiyo jenereta. Sasa je, mradi kama huu unafikiri kwamba utadumu kwa muda gani?

Na tatizo hili ndiyo limesababisha mradi wa maji wa Kibiti kuwa sasa hivi unasuasua kwa sababu unakuta pampu inafungwa leo, baada ya mwezi mmoja inaharibika ile Kamati ya Maji inahangaika kwenda kutafuta matengenezo ya hiyo pampu, lakini hawafanikiwi, gharama inakuwa kubwa.

Kwa hiyo, mimi ninakuomba Mheshimiwa Waziri utuambie mradi wa maji wa Ikwiriri, mradi wa maji wa Kibiti, mradi wa maji wa Ikwiriri ulitakiwa kuwa na pampu mbili lakini una pampu moja, jenereta kule *site* haipo. Kwa hiyo tunataka tujue nini hatima ya mradi ule, kwa sababu hata kama utakabidhiwa kwa Kamati ya Maji, ina maana hautadumu kwa muda mrefu, watahinda kuendesha, kwa hiyo mambo hayatakuwa siyo mazuri sana.



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakandarasi wetu hawa mimi nilipata bahati ya kutembea na Kamati ya Serikali za Mitaa kwenye miradi ya maji. Kati ya miradi ambayo ina matatizo, kwa kweli miradi ya maji ina matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulimsikia hapa Mheshimiwa wa Longido hapa alikuwa ana *claim* hapa mradi wake ule maji hayapo lakini bado watu wakaenda kusambaza miundombinu wanasambaza maji gani wakati maji kwenye *source* hayapo? Kwa hiyo unakuta mradi unajengwa, kisima kinaonekana maji hayatoshi, lakini mkandarasi, watu wanachukua 10% wanasambaza mabomba kutoka kwenye chanzo, chanzo ambacho maji hayatoshi. Sasa unategemea unapeleka maji gani kule kwa wale wananchi wakati maji yenyewe kwenye kisima hayapo. Sasa watu wanaangalia tu wao wananufaika vipi, wao wanamaliza vipi kazi wanapata pesa zao, lakini hawaangalii wale ambao wanawatekeleza ule mradi wananufaika vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ni mingi sana lakini pia kumekuwa na siasa katika miradi ya maji. Mimi nimekwenda baadhi ya maeneo, unakuta mradi wa maji ambao ungeweza kuwanufaisha watu 3,000 unakwenda kujengwa kwenye Kata au kwenye Kijiji ambacho kinawanufaisha watu 200 tu. Mfano mimi nimekwenda Kilwa, Mitolwe kule kwa sababu tu Diwani, Mwenyekiti wa Halmashauri/Makamu Mwenyekiti ndiyo Kata yake, kapeleka maji sehemu ambayo ina watu 200, mradi wa watu 3000, mradi ambao umegharimu takribani milioni 200. Sasa *sustainability* ya maji inakuwaje? Baada ya wale watu 200 kupewa ule mradi badala ya watu 3000, wanautunza vipi ule mradi? Kwa hiyo, ninaomba muangalie sana hili, kuna siasa sana kwenye miradi ya maji.

Hatuwezi kufanikiwa kama kila kitu tutaweka siasa. Maji ni uhai, hivi mradi wa watu 3000 unapeleka kwa watu 200 ili tu uoenekane kwamba ukisimama unasema mnaona nimewaletea maji! Nini tija yake? Nani anachangia gharama za kuitengeneza kama vitu vikiharibika? Kwa hiyo, ninamuomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo kwenye miradi ya maji hasa kule miradi inapotekelezwa.

Bado narudia palepale kwamba miradi ya WSDP, CAG alishauri, kwa mfano Kilwa ilitakiwa wapate takriban bilioni tatu ili miradi yao ya maji iweze kukamilika, lakini bado ni hadithi, chenga tu, Lindi bilioni 200, hadithi chenga tu. Sasa tunafanya nini Mheshimiwa Waziri? Tunapitisha bajeti, bajeti haitoshi, mnakuja hapa tunalia tunaongeza bajeti na bajeti haitoki. Hivi ni Serikali ya aina gani? Hii Serikali ya CCM kweli ina nia nzuri ya kuwapatia maji Watanzania?

Kwa mfano maji Dar es salaam niwaambieni, Mheshimiwa Rais alisema atakutana na DUWASA, sijui na nani ili kutatua tatizo la maji Dar es salaam, mpaka leo chenga tu, Rais hajafanya hilo, maji Dar es salaama bado ni shida, bado tunaendelea kuwahidi Watanzania. Sasa hivi Kinana anapita anahidi watu, aa maji hapa! Nini? Hivi kila siku ni ahadi, ahadi ambazo hazitekelezeki? Mwambieni Kinana aache kuwahidi Watanzania uongo maana mmeshindwa kutekeleza miaka yote, sasa hata akiahidi leo hii kesho ni uchaguzi, lengo ni kupata kura?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusiwe tunaahidi miradi ambayo hatuwezi kutekeleza. Mimi ninawashauri watu wa CCM, maji ni uhai, tukipata maji safi na salama magonjwa yatapungua. Wewe mwenyewe Mheshimiwa Makalla unaweza kuja hapa bila ya kuoga bwana? Kwa hiyo, mimi ninawashauri tuwe na nia ya dhati ya kutatua tatizo la maji katika nchi yetu tupeleke pesa za kutosha kwenye miradi ya maji, tuache hadithi, tuache *story* Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia usimamizi, wale watu wa maji ambao wako Wilayani Wahandisi wetu na wengineo nawaomba usimamizi uwe ni usimamizi wa uhakika kwa sababu nao pia wanatuangusha sana, wanafanya miradi mingi ishindwe kutekelezeka na kuleta tija kwa wananchi.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yangu ni hayo, nawashukuru sana. Lakini Mheshimiwa Waziri uende Ikwiriri ukajue tatizo la maji ya pampu na Kibiti uende. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lembeli, mchangiaji wa mwisho kwa mchana huu.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipa ili na mimi niweze kuchangia kwenye mada hii. Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina maneno mengi, nina mambo mawili ambayo nitamuomba sana Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha ayafafanue, vinginevyo hatutaelewana.

Moja, maji kutoka Ziwa Victoria kuja Kahama, tunaishukuru Serikali tatizo la maji ambalo limekuwepo kwa muda mrefu sasa halipo. Lakini maji yale yako eneo la katikati ya Mji wa Kahama tu. Mitaa na maeneo ya viunga vya Mji wa Kahama hayana hayo maji. Na jambo la kusikitisha pale yalipo matanki yale makubwa yanayohifadhi maji kutoka Ziwa Victoria wananchi walipisha ili matanki hayo yaweze kujengwa pale, wale wananchi hawana maji maeneo ya Shunu, Malunga, Lugela, Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo ya ajabu sana maji yanatolewa pale Mjini yanapelekwa Buzwagi, wananchi wanaozunguka Mgodini ule hawana maji, wanatembea kilomita sita/saba, hakuna maji. Sasa mimi nilikuwa nasoma hiki kitabu ukurasa wa 77, miradi ya maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka katika miji mbalimbali, nasoma kipengele kinachohusu yale maji yaliyoko pale Kahama.

Vilevile maji yatapelekwa miji ya Kagongwa, Isaka, Tinde na nasikia sijui Tabora na Bukene. Sasa haya ni mambo ya ajabu sana, unatoa maji Kahama Mjini unapeleka Tinde, unapeleka Bukene, wananchi wale wanaoishi nusu kilomita kutoka yalipo yale matanki hawana maji. Vitu vya ajabu sana. Na hapa wametenga shilingi bilioni nane, Nitataka kujua Mheshimiwa Waziri atuambie/ aniambie na watu wa Mji wa Kahama wasikie hizi bilioni nane pia zitatumika kusambaza maji katika maeneo ya Mji wa Kahama? Vinginevyo hii ni hadithi maji haya yako kwa ajili ya watu wachache katikati ya mji pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji haya haya, urasimu katika *connection* wananchi wanahangaika sana, wanatozwa pesa, wanapotaka kuunganishiwa maji, kero. Mheshimiwa Waziri, hili naomba pia ulizungumze. La pili, maana leo sina maneno mengi. Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia. Wilaya ya Kahama tuna Majimbo mawili, Jimbo la Msalala na Jimbo la Kahama.

Naongelea Jimbo la Kahama. Jimbo la Kahama lina visima vitano, nashukuru Mungu vijiji viwili mradi huu uko katika hatua za mwisho, Kijiji cha Shaka na Kijiji cha Nyamelangano, ujenzi wa miundombinu uko katika hatua ya mwisho. Sasa tatizo langu ni kwa vijiji vile vingine vitatu, Kijiji cha Uloa, Kijiji cha Mbika na Kijiji cha Iboja, wamekuja watu mimi ninawaita ni matapeli, wamepima na kusema hapa kuna maji, kaja mtu mwingine akawaambia hakuna maji.

Sasa miaka kumi wananchi hawa kila siku wananiuliza Mheshimiwa Mbunge vipi? Mheshimiwa Waziri mimi nataka kujua na hatima kwa sababu mradi huu unafikia mwisho, inamaana wananchi hawa wa vijiji hivi vitatu wametapeliwa? Na kama ni kutapeliwa wametapeliwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ambapo mimi ni Mbunge wake. Sasa Mheshimiwa Waziri nitapenda kupata majibu.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo sina maneno mengi sana, lakini majibu yako ndiyo yatanifanya niunge mkono au nisiunge mkono. Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo; ninaomba kuwatangazia Wabunge kuwa Shirika la *PSI* Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wanafanya maonesho mbalimbali ya huduma za kiafya na kutoa maelezo juu ya mambo yafuatayo katika viwanja vya tafija vya Bunge:- Malaria na namna ya kujikinga, uzazi salama na UKIMWI, kansa ya shingo ya kizazi, dawa za kupunguza kutokwa na damu wakati wa kujifungua. Wabunge wote mnakaribishwa kuanzia tarehe 2 hadi 4 Juni, kujifunza juu ya huduma hizo.

Waheshimiwa Wabunge, jioni mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Rose Kamili, Mheshimiwa Mbarouk Ali, Mheshimiwa Mfutakamba na Mheshimiwa Makilagi. Naomba kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi Jioni.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nilitaja majina ya watu watakaoanza. Tunaanza na Mheshimiwa Rose Kamili; ajiandae Mheshimiwa Mbarouk Ally, Mheshimiwa Mfutakamba na Mheshimiwa Amina Mwakilagi. Mheshimiwa Rose Kamili!

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia, lakini pia niungane na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa Waheshimiwa Zitto Kabwe na Martha Mlata kwa kupoteza wazazi wao wapendwa na Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Wizara hii imetengewa fedha ndogo sana ambayo kwayo ilitakiwa itolewe bilioni 312, matokeo yake wakapata bilioni 86, ni kuidhalilisha kwa sababu kwanza kabisa ipo kwenye mpango wa *BRN* na kama ipo kwenye mpango wa *BRN* ni kwa nini Wizara ya Fedha haikuweza kutekeleza wajibu wake? Haya majibu nitayahitaji na nitaomba Mheshimiwa Waziri aweze kutupatia haya majibu kwa sababu karibu kila Wizara hayo yamejitokeza. Lakini

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda kuzungumzia suala la usimamizi mbovu wa Wizara hii kutokusimamia vizuri fedha ambazo hata kama ndogo zimepatikana. Nikianza moja kwa moja namna walivyotoa fedha. Niangalie kwa upande wa Wilaya ya Hanang, fedha zilizotolewa kwa Wilaya ya Hanang kwa Wizara ni sh. 1,000,092,484/=, lakini cha ajabu Halmashauri ya Wilaya ya Hanang hiyo hiyo inasema kwamba imepokea sh. 478,368,353/= halafu na bakaa sh. 126,981,042/= . Kwa hiyo, jumla ina sh. 600,005,449/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza na naomba Mheshimiwa Waziri atujibu, mwizi na Mheshimiwa Waziri au ni Halmashauri ya Hanang kwa sababu kama Wizara imetoa bilioni 1.9, halafu Halmashauri inasema ina milioni 600, hivi nani mwizi? Hapo napenda kujua hili lipo kwake Mheshimiwa Waziri. Tumejaribu kulalamika sana kila wakati kumweleza Mheshimiwa Waziri suala la kwamba fedha zetu zinatumiwa vibaya katika Halmashauri zetu, yeye anawatetea, sasa atujibu leo kwenye kikao hiki, je, nani amepoteza hizi fedha hapa katikati, yeye au Halmashauri ya Hanang?

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kuzungumzia suala la ahadi ya Rais. Napenda kufahamu, je, fedha hizi bilioni 1.9 zilizotolewa zipo pamoja na ahadi ya Rais au ahadi ya Rais ni nyingine? Kwa sababu nafahamu kwamba tulitenga sisi wakati ule sh. 1,000,092,000/= 2013/2014. Sasa hivi wanazungumza kwamba kuna ahadi ya Rais, ahadi ya Rais hesabu yake iko wapi na je, ni nani anasimamia hizi fedha za ahadi ya Rais kwa ajili ya utekelezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa sababu Mheshimiwa Waziri anakumbuka nilimweleza eleza matatizo ya Hanang wakati fulani. Leo nakueleza fedha za Rais zimetolewa sh. 337,000,000/=, lakini kule mpaka leo hela zote zimetumika, lakini bado Mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati wa Bunge la Katiba Mheshimiwa Waziri alisema atakwenda kufungua ule Mradi, lakini namweleza kwamba mpaka hivi sasa ninavyoongea hapa ule Mradi bado. *Pipe* zinapasuka, hivi hizo *pipe* zinapasuliwa na nini? Kama ndio hiyo *pressure* ya maji, kama *pressure* ya maji inaonesha ni 21 inatakiwa *size* za *pipe* ziwekwe ni 21, lakini wanakuja kuweka 16, haoni kwamba wataalam wakw sio wazuri na kwa nini anawabembeleza na kuwatetea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wanaharibu hizo hela milioni 337, *pipe* zimepasuka zaidi ya kilomita tatu, nani analipa hizo hela? Je, ni Halmashauri ya Hanang? Kwa hiyo itoke kwenye Mfuko gani? Napenda kujua hela za Rais zimetumika asilimia 95 na *pipe* zimepasuka na Mradi haujafika Katesh, nani anaufikisha huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya majibu nayahitaji kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na kama ni hivyo pia ninachohitaji ni kwamba, atuambie huyu Mtaalam wake ambaye ni Mhandisi atamfanya nini? Awaambie Watanzania hapa kwamba Wahandisi ni wabovu kwa sababu wanafanya makosa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu mgao wa fedha, naona muda unakimbia. Wabunge wengine wamezungumza habari ya mgao wa fedha kwamba kuna upandeleo na nataka kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka jana kwenye bajeti mimi mwenyewe nilizungumza suala la bajeti, Mwanga mmepata bilioni 57, sio bilioni moja! Maana yake bilioni 56.1 ilikuwa ni hela ya Mradi uliochangiwa na OPEC na wenzetu wale wengine waliochangia ambaye ni bilioni 56.1 tulipitisha sisi. Halafu pia kukawa na hela bilioni moja, zingine jumla bilioni 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atuambie miradi yake kule inakwendaje? Kwa sababu huku kwetu yeye anakwenda kuzindua zindua atuambie na kwake inakwendaje, imekamilika au ni nini kinachotokea? Sasa tunasema mgao huo sio sahihi kwa sababu Wilaya ya Hanang, ametenga milioni 856, hivi itatosha nini kwa Watanzania hao wa Hanang ambao Wilaya ile ni kame, hakuna visima vya kutosha, watu wanachota maji mbali, je, tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri akabadilisha bajeti yake. Hizi bilioni moja za Mwanga, bilioni 1.6, naomba azipeleke Hanang ziungane kwenye milioni 800 ili na sisi tukomboke. Yeye ana bilioni 57, hajamaliza bado, tayari anataka zingine! Hivi ni kwa nini hatuonei huruma sisi Watanzania pia tukapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Hanang haina maji, tuna Vijiji 63, tuna Kata 25, ni Kata kama tano tu ndio zina maji, lakini Vijiji havikutimbia hivyo 53 karibu havina maji, je, sisi tutafika wapi? Tunasema eti tumetimiza asilimia 74, sasa hivi kwenye huu mpango wa maji umevuka, umevuka wapi? Anevuka yeye Mwanga, lakini sisi kule hatuna maji!

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anadanganywa, naomba kabisa tufuatane na yeye. Nilimwomba siku ile kwamba tufuatane pamoja twende tukaangalie Wilaya ya Hanang kama kuna maji. Anadanganywa visima vingine ni hewa, vimechimbwa, hakuna maji, lakini hela za Watanzania zimetumika. Mheshimiwa Waziri namwomba kwa hili alione sana na alifuatilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumza suala la ahadi hizi zinazosemwa na Katibu wa CCM. Napenda kuzielewa anapita kila Wilaya, Kijiji anaahidi maji, hivi tuambieni Katibu wa CCM ahadi anazotoa ni hizi hela tunazotenga sisi Wabunge au ana zingine maana yake tufahamu. Tunashindwa kuelewa kule kwamba mnasema tunapewa ahadi kwamba tutaletewa maji, nitaifuatilia na kuiagiza Serikali. Sisi tunashindwa kuelewa yeye ana maji au ni hizi hela ambazo Bunge tunazipitisha. Kama ni hela hizi Bunge tunazipitisha asidanganye Watanzania hizo hela hazitoshi na hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk Ali!

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ili kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba kuna jambo linanitia uchungu sana ninaposikia Profesa na Naibu wake wanaitwa ni mizigo, kwa sababu wote nawafahamu Profesa ni Mwalimu wangu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarouk, humu ndani tunatambuana kwa vyeo na nafasi tulizokuwa nazo. Nakuomba tuelekeze kwenye hoja, ni Waziri wa Maji kama ana upungufu sema upungufu wake. Haya majina mengine ni majina ambayo hayatumiki ndani ya Bunge hili nakuomba.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nataka kuwaambia tu Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mizigo ni hilo dubwana ambalo wamelibeba la Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambalo haliendi mbele. Sasa nawashauri tu kwamba uchaguzi unakaribia, waje tu kwenye kambi nafikiri tutawatafutia Kurugenzi, watafanya kazi vizuri tu na hawataonekana kwamba ni mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ambalo nalihisi la Serikali hii ni utekelezaji wa Sera na Sheria ambazo zimepitishwa na jambo hilo hilo utalikuta katika maji. Inakuwaje kwamba maji yatoke yalikutoka tuseme Ziwa Victoria yafike mpaka Magu, lakini Mwanza Mjini hakuna maji? Kuna maeneo mengi ya Mjini Mwanza hakuna maji, sasa inakuwaje na Sera zinasema kwamba popote pale ambapo itapita nyaya ama nguzo za umeme, basi vile Vijiji ambavyo vinapitishiwa bomba zile waweze kufaidika na huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha ni kwamba, huduma hiyo haipatikani kwa Vijiji ambavyo vimepitiwa na bomba hizo za maji. Nikienda huko huko kwenye Sera na Sheria, Sera ya 2002 ya Maji na Sheria ya mwaka 2009 ya Maji, kwa kweli haina usimamizi madhubuti kwa sababu Sera inamaanisha wazi kwamba kuna hizi Jumuiya za watumiaji wa maji ambazo ni Jumuiya huru na ambazo zinatakiwa ziwe na mamlaka kamili na ziwe huru katika utendaji wake wa kazi hizi, lakini la kusikitisha Jumuiya hizi mpaka leo hii hazina fedha za kiutendaji, lakini pia hazina vyombo vya usafiri, sasa sijui kazi hizo wanaweza kuzifanya vipi?

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hapo ndipo Wizara hii inapofeli na hata tuwe na maji kiasi gani kama tutashindwa kuzitumia Jumuiya hizi kwa kweli maji bado itakuwa ni tatizo na itakuwa ni migogoro mikubwa na hayatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye mada yangu nyingine ya pili ni kwamba, hadi sasa Serikali inaonekana kwamba imejikita zaidi katika upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na usafi wa mazingira, lakini tumesahau kabisa wakulima wadogowadogo na hilo ni tatizo kwa sababu kuna sehemu nyingi ambazo kwa miaka yote Serikali imekuwa ikitoa misaada kwa ukame na njaa kwa baadhi ya maeneo hususan maeneo kame kama vile Dodoma, Same, Kilimanjaro na baadhi ya maeneo, lakini bado tunashindwa kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya tabianchi, tuhakikishie tu kwamba, hili zoezi la kutoa misaada kwa watu ambao wanafikwa na kadhia za njaa na ukame na jinsi tunavyokwenda kwa kweli linaweza likaendelea. Kwa sababu kuna maeneo ambayo yana mabwawa ya muda mrefu, lakini mabwawa hayo ni machakavu, lakini Serikali haionekani kuchukua juhudi za ziada kuyatengeneza mabwawa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna maeneo ambayo hayana mabwawa kabisa lakini kame, kulikuwa kunahitajika teknolojia rahisi tu ya kuwawezesha wakulima na wafugaji ili waweze kutekeleza na kupata maji kiurahisi na Serikali iwasaidie ili waweze kuzalisha na waondokane na ukame na matatizo ya njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kuna Miradi zaidi ya 78 ambayo iko mbioni kutekelezwa na Wizara hii, lakini utaikuta miradi hiyo ipo katika maeneo nyepenyepi yaani tumesahau kabisa huwezi kuikuta Miradi hiyo Dodoma, Same wala Kilimanjaro yale maeneo ambayo ni kame, lakini utakuta ni yale maeneo ambayo yana maji mengi. Kwa hivyo tunafuta ule rahisi tu na tunasahau kwamba watu wanaoishi katika haya maeneo pia na wao ni wapiga kura wetu na ni ni Watanzania wenzetu pia wanahitaji hizo huduma za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naisisitiza sana Wizara kwamba, pamoja na uhaba wa pesa ambayo wamepata, lakini hayo maeneo pia na wao wayaangalie kwa kiasi kikubwa. Kwa hayo, machache naomba nichangie tu hayo kwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mfutakamba, ajiandae Mheshimiwa Makilagi!

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wenzangu kuwapa pole ndugu zetu Zitto Kabwe na Martha Mlata kwa kufiwa na wazazi wao wapendwa, Mungu aziweke roho za marehemu peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mada. Jimbo la Igalula lina Vijiji 96, lakini ni Vijiji tisa tu ndiyo vina maji, kwa hiyo, tuna chini ya asilimia kumi, kwa hiyo, katika kila Wanaigalula kumi na moja ni Mwanaigalula mmoja tu ndio anayekunywa maji safi na salama. Hii ni hatari kubwa sana. Pamoja na kupongeza Wizara kwa mradi wa *World Bank* kutoa Vijiji, kuchimba Visima Vijiji vya Lutola, Miswaki, Mwakadala, Malongwe, Kizengi na pia pesa za kuchimba Visima Sekondari ya Goweko na Lutende na pia *JICA* kutoa Mradi wa Mpumbuli, lakini Vijiji vyote tisini na moja havina maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni tete sana lakini pia tuna tatizo Mheshimiwa Waziri alishatembelea pale Isikizya Makao Makuu ya Wilaya. Serikali imewekeza majengo, inajenga sasa hivi Kituo cha Polisi, Makao Makuu yako pale, lakini chanzo cha maji kimekauka. Tunaomba ingawa TUWASA (*Tabora Urban Water Supply Authority*) wao wamekubali kusaidia,

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

lakini Mheshimiwa Waziri atenge pesa ili pia Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui waweze kupata maji, Makao Makuu yako kwa Mbunge jirani yangu Mheshimiwa Sumar, lakini ni Wilaya yetu moja, lakini na sisi tuna utaratibu wa Halmashauri mbili, Halmashauri ya Igalula na Uyui. Baadaye Igalula naamini itakuwa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa hali ya maji tatizo ni kubwa sana, tunaomba pesa za kutosha zitengwe kwa ajili ya Jimbo la Igalula. Jimbo la Igalula study ya Profesa Sykes, ameeleza kwenye study yake ya chandarua kimoja kwa Mtanzania mmoja ni kwamba, Wilaya ya Uyui ndiyo Wilaya ya mwisho katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kimaendeleo na ni Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba sana huu Mradi wa Maji unaotoka Ziwa Victoria upite pia katika Vijiji vilivyo jirani, Vijiji vya Kigwa, Mbuyuni, Zingala, Igalula Barazani, Utundaukulu, Chabutwa, Imalakaseko na Kalumwa. Tatizo la maji ni kubwa na ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kimoja nipendekeze, moja ya tatizo kubwa tulilondalo ni kwamba tumeharibu sana mazingira. Miti imekatwa karibu Jimbo zima la Igalula. Wako ndugu zangu wanafuga, lakini pia wanalima, nawakaribisha kwa sababu ni wapigakura wangu, lakini mazingira yameathirika sana. Sasa ningeomba Wizara ya Maji, Wizara ya Mifugo, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira zishirikiane pamoja na TAMISEMI, utaratibu wa kupanda miti na kuokoa sehemu oevu ambazo chepechepe zimepotea, Mito yote Jimbo la Mgalula imepotea na kama hatutunzi hivi vyanzo vya maji, ukame utaendelea kukua kwa kasi kubwa na litatokea tatizo hata la upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwiano wa miti na hidrolojia ya maji. Miti ni pampu ya asili inavuta maji kutoka ardhini, inapeleka kwenye mawingu unapata mvua. Sasa kama hatupati msaada wa kutoa elimu kwa wananchi wetu ili kuweza kupata vyanzo vya maji virejee, misitu nayo iwepo, mvua za kutosha zipatikane, tatizo la maji litaendelea kutukabili nchini miaka hii na ijayo.

Mbunge amejitahidi kwenye Mfuko wa Jimbo, nimechimba visima vitatu, Mienze, Migomgwa na Nsololo, lakini bado nina tatizo kubwa kwenye Kijiji changu cha Mabondo. Maji yako hali mbaya, Misaki kweli maji yametoka, lakini kuna chumvichumvi nyingi wananchi wanashindwa kuyatumia yale maji vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana, Mheshimiwa Waziri alitazame Jimbo la Igalula kwa jicho la huruma. Vijiji tisa kati ya Vijiji 96 hali ya maji ni mbaya, ni tete, naomba litazamwe kwa jicho la huruma ili wananchi wa Igalula nao waweze kutatuliwa kero hii kubwa ya maji ambayo imekuwa inawakabili kwa miaka nenda, miaka rudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Makilagi!

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili jioni ya leo niweze kutoa mchango wangu katika Sekta muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niungane na Wabunge wenzangu kutoa pole nyingi sana kwa Wabunge wenzetu walioondokewa na wazazi wetu wapendwa, lakini kipekee nitoe pole nyingi na niungane na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa familia ya mtoto Nasra aliyekaa kwenye boksi miaka minne na Mwenyezi Mungu amemwita. Tunaomba Mwenyezi

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mungu amweke mahali pema peponi. Vilevile niombe Serikali yetu, ichukue hatua kwa wale wazazi waliofanya kitendo hiki cha kumweka mtoto miaka minne bila matunzo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya utangulizi huo, naomba sasa nijielekeze katika mchango wangu kama ifuatavyo:-

Kwanza, naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kazi nzuri sana inayoifanya ya kuhakikisha inajenga miundombinu ya maji katika Majiji yetu Miji yetu na hata katika Vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba, ukiangalia kitabu cha Wizara ya Fedha, kazi iliyofanyika mwaka huu ni ya kupigiwa mfano kwa sababu tangu vipindi vinne vilivyopita, tulikuwa tunahudumia wananchi laki nne kwa kila mwaka, lakini mwaka huu ni zaidi ya wananchi milioni mbili na kitu. Naomba niipongeze Serikali na naiomba iendeleo hivyo hivyo na kipekee nimpongeze sana Waziri na mwenzake Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya pamoja na kwamba walipata fedha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizi, naomba sasa nitoe ushauri kwa Serikali na nitumie nafasi hii kuiomba sana Serikali yetu na nimefurahishwa sana na Waziri Mkuu juzi alitoa kauli kwamba, fedha zote ambazo zilikuwa zimetengwa na ambazo hazikutoka kwa bajeti hii ya Wizara ya Maji, zaidi ya asilimia 74 zitatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba kabla Waziri hajafanya *wind up* yake, tupate maelezo ni lini zinatoka, maana wakati wa Wizara ya Nishati, Waziri wa Fedha alisimama akatuambia wiki iliyopita walipeleka zaidi ya bilioni thelathini na akatuambia Jumatatu ya leo kuna fedha zimeingizwa. Nataka leo pia nisikie kauli ya Serikali ni shilingi ngapi zitatengwa na zitawekwa lini na sisi wananchi tusikie kwa ajili ya maendeleo ya miradi yetu hasa Vijijini. Kwa sababu kama Wizara hii ingepata fedha kama ambavyo Bunge lako Tukufu lilipitisha, nina imani mambo yangekwenda sawasawa kwa sababu mfano ni hizi fedha kidogo umeona wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niungane na Wabunge wenzangu kusema kwamba tukiendelea kutegemea bajeti ya Wizara hii itokane na bajeti ya Serikali kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji na hasa Vijijini tutachelewa sana. Naomba tuanzishe Mfuko wa Maji kama ambavyo tumeanzisha Mfuko wa Barabara, nina imani tukianzisha Mfuko huu, suala la maji vijijini na lenyewe litabaki kuwa historia kama miradi mingine ambavyo tunaiona. Naiomba Serikali yetu ilete sheria tena katika Bunge hili, tuweze kuipitisha na tuanzishe Mfuko huu kwa ajili ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sasa utaratibu wa kutoa fedha. Lipo tatizo kubwa sana la utaratibu wa kutoa fedha kati ya Hazina, Benki Kuu na kufikia kwenye Halmashauri. Naomba sana utaratibu huu uangaliwe upya, kwa sababu unakuta Serikali inachanga fedha, mfano, Wizara ya Maji inatengewa bajeti pengine milioni mia sita, zinakaa pale Benki Kuu wanasema ni *exchequer*, fedha hazitoki, lakini wakienda kwenye mtandao wanaona zile fedha. Naomba huu utaratibu uangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta fedha zinatengwa, kule kwenye mtandao zinaonekana, lakini fedha hazitoki, kuna tatizo gani hapa? Utaratibu huu siyo mzuri na unachelewesha maendeleo ya miradi yetu. Naomba tuangalie upya na ikiwezekana tuufute, tutafute utaratibu unaokubalika, ambao utapeleka fedha kwa haraka. Maana hata kama zitapitishwa leo, upo uwezekano pia tukamaliza mwaka wa fedha, lakini fedha hazijafika huku tumeambiwa fedha zimetengwa, zinabaki zina-*hang* hapa hewani bila kwenda kwenye miradi ya maendeleo.



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizingumzie mradi wa Musoma Mjini na nizingumzie mradi mkubwa ambao Serikali inauendeleza pale, kwa niaba ya wananchi ya Musoma, wananchi wa Mkoa wa Mara naomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa ujenzi mkubwa wa mradi wa maji katika Mji wa Musoma. Sisi Wabunge wa Mkoa wa Mara katika bajeti iliyopita tulishikana tena bila kujadili itikadi zetu, tulishikana kwa pamoja na Serikali ikasikia kilio chetu ikatenga fedha na mradi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, kwa kuwa mradi huu unazunguka, uko karibu na Halmashauri ya Musoma, Musoma kuna Kata kama nne, Kata ya Itaro, Kata ya Nyegina, Kata ya Nyakatende na Kata ya Mkirira mradi huu pia uwahudumie wananchi wa pale, kwa sababu kama hawakupata msaada kupitia mradi huu, suala la maji safi na salama katika Halmashauri ile ya Musoma itabaki kuwa ni ndoto, maana miradi mingine kwa kweli itachelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakwenda mimi na Mheshimiwa Waziri pale, aliwasikiliza wananchi na aliwaahidi, leo wamenituma kwamba nikisimama wanataka kumsikia anasema nini juu ya mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie mradi wa Mugango-Musoma-Kyabakari na ule unaofika Butiama. Pia niishukuru sana Serikali na kwa kweli kipekee nimshukuru sana Waziri, tulikwenda na yeye mpaka Butiama, akaonana mpaka na Mama Maria Nyerere, akajionea hali halisi ilivyo. Nimefurahi sana kuona kuna mradi unakuja kupitia BADEA na naiomba sana Serikali isukume mradi huu uweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama fedha hazitatoka, maana fedha za kutegemea wahisani inawezekana mradi usianze, ombi langu ni kwamba, kwa kuwa mradi ule wa Musoma Mjini unao uwezo wa kufika mpaka Butiama, basi tuunganishe mradi huu ufike mpaka Butiama na mradi wa BADEA kama utakuja kwa kuchelewa, uweze kuwahudumia wananchi wa Tarafa ya Nyanja ambako huko pia kuna Kata zaidi ya 20 na zenyewe pia hazina maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie mradi wa Mji wa Mugumu ambapo tuliiongozana na Mheshimiwa Waziri, aliona yale maji hayafai, yale maji ni tope kabisa. Niliona jitihada zake za kutafuta fedha na waliwapelekea fedha kwa ajili ya mradi huu, atakapokuwa una-*wind up*, ningependa kujua mradi huu umefikia wapi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nyangwine! Ajiandae Mheshimiwa Profesa Msolla.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maji. Kwanza niweke wazi kwamba sitaunga mkono hoja hii kwa sababu mbalimbali. Kwanza naomba Waziri aniambie kwamba tangu Serikali ya Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa alitoa ahadi ya kuondoa tatizo la maji Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya Mheshimiwa Dkt. Kikwete ametoa ahadi mara mbili na hakuna chochote kile kinachoendelea. Waziri mwenyewe mwaka 2012 alisimama hapa akasema kwamba, sasa tatizo la maji Tarime tutalishughulikia, lakini hakuna juhudi zozote zile ambazo zinaonekana. Mwaka jana Waziri alisema kwamba, ametenga hela kwenda Tarime, mpaka sasa hivi hakuna shilingi moja ambayo imeshaingia katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Ziwa Victoria lipo umbali wa kilomita 25 kutoka Tarime, nauliza ni kwa nini Mheshimiwa Waziri sisi tuangalie maji ya Ziwa Victoria yanapita tu hatuyatumii, yanakwenda sehemu nyingine? Kwa kweli hiyo hatuwatendei haki watu wa Tarime na watu wa mikoa yote ambayo inazunguka Ziwa Victoria; Mkoa wa Kagera, Simiyu, Mara na mingine yote. Vile vile kuna mto Mara upo umbali wa kilomita zero, wananchi wanaangalia ule mto unapita tu, lakini wana matatizo ya maji, naomba hilo Waziri alitafakari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Ziwa Victoria kwamba limejaa tope, kwa kuwa lile Ziwa limejaa tope na hakuna juhudi zozote zile za kuondoa lile tope, yale maji sasa hivi yanarudi kwenye bonde la Mto Mara na yamesababisha baadhi ya Vijiji kama vile vya Misanga, Sulugu, Guta, Nyarukoba katika Kata ya Buswahili na kisha Kelege, Kata ya Kiole, yameleta matatizo makubwa sana. Matope haya yamesambaa katika bonde la Mto Mara na yamesababisha matatizo katika makazi ya wananchi, kilimo hakifanyiki, mifugo ni tatizo. Naomba Serikali iniambie leo ina mkakati gani wa dharura au itachukua hatua gani za dharura za kuondoa tope katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; naomba Waziri anieleze, sasa hivi kuna miradi inafanyika mijini na vijijini, lakini utakutaangalia kabisa kwamba tunaegemea zaidi mijini ambako kuna wakazi wachache tunasahau vijijini. Hii hatuwatendei haki Watanzania, ikiwa tunaelekeza nguvu nyingi sana mijini, kule vijijini tunawaacha kwa kweli ni lazima tukae tutafakari, wananchi wa vijijini wanapata shida kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mkubwa wa maji kwa mfano Musoma ambao dada yangu Makilagi ameuongelea, unakwenda mpaka Butiama, lakini utakuta kwamba kuna Tarafa ya Kiagata, kule ni ukame enzi na enzi, ukienda pale ni matatizo makubwa sana. Serikali mna mpango gani wa kuchukua maji hata Mto Mara mpeleke kule Kiagata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kuongelea ni kutaka kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri na anisaidie, juzi nafikiri wiki iliyopita, kuna mtu aliuliza kuhusu matumizi ya Mto Nile. Waziri wa Mambo ya Nje alijibu kwamba, sasa hivi kuna mikakati ambayo inaonekana kabisa kwamba kuna sheria kali zimewekwa tangu enzi za ukoloni na hizo sheria ni lazima tuzifuate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonekana dhahiri kabisa kwamba, Mwalimu Nyerere alishawahi kusema kwamba nchi zote zinazotumia Mto Nile ni vizuri zikanufaika na hayo maji ya Mto Nile. Sasa inaonekana kwamba Serikali ina mpango wa kutaka kufuata yale masharti yaliyowekwa na Mkoloni. Naomba Waziri atuambie wana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba maji ya Mto Nile kwanza yanatoka katika Ziwa Victoria ambalo lipo Tanzania na sisi tuweke sheria au tuweke mkataba maalum wa kuizuia Misri isiumiliki ule mto kama mali yake. Kwa sababu kupanga ni kuchagua, yale maji yanatoka kwetu, tutumie mbinu gani ili kuhakikisha kwamba wale watu wote ambao wanatumia yale maji ya Bonde la Mto Nile zinanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nataka kuliongelea kwa kirefu sana ni kuhusu tatizo la maji Wilayani Tarime. Wilaya ya Tarime ina vyanzo vikuu vya maji viwili. Kuna Mto Mara na kuna Ziwa Victoria. Utakuta tangu enzi na enzi tunatumia kuchimba visima vijijini na kule Mjini na sasa hivi tuna Halmashauri mbili; kuna Halmashauri ya Mji ambayo Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake amesema ni Mji Mdogo, siyo Mji Mdogo ni Halmashauri ya Mji wa Tarime ameitengea shilingi milioni mia tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizingatia kwamba Wakazi wa Tarime wenyewe wanakaribia laki tatu na kitu, ukipeleka milioni mia tano, mwaka jana alitenga milioni mia tano ambayo

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

haikufika, naomba aniambie wana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba Halmashauri ya Mji wa Tarime inapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu ukienda nchi ya jirani ya Kenya kule Sirari wenyewe wanatumia maji safi na salama, ukija Tarime utakuta kwamba ni matope, yale maji utafikiri kwamba ni *juice* imetengenezwa. Naomba aangalie, tutumie mbinu gani au afanye nini ili aondoe tatizo la maji Tarime. Juzi nilimwandikia ki-note nikasema kwamba anapokuja leo aje na majibu sahihi ya kuondoa tatizo la maji Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, vijiji vya Tarime karibu vijiji 105, kati ya vijiji hivyo utakuta karibu vijiji kumi ndiyo vina maji safi na salama vijiji vingine vyote havina maji. Tumejitahidi kuchimba, lakini ukiangalia wanaokwenda kuchimba, maji yanatoka siku mbili, tatu yanakauka. Huu ni wizi wa hela za Halmashauri na ni wizi wa hela za wananchi wa Tanzania wote kwa ujumla. Kwa hiyo, ni lazima tukae tutafakari ni kwa nini matatizo ya maji katika Wilaya yangu ya Tarime yamekuwa enzi na enzi, huu ni mwaka wa nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anapokuja huku anatoa majibu ya kuridhisha kabisa, wananchi wa Tarime wanampigia makofi, lakini hayo majibu anayoyotoa hakuna chochote kinachoendelea. Naomba leo atoe majibu ambayo ataweka *commitment* ya Serikali ya kuondoa tatizo la maji Wilayani Tarime, la sivyo mkakati ambao nitaupanga utakuwa kwa kweli, ni mkali sana ili wananchi wangu waweze kupata maji. La sivyo nitawazuia wote msiweze kufika katika Wilaya yangu ya Tarime ili mjue kwamba ni nini tufanye, maana sasa inaonekana kama ni danganya toto, hapana! Mheshimiwa Waziri siridhiki na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nasisitiza ni kwamba, tope katika Ziwa Victoria liondolewe, maji ya Ziwa Victoria yawanufaishe wananchi wote wanaokaa Mkoa wa Mara, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Simiyu na mikoa yote inayozunguka Kanda ya Ziwa, wanufaike kwanza, ndiyo maji yatoke yaende sehemu nyingine. Ina maana wananchi wa mikoa hiyo hawajui kutumia maji? Tuka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Msolla ajiandae Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Kilolo nianze kwanza kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa Wizara hii na hususani bajeti yake, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wote wa Wizara hii kwa kufanya kazi yao vizuri sana licha ya kwamba rasilimali wanayopewa ni kidogo sana. Nina hakika wangeweza kufanya kazi nzuri zaidi kama tu wangeweza kupewa kile ambacho kilikuwa kimepitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwamba wakati idadi ya watu duniani inazidi kuongezeka, pamoja na mifugo, rasilimali maji inazidi kupungua. Hivyo, kuna kila sababu ya sisi kuendelea kujipanga vizuri ili kutunza vyanzo vya maji, kuvuna maji ya mvua na kutafuta vyanzo vingine vya maji, kwa kuzingatia kwamba kuna mabadiliko makubwa ya tabia ya nchi kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba maji ni uhai kama kila mmoja wetu anavyozungumza, lakini kwa hali ya sasa tuliyonayo maji pia ni siasa na hasa ukizingatia mwaka

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

huu 2014 mnajua kuna matukio gani na vilevile mwaka 2015 ambapo kutakuwa na matukio makubwa sana. Hivyo, Serikali hii ambayo ni sikivu ni vema ikajipanga vizuri ili kusudi tatizo la maji lizidi kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mategemeo yetu yalikuwa kwamba, huu mradi wa vijiji elfu kumi ifikapo Juni mwishoni, ungekuwa umekamilika kwa kila Halmashauri, lakini dalili zilizopo ni kwamba lengo hili haliwezi kufikiwa kwa sababu ya fedha kutokupatikana kwa wakati na kwa kiasi ambacho kilikuwa kimeombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika Wilaya yangu ya Kilolo. Katika Wilaya ya Kilolo nina tatizo sana la maji. Katika Mji mdogo wa Ilula ambao hivi karibuni tunagemea kwamba utakuwa na Halmashauri yake, Mji huu una watu wengi, kuna watu zaidi ya 45,000 na kuna shughuli mbalimbali za kimaendeleo, lakini watu wake wanatumia muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alifika Ilula tarehe 29 Novemba, 2013, yeye mwenyewe alijionea hali ilivyo tete kwa sababu watu wanahitaji maji ya kutosha na maji safi na salama. Kutokana na msukumo huo, mimi binafsi nimejitahidi kuchimba visima vinne vya maji na kuweka hata pampu, lakini sijaweza kukamilisha miundombinu mingine ili hayo maji yaweze kufikiwa na kuanza kutumiwa na watu. Ni mategemeo yangu kwamba, Wizara hii itaniunga mkono nimalizie huo mradi, pamoja na Serikali yenyewe kuhakikisha kwamba tunapata maji ya kuaminika kwa muda wote kwa Mji huu mdogo wa Ilula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ule mpango wa Vijiji Kumi kwa kila Halmashauri, katika Wilaya yangu utekelezaji upo katika sehemu tatu. Kuna sehemu ya kwanza ambapo vijiji vitatu vya Kipaduka, Ikuka na Vitono mradi umekamilika na watu wanapata maji. Kuna vijiji saba ambavyo hivyo vipo katika ngazi mbalimbali. Vijiji hivyo ni Ihimbo, Lulanzi, Ilamba, Mwatasi, Ipalamwa, Muruwe na Ilindi. Hivi vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Hata hivyo, kazi katika sehemu nyingi zimesimama kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji vingine nje ya mradi wa Benki ya Dunia, Vijiji hivyo ni Kiterewasi, Bundamatwe na Ihomingate ambapo kazi haijaanza hata kidogo. Ni matarajio yangu kwamba, Wizara itafanya kila linalowezekana ili kusudi maji yaweze kupatikana na kazi ziweze kuanza katika Vijiji hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mji mwingine ambao unakua kwa haraka sana ni Mji wa Ruaha Mbuyuni ambako kullikuwa na mradi wa maji safi na salama kwa matumizi ya wananchi. Mradi huu haujaanza kamili, japokuwa *sife* ya kujenga tanki umeanza, ningepomba sana Wizara itazame kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi haya yametokana na kutokuwa na bajeti ya kutosha na hili tumelizungumza sana na wote hapa wanaolia nafikiri wanalia kwa sababu ya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ningependa kushauri kwamba pamoja na kupata bajeti ya Serikali, ni vizuri kama walivyoshauri watu wengine kwamba, tuanzishe Mfuko wa Maji ambao utatokana na fedha za ndani ambao utakuwa endelevu na tunaweza wakati wowote tukajua kwamba tuna fedha za kutosha, tutakamilisha miradi gani kuliko hali tuliyo nayo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu kwamba Waziri atakaposimama; moja, atatoa tamko juu ya kuanzishwa kwa Mfuko huo kwa sababu jambo hili lilishazungumzwa.

Pili, Waziri anieleze kwa uhakika ni lini, watu wa Mji Mdogo wa Ilula wategemee kupata maji safi na salama katika kipindi hiki kinachokuja mbele yetu.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya, naunga mkono hoja nikitegemea kwamba Mheshimiwa Waziri atatoa matamko ambayo yatawapa matumaini watu wa Jimbo la Kilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwijage! Wajiandae Mheshimiwa Mgalu na Mheshimiwa Opolukwa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Maji. Nina ushauri kwa Serikali, Mheshimiwa Mchemba na Waziri wako mnisikilize, hii inawahusu nyie Watalaam wa shughuli za maendeleo ya binadamu wanakwambia kuna shughuli kuu mbili, shughuli ya kwanza ni maji na shughuli nyingine ni umeme. Yote hayo, mngepiga kura za maoni na kuulizia wananchi watakwambia tunahitaji maji, tunahitaji umeme, mengine yanakuja baadaye. Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya kuwa na Mfuko wa Maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maji si hoja, hoja ni kuwa na Mfuko ambao uko *ring fenced*, Mfuko wa Umeme wa REA haufanyi vizuri kwa sababu kuna mtu anaweza akauchukua, akafanyia lolote kwa sababu hauko *ring fenced*. Mfuko wa Barabara umefungwa. Kwa hiyo, yule mtu wa barabara anajua ni lita ngapi za mafuta zinashushwa na anaweza akajua kiasi gani kitaingia. Ifanyike hivyo kwa umeme, ifanyike hivyo kwa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikueleze, Watanzania hawa mkiwaambia, mnayo biashara ya kutafuta trilion moja, waweke ushuru wowote kwenye bidhaa yoyote iwe simu, maji au nini Watanzania hawa watakubali kwa kiwango chochote ili mradi mfanye biashara hii iishe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulizungumza sana hapa kuhusu bajeti ya maji, tukaongeza bilioni 180. Bahati mbaya hazikutoka na niwaambie wapiga kura wangu wa Mji mkongwe wa Kamachumu, *Kalinga Water Project* haikutetelezwa, lakini nina imani mradi wa maji sasa hivi kwa ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na pesa zilizotengwa bilioni 500 lazima mradi huo msiniache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwa jinsi mliyokwenda kutengeneza mradi wa maji Nyaburo, Kisiwani kule Kinagi, Katoke na Ruwanga. Jambo la muhimu katika miradi hii na pale ndipo ninapoiomba kuishauri Serikali. Naomba Wilaya yangu muichukulie mfano. Mheshimiwa Waziri nakuomba na Wataalam wako na boss wangu wa zamani Katibu Mkuu huko uliko, nataka miradi yangu ya Wilaya ya Muleba inapochambuliwa Wilayani isianze mpaka Wizara itoe *no objection*. Walete makaratasi yao yaje Wizarani mridhike, miradi Waheshimiwa Wabunge inayokwama ni kwamba wale Wakandarasi wanafanya uchakachuaji, mtu anapewa mradi, hajui kazi inayofanyika, mara anachukua *advance* anakimbia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana na naunga mkono Wizara hii kwa sababu najua Waziri atakubali miradi ya Muleba, yote kabla Mkandarasi hajawa *awarded* iletwe Wizarani ipitiwe upya, *performance bond* iwe *in place*, *Contractor* awe mwenye uwezo, kusudi akafanye shughuli. Tungependa kumaliza shughuli za maji kabla ya mwezi wa 12, sijui mwaka kesho kuna shughuli gani, lakini ningependa mwezi wa 12 shughuli hizi ziishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Wataalam, nisikitike pamoja na Serikali. Suala la kukosa wataalam siyo la kutupigisha kelele, tulifanya makosa, tukawaondoa ma-Craftsman na ma-Technician, tukatengeneza watu wa vyeti wale ma-Engineer. Ningeomba hili suala

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

tusiliseme, tukimbie kimya kimya, vijana wapo, tufundishe vijana wengi. Hii miradi mikubwa ya maji tunayotengeneza kwa mabilioni na kuipeleka kule vijijini, kama haina mafundi wa kuisimamia, ni kwamba tunatupa pesa. Ningewaomba watoto watusikie, vijana wapo, wafundisheni ufundi, waende wasimamie hii miradi iweze kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie miradi ya *World Bank*. Ninayo Kata ya Muhutwe na Kata Mayondwe, zina vijiji vinane, kuna maji yanatiririka kutoka Kambi ya Jeshi Kaboya, Kawalinda. Ni afadhali kuchota maji pale, kutengeneza *reservoir* moja pale Kangantebe, ikamwaga maji kwenye vijiji nane utatumia pesa zisizozidi milioni 600 kuliko vijiji nane vya *World Bank* ukaweza kutumia mapesa ya ajabu ajabu ambayo hata naona uchungu kuyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwaeleze Kata yangu ya Nyakatanga, Rutoro, Ngenge, Mushabago zina shida ya maji. Nahisi kule hawawezi kupata visima, wanahitaji malambo, wanahitaji kuvuta hii *surface water*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa mnapokuja kwenda nyie wataalam, sisi ambao siyo wataalam, afadhali mtuulize. Mtaalam anayekwenda kuchota maji, kuchimba maji kisima, eti mwelekezi, akachimba akakosa, afadhali akaniuliza mbumbumbu mimi nikakuonesha mahali pa kuchukua maji. Hawa waelekezi wanakula mabilioni ya pesa, wanatoboa hawapati maji. Sasa niulize afadhali uchukue *surface water*, ulete watu waridhike, wataweza kuchemsha, wataendelea, kuliko kutoboa kisima unasema bilioni 250 au milioni 300 na maji tumekuta hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza suala la wananchi kutunza ile miundombinu, suala la kutunza miundombinu Wabunge ni letu wote na ningependa Serikali kupitia taratibu itungwe Sheria kali kama mtu ana-*vandalize* miundombinu ya maji, achukuliwe Sheria kali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningependa niwashauri, mshirikiane na Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mkoa. Mkuu wa Wilaya ya Muleba anapoona upungufu kwenye mfumo wa maji anabaki analia. Hakuna anayemsikiliza, anasema mradi huu umehujumiwa, hakuna anayemsikiliza. Sasa mtengeneze utaratibu nyie watu wa Wizara, mzungumze na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya mambo yanakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkimwuliza Mkuu wa Mkoa wa Kagera anakwambia miradi ya maji ya Muleba haiendi vizuri. Ukimweleza DC anakwambia *pressure* inapanda. Sasa mtengeneze utaratibu nyie Serikali kuwasiliana kusudi sisi tubaki kwenye shughuli nyingine za kuwahamasisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti hii kwa sababu najua mradi wa Kalinga, Kamachumu, utatengenezwa sina wasiwasi na Mheshimiwa Alhaj, mambo yatakwenenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mgalu, ajiandae Mheshimiwa Opolukwa.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Maji. Nianze pia kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapa pole Wabunge wote ambao wamefiwa na wazazi wao Mheshimiwa Zitto na Mama yetu Mama Martha Mlata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nianze kwa kutoa ushauri kwa Serikali na nimshukuru Waziri Mkuu kwa ahadi yake aliyoitoa, lakini niseme kwa kipindi cha mwaka wa

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

fedha unaokuja, kwenye pesa hizi zinazotengwa kwenye miradi ya maji na hususani kwenye pesa za ndani, nadhani pamoja na kwamba BRN ina vipaumbele sita, lakini ukiangalia kipaumbele ambacho kilipashwa kipewe uzito unaostahili ni maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini miradi ya maji ikitokelezeka Watanzania wakapata maji kwa wakati, wanaweza wakatenga muda wao mwingi kujishughulisha na shughuli mbalimbali za maendeleo wakaweza kuongeza uzalishaji. Pia wawekezaji ambao wengi wanakwama kuwekeza kutokana na upungufu wa maji katika maeneo yetu watawekeza. Mwisho wa siku pato la Taifa litakua na kipato cha Mtanzania kitakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndiyo watakapotumia miundombinu ya barabara, miundombinu ya reli, lakini kama tutaacha kipaumbele hiki cha maji kinasuasua na ukiangalia kwa mwaka huu ambao unaishia 30 Juni, mpaka sasa bilioni 222 hazijapelekwa kwenye maeneo yanayohusika, kwa kweli hata hizo barabara zinazojengwa na miundombinu inayoboreshwa, umeme unaosambazwa kwenye maeneo yetu itakuwa haileti tija kama Watanzania hao watakosa maji na watumia muda mwingi zaidi ya masaa nane kumi au ishirini kutafuta maji. Hapa kwa kweli tutakuwa tunatwaga maji kwenye kinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nijielekeze kwenye hoja zangu za msingi. Kwanza kabisa, nianze na miradi ya upanuzi wa miradi ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na nianze moja kwa moja na ujenzi wa bwawa la Kidunda. Pamoja na maelezo mazuri yaliyo kwenye kitabu cha Waziri, lakini ningeomba sana wawatazame wakazi wa maeneo ya Kidunda. Bwawa hili ni la muda mrefu, lakini lina tija likikamilika kwa wakazi wa Dar es Salaam. Barabara inayotarajiwa kujengwa mpaka sasa hivi haijajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Waziri anasema wanasubiri tathmini ya mkandarasi. Mheshimiwa naomba niulize tathmini hiyo mpaka lini? Katika kijiji kile cha Kidunda hata mvua za mwaka huu eneo zima lile walipata mafuriko makubwa kiasi kwamba watahitaji kijiji kizima kile kuhamishwa. Je, Serikali imejipangaje? Lakini pia upande wa malipo ya fidia, mpaka mwaka huu pia Serikali imefanya tathmini upya baada ya kuona fidia imecheleweshwa, lakini ukiangalia imejipanga kwamba italipa bilioni saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtindo huu inawezekana fidia hii ikaongezeka zaidi na gharama za ujenzi wa bwawa hili zikawa kubwa na pia nishukuru Serikali kwa miradi mbalimbali ya maji iliyotekelezwa katika Mkoa wa Pwani, uchimbaji wa visima 28, Wilaya ya Kisarawe, lakini pia mradi wa awamu ya pili Chalinze na vijiji 47 tunasubiri kwa hamu utekelezaji wa maji wa mradi huu, lakini ningeomba sana Wizara iangalie miradi iliyokuwepo kwenye kipande (H) ambacho kinahusisha Vijiji vya Msolwa, Mdaula, Matuli, Ubena Zomozi, Mwidu, Kaloleni na Tukamisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi alishindwa, amewekwa mwingine, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri alikuja alitembelea Kibindu pia aliwaahidi kwani kuna uhaba mkubwa wa maji. Naomba Mheshimiwa Waziri miradi hii Mwenyezi Mungu akipenda ikamilike mwaka huu kwa kweli shida ya maji ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimalizie kukumbusha kama alivyosema Mbunge wangu wa Jimbo la Muheza, kama alivyosema Mheshimiwa Rais mbele ya mkutano wa hadhara tarehe 26 Machi, 2014 aliwathibitishia wakazi wa Muheza kabla hajaondoka madarakani kwamba pesa za mradi huu zitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Mheshimiwa Waziri na Rais alitoa maelekezo mahususi akiomba Wizara ya Maji na Wizara ya Fedha iendelee na mazungumzo ya wadau ambao

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

walijitokeza kutaka kufadhili mradi huo. Niombe sana wakazi wa Muheza wamesubiri kwa hamu sana, maji yanatoka Zige yanaenda Tanga, lakini Muheza hakuna, leo unawaambia watunze vyanzo, tunatunza vipi, hata sisi wasimamizi hususani wa maeneo hayo tunajisikia vibaya, hivyo unamlazimishaje mwananchi wa maeneo ya Muheza atunze chanzo cha Mto Zige maji hayo yanampita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri ahadi yake ya bilioni moja Muheza. Nimkumbushe pia ahadi yake ya vijiji 45 vinavyopitiwa na mto huo kupata maji kabla ya mwaka 2015. Chonde Mheshimiwa Waziri namwomba, nimeona niseme hivyo kwa sababu na mimi ni mkazi wa kule, hali si nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu, kuongeza upatikanaji wa maji katika Miji ya Mlandizi, Kibaha, Bagamoyo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri na watekelezaji wa mradi huu kwa kweli kasi yake iende kwa nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo ndani ya Bunge jioni hii; Mheshimiwa Omary Badwel, Mbunge wa Bahi anaomba kutangaza wageni wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Bahi na Wakuu wa Idara wote, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Opolukwa!

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia kwenye bajeti hii muhimu ya Wizara ya Maji. Ningependa nianze moja kwa moja kwa sababu ya ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo ningetaka kuzungumzia kuna bwawa pale Meatu linaitwa Bwawa la Mwanyahina na bwawa hili lina-supply maji kwenye mji wetu Mwanuzi ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya, lakini pia na maeneo yale ambayo ni ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ujenzi wa bwawa hili mchakato ulianza mwaka 1999 zaidi ya wakazi 34 waliambiwa kupisha ili kuweza kutengeneza bwawa hili kwa ajili ya kusaidia upatikanaji wa maji kwenye mji wetu wa Mwanuzi pamoja na vitongoji vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa ambao walikuwa *displaced* ambao ni 34 waliachia eneo lenye ukubwa wa ekari 461. Serikali ikawaambia kwamba tunaomba mpishe eneo hili na baada ya kuwa mmeshapisha tutakuja kuwapatia fidia baadaye. Cha msingi, kwanza watu mpishe halafu tuweze kujenga bwawa hili, watu wapate maji, fedha zenu mtakuja kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 1999 mpaka leo wananchi hawa hawajalipwa fidia wanayodai ya milioni 356 na kwa bahati mbaya sana bwawa hili wakati linaanzwa kujengwa lilikuwa na eneo dogo ambalo nimesema ilikuwa ni ekari 461, lakini baadaye bwawa hili lilikuja likapanuliwa.



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza watu ambao walikuja kupewa fidia ya malipo katika eneo hili ni wale watu ambao walihusika na ule upanuzi wa bwawa, wakalipwa zile pesa na hawa watu ambao waliopisha lile eneo kama watu ambao walikuwa ndiyo *original* kwenye eneo lenyewe, hawakuweza kupewa zile fedha mpaka leo wanadai fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sasa Waziri wa Maji, kwa kuwa sasa watu wanadai fedha zao na imekuwa ni kwa muda mrefu na kwa bahati mbaya sana watu wanapoendelea kuwa wanadai fedha zao tangu kipindi kile mpaka leo, imefikia hatua sasa Halmashauri, Mkurugenzi wa Halmashauri kupitia Mwanasheria wake amemwandikia barua ya kuwatishia. Ningependa nisome halafu nitaiweka Mezani kama kumbukumbu rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye barua iliyoandikwa tarehe 29 mwezi wa Nne inasema madai ya fidia ya shilingi milioni 356. Kwenye ile *paragraph* ya pili naomba nisome kwa ruhusa yako, wanaandikiwa hawa watu wanaodai fidia ya shilingi milioni 356. Ofisi hii imekuwa ikiwaeleza mara kwa mara kuhusu jambo hili, lakini imeonekana kuwa wewe umekuwa ukiwapotosha wananchi kuhusu suala hili. Anaandikiwa Mwenyekiti wa kikundi cha wanaofuatilia madai ya kulipwa fedha zao. Naomba maelezo haya sasa yawe ni ya mwisho na kama utaendelea na tabia yako hii ya kuwapotosha wananchi, hatutasita kukuchukulia hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuwa na chama ambacho kinatishia wananchi wake, tunakuwa na viongozi wanaotishia wananchi wanaodai haki zao. Tena anasema kwamba eti watachukuliwa hatua kali za kisheria kwa makosa ya uchochezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuweka Mezani barua hii ili angalau basi Mheshimiwa Waziri pamoja na Meza yako waweze kuifanyia kazi. Naomba wananchi waweze kulipwa. Sitaunga mkono hoja hii kwani wananchi wamedai kwa muda mrefu, Mheshimiwa Waziri alikuja Mwanjoro, alipokuwa akipita pale kwenye bwawa kuangalia ujenzi wa bwawa la Mwanjoro ambalo fedha zimetafunwa zaidi ya milioni 819 na Mkandarasi amekimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu leo katika majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kwa vile Mkandarasi amekimbia, tunatenga tena fedha zingine shilingi milioni 428 kwa ajili ya kwenda kumaliza kazi ambayo tayari imeshalipwa fedha yake. Hatuwezi kuendelea kuchezea fedha ya walipa kodi kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hawa walioiba fedha za bwawa la Mwanjoro wanajulikana ni watu wa Wizarani kwa sababu bwawa hili halisimamiwi na Halmashauri, watu wa Wizara hawataki hata kuwashirikisha Watendaji wa Halmashauri, wanatoka juu na ndege, wanatua Mwanza, wanatua Shinyanga wanakimbia Meatu, wanavuna pesa wanarudi kwao. Ni wizi mtupu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha milioni 428 kwa ajili ya fidia kwenye bwawa ambalo fedha yake imeshatumika, hebu ziende sasa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika maeneo mengine ambay hayana maji. Nina maeneo mengi sana ambayo hayana maji kule kwangu. Kuna Kata ya Mwamanongwi, hakuna maji kabisa watu wanataabika, kuna Kata ya Mwabuzo, kuna Kata ya Nkoma, Kimali, Bukundi, Mwamalole, Mwamanongwi hizi milioni 428 kwa nini zisipelekwe katika maeneo haya ambayo tayari wananchi wanateseka, lakini fedha inapelekwa kwenda kuongezea watu ambao ni wezi, wameiba fedha ya umma halafu tunawapelekea kuongezea fedha nyingine. Hili halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, siungi mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga! Ajiandae Mheshimiwa Zabein.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Waziri na Wizara yake kwa kazi nzuri mbalimbali ambazo wamekuwa wakifanya ndani ya Wizara hii, maana tukisema hakuna kazi ambazo zimefanyika si kweli. Ziko baadhi ya sehemu kwa mfano Iringa, Iringa wanapata maji kwa asilimia mia moja na mahali pengine. Kwa hiyo, kusema kazi hazijafanyika si kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko changamoto ambazo bado kuna maeneo fulani ambayo maji hakuna. Nikushukuru kwenye Jimbo langu la Njombe Kaskazini kwa kunipa hela pale Kata ya Kidegembye, katika Kijiji cha Image. Kijiji hiki mradi huu ni mkubwa ambao mlitupa fedha unatakiwa uhudumie vijiji tisa, jumla vijiji 10 pamoja na Image.

Kwa hiyo, bado pale utakuta sasa mradi huu hamjatoa hela za kutosha ili uweze kukamilisha Vijiji vya Kata ya Idamba, Kata ya Lupembe na Kidegembye yenyewe ambayo ndiyo mradi ambapo upo. Mheshimiwa Waziri uniambie sasa kwamba mradi huu utakamilika lini ili hivi vijiji vinavyozunguka ile Lupembe na Kidegembye na pale Kanikerere uweze kukamilika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia pale Kifumbe, Kata ya Mahongole. Mmenipa fedha pale, mradi huu unaendelea na unaendelea vizuri, lakini kuna Kata hii ya Kitandililo, katika Kijiji cha Mbugani, bado hatujapata fedha wakati tayari Mkandarasi alishatangazwa na bado sijajua ni nini ambacho kimekwamisha. Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho nipate taarifa zake hali yenyewe ikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie hali ya Makambako yenyewe. Pale Makambako tuna tatizo kubwa sana. Hasa inapofika mwezi wa Tisa, Kumi, Kumi na moja na Kumi na Mbili. Waziri mwenyewe anajua mwaka juzi hali ilikuwa ni mbaya sana na tulimwomba aje, alikuwa aje, bahati mbaya akapata dharura nyingine ili aje aone mwenyewe halisi ilivyo Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenyewe anajua mwaka juzi hali ilikuwa ni mbaya sana na tulimwomba aje, ilikuwa aje, bahati mbaya akapata dharura nyingine, ili aje aone mwenyewe hali halisi ilivyo Makambako. Nikushukuru kwa hela chache hizi ambazo ametupa ambazo tunaendelea kuchimba visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini iko ahadi ya Mheshimiwa Rais ya shilingi milioni 600 ambayo, tuna bwawa pale tulipanga kwamba, bwawa liweze kufufuliwa, ili kusudi liweze kuhudumia katika Mji wa Makambako, ni kilomita mbili tu kutoka mjini pale kwenda kwenye eneo hili, ambalo lilitengewa sh. 600,000,000/= ambazo Mheshimiwa Rais alipokuja, pale tulipofanya mkutano wa Lupembe, alisema fedha hizi atatupa ili bwawa hili liweze kufufuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Makambako kuna mradi mkubwa ambao Mheshimiwa Waziri anaujua ambao walitupa hela, walifanya upembuzi yakinifu na shughuli hii iko mezani kwake. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, hivi sasa hili Ziwa Victoria, maji yametoka Mwanza yamekuja Shinyanga, hivi kuna tatizo gani pale Njombe, Ruhuji, ni kilomita 58 kuja Makambako, kwa nini msije mkafanya ubunifu pale kutoa maji Ruhuji kuleta Makambako? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vile vile pale Njombe Mjini, tuna tatizo la maji Njombe Mjini ambao ndio Mkoa Mpya. Ni kilometa mbili tu kutoka maji yalipo kwenda pale Njombe mjini. Hivi kweli mtu akipita pale, mtu wa kawaida, anasema hivi Njombe na ninyi mna tatizo la

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

maji? Watu wanapita pale kwenda Songea, tunaposema hatuna maji, wanasema hivi kweli hakuna maji wakati maji chungu nzima yako pale Ruhuji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anafanya majumuisho hebu atwambie mikakati yake. Ni namna gani atatatua tatizo la maji kutoka Ruhuji kwenda pale Njombe Mjini na kutoka Ruhuji kuja Makambako?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tuna chanzo kingine cha siku nyingi kiko Fukulwa pale Mtwango. Ambacho, hiki kimekuwa kikikauka inapofika mwezi wa 9, 10 na wa 11 na wa 12. Hivi kwa nini tusiyatoe sasa kutoka Ruhuji kuleta Fukulwa ambapo kutoka Fukulwa pana miundombinu tayari, ni kilomita 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, tatizo la Makambako ni kubwa na inapofika mwezi wa Tisa, Kumi, Kumi na Moja na Kumi na Mbili, mpaka suruali huwa zinatoka tunapokuwa kwenye mikutano, hali inakuwa ni mbaya na yeye analijua. Kwa hiyo, nimwombe sana, ili wananchi wangu wa Makambako wawe na imani, tutakapomaliza bajeti hii bado nimwombe aje awaambie mwenyewe mikakati ya Serikali ambayo amepanga kutatua tatizo la maji pale Makambako. *(Makofi)*

**WAJUMBE FULANI:** Suruali zinatoka kwa nini?

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eeh, zinatoka kwa sababu ya maji, hali inakuwa ni mbaya kweli kweli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zabein, wajiandae Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Azzan.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote naomba nimshukuru *Allah Subhanah Wataala* kwa kunipa afya njema ili nami leo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kondo Kaskazini, niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli, Waziri wa Maji, Naibu Waziri wa Maji, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu ni Watendaji wazuri sana. Ni hodari, tatizo ni kwamba, pesa ndio haitoshi, lakini wakipata pesa naamini kabisa kwa kweli, watafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema pamoja na matatizo makubwa ya maji tuliyonayo katika Jimbo letu la Kondo Kaskazini, bado kuna mambo ambayo yamefanyika. Lazima niishukuru Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa kazi ambayo imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa ahadi ya kukarabati mtaro wa Ntomoko, ambao ulikuwa unagharimu bilioni 3.3, lakini tayari bilioni moja imekwishatolewa na kazi imeanza. Wizara iliandika barua kuonesha *commitment* yake ya kuongeza bilioni 2.3 ambazo zimebaki na naamini *commitment* hii itazingatiwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kuna miradi mitatu ya maji katika Jimbo la Kondo Kaskazini; kwa Delo, mradi umeshakamilika, Choka mradi umeshakamilika, Madisa mradi huu hivi karibuni nao utakamilika. Naongea kwa kutumia takwimu. *(Makofi)*

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe salamu za shukrani Mheshimiwa Waziri kutoka kwa wananchi wa Kwadelo, ambako alifika kuzindua mradi wa maji, aliona furaha yao ilivyokuwa, kuonesha umuhimu wa maji. Wanamshukuru sana na wanamkaribisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Ntomoko ambacho ndio chanzo cha maji ya mtaro wa Ntomoko hakina maji, lakini wananchi hao ndio wanaotunza chanzo hicho cha maji. Naomba niulize, je, Sera ya Maji inasemaje kwa wananchi wanaolinda chanzo cha maji kupatiwa maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini wananchi ambao wanalinda chanzo cha maji ndio wanatakiwa wapate maji kwanza, tena kwa haraka kabisa. Naomba basi wananchi wa Ntomoko wanaolinda chanzo cha maji wapatiwe maji, ili wapate moyo wa kuendelea kukitunza chanzo hicho cha maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Kondoa ambao ndio Mji Mkuu wa Wilaya yetu una tatizo kubwa la maji. Nimesema nitasema kwa takwimu, tayari Halmashauri imeleta andiko kuomba bilioni 1.78 kwa ajili ya shughuli zifuatazo:-

Kufanya ukarabati mkubwa kutokana na uchakavu wa mabomba ambayo yapo; Kuchimba visima kwa kuwa, chanzo cha maji cha chemchemi hakitoshelezi mahitaji na wananchi wameongezeka sana katika Mji wetu wa Kondoa; lakini vilevile kusambaza maji ya visima viwili ambavyo vimechimbwa na Halmashauri kule Bicha, lengo lake likiwa nini? Lengo likiwa maji yale ya vile visima viwili yatumiwe na wananchi wa Bicha na yatumiwe na wananchi wa Kilimani; ndio hiyo 1.7, mojawapo ya kazi ambayo tumeomba ifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumepata milioni 400. Namwamini Mheshimiwa Waziri, naomba atuongeze pesa, ili wananchi wa Kondoa Mjini ambako ndio Makao Makuu nao waweze kunufaika na maji haya na waondokane na usumbufu wa kuhangaika kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kondoa Kaskazini wananchi wanaopata maji safi na salama ni chini ya 40%. Naomba mliangalie Jimbo hilo kwa macho ya huruma; Rumburya litazame Jimbo la Kondoa Kaskazini kwa macho ya huruma, mwanangu Makala, wewe hutaki kuja Kondoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimesema nitaongea kwa takwimu; katika Jimbo letu tuna visima 14, ambavyo vimechimbwa, vina maji, lakini visima vimefunikwa. Visima hivyo Chololo, Wisi kwa Ntisi, Changaa, Mwongoroma, Isari, Tumbelo, Kidongo Cheusi, Mtiryangwi, Mahongu, Kwadilu, Hororimo, Munguri, Kwamafuchi na Serya; visima vipo tayari vimechimbwa, Mheshimiwa Waziri tunaomba pesa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Azzan! Wajiandae Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Mwigulu.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi angalau nizungumzie kuhusu suala la maji. Tangu mwaka 2006 wakazi wa Jiji la Dar-es-Salaam tulilalamikia sana ukosefu mkubwa sana wa maji, tukaahidiwa 2009 maji yatapatikana Dar-es-Salaam, lakini mpaka hivi tunavyosema 2009 imepita. Tunayo ahadi nyingine ambayo ni 2014/2015 kwamba, Jiji la Dar-es-Salaam litapata maji ya kutosha. *(Makofi)*

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwa jitihada ambazo zinafanywa na Serikali kwa sababu, Waswahili wanasema dalili ya mvua ni mawingu. Tumeona jitihada ambazo Serikali imechukua, mabomba ambayo yametandazwa, mitambo mipya iliyonunuliwa. Kwa hiyo, tuna hakika kwamba, ifikapo 2014 mwishoni na 2015, tatizo la maji litakuwa limeondoka Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufahamu tu kwamba, wakati wa mitandao hii ya maji ilivyowekwa Dar-es-Salaam miaka ya 60, Dar-es-Salaam ilikuwa na watu wasiozidi 500,000; leo tuko 5,000,000 kwa hiyo, nafahamu pia kwamba, kutandaza mabomba haya kunachukua muda, si suala la kusema kwamba, utaahidi leo, kesho uwe umekamilisha ni suala ambalo linachukua muda, lakini pia linahitaji pesa nyingi. Kwa hiyo, nipongeze sana kwa juhudi hizo, Mheshimiwa Waziri, kazi nzuri anafanya, lakini na ndugu yangu Makala, najua tulikuwa kwenye michezo kule Wizarani alifanya kazi nzuri, amekuja maji nina hakika kazi itakwenda kwa sababu, yeye ni jembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo tunalo na bahati mbaya sana sikuona kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na jitihada za maji safi, lakini pia kuna tatizo kubwa la majitaka katika Jiji la Dar-es-Salaam. Maeneo mbalimbali yamekuwa yakikabiliwa na tatizo hili, ama mitandao haipo ama mitandao imechoka kwa maana maji yanavuja hovyoy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikuona, lakini niombe tu kwamba, pamoja na jitihada nzuri zinazofanyika kwa ajili ya kuleta maji safi, lakini tuangalie pia na suala la majitaka katika Jiji la Dar-es-Salaam kwa sababu, ni kero mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingia katikati ya mji pale mi-chamber inamwaga mimaji taka hovyoy, Kariakoo hali ni hiyo hiyo, ukienda Mwenge, Kijitonyama, Block 41, Kinondoni Shamba na kadhalika. Kwa hiyo, naomba sana tuone Jitihada ambazo tunaweza kufanya kuhakikisha kwamba, mitandao inakuwa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila, nimpongeze sana Mkurugenzi wa DAWASCO, ndugu yangu Jackson Midala kwa kazi nzuri anayoifanya. Tunao wezi wa maji wengi Dar-es-Salaam, lakini ameendelea kupambana nao na namwomba aendelee kupambana nao kwa sababu, tatizo hili la wizi wa maji ni kubwa. Amefanya kazi nzuri kwenye baadhi ya maeneo Soga na kadhalika, Humudi, lakini pia nataka ajitahidi sana kuhakikisha kwamba, Dar-es-Salaam wizi wa maji unakoma. Haya maji kidogo tunayoyapata hivi sasa yakitumika vizuri, nina hakika wananchi wetu watapata maji bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa maji umekithiri. Wananchi wanauziwa maji kwa bei mbaya sana. Kwa hiyo, niombe kabisa Mheshimiwa Waziri apambane na hilo wakati tunasubiri neema ya maji, hii ambayo tunatarajia kuipata mwishoni mwa mwaka huu ama mwanzoni mwa mwaka unaokuja.

Magomeni tatizo ni kubwa ndugu yangu Midala, tunatumia maji ya visima bado kwa sababu kuna wezi wa maji, hata Mbunge wako naendelea kutumia hivyo hivyo na wananchi wangu pale. Kwa hiyo, nafikiri utaona ni jinsi gani ya kuhakikisha kwamba, tatizo linakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngeleja, ajiandae Mheshimiwa Mwigulu na mwisho atakuja Mheshimiwa Mwandosya ambaye, kwa nafasi yake leo vile vile Mheshimiwa Waziri

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mkuu amemteua kukaimu nafasi ya Kiongozi Mkuu wa Serikali, lakini tutampa vile vile muda kutokana na kwamba yeye alishakuwa kwenye Wizara hii, kwa hiyo, majibu mengi anayo na atasaidia Bunge na Serikali kutoa majibu.

Mheshimiwa Ngeleja!

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kuwapa pole ndugu zetu Mheshimiwa Martha Mlata pamoja na Mheshimiwa Zitto kwa misiba mikubwa iliyowakumba, lakini tunakumbushwa katika Maandiko Matakatifu tuendeleo kumtumaini Bwana kwa kila jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, lakini kabla ya kuanza kuzamia kwenye mjadala naomba nitoe jambo moja la ufafanuzi. Yamesemwa mambo hapa kuhusu ziara inayofanywa na Mheshimiwa Kinana, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Ni kwa nini anapita huku anaahidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaofuatilia na wanaoamini katika hili na hasa katika nchi inayoongozwa kidemokrasia kama tulivyo Tanzania, Serikali ni matokeo ya Vyama vya Kisiasa na Vyama vya Kisiasa vinakuwa na ahadi zake ambazo zinakuwa zimeunganishwa katika Ilani ya Uchaguzi, lakini chama kinachotawala, kupitia Serikali yake kinaendelea kuwahidi Watanzania wakati wote kinapokuwa madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachofanya Mheshimiwa Kinana sasa hivi, kwa sababu yeye ndiye msimamizi mkuu wa utekelezaji wa ahadi za Chama cha Mapinduzi, anachokifanya ni sahihi, ni kwa mujibu wa Katiba ya Chama cha Mapinduzi hivyo, ni jambo linalokubalika Kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nirudi kwenye mjadala na hasa Jimbo la Sengerema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 120 mpaka 122, utaona pale anatoa shukrani kwa wadau wa maendeleo wanaoendelea kuisaidia Tanzania. Mmojawapo wa wadau aliyetajwa pale ni Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia Bunge lako Tukufu niwashirikishe Watanzania kinachoendelea Jimboni Sengerema, ambacho sisi ni wamojawapo wa wanufaika wa miradi ambayo inafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Tuna mradi mkubwa pale unaitwa mradi wa maji katika Miji ya Geita, Sengerema na Nansio, kwa sababu ya muda, nitajielekeza Sengerema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anakumbuka tarehe 10 Septemba, 2013 yeye aliambatana na Mheshimiwa Rais alipokuwa anafanya ziara Mkoani Mwanza. Tuna mradi mkubwa pale ambao gharama yake ni dola milioni 14. Mradi huu ni mkubwa na unaanzia eneo linaitwa Nyamazugo, lakini ninachotaka kusisitiza na naomba Mheshimiwa Waziri anakumbuka, lakini pia nafahamu Wataalam wa Mamlaka ya Maji Safi Mwanza (MWAUWASA) wako hapa, ambao ndio wasimamizi wa mradi ule; jambo ambalo limelalamikiwa kwa muda mrefu hapa, naomba wazingatie sana kwamba, miradi hii inapoibuliwa, inakoanzia katika ile njia ambako miundombinu inapita, wananchi wanaopitiwa na maeneo hayo wasirukwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusisitiza hapa ni kuhusu maeneo ya Luzunguti, Kongwa, Bungonya, Kakungurus, Nyanguku, Ng'wakhalinga, Kang'wash, Mwaliga 'A' na Mbogwe. Haya ni maeneo ambayo mradi unapita, lakini hayamo katika mradi huu. Sasa

## ***Nakala ya Mtandao (Online Document)***

naomba sana Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Watendaji, naamini wako hapa wanasikiliza kwa makini, shirikianeni na MWAUWASA kuhakikisha kwamba, maeneo haya yanakuwemo ndani ya mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini iko miradi mingine ambayo tunaendeleanayo katika utekelezaji. Nataka nitambue utekelezaji wa miradi iliyoko ndani ya Mpango wa Tekeleza Sasa Kwa Matokeo Makubwa. Miradi hii ni mingi, lakini pia nizungumze kwa niaba ya mwenzangu hao, Mheshimiwa Dkt. Tizeba, yuko hapa jirani yangu, kuhusu Jimbo la Buchosa. Tunaomba miradi yote ambayo imeainishwa katika mpango huu wa *BRN*, fedha ambazo zilitengwa mwaka jana zitoke, ili ikakamilishwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba, sasa hivi fedha zilizotoka hazifiki hata 50%, lakini tunafarijika na ahadi ya Serikali kwamba, muda si mrefu ndani ya Mwaka huu wa Fedha, siku za mwisho za mwezi huu, fedha itatoka iliyokuwa imekasimiwa mwaka jana ili kuweza kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilisisitize katika hili ni ile awamu ya pili ya mradi huu unaotekelezwa pale Sengerema mjini. Nafahamu kwamba, tarehe 17 mwezi huu Mkandarasi atapatikana na tumeahidiwa na Serikali hapa kwamba, Mikataba hii ya utekelezaji wa miradi hii inatarajiwa iwe imesainiwa ifikapo mwezi wa Nane mwaka huu. Naiomba sana Wizara, izingatie ratiba ya utekelezaji wa mradi huu kwa sababu, kinyume chake wananchi wataendelea kunung'unika, lakini kwa kweli, hatutakuwa tunawatendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maombi katika Wizara ya Maji. Mheshimiwa Waziri anafahamu, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu, Mheshimiwa Katibu Mkuu anafahamu na Watendaji wengine; nimeomba miradi ya maji mipya katika maeneo ya Lubungo ambako ndio sehemu ya Ziwa. Tunataka kupeleka maji katika Vijiji vya Kainingu, Nyasigu, Nyabira, Nsota pamoja na Ngoma 'A'. Tuna ombi letu kuhusu Kijiji cha Mabanda hadi Kasomeko, Nyantakubwa hadi Kasungamire. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Watendaji wazingatie maombi haya ambayo tumeyaweka, lakini pia tunaendelea kuishukuru Serikali kwa utekelezaji wa miradi ya Buyagu, Karangala hadi Kitoto anakotoka Mbunge wa Jimbo la Sengerema. Mradi huu pia unatarajiwa kufikisha maji katika eneo la Mlaga na Isore. Mradi wa Kahumuro hadi Nyampande, Kamanga, Chifumfu na miradi mingine kama nilivyosema ambayo iko kwenye Jimbo la Mheshimiwa Tizeba; miradi ya maji ya bomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwigulu Mchemba!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii. La kwanza, nitoe pole kwa Viongozi wenzetu walioondokewa na wazazi wao, dada yangu Martha Mlata na rafiki yangu wa tangu shuleni, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Kiti chako wakati mwingine kiwashauri wanasiasa angalau, pamoja na kwamba, wanasema hujafa hujambika, basi tujenge tabia ya kujali watu wangali wanaumwa. Maana kuna kauli zimetolewa hapa kwamba, Mama yake Zitto alikuwa

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama ilhali hamna Kiongozi hata mmoja wa chama aliyekwenda kumsalimia...

**MBUNGE FULANI:** Acha kupotosha wewe. Acha uongo wako.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Wala kumtumia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu, nenda kwenye hoja. Kuna *very serious topic* hapa, nakuomba nenda kwenye hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo la uwongo! Kuhusu utaratibu! Kuna jambo la uwongo!

**MBUNGE FULANI:** Fanya heshima!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na jambo la kwanza. Jambo la kwanza Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana kuhusu fedha ambayo iliahidiwa na Serikali. Niwahakikishie kwamba fedha ile imeshakuwa tayari iko kwenye utaratibu wa kibenki, kwa hiyo, muda wowote itakuwa imeshaingia kwenye akaunti husika kwa ajili ya utekelezaji na ni Shilingi bilioni 80. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye nishati, sisi kama Wizara, tumesema vipaumbele vya Wizara itakuwa nishati, maji na mambo mengine yale ya Matokeo Makubwa Sasa.

Kwa hiyo, tumesema, tumeanzia katikati lakini tunakoendelea tutahakikisha tunaenda na utaratibu wa kuhakikisha tunatoa hizo fedha kadiri ya ratiba ili kuweza kuhakikisha kwamba miradi hiyo haikwami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nifafanue tu baadhi ya mambo ambayo yamesemwa hapa. Jambo la kwanza, Waheshimiwa Wabunge wamejiuliza sana kwamba kwa nini fedha hizi hazikutoka? Naomba nikukumbushe kwamba mwaka 2013 bajeti ya Wizara ya Maji tuliirudisha tukaipa siku ya Serikali kushauriana na Kamati ya Bajeti, nami ndio nilitoa hoja hiyo. Tukawa tumeanzisha chanzo kipya cha kuongeza bajeti ya Serikali ambacho kilikuwa kinapata Shilingi bilioni 178.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba kodi ile haikukusanywa. Nami niseme tu kwamba tunapokuwa tunapitisha bajeti hizi, kama viongozi, ni vyema sana tukawa pamoja kwenye hamasa ya mapato. Tulipitisha fedha ile tukijua kwamba itakwenda na kwenye maji kwa namna kwamba ingepatikana ingeweza kusababisha Serikali ipeleke ile Shilingi bilioni 178 ambayo ingeongeza Mfuko na ingeweza kwenda kwenye maji. Lakini haikufanyika na walikuwepo wengine ambao walishawishi kwamba hilo lisifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengine ya hamasa ya kodi ambayo tumekuwa tukifanya, lakini lengo lake ni kwanza tuweze kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimekuwepo lawama nyingine zinazosema tatizo ni Wizara ya Fedha, na wengine hata wanasema mbona TRA imeshakusanya asilimia 90. Niwaambieni, hata kama TRA ingekusanya asilimia 100, maana yake ile ingekuwa ni asilimia 52 mpaka mpaka 57 ya bajeti nzima. Hata kama mapato yote ya ndani kwa sasa tungekusanya kwa asilimia 100,



## ***Nakala ya Mtandao (Online Document)***

maana yake ingekuwa ni asilimia 62 ya bajeti. Ndiyo maana tunasema, changamoto tuliyonayo ambayo Wabunge wote, kama Viongozi tunatakiwa tushirikiane kwanza, ni namna ya kuweza kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalisema kuwaomba Waheshimiwa Wabunge mje muunge mkono jitihada ambazo kama Wizara tunachukua kuweza kuongeza mapato. Moja niliisema katika maswali, niliisema siku naapa na niliisema juzi wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Nishati katika kupunguza misamaha ya kodi na kutengeneza Sheria ambayo itaziba mianya ya kukwepa kodi na ambayo itaimarisha usimamizi wa fedha za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hapa siyo kwamba fedha zipo Wizarani zinakwama, linalokuwepo ni kwamba, fedha nyingi za miradi nyingine tunategemea kutoka nje ambazo wanatoa wakipata.

Kwa hiyo, tunachotakiwa ni sisi kama Viongozi tutumie utaratibu wetu wa kisheria na wa kihamasa kuweza kuhakikisha kwamba mapato yanayopatikana yanatosheleza na hapo kama fedha zitakuwepo na zisitoke, hapo lawama itakuwa ni sahihi.

Kwa hiyo, kwa wakati huu nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, ameshajitahidi sana mpaka sasa, nakushukuru ulifika mpaka Kinampanda, tumepata maji Mingela, Ndago, Ng'anguli na umeahidi Ulemo na Kinampanda na Makunda na vijiji vingine kama Mlandala. Kwa hiyo, tunalotakiwa kwa sasa, nimpongeze sana Waziri wangu; Mheshimiwa Mbunge ambaye yupo na kwenye *Budget Committee* na yeye amerusha lawama kwa Mheshimiwa Waziri.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, kama tatizo siyo upatikanaji wa fedha, lawama kwa Wizara na kwa Mheshimiwa Waziri ingekuwa sahihi. Lakini kwa sasa mimi nadhani mnetia moyo Mheshimiwa Waziri. Kwa sisi ambao tunamsaidia, tumeona mipango ilivyo mizuri na mtaiona tofauti kwa bajeti hii tunayoanza nayo kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba tu muunge mkono jitihada hizi ambazo tutakuja nazo ambazo ni za kisheria.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwigulu. Sasa namwita Mheshimiwa Mwandsya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Pili, naungana na Bunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuwapa pole wote ambao wamefiwa, nadhani tuliwasahau katika orodha ile Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro ambaye amefiwa na dada yake, nampa pole; na vile vile tulimsahau Mheshimiwa Lukuvi, amefiwa na baba mkwe; pia Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Mlata kwa kweli wote tunawapa pole na tunaomba Mwenyezi Mungu awape subira wao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kujaribu kutoa ufafanuzi wa misingi ambayo inatumika kugawa rasilimali kidogo tuliyonayo hasa kwenda kwenye Sekta ya Maji. Nafanya hivyo kufuatia michango ya Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Kirigini na Mheshimiwa Christina Mughwai. Kuna misingi ifuatayo; kwanza, aina ya vyanzo. Hii siyo nchi

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

nzima itakuwa na aina ya vyanzo vinavyofanana. Kuna mvua, kuna maji chini ya ardhi, kuna chemchemi, kuna mito na kuna maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni umbali wa vyanzo vya maji kutoka watu walipo, nacho ni kigezo kikubwa. Tatu, ni kina cha uwepo wa maji chini ya ardhi. Inaweza kuwa chini sana, kati na inaweza kuwa juu; nayo ni sehemu mbalimbali za nchi zinatofautiana.

Nne, ni teknolojia na jinsi hiyo teknolojia inavyofaa katika maeneo mbalimbali ya nchi. Kwa mfano, visima; kuna visima virefu, visima vifupi, visima vya kati; kuna maji ya mtiririko, kuna mabwawa, kuna maji ya mapaa ambayo tunasisitiza katika maeneo mbalimbali hasa katika maeneo ya Taasisi zetu. Kwa hiyo, kuna aina nyingi sana za teknolojia na vile vile aina za vyanzo vya maji, na haviko *uniform*, yaani haviko sawa sawa nchi nzima.

Tano, ni idadi ya watu, na vile vile idadi ya watu kwa kilomita moja ya mraba. Sita, ni mtawanyiko wa watu; wengine wako karibu sana na wengine wako mbali sana. Yote hii inaingizwa katika gharama ambayo ni kigezo cha saba. Gharama na vile vile bei ya teknolojia inayotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yote haya haiwezekani kabisa Mkoa mmoja ukawa sawa sawa na Mkoa mwingine mambo yote yakiwa sawa.

Halafu lingine limezungumzwa na lawama zimeelekezwa sana kwa Mheshimiwa Profesa Maghembe kama vile anajipendelea kwa kupeleka fedha nyingi sana Mwanga. Mwaka 2013 nilijaribu kueleza, lakini labda kwa sababu hali yangu ya afya ilikuwa siyo nzuri, labda hamkunielewa vizuri sana au wala hamkunisikiliza, mlikuwa mnanipa pole tu, mnamniona huruma.

Narudia tena, huu mradi wa Same, Mwanga na Korogwe, sisi tuliuita wakati ule mradi wa Same, Mwanga, Korokwe, *Orkesmet* na umo katika mpango wa maendeleo ya Sekta ya Maji. Wala Mheshimiwa Profesa Maghembe hakuhusika kabisa katika uandaaji wa *program* hiyo. Wala hakuwepo wakati huo katika Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 Mkurugenzi wa *BADEA* alikuja hapa Dodoma ndipo tulipoanza mazungumzo kuhusu rasilimali fedha kwa ajili ya mradi huo, wakati huo Mheshimiwa Maghembe ni Waziri wa Elimu, wala hana habari kabisa na huo mradi, nami mwenyewe nilizungumza na huyo Mkurugenzi wa *BADEA*. Halafu yaliyofuatwa kwa kweli mimi nashukuru kwamba wenzangu baada ya mimi kutoka, wameusukuma na sasa tunakamilisha ifikapo Septemba, kupata fedha kutoka *BADEA*, kutoka Mfuko wa Saudi, kutoka *Kuwait Fund* na kutoka *Opec Fund*; karibu kila kitu kipo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kwamba Mheshimiwa Maghembe asilaumiwe kabisa. Kama analaumiwa, labda maji vijijini Mwanga, kama Mbunge lakini siyo kama Waziri. Hii ndiyo asili ya ule mradi. Mradi wenyewe utaipatia maji Miji miwili ya Same na Mwanga; Vijiji 38 vya Mwanga, Same na Korogwe na utahudumia watu zaidi ya 400,000.

Kwa hiyo, labda niseme tu kwamba wakati huo tunaandaa huu mradi, Mheshimiwa Maghembe alikuwa Waziri wa Elimu.

Kwa hiyo, mimi nachukua lawama yote hiyo kwa sababu nilihusika katika uandaaji wa mradi huu. Naomba kwa hili, asilaumiwe yeye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu maji Mvomero. Mvomero ni Wilaya kubwa na Jimbo hilo la Mvomero ni kubwa sana, lina kilomita za mraba 7,000 na zaidi kidogo, ambayo ni

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

zaidi ya nusu ya Mkoa mzima wa Kilimanjaro. Jimbo moja! Sasa kupeleka Shilingi bilioni moja, kwa kweli ni kitu kidogo sana! Kabisa, kabisa! Tuna kazi kubwa sana, kupeleka maji kwa watu zaidi ya robo milioni kwa watu wa Mvomero ni kiasi kidogo sana, ni kama tone ndani ya bahari. Kwa hiyo, kwa kweli asilaumiwe hata kidogo Mheshimiwa Makalla! Ana kazi, nami namwonea huruma sana, ana kazi kubwa sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, kwa jinsi tunavyofanikiwa, kwa mfano kupeleka maji katika maeneo fulani ya nchi, ndivyo ambavyo kwa kipindi kinachofuata tunakuwa na fedha nyingi zaidi kupeleka maji katika maeneo mengine ya nchi. Kwa hiyo, tusiwalaumu watu wanapopata maji katika kipindi fulani kwa wakati ule wakati haiwezekani kufanya kazi hii kwa nchi nzima kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niseme kwa uhakika kabisa, kwamba wananchi wa Same, Mwanga, Korogwe, Simanjiro kwa maana ya Orkesmet, kwa kweli wana haki ya kupata maji safi na salama kama wananchi wengine wa nchi hii! Wawepo hao Mawaziri au wasiwepo, ni kazi ya Taifa kuwapelekea maji. Ni wajibu wetu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 20!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii nami niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji nikiwa kama Naibu Waziri. La kwanza, nami niungane na wenzangu kuwapa pole Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Martha Mlata kwa kumpoteza mama na baba.

Pili, nami nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kuniamini na kunipa nafasi ya kuwa Naibu Waziri wa Maji, maana yake ni kwamba nilikuwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; nayo nimeitendea haki kama Mheshimiwa Idd Azzan alivyosema, lakini niwatoe hofu kwamba hata hii Wizara nitaitendea haki vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru sana wananchi wa Mvomero. Nasimama hapa kwa heshima kubwa kwa sababu yao. Nasimama hapa kuwashukuru sana kwa kunipa ushirikiano, hatimaye katika Jimbo ambalo amelisema Mheshimiwa Profesa, ni Jimbo kubwa sana, lina vijiji 115, lakini katika vijiji vyote hivyo, nimezunguka, nimejionea, nimetoa mchango na nimeshirikiana nao. Nawapongeza na Kamati ya Siasa wako hapa, Mkuu wa Wilaya na Mwenyekiti wa Halmashauri na Mwenyekiti wa Chama na Sekretarieti tumefanya kazi kubwa sana kuwahudumia wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Maghembe. Kwa kweli kufanya kazi na Profesa, unafaidi vitu vingi sana. Ni mzee makini sana, ni Mwalimu mzuri sana na kwa kweli naweza nikasema katika Manaibu Waziri wanaofaidi kwa kupewa ushirikiano, mimi naweza kuwa napata upendeleo mkubwa sana kutoka kwa Mheshimiwa Maghembe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wale wote ambao wanatengeneza fitina ya kutufitinisha, hapana, ikome kabisa! Ni kwamba mimi na Mheshimiwa Profesa Maghembe mambo yetu ni safi kabisa na ninafanya kazi kutokana na maelekezo yake na maagizo yake. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba Profesa chapa kazi, mimi nakuaminia sana, unanipa ushirikiano mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Kamati, imetoa ushauri mzuri, lakini pia wametupa ushirikiano mzuri sana, Kamati inayoongozwa na Profesa tena, Waziri wa Maji ni Profesa,

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mwenyekiti wa Kamati ni Profesa akisaidiwa na Makamu wake Mheshimiwa Said Nkumba. Kwa kweli wameendelea kutupa ushirikiano mkubwa sana, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naipongeza hotuba ya Kambi ya Upinzani. Kwa kweli ni tofauti kidogo na hotuba nyingine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Sakaya nakupongeza sana kwa hotuba nzuri ambayo haijapishana sana kwa sababu wewe ni Mjumbe wa Kamati.

Kwa hiyo, takwimu nyingi umezipata kwenye Kamati na mawazo yale yote siyo ya kipanzani sana umeyatoa kwenye Kamati. Nakupongeza sana kwa hilo, kwa sababu umeitendea haki kuliko hotuba nyingine ambazo zimekuwa zikitolewa za kushutumumu na kila kitu, lakini wewe nakupongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri sana, kwa sababu mmetoa michango mingi ya kujenga, lakini hawakosekani wa kulaumu kwa sababu binadamu wote hatuwezi kuwaza jambo moja kwa wakati mmoja. Lakini pia katika ukosoaji upo ule wa kujenga na ushauri. Vile vile nataka niseme kwamba, ni wajibu, kwa sababu kuna msemu unasema, ukiwa unajua tatizo, nawe huonyeshi njia ya kutatua tatizo, wewe pia ni tatizo.

Kwa hiyo, ushauri mlioutoa, nyinyi hamtaki kuwa tatizo, ni kutuelekeza ili tufanye kazi. Sisi tutawafanyia kazi, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja. Katika siasa, nimejifunza kwa nyakati tofauti vitu viwili. La kwanza, nilikuwa nasoma falsafa ya maandalizi ya Umma. Maandalizi ya Umma falsafa hiyo inasema, Umma hauandalizi kwa nguvu, unakubali wenyewe na hasa ukiwa na agenda, ukiwa na watu, pia ukitoa matumaini.

Kwa hiyo, harakati zozote, wakati wa kuandaa Umma, ukiwa na vitu hivyo, Umma huwezi kuulazimisha, utakubali wenyewe. Hili ndilo Chama cha Mapinduzi kinajivunia. Kwa sababu tulikwenda na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaeleza katika ukurasa wa 119, imeeleza kuhusu Sekta ya Maji na ahadi za maji. Kwa hiyo, kama Chama Tawala, ni lazima tutekeleze ilani hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachofanya Mheshimiwa Kinana, ni kufuatilia utekelezaji wa Ilani hiyo ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu yeye ndio Katibu Mkuu wa Chama. Ilani ile ni ya Chama cha Mapinduzi, yeye kufuatilia, kuna dhambi gani? Hakuna dhambi! Lakini lingine Mao Tse Tung alisema hivi, *“ukiona adui yako anakupongeza kwa jambo, jambo hilo liache mara moja. Lakini ukiona adui yako anakukosoa, jambo hilo ni jema, lifanye sana.”* *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi niseme, Mheshimiwa Kinana kwa sababu unakosolewa, fanya sana hii kazi ya kupitia miradi na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nililojifunza ni kuhusu *propaganda*. Kwanza kuna mtu mmoja anaitwa Joseph Gobes, alikuwa *propagandist* mkubwa wa Hitler. Moja ya jambo lake kubwa aliloliweka akilini mwake, ni kwamba ukitaka kufanya uwongo, tengeneza uongo ulio mkubwa, lakini pia urudie rudie sana ili Umma uamini. Sasa hatuwezi kuacha mambo mengine yakapita hivi hivi bila kujibiwa. Maana yake ni nini?

Pia katika hotuba ya Upinzani kuliingizwa vigezo kwamba Watawala wanaeneza mambo na mafanikio ambayo hayapo. Sasa huu ni uwongo mkubwa, lakini ukiachwa upite hivi hivi, utaendelea kujirudiarudia halafu baadaye utaaminika.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, watawala hawaenezi mambo ambayo hayafanyiki. Tulianza utekelezaji wa Matokeo ya Haraka Sasa, lakini huko nyuma kila mwaka idadi ya watu kwa mwaka wanaopata maji ilikuwa 200,000, lakini baada ya utekelezaji wa BRN, watu milioni 2.6 wanapata maji katika mpango huo. Sasa haya matokeo unataka nani ayatangaze kama siyo watawala na Chama Tawala chenyewe? Ni lazima watangaze mambo haya, na hayawezi kupita hivi hivi! *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunatangaza kile ambacho tutafanikiwa na kile ambacho tuna mipango nayo tutawaeleza wananchi na kutoa matumaini, kwa sababu tunayo dhamana hiyo ya kuwahudumia Watanzania. Kwa hiyo, leo tunakamilisha miradi 248, haya ni matokeo makubwa, lakini mikataba katika vijiji 1,555 imeshasainiwa na ikikamilika, watu milioni nane watapata maji. Kwa nini tusitangaze mambo haya? Kuna dhambi gani? Kwa hiyo, ni vizuri tuendelee kuyasema ili wananchi waendelee kutuamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumesemwa, namshukuru sana Profesa ameeleza vizuri kuhusu suala la upendeleo. Mimi nataka kusema tu kwamba hii ni nadharia ambayo inaanza kujengeka na kutugawa Watanzania. Kama tungekuwa na nia mbaya, Mheshimiwa Rais asingehidi maji pale Karatu ambalo ni Jimbo la Upinzani, na amekwenda kuzindua mradi ule. Kwa hiyo, tuache haya mambo, na bado tumepanga katika mipango kwamba tutatekeleza mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alisimama Mbunge wa Jimbo akapongeza, alisema Mheshimiwa Pareso hapa, itakamilika lini? Tunasema, tunapeleka hela, hilo ni Jimbo la Upinzani. Lakini leo hata pale Jijini Mwanza kuna Majimbo mawili ya upinzani. Kuna hela nyingi inapeleka pale kutekeleza mradi mkubwa. Hapo, katika maeneo yale yote ambayo hayapati maji katika miinuko, mradi huo anatafutwa Mkandarasi wa kusanifu, utanzwa kutekelezwa. Lakini pale tungekuwa na nia mbaya, tusingefanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa yote, wapo ambao ni Wabunge wa Upinzani, hatuwezi kubagua, lakini mwisho wa yote tukienda huko, wananchi wataelewa, nani kafanya jambo hili? Tuwaachie wapiga kura wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, nimwambie tu dada yangu Mheshimiwa Buyogera, nimtoe wasiwasi; ameeleza kwa chungu suala la Kasengeza na Nyarugusu. Lakini nampongeza kwa jambo moja, ana imani kubwa na Chama cha Mapinduzi. Kwa sababu amesema katika mchango wake wa maandishi, inakuwaje Jimbo ambalo Mbunge wa Viti Maalum anatoka hapo, na ni Mwenyekiti wa UWT, sasa ni wa Chama cha Mapinduzi; ana imani hiyo, kwamba kuwepo kwake huyu, lazima kuwe na msukumo. Anasema, kuna Mwenyekiti wa CCM anakaa pale, anasema kuna Mwenyekiti wa Halmashauri ya CCM, kwa maana hiyo alikuwa anamwongelea Mheshimiwa Ngenzabuke.

Kwa hiyo, naamini kabisa anafanya kazi vizuri na atasukuma jambo hili kukusaidia wewe ili waweze kupata maji katika Jimbo lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba mengine haya yalikuwa yanachelewa kutokana tu na yule Mkandarasi kwamba alikosa sifa kidogo, kwa hiyo, ndiyo maana kumechelewa. Hakuna hila yoyote! Mimi nikuhakikishie, tutatekeleza mama yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la vijiji kumi ambalo limeongelewa sana na kila Mbunge. Nami niseme tu kwamba, mara ya kwanza kulikuwa na mlolongo mkubwa sana wa kuweza kufanikisha hili; kuwashirikisha wananchi wachange ile asilimia tano, mtafiti yule mshauri

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

atafiti maji, ripoti ipelekwe Wizarani, Benki ya Dunia, mara Halmashauri itangaze, ipelekwe Wizarani, hizo *no objection* na mpaka fedha zote zipatikane ndiyo mradi utekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, mnyonge, mnyongeni, haki yake mpeni. Tumebadilisha tu, kuna mambo yamefanyika ya kuondoa kero hii na mlolongo, na kwamba sasa tumeamua, anayetafiti maji, huyo huyo apewa kazi ya kuchimba maji kusiwe na kisingizio. Pia zile fedha za asilimia tano zinaendelea kubaki pale, zitakuwa za uendeshaji, fedha zitatafutwa kutekeleza miradi hiyo.

Kwa hiyo, nilichotaka niseme tu ni kwamba baada ya kupitishiwa fedha katika bajeti hii, niwaahidi kwamba tutatekeleza kwa nguvu zote na haraka sana ili kuona kwamba vijiji hivyo vinakamilika. Katika hili niseme tu, hata mimi Mvomero kuna vijiji kumi, lakini kilichokamilika ambacho kiko katika majaribio ni kimoja. Sasa ingekuwa ni upendeleo, si ingefanyika vijiji vyote? Ni kijiji kimoja tu katika vijiji kumi. Kwa hiyo, yote hii inathibitisha kwamba hakuna upendeleo katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, niongelee suala la maji Mkoa wa Dar es Salaam. Namshukuru sana Mheshimiwa Idd Azzan kwa sababu yeye ameona jitihada zinazofanyika, ametutia moyo. Lakini kuna wengine ambao hata tungefanya nini, hawawezi kushukuru. Hawataki kuamini tunachokifanya. Lakini leo hapa mimi nimtake Mheshimiwa Mnyika, na wananchi wakusikie, kama leo utakataa bajeti, maana yake hutaki wapewe maji pale Dar es Salaam, kwa sababu mipango ipo. Ndiyo! Mipango ipo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ni kwamba, uzalishaji wa maji sasa Dar es Salaam ni lita milioni 300, mahitaji ni lita milioni 450. Kwa hiyo, upo upungufu wa lita milioni 150. Kwa hiyo, tunachotaka kusema ni kwamba, tunajitahidi ili sasa tukarabati Ruvu Chini, tutandaze mabomba, na kazi imefanyika. Lakini Ruvu juu pale, kama mtu haamini, aende aone.

Katika chanzo, upanuzi na sasa kazi ni kuchimba kuweka mabomba kuja Dar es Salaam na uchimbaji wa visima vya Kimbiji na Mpera, na tarehe zimewekwa, Mheshimiwa Waziri alitoa kauli hapa kila mradi utakamilika lini. Sasa hatuna jambo lingine lolote la kuweza kusema zaidi ya hayo. Tuacheni tu jamani, tuwezesheni fedha sisi tukatekeleze.

Tatizo la maji, mpaka mwakani Dar es Salaam kufika mwezi Septemba/Oktoba tutakuwa tumelitatua kwa kiasi kikubwa sana. Naomba mtuamini. Mheshimiwa Mnyika, tuwezesheni leo fedha, tupitisha, sisi tukafanye kazi jamani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Mheshimiwa Mnyika anasema jamani kulikuwa kuwe na Kikao Ikulu, tujadili jambo hili. Sasa Wizarani hizi zote ni za Mheshimiwa Rais mwenyewe, lakini Mheshimiwa Rais naye anampa kipande kwamba Mheshimiwa Profesa Maghembe nakupa maji. Sasa Mheshimiwa Rais anamwamini Profesa Maghembe na Mheshimiwa Makalla katika Wizarani ya Maji. Kwa hiyo, sisi tutatekeleza kwa niaba yake!

Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba siyo vizuri kuanza kumsikingizia Mheshimiwa Rais kwamba ameshindwa kutekeleza ahadi. Sisi tumepewa majukumu hayo, tutayafanya. Kwa sababu hiyo, mimi nataka niseme kwamba, huwezi kuchagua *nurse* wakati uko tayari kujifungua. Huwezi kuchagua kwamba nataka *nurse* fulani tu anihudumie, hapana. Sisi ndio tupo tunafanya kazi hiyo leo, utuamini tu. *(Makofi/Minong'ono)*

**WABUNGE FULANI:** Umedhalilisha wanawake!

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwamba, kufikisha meseji ni kwamba, huwezi kwenda Hospitali, ukafika leba ukasema namtaka mtu fulani. Lakini sisi ndio tumepewa majukumu, ni lazima tufanye kwa niaba ya Mheshimiwa Rais.

Lingine niseme tu kwamba liko suala ambalo linahusu Kidunda. Mimi nimhakikishie Mheshimiwa Innocent Kalogeris na Mheshimiwa Dkt. Nkya kwamba Serikali inayo dhamira ya dhati ya kutekeleza mradi huu. Limepigwiwa kelele kwa muda mrefu, wameongea Waheshimiwa Wabunge wengi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani, kwamba lazima kuwe na uhakika wa maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam, na ni lazima bwawa la Kidunda lijengwe.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Innocent kwamba Serikali inayo dhamira ya dhati na kazi itakayoanza ni kuhakikisha kwamba tunalipa fidia na nilifika kule tukaongea na wananchi wa pale Bwira chini. Ni kwamba fidia, fedha zilishatoka Shilingi bilioni tatu, lakini bahati mbaya sana baadaye wakasema kwamba imebadilika; yaani thamani ya pesa na kwa wakati ule inakuwa ni tofauti, ni bora liangaliwe upya.

Kwa hiyo, taarifa ile tunaipokea, ndiyo wanaikamilisha. Ikishakamilika, tutalipa fedha haraka na kitakachoanza kujengwa ni barabara ya kwenda Kidunda halafu baada ya hapo, litafuata bwawa.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba tunayo nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni lile suala la pale Tinde. Nilikwenda Tinde, kuna tatizo kubwa sana la maji. Nilipofika pale, cha kwanza, walichota maji kwenye visima vitatu, wakanipa kwenye chupa ya kisima kimoja, kingine wakampa Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa Ahmed na kingine wakampa Mheshimiwa Aza. Wakasema Mheshimiwa Waziri unywe haya maji, na tunakupa na *Panado* ukizidiwa, basi na dawa hizi hapa. Lakini nilijua kwamba walikuwa wanatufata *head line*, nilikunywa yale maji ya kisima kwa sababu mimi pia ni mtoto wa mkulima, nimekulia huko, nikasema hili siyo tatizo. Lakini niliwaahidi kwamba wafanye utafiti pale Halmashauri, wabainishe maeneo ambayo tunaweza tukachimba maji kwa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ataeleza mpango wa muda mrefu wa maji ya kutoka Ziwa Victoria. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Aza na Mheshimiwa Ahmed kwamba utafiti umekamilika, maeneo mawili yamebainishwa ambayo ni Nsalala na Nchisinuru. Vyote vimeainishwa, urefu wa vile visima vitakuwaje, na kwamba baada tu ya kupitisha bajeti yetu tutawaelekeza Wakala wa Kuchimba Visima kwa dharura wakachimbe kisima maeneo hayo.

Pia nampongeza Mheshimiwa Aza na Mheshimiwa Ahmed kwa kuahidi Shilingi milioni kumi mara tutakapoanza kuchimba kisima kwa maana ya kutandaza hayo maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la bwawa la Mwanjolo, limeongelewa vizuri sana na Mheshimiwa DC wa Meatu na Mbunge, Mheshimiwa Opolukwa kuhusu suala la hasara ambayo Serikali imeipata. Nami bahati nzuri nilifika mpaka Kijiji cha Jinamo, kwa kweli kuna tatizo kubwa la maji. Nimejionea ng'ombe wanafukua maji kwenye mito. Kwa hiyo, bwawa lile lingesaidia Kata karibu tatu au nne na vijiji vingi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie DC, Mheshimiwa Rose Kirigini na Mbunge, kwamba katika miezi mitatu tutafuta Mkandarasi mpya, na baada ya hapo, baada ya miezi mitatu litatekelezwa, kwa sababu hili nililiahidi mbele ya kikao chako Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi. Sisi tutalitekeleza jambo hili na lile suala la kwamba hatua gani tutachukua, nililisea asubuhi, kwamba tutachukua hatua kali ikiwemo kwamba Idara yetu ya Manunuzi kuwasilisha kwenye Bodi ya Wakandarasi ya Usajili ili huyu

## ***Nakala ya Mtandao (Online Document)***

Bwana ambaye alihusika na mradi huu, pamoja na kudaiwa fidia, lakini pia asipate kazi ndani ya Tanzania na nje ya Tanzania na hili litakuwa fundisho kwa watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zabein Mhita naye nimpungeze, niseme tu kwamba suala aliloongelea la Ntomoko tutalishughulikia, lakini pia amekuwa akija Wizarani mara kwa mara kutusumbua kuhusu suala la maji pale Kondoa Mjini, na mwaka huu tumesikia kilio chake, tumetenga Shilingi milioni 400. Kwa hiyo, haya yote tutaendelea kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alisema mtani wangu Mheshimiwa Rose Kamili kwamba Hanang hatujawajali sana, lakini nilikuwa nataka kumwambia tu mtani wangu kwamba hebu jitahidi basi, angalia katika ile miradi ya *quick wins*, Endasaki iko kwako, imetengewa fedha Shilingi bilioni 1.3, angalia mama! Wewe umekwenda tu kwenye ile ya kupeleka katika Wilaya. Maskata iko huko, imepangiwa fedha... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana wewe, namshukuru Mheshimiwa Spika, na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutusikiliza kwa michango mizuri na kwa kututia jasho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kuwapa ple wenzetu ambao wamepata misiba; Mheshimiwa Zitto Kabwe, mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro, Mwenyezi Mungu awajalie na kuwaweka Marehemu hao tuliowataja mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mingi katika sekta yetu. Wabunge 40 waliongea na wakatoa hoja za maji wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge 60 leo wameleta michango yao kwa maandishi na Wabunge 40 ukiwajumuisha Mheshimiwa Prof. Mwandosya, ambaye leo ni Kaimu Waziri Mkuu hapa, na Mheshimiwa Amos Makalla. Jumla ya Wabunge wote waliotoa michango katika hoja yangu hii, ni Wabunge 140. Nawashukuru sana na Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambazo tumezipokea, ni nyingi na ni hoja zenye maana kubwa, nasi tunazithamini sana. Kama ambavyo tulitoa majibu katika hotuba yetu ya mwaka jana, basi na mwaka huu tutatengeneza kitabu cha aina hii na kukigawanya kwenu ili muweze kuona majibu mbalimbali ambayo yametolewa kwa hoja zenu ambazo ni muhimu sana.

Cha muhimu zaidi ni kwamba Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji inafuatilia majibu haya na kuyapitia wakati wa kazi zake. Kwa hiyo, nawashukuru sana, tutaendelea kushirikiana katika kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji katika nchi yetu, ni kubwa sana. Nchi yetu ni kubwa, mahitaji ya rasilimali ni makubwa kwa ajili ya utekelezaji wa hii miradi, lakini tumedhamiria kwamba miradi hii tutaitokeleza kutokana na uzito wa hoja zenu, malengo ya Serikali na nia ya Serikali ya kuhakikisha kwamba zaidi ya watu asilimia 74 wanaoishi vijiji wanapatiwa maji safi na salama ifikapo mwisho wa mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepanga kutekeleza miradi 1,810 katika awamu hii, na kwamba Mungu jalia tukipata Shilingi trilioni 1.45 miradi hii itakamilika bila wasiwasi.



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya vijijini, miradi 1,473 tayari imefanyiwa usanifu, tayari kuna Wakandarasi. Katika miradi 538, Wakandarasi wamefanya kazi na wamefikia hatua mbalimbali kuanzia asilimia 40 mpaka asilimia 95 katika maeneo mengine.

Kwa hiyo, hotuba iliyotolewa hapa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ni jambo la faraja kubwa kwetu sisi. Maana kwa uhakika, wanasema jambo hili kwa vitendo na siku ya leo ya tarehe 2 Juni, tumepokea Shilingi bilioni 80 kutoka kwenye Wizara ya Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Ahadi niliyopewa ni kwamba fedha hizi zitaendelea kutolewa siku hadi siku tunavyokwenda mbele mpaka fedha ambazo zilikasimiwa katika bajeti hii kukamilika kutegemeana na upatikanaji wa fedha za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tunayo taabu kubwa sana ya maji ni katika Miji Mikuu ya Wilaya ambayo iko 96 ambayo ina shida kubwa na Miji mingine midogo kama ile ambayo aliieleze Mheshimiwa Sanga ambaye ni Mbunge wa Njombe Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miji hii katika bajeti hii tumeihudumia kwa nguvu tulivyoweza, lakini kwa ajili ya kuondoa Miji ile ambayo ina matatizo makubwa sana, tumetenga Shilingi bilioni 17.1 kwa ajili ya kupeleka maji kwa dharura katika Miji 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kwamba Miji hii tukiuhudumia kama ambavyo tumehudumia Mji wa Karatu na Mji wa Ngudu, tukirudi tena mwaka kesho, tutakuwa na taarifa tofauti kabisa tunayotoa hapa juu ya watu ambao wamefaidika na juhudi za Serikali katika kutatua tatizo hili ambalo linawasibu wananchi wetu wengi sana.

Mheshimiwa Spika, katika Miji mikubwa, kazi ambazo zinafanywa ni kubwa sana, lakini bado tatizo ni kubwa. Tatizo hili tunakabiliana nalo kwa nguvu kubwa sana. Nawaomba ndugu zangu, mwelewe, watu wanaoishi kwenye Miji Mikuu ni Watanzania, wanaoishi kwenye Miji midogo ni Watanzania, na wanaoishi kwenye Vijiji, ni Watanzania. Juhudi zetu ziwe ni kuhakikisha kwamba Watanzania wote tunawaondoa kwenye lindi hili la kukabiliwa na matatizo ya maji ambayo ni jambo ambalo linaondoa ustaarabu wa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ningependa niishukuru sana Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano mkubwa ambao imeipa Wizara yangu katika kutekeleza kazi zake. Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji imetupa maoni, ushauri ambao imekuwa ikiutoa mara kwa mara na imehakikisha inaangalia miradi yetu ya maendeleo, inafuatilia upatikanaji wa fedha na namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zinatukabili. Naishukuru Kamati kwa shughuli za ufuatiliaji wa fedha zile ambazo ziliongezwa na Bunge katika mwaka 2013/2014 na kuiwezesha Wizara kupata Shilingi za ziada bilioni 184.5.

Aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelekezo ambayo yameanza kutekelezwa ikiwemo upatikanaji wa fedha mara moja, Shilingi bilioni 80 ambazo nimezisema hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeshiriki kikamirifu katika kukagua utekelezaji wa miradi ikiwemo kutekeleza miradi ya teknolojia ya kuondoa madini ya *floride* kwenye maji kule Arusha. Imefuatilia na kuangalia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima kule Kimbiji na Mpera; miradi ya maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Aidha, Kamati imeshiriki kikamilifu katika maadhimisho ya wiki ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki ya maji ni wiki ambayo inatuwezesha sisi pamoja na wananchi kuangalia mahali tulipofika, matatizo tuliyonayo na changamoto zinazotukabili. Wadau wetu katika utekelezaji wa Sekta ya Maji (*water sector development program*) wameshiriki kikamilifu katika kazi hii na wanachangia utekelezaji huo. Katika mwaka uliopita wa

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

fedha wamechangia Shilingi 100 na Serikali imechangia Shilingi milioni moja. Hakuna mabilioni ya fedha yaliyotumika katika kuadhimisha wiki ya maji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na Kamati kuhusu upungufu mkubwa wa wataalam katika Sekta ya Maji, lakini Serikali imeanza kushughulikia jambo hili na mwaka huu imeturuhusu tuajiri wataalam na mafundi 412 na kazi hiyo ya ajira tunaendelea nayo. Aidha, Kamati imetuasa tuchukue hatua kali kuhusu hali mbaya ya hujuma kwenye miundombinu ya maji na baadaye tunategemea kuleta mabadiliko ya Muswaada wa Sheria Na. 12 ya Maji ili kuongeza adhabu kwa wale ambao wanahujumu miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa nielezee hoja ambazo zimechangwiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Moja ya hoja hizi ni tamko ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wakati akitoa majumuisho ya Wizara yake akijibu swali la Waheshimiwa Wabunge tarehe 26 Mei, 2014.

Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alitamka kwamba, Serikali ina mpango wa kuitisha kikao cha Mawaziri wa Mambo ya Nchi za Nje hapa Tanzania zikiwemo nchi ambazo ziko kwenye Bonde la Mto Nile mnamo mwezi Julai mwaka huu ili kupitia mkataba wa ushirikiano wa Bonde la Mto Nile, yaani *Nile Basin Comprehensive Framework Agreement*. Mheshimiwa Waziri alieleza kwamba, mashauriano yatazingatia umuhimu wa mto Nile kwa uchumi wa nchi ya Misri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tamko la Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa limetafsiriwa vibaya miongoni mwa wadau wa mto Nile baada ya vyombo mbalimbali vya habari vya ndani na nje ya nchi kulitangaza na kulisambaza kwamba sasa Tanzania inaanza kuwa Wakala wa Misri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilisaini Mkataba wa Ushirikiano wa Bonde la Mto Nile tarehe 14 Mei, 2010 kwenye kikao cha ufunguzi wa kusaini kilichofanyika Mjini Entebe Uganda tarehe 14 Mei, 2010. Tarehe hiyo pia nchi ya Ethiopia, Rwanda na Uganda nazo zilisaini mkataba huo. Kwa nyakati tofauti, nchi za Kenya na Burundi zilisaini mkataba huu kabla ya tarehe ya mwisho wa kutia saini tarehe 13 Mei, 2011. Hatua ya nchi za Burundi na Kenya kusaini mkataba huo zilitimiza sharti la kusaini nchi sita lilokuwa linatakiwa na mkataba huo ili kuweza kuanzisha Tume ya Bonde la mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusaini mkataba, Tanzania ilianza taratibu za kuridhia mkataba ambapo hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kwamba Waraka Baraza la Mawaziri umekwishakujadiliwa na Kamati ya Makatibu Wakuu, yaani IMTC na kinachosybiriwa ni kufanyika tu kwa kikao cha Baraza la Mawaziri na Waraka huu uko kwenye ratiba. Tayari nchi za Ethiopia na Rwanda zimeridhia mkataba huo na nchi ya Burundi imewasilisha rasimu kwenye Sekretarieti ya Baraza lake la Mawaziri. Nchi ya Kenya na Uganda zipo kwenye hatua za mwisho za kuridhia kama Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mkataba huu, majadiliano yalishafungwa. Hivyo nchi yoyote haina mamlaka ya kuanzisha majadiliano mapya. Nafasi ya majadiliano kwa vifungu vya mkataba ambavyo havijafikiwa na nchi zote, itapatikana baada ya kuundwa kwa *commission* ya Mto Nile kama ambavyo mkataba unasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imesaini mkataba wa ushirikiano wa nchi za bonde la Mto Nile kwa sababu; moja, Mkataba unaimarisha ushirikiano wa matumizi ya rasilimali za Mto Nile kwa kuwa sasa kutakuwa na chombo cha kisheria kinachotambulika na nchi zote wanachama na jamii ya Kimataifa; pili, nchi wanachama zitapata chombo cha kutatua migogoro ya maji itakayotokea baada ya hapo; na tatu, kila njia ya ushawishi imetumika katika

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

kufikia maridhiano kwa zaidi ya miaka kumi bila mafanikio. Hakuna dalili kwamba kusuburi miaka kumi mingine kutabadili msimamo wa nchi mbili ambazo bado hazijatia saina mkataba huo, ambazo ni Misri na Sudan. Tanzania na nchi nyingine zinaafiki mkataba, zinapenda kusonga mbele bila kungojea zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania itaendelea na kutumia maji ya Mto Nile kutokana na maridhiano na nchi nyingine bila kumjali mtu mwingine yeyote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mjadala mkubwa wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali, nami nitajaribu kutoa maelezo ya miradi ile ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa hajaiifikia na miradi ambayo nitaanza nayo ni miradi ya kuzunguka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko mradi mkubwa ambao unafadhiliwa kati ya Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, *European Investment Bank* na Benki ya Maendeleo ya Ufaransa AFD na Serikali ya Tanzania kwa Euro milioni 105. Mradi huo utakamilisha upatikanaji wa maji katika Mji wa Mwanza kwa asilimia 100 kwa 100 kwa miaka 20 ijayo.

Mradi huu umewekewa saina mwezi Machi, 2014 na Viongozi wa *European Investment Bank* na Benki ya Maendeleo ya Ufaransa, walitembelea Mwanza, wakachezewa ngoma, wakaonyeshwa mahali mradi utakapojengwa, wakaonyeshwa watu wanaokaa juu ya mawe.

Kwa hiyo, watu wanaokuja hapa kuanza kuongea kwamba kazi haifanywi kule Mwanza, wamelala. Mko wapi? Fedha zimeshasainiwa, ziko kwenye Wizara ya Fedha, tunangojea sasa Mkandarasi apatikane na mradi uanze kujengwa Mwanza, Magu, Lamadi na Misungwi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo pia zitatumika katika kujenga mfumo wa kuondoa maji taka katika Miji ya Mwanza, Msoma na Bukoba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukawa wakweli. Miradi hii iko katika mpango ambao umeainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Hakuna hotuba yoyote hapa itakayotolewa na kuhalalisha kwamba, sasa chanzo cha mradi huu ni Mbunge fulani bin fulani, hata kidogo! Miradi hii inatekelezwa katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hii, na kwa kuwa miradi hii ni mikubwa, matayarisho yanaweza kuchukua muda, nasi tunajua kwamba Mji wa Magu una matatizo makubwa sana ya Maji; vivyo hivyo, Mji wa Lamadi una matatizo makubwa sana ya maji. Kwa hiyo, mwaka huu, 2014 tumepanga kufanya miradi ya dharura kuondoa hayo matatizo makubwa ili wananchi ambao wana matatizo hayo waweze kupata maji wakati wanangojea mradi mkubwa utekelezwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi ambayo inatekelezwa, Sengerema, Geita na Nansio. Miradi hii awamu ya kwanza imekamika na sasa utekelezaji unaofanywa ni utekelezaji wa awamu ya pili. Nawahimiza Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika maeneo haya, mshirikiane na Mamlaka inayotekeleza miradi hii ambayo ni Mamlaka ya Maji ya Mwanza ili kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa kufikia viwango ambavyo wananchi wanategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Geita, Kampuni ya GGM imetengeneza intake ya maji kwa ajili ya mji ule, ikatengeneza na tanki kubwa la kupokea maji safi na Halmashauri ya Mamlaka ya Mji wa Mwanza imeunganisha tanki hilo pamoja na mtandao ule wa zamani uliopo ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaanza kupata maji wakati huu ambapo mradi unaopanua upatikanaji wa maji pale mjini haujakamilika. Katika mwaka huu wa fedha, Serikali

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

imechangia Dola 400,000 na machimbo ya GGM yametoa Dola milioni moja ili kuongeza usambazaji wa maji kufikia asilimia 35 ya kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mradi huu kukamilika, Mji wa Geita utapata maji na kufikia asilimia 80 na Miji ya Sengerema na Nansio itapata maji ya kufikia asilimia 100 kwa miaka 20 mbele ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga mradi wa Kangongwa, Isaka na Tinde. Maji kwa ajili ya Miji hiyo yatatoka kwenye Bomba karibu na Kahama. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Kahama, kwamba nimetembelea mradi wa maji wa Mjini Kahama na napenda nimpongeze sana Kiongozi wa Mamlaka ile. Mamlaka ile inafanya vizuri na yule Mtaalam ni mtaalam ni mzuri sana na Mji wake tutaupandisha *grade* kutoka *grade* 'C' kuja *grade* 'A' kwa sababu ya *performance* nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama sehemu ya utekelezaji wa mradi kutoka Kahama kwenda Kagongwa, Tinde na Isaka, vijiji vyote ambavyo viko njiani, vitapata maji. Shilingi milioni 500 zitatumika katika kusambaza maji pale Mjini Kahama katika maeneo ambayo bado hayajapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa maji kutoka Mhalo mpaka Ngudu urefu wa kilometa 46. Mradi ule umekamilika na sasa uko katika majaribio na kabla ya mwisho wa mwezi huu tutaukamilisha na kuufungua. Kama sehemu ya kazi hii, tutatoa maji pale Ngudu mpaka Sumve na Malya ili kuhakikisha kwamba wananchi wa eneo lile wote wanapata maji pamoja na vijiji ambavyo vinaunganisha Miji ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko pia mradi wa Meatu, Bariadi na Maswa ambapo Shilingi bilioni sita zimetengwa kwa ajili ya kuongeza upatikanaji na kuondoa shida ya maji katika Miji hiyo. Aidha, kuna mradi wa Mgango, Kyabakari mpaka Butiama ambao tumewekeana saini kati ya Serikali na Benki ya Kiarabu ya BADEA na *Saudi Fund*. Shilingi bilioni 30.9 zitatumika katika utekelezaji wa mradi huo na mradi huo utatekelezwa mwaka huu, 2041. Kwa hiyo, hakuna haja ya kubadilisha *design* ya mradi wa Musoma ili kushughulikia maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kidogo kuhusu mradi wa kupeleka maji kutoka Shinyanga hadi Tabora kupitia Nzega na kupeleka Tawi mpaka Igunga. Wizara yangu ilingia *Memorandum of Understanding* na Kampuni ya Serikali ya Kihandisi ya India inaitwa WAPCOS. Kampuni hii imefanya *feasibility study* na kukamilisha urefu wote wa mradi kutoka Shinyanga mpaka Tabora. Jambo lingine iliyokamilisha ni kutafuta *estimates* au kutafuta makadirio ya fedha za ujenzi wa mradi huo.

Baada ya kazi hiyo, tumepeleka maombi kwenye Serikali ya India na taarifa ambazo tunazo sasa ni kwamba Serikali ya India sasa inatafuta takwimu zaidi ili kukamilisha makubaliano kati yetu na India ili mradi huo upate fedha na sisi tuanze kuutekeleza. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia ndugu zangu, Mheshimiwa Aden Rage, Mheshimiwa Dkt. Khamis Kigwangalla, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga kwamba, mradi huu sasa uko nje, hauko tena chumbani ambako ulikuwa umefungiwa wakati tunajitayarisha kuanza kazi yake.

Kwa hiyo, nawaomba sana Wabunge wenzangu kutoka Nzega, Igunga, Tabora Kaskazini, Bukene kwamba mategemeo ni makubwa na tutakapokuwa tumepata taarifa bomba linapita wapi hasa, tutajua ni vijiji vipi ambavyo viko *mile* 12 kila upande wa bomba na hivyo tutawaeleza wawaeleze wananchi kwamba vijiji vipi vitaanza kutekelezwa.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea leo jambo ambalo liko kwenye moyo wangu sana. Hili ni kuanzisha Mfuko wa Maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumehangaika kweli kweli kujaribu kutekeleza miradi ya maji na kutumia fedha kidogo ambazo tumepata ili tuweze kuwafikia wananchi wengi iwezekanavyo. Kwa wastani, Wizara yangu imekuwa na uwezo wa kuwapelekea maji vijijini watu 200,000 mpaka 300,000 kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha, tumepelekea watu maji 2,640,000. Kazi hii tumeifanya kwa miezi tisa na hakuna hata siku moja tumelala; hakuna hata wiki nzima, tumekaa pale Ofisini kuanzia Jumatatu mpaka Jumamosi, hakuna! Kila siku tumekuwa tunatembelea Mikoa, tunakwenda Wilayani, tunakwenda kwenye Vijiji, nataka nikubaliane na wale Wahenga wanaosema, kinachotolewa na kuwasilishwa ni kile unachosimamia. Kile unachoelezwa kwamba kinafanyika, hakiwasilishwi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, Naibu Waziri ameeleza hapa, kwamba tulikubaliana kwamba tuondoe *no objection*, tulikubaliana kwamba tumeshapata fedha ya kuanza, tuanze utekelezaji. Tulikubalina tuondoe vizingiti vyote vya utekelezaji wa miradi vijijini, tukakubaliana kwamba, sisi, Kamati yetu na Wabunge wote; kila mtu kwenye Jimbo lake, na kila Mbunge wa Viti Maalum, kwenye Mkoa wake, asimamie miradi hiyo, kwa sababu sasa inasimamiwa na Halmashauri yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vizuri kuja Dar es Salaam na kuja huku Dodoma kusema, hamjasimamia hiki, wakati tuligawana kazi hapa, tukasema, tumeondoa *no objection*, kila mtu ajitahidi, ashirikiane na sisi, tuhakikishe kwamba miradi inakamilika. Kweli, katika miezi tisa, miradi 228 imekamilika, na watu zaidi ya milioni mbili wamepata maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kwamba mpaka mwisho wa mwaka huu, 2014 baada ya kupewa hizi fedha tulizotengewa hapa, karibu ile miradi yote 538, ambayo iko katika hatua mbalimbali za ujenzi, itakamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko pia miradi ambayo imesemwa sana hapa, pamoja na hisia za kutoa Shilingi. Mradi wa Bunda, Mbunge wake hawezi kutoa Shilingi, lakini amesema hapa, kama angekuwa anaweza angeitoa. Lakini na taka nimhakikishie kwamba mradi wa Bunda niko nao kila siku. Wale wanaofanya kazi pale, niko nao kila siku; wale wanaosimamia, niko nao, na mmoja wao yuko hapa na wananchi wanashiriki sana. Kati ya mita 25 za mabomba ambazo zinatakiwa kulazwa, zimeshalazwa mita 16 na bomba la urefu wa mita nne, ziko pale zinaendelea kulazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa kwamba huyo Mkandarasi ameanza kupunguza nguvu katika utekelezaji; nami nataka nimpelikee taarifa, kwamba kama haukukamilika katika muda wa mwezi huu hizo kilomita zilizobaki, basi yeye tutaanza kumfanyia utaratibu wa kumstaafisha kwenye mradi wetu.

Jambo la pili, mradi wa Manchira, tayari tumepeleka Shilingi milioni 350 na Mkandarasi ataanza kutafutwa kwa ajili ya kujenga chujio la maji katika bwawa hilo. Aidha, siyo kweli kwamba fedha hazijapelekwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa Mji wa Tarime. Tayari Shilingi milioni 150 zimepelekwa na nimeagiza kwamba mamlaka ya maji pale Musoma watangaze na kuanza kumtafuta Mkandarasi wa kujenga mradi wa maji wa Tarime. Kwa sababu kwenye bajeti tumeweka Shilingi nyingine milioni 500, kwa ajili ya mwaka unaofuata, Mkandarasi akianza kazi sasa ataweza kuendelea na kazi hiyo, kwa sababu fedha zaidi za ujenzi zinakuja.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda pia nimjibu Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ambaye ameuliza maswali *very specific* kuhusu Mji wake wa Ilula. Niseme kwamba nimeshatembelea Wilaya ya Kilolo mimi mwenyewe na Mkoa wa Iringa, na Mamlaka ya Maji ya Iringa inashughulikia hatua za awali za kuondoa taabu kubwa ya maji iliyoko pale. Lakini zimetengwa fedha kwa ajili ya kutoa maji katika chanzo cha maji ya mto karibu na Mji wa Ilula na kuyaleta katika Mji wa Ilula ili kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sasa niangalie hotuba ya Waziri Kivuli katika Wizara ya Maji. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Sakaya kwa hotuba yake. Amejitahidi kweli kuandika hotuba nzuri, na mambo haya kama atayaleta kwenye Kamati, sina shaka kwamba hata Kamati ile kubwa itaweza kujadili mengi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu niseme, tunatekeleza miradi ya maji vijijini kwa sababu tunajua kwamba kuna tatizo kubwa. Hatutekelezi miradi kwa sababu tunafanya usanii, hata kidogo! Tunatekeleza miradi ya maji vijijini kwa sababu kuna shida kubwa. Sasa hivi tumesema kwamba tumefikia asilimia 49 ya upatikanaji wa maji vijijini. Mwanzoni, hata mwaka 2012 nilipoingia kwenye sekta hii, ripoti ya maji vijijini ilikuwa inaonyesha kwamba watu asilimia 57 vijijini, wanapata huduma ya maji. Lakini katika mpango wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo makubwa, (*Big Results Now*), wataalam walifanya *detailed analysis*, wakakuta kwamba kweli iko miradi katika vijiji vingi, ambayo ukijumlisha pamoja kwa Tanzania nzima, inaweza kuwapa Watanzania asilimia 57 maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ikaonekana kwamba miradi mingine ina uchakavu mdogo mdogo na haitumiki, au chanzo cha nishati hakifai na haitumiki. Kwa hiyo, watu ambao wanapata maji hasa, ni asilimia 40. Kwa hiyo, tukaazimia kutoka pale, tutoke asilimia 40 twende mpaka asilimia 74. Tuko njiani, nategemea kabisa kwa fedha tulizopata hapa, hatutagota chini ya asilimia 62. Mungu atulinde huko mbele. Vile vile nakushukuru sana kwa ku-*point out* jambo hili ambalo ni la msingi sana. Mambo mengi ambayo umeyatoa hapa kama taabu za akina mama, hizi ndiyo zinatusukuma tutumie maji vijijini. Natumaini katika hili tutashirikiana ili kuhakikisha kwamba maji yanafika vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mijadala iliyopita, hasa wakati wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ally M. Kessy, alisema, kule Namanyere hakuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda Namanyere, lakini sikutumia petroli bure. Nilipofika kule nilikuta hali ni mbaya sana, hakuna maji kabisa. Tumepeleka Shilingi milioni 100 kununua generator mpya, pump mpya na kununua mabomba ya kusambaza maji katika Mji ule.

Katika maeneo yale ambayo hayakuwa na mabomba mapya, mabomba yale yanaendelea kupasuka na tumetenga fedha, Shilingi milioni 150 kwa ajili ya kulekebisha hali hiyo, na kazi hiyo itaendelea kufanywa mpaka tutakapofikia hatua mbapo mradi wa bonde la Ziwa Tanganyika utatekelezwa. Kwa maana hiyo, namwomba Mheshimiwa Keissy avute subira, maana utengenezaji wa maji katika Mji ule utaendelea vizuri kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia niongee juu ya utekelezaji wa mradi wa maji katika Mji wa Gairo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Gairo umetekelezwa chini ya *Water Sector Development Program*, tangu mwaka 2010, na ujenzi wa Mji ule umefanywa ukitumia chanzo cha maji cha visima, nadhani ni visima vitatu, sina uhakika, lakini visima vimetekelezwa na mfumo wa maji mzima umejengwa, isipokuwa visima vile vina chumvi nyingi sana.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, chumvi inayoruhusiwa kwenye maji kitaalam, ni *electrical conductivity* 2000. Maji yale yana *electrical conductivity* ya 8000, kwa hiyo, hayafai.

Wizara inaendelea kutafuta mtambo wa kuchuja chumvi hiyo ili yafae kunywa. Lakini sasa hivi vinachimbwa visima ambavyo niliagiza nilipotembelea Mji wa Gairo; kisima cha kwanza kimeshakamilika na kingine kinachimbwa hapo, ambavyo vinategemewa kuwa na maji baridi na maji hayo yatapelekwa kwenye tenki kubwa lililopo ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji wakati ambapo wanangojea mradi wa mto, kaskazini ya Mji ule kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza pale awali, hoja ambazo tunazo ni nyingi, ziko hoja kutoka kule Kondo, kutoka Makambako, kutoka Maji taka Dar es Salaam, nataka tu kuwaeleza kwamba kule Dar es Salaam, maji taka tumetenga Shilingi bilioni 10 mwaka huu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Toa hoja!

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. SAADA S. MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja hiyo, imeungwa mkono, Katibu!

### **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

### **Fungu 49 - Wizara ya Maji**

Kif. 1001- *Administration and HR Management*... ... Tshs. 3,946,173,400/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni zetu, majina nimeshayapokea. Tutatazama kwa namna tunavyokwenda, tukiweza tutaongeza wachangiaji kutegemea ushirikiano wenu utakavyokuwa unakwenda. Ninaanza na Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia miradi ambayo imekwama, hasa ile ya BRN. Miradi hiyo ni ya vijiji vya Majalila, ambao una thamani ya Shilingi milioni 543; mradi wa Kijiji cha Igagala, wenye thamani ya Shilingi milioni 407; mradi wa Kijiji cha Sarema, sambamba na mradi wa Kijiji cha Mwese.

Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie miradi hiyo inakamilika lini na fedha zitatumwa lini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Majalila, Igagala na Mwese ni miradi ambayo inatekelezwa chini ya Tekeleza Sasa kwa Matoke Makubwa.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Kama ambavyo tulieleza katika bajeti yetu, miradi hii haikukamilika kwa sababu tulipata kiasi kidogo sana cha bajeti, na raha ambayo tunayo hapa leo ni kwamba tumeanza kupewa fedha na leo tumepewa Shilingi bilioni 80. Kwa hiyo, tutaendelea kuitekeleza hii miradi kwa *BRN*, kwa kadri ambavyo tunaendelea kupokea fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye hotuba yangu, nilipenda Waziri alieleze Bunge kuhusiana na mradi wa vijiji 10, na nikaeleza mchakato mzima kuanzia mwanzo kwa jinsi ambavyo ule mradi unaanza kwamba, wataalam waelekezi wanapewa kazi ya kwenda kufanya utafiti. Nikaeleza kwamba katika Wilaya zote, wale wataalam waelekezi walikwenda kufanya utafiti kwenye vijiji vile na asilimia 70 ya vile vijiji, havikupatikana na maji, lakini wakati huo walikwaa wameshalipwa fedha zote na wameondoka na hakuna kilichofanyika.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka kujua, kwanza, ni hatua gani zimechuliwa kwa fedha ambazo zilikuwa zimeshachukuliwa na wale wataalam waelekezi, kwa sababu walichukua asilimia 10 ya mradi. Kwa hiyo, mradi wa milioni 210, asilimia 10 imekwenda kwa mtaalamu mwelekezi; wamechukua fedha na maji hayakuonekana. Walivyokwenda wachimbaji, maji hayakuonekana katika vijiji zaidi ya asilimia 70 ya vijiji vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nikataka kujua, wale wananchi ambao waliambiwa kwamba maji yapo kwenye vijiji vyao, walipokwenda wachimbaji hawakupata maji, na mpaka leo Serikali imekaa kimya tangu mwaka 2010; mpaka leo wananchi wameweka fedha yao benki, inaendelea kukatwa makato, hakuna kinachoendelea na hakuna mpango mwingine wowote wa Serikali kuhakiksha kwamba vile vijiji vinapata maji.

Kwa hiyo, nataka nijue kwanza kabisa kwamba, hatua gani zimechukuliwa kuanzia zile fedha ambazo zimeliwa na wataalam elekezi, lakini la pili, nini hatima ya wale wananchi ambao vijiji vyao vimekosa maji, nini mpango ulioandaliwa na Serikali waweze kupata maji ili fedha yao ambayo iko benki, iweze kufanya kazi kwa ajili ya kuwaletea maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa tahadhari kwamba, kama sitapata majibu ya kutosha, nitakamata Shilingi ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Sakaya kwa swali lake. Niseme tu kwamba, siyo kweli kwamba asilimia 70 ya visima havikupata maji, hii siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na utalam na teknolojia iliyoko sasa ya kutafuta maji chini ya ardhi, *success rate* ni 70%. Hakuna au *method* au *new technic* ambayo unaweza kuitumia kwa kuchimba *mass drilling* ukapata zaidi ya 70% *success*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu yake ni kwamba katika miamba chini ya ardhi, kuna maeneo ambayo unaweza kuwa na kidimbwi cha maji kama ambavyo unaweza kuwa na dimbwi juu ya ardhi ukadhani kuna maji na ukichimba utakosa. Lakini kuna maeneo mengine pia ambayo yana *elements* ambazo zinashabihiana na maji katika ile teknolojia. Lakini ile teknolojia kuna *a few chances* ambazo zinaweza kutokea, ukapata jawabu kama kuna maji, halafu ukichimba usiyakute. Hiyo ndiyo inapunguza *success rate*.



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Kwa hiyo, kama yakifanywa vizuri asilimia ya success haiwezi kuzidi asilimia sabini kwa maana kuzidi *significantly* kitakwimu (*statistical significance*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi ule mradi ulivyokuwa umepangwa na ni makubaliano yenye *memorandum of understanding* kati ya Serikali na wale washirika wa maendeleo ambao wamechangia *basket* ya maji kwamba Mhandisi yule anayepima kutafuta maji atakuwa ni Mhandisi tofauti na yule anayechimba. Kwa hiyo, yule mtu alipopima anangoja yule anayechimba, baada ya kuchimba na mradi kuwa tayari anakuwa na mkataba wa kusimamia na kupima na kusimamia ni *ten percent* ya *value* ya huo mradi, hayo ndiyo yaliyokuwa makubaliano. Kwa bahati mbaya, matatizo kama haya yametokea, ndiyo maana mwaka jana tukasema tunatenganisha kabisa. Kama unaomba kuchimba visima ni lazima wewe uweze kuwa unayechimba na sisi tunataka kisima chenye maji, si kisima chenye *probability* ya kuwa na maji, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, katika wale watu ambao vijiji vyao vimechimbwa hapakupatikana maji, tuna maagizo *specific* kwa Wahandisi wale ambao wako kwenye mabonde katika maeneo yao, kama ni Dodoma na Singida ni bonde la kati, kama ni Kigoma ni bonde la Ziwa Tanganyika na kadhalika, wafanye *survey* kuhakikisha wanakuta maeneo ya kuchimba na miradi ile yote inaingizwa kwenye utekelezaji katika mwaka huu wa fedha kwa jinsi ambavyo tutapata fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo natoa shilingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hapa anatuambia kwamba *success rate* ni asilimia sabini lakini nilitoa mfano halisi kwenye hotuba yangu. Kwa mfano, Wilaya ya Urambo ambayo tulipata vijiji 12 vilivyoingia kwenye mradi ni vijiji vitatu tu vilionekana vina maji. Hivi leo tunavyoongea vijiji vyote tisa vingine havikupata maji na mpaka leo hawajui kinachoendelea na hela yao iko benki. Leo Waziri anatuambia kwamba ametoa maagizo kwa Wahandisi wa Mabonde waende wakaangalie vile vijiji; tangu mwaka 2009/2010 mpaka leo ni miaka mine au mitano, hata ninavyoongea hapa wananchi wanapiga simu hawajui kinachoendelea. Ni hakika kwamba majibu ya Mheshimiwa Waziri yako juujuu, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge wanyanyuke wachangie hoja hii, mradi ambao ulileta matumaini makubwa kwa Watanzania, wamejinyima wamechangia fedha zao benki, mpaka leo hawajui kinachondelea, majibu yanayotoka hapa ni majibu ya kuwapa matumaini, wanataka maji hawataki maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shilingi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Christina, Mheshimiwa Mkiwa, Mheshimiwa Rajab, Mheshimiwa Mgalu, Mheshimiwa Assumpter, Mheshimiwa Sitta, Mheshimiwa Kisangi na Mheshimiwa Silinde.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

**MWENYEKITI:** Sijakuita bwana, kaa. Haya simama sasa. (*Kicheko*)

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa unavyotumia nafasi vizuri.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya juu ya matatizo ya mradi wa maji vijijini ambao haukufika, matumaini ya wananchi yaliyotegemewa hayapo na mliingia mkataba na hao wakandarasi na wadau wengine lakini maji hayakupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni wa tangu mwaka 2008, ni miaka saba sasa na katika Wilaya zote, ni Wilaya chache ambazo katika maeneo hayo na vijiji vilivyotengwa ndio walipata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama fedha zimetolewa, maji hayakupatikana, ukatoa fedha za watafiti lakini maji katika maeneo hayo hayaupatikana, hili ni tatizo na hii ni aina ya ubadhirifu wa fedha. Wakandarasi ambao walikwenda kuchimba visima vya maji, mkawalipa kiwango chote cha fedha lakini hakuna maji yaliyopatikana, huu ni wizi, ubadhirifu na ufidadi katika eneo hili na hili halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sakaya kasema hapa kwamba katika Wilaya ya Urambo katika vijiji vile 12 ni vijiji vitatu tu ndivyo vilivyopata maji na vijiji tisa havikupata maji na fedha zao ziko benki na wananchi hawajui hatima yao, hili ni tatizo kubwa. Tunasema, hiyo asilimia 10 ya fedha ya Wataalam Elekezi iliyotolewa, hili nalo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii inaonekana kwamba usimamizi wa watendaji wakuu, Naibu Waziri, Waziri nyote kwa pamoja suala hili bado hamjalipa uzito unaostahili na ninyi ndio wa kulaumiwa. Haiwezekani iwe kuna vijiji 12, vijiji vitatu tu ndivyo vipate maji, bado vijiji tisa, iwe kila siku majibu ni yaleyale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Sakaya, ni lazima jambo hili lipatiwe ufumbuzi wa kudumu na wa haraka sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Silinde. Mheshimiwa Silinde vipi, uko Bungeni au uko Jimboni? *(Kicheko)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa- Mwenyekiti, nipo Jimboni, nilikuwa napata ufafanuzi kidogo.

**MWENYEKITI:** Haya tuendeleo.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu hapa nilijaribu kueleza takwimu za hesabu nyingi sana ambazo Kaimu Waziri Mkuu amejaribu kuzifafanua kidogo kwamba yeye ndiye wa kubeba lawama. Hata hivyo, bado tunahitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mwanga kutengewa mabilioni ya shilingi ukitofautisha na Mji wa Tunduma, Tunduma tu, mwaka wote wa fedha uliopita milioni ishirini na sita tu ndizo ambazo zimefikishwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde jenga hoja ya Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nakwenda huko...

**MWENYEKITI:** *No! no! no!* Hapa tunazungumzia hoja ya Mheshimiwa Sakaya. Sasa usiibue hoja nyingine, jirudishe kwenye hoja ya Mheshimiwa Sakaya, ndiyo hoja.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nakwenda huko.

**MWENYEKITI:** Usiizungushe hoja, twende sasa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Sasa kutokana na utaratibu huu mbovu wa kupeleka fedha matokeo yake ni nini? Ni kwamba hata katika Jimbo langu la Momba katika visima vitano vile tulivyokuwa tumepatiwa, maana katika Halmashauri ya Momba kule kama Halmashauri ya Mbozi tulikuwa na visima kumi, sasa matokeo yake ni kwamba Momba tulipata vitano na Mbozi Mashariki kwa maana ya Mbozi ya sasa tulipata vitano. Katika visima hivyo mpaka leo hii ni kisima kimoja tu ndicho kimekamilika cha kijiji cha Namtambalala na visima vingine vyote mpaka sasa hivi bado havijakamilika na fedha zile za mradi wa Benki ya Dunia na hivyo visima vingine vyote ni kwamba havitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mimi nikawa nasema kwamba ukiacha tu hizi fedha, pamoja na hiyo miradi ya hizo fedha nilizokuwa nimezielezea, ni kutokana na utendaji mbovu wa Serikali na Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu andijua hilo. Kwa hiyo, tunachoka na hizi ahadi ambazo hazitekelezeki na tunataka sasa ufafanuzi, ni kwa nini Serikali inashindwa kueleza ukweli kwamba miradi ya visima kumi imeshindwa kutekelezeka kuliko ambavyo inafanyika sasa hivi. *(Makofi)*

**MHE. SUBIRA K. MGALU-:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nilitaka kuchangia hoja hii kwa kusema kwamba maeneo yanatofautiana na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, inategemea na usimamizi wa eneo hilo. Kwa mfano, mimi kwangu Muheza tulishakamilisha miradi ya vijiji sita, tumepata maji na imefunguliwa na viongozi mbalimbali akiwemo Mkuu wa Mkoa wetu, Mheshimiwa Rais na ipo ambayo imekamilika na tunaendelea kumalizia vijiji vichache vilivyobaki. Maji yamepatikana, miradi imekamilika na wananchi wamepata huduma. Hata Mkoa ninaouwakilisha, Mkoa wa Pwani, Jimbo la Kibiti, vijiji sita maji yamepatikana na miundombinu inaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilichotaka kusema inategemea na maeneo, tusifanye kwamba ni Tanzania nzima. Yapo baadhi ya maeneo ambapo miradi hii imefanikiwa na maji yanapatikana na miradi imefunguliwa na inategemea pia utekelezaji wa Mhandisi huyo na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo na pengine na viongozi wa Wilaya hiyo wanaohusika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA-:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi kwa nguvu zote nimuunge mkono Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa hoja yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Katika moja ya ziara ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuja Urambo, mimi mwenyewe nikiwa Mbunge wa Viti Maalum nilisimama nikamwambia katika matatizo tuliyo nayo mjini Urambo ni matatu makubwa. La kwanza, maji...

**MBUNGE FULANI:** Ni Mkoa mzima.

**MHE. MARGARET S. SITTA-:** Mkoa wa Tabora kwa ujumla lakini siku alikuja sasa pale Urambo nikasema maji, pili mauzo ya tumbaku na tatu nikasema kumalizia barabara ya lami. Kwa hiyo, nasimama kuunga mkono kwa sababu ni tatizo kubwa sana, kwa nini watu wachange fedha zao na wasipate maji? *(Makofi)*

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi itoe tamko, lini wanapata maji watu wa Urambo hasa hivyo vijiji vilivyokosa, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA-:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nami nichukue fursa hii kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Sakaya, pamoja na kwamba Jimbo langu la Iringa Mjini lina maji asilimia tisini na tisa lakini hii ni kwa sababu ya kuwasemea hata Wabunge wa CCM ambao wanaona aibu kusema wakati hawana maji kwenye Majimbo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono hoja kwa kusema kwamba matatizo ya mradi huu wa *World Bank* yame-*fail*. Nimuombe tu Mzee wangu Profesa Maghembe, najua mimi sina ugomvi na wewe kwenye Jimbo langu lakini mkiri tu na msembe ni namna gani mtatekeleza. Kwa sababu Majimbo jirani yangu, Kalenga hakuna maji, visima vime-*fail*, ukienda kwa Mheshimiwa Lukuvi pale hakuna maji ni ukame, ukienda hata kwa Profesa Msolla kule amezungumza hapa hakuna maji, visima vime-*fail*. Naomba mtuambie ni lini mradi huu mtautekeleza, kama haziwezekani msembe na Wabunge wa CCM tusione aibu hapa, mnatoka kwenye maeneo ambayo wananchi mnafikua maji kama nguruwe, hamsemi mnaona aibu na kazi yetu hapa ni kuisimamia Serikali. Meatu, Rorya na sehemu nyingi hakuna maji, tumekaa hapa tunaona aibu. Kwa nini tusiseme tuibane Serikali ilete maji na ndiyo kazi wananchi wametutuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Sakaya, wananchi wote tushirikiane, hakuna maji nchi hii, ni lini visima hivyo vitatoa maji kama ambavyo Serikali ilisema? Ninaunga mkono hoja hii na naomba Wabunge tuibane Serikali iseme ni lini visima hivyo vitatoa maji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christina Lissu.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI-:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nimesimama ili niweze kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Sakaya. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yako, nakubaliana na maelezo ya *success rate*, mtu anapotafuta maji ardhini lakini inaonekana hii *success rate* basi inatofautiana Mikoa na Mikoa, labda ni kutokana na hali ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Singida tumeambiwa pamoja na kufanyiwa upembuzi yakinifu na visima kuchimbwa, visima vitatu vimekuwa havitoi maji. Sasa sijui hiyo hela iliyopotea katika kufanyia huo upembuzi yakinifu itafidiwa vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pale Ikungi, Makao Makuu ya Wilaya ya Ikungi wananchi wanatumia maji ya madimbwi. Kuna visima maarufu kama visima vya Wajapani lakini vyote pale Ikungi havitoi maji. Naomba nako Mheshimiwa Waziri wa Maji atoe maelezo kuhusu visima vilivyopo katika Halmashauri ya Ikungi ambavyo havitoi maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ataidiaje ikiwa sekta ya maji inapata bajeti finyu, lakini kuna vijiji ambavyo walichimbiwa visima miaka mingi na TCRS lakini visima hivi havifanyi kazi. Je, Wizara inaweza ikafufua visima hivi vya TCRS ambavyo bajeti yake inaweza kuwa ni ndogo na ikasaidia kutatua tatizo la maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkiwa, ajiandae Mheshimiwa Assumpter na Mheshimiwa Chiza.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa, napenda niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Sakaya ya visima kuchimbwa bila kutoa maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mfano katika Wilaya ya Longido, kisima kimechimbwa na kimetumia zaidi ya shilingi milioni mia tatu na hakitoi maji. Mheshimiwa Waziri pia afahamu wazi kuna maeneo ambayo hayahitaji visima na yeye anang'ang'aniza kupeleka visima, hata sisi Mwanza tulikataa visima, tukasema tunahitaji maji ya kutoka Ziwa Victoria na hatuhitaji kuchimbiwa visima kwa sababu maji yako karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuomba Mheshimiwa Waziri afuatilie na kujua hasara inayopatikana na ni kwa nini hawa Wakandarasi wanachimba visima na wanamaliza wanapewa pesa kamili bila visima hivyo kutoa maji kwani tunapoteza pesa za walipakodi pasipokuwa na sababu. Mheshimiwa Waziri asipende kufurahia kucheze ngoma, wananchi hawataki ngoma, wananchi wanataka maji na hata wananchi wangu wa Mwanza ni lazima tuwaseme, sisi ndio Wabunge wa Mwanza na Chama cha Mapinduzi katika Ilani yenu mmesema mtaeneza maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Assumpter.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA-:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, angalau nimeonekana. Kwa nguvu zangu zote namuunga mkono Mheshimiwa Sakaya. Kusema ukweli, katika ukweli uwongo utajitenga. Tuna tatizo kubwa la maji na hasa kwa visima hivi vinavyotamkwa visima vya *World Bank*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie, katika Jimbo langu tu la Nkenge wamechimba visima vyote kumi kimoja tu ndicho kimepata maji na hicho kimoja kilichopata maji tayari kiko hapo kama pambo tu, maji hayawezi kwenda kwa wananchi kwa sababu inasemekana hakuna pesa za kuweza kusambaza maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninayo Kata ya Bubale, Kilimilile, Kibeo, Kakunyu, maeneo haya wananchi wanakunywa matope kabisa na miradi imekwenda pale, watu wamechanga hela zao na mpaka leo hawajapata hayo maji. Je, kuna haja gani ya kuendeleza visima hivyo hasa kwenye maeneo ambayo yana maji? Kwa mfano, katika eneo letu kuna mto, kwa nini tusitumie *gravity* kuchukua maji ya Kagera badala ya hela hizo kuziweka kwenye visima ambavyo havina maji? Naomba tu kupata majibu.

**MWENYEKITI:** Waziri Chiza.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona mengine kama Wajumbe wameyachangia lakini nataka nisisitize hivi, masuala ya utafiti wa maji kwa kweli ni tofauti kabisa na masuala ya *design* ya nyumba hapa kwenye *ground* kwenda juu. Tunavyotafuta maji, tunafanya *geophysical prospecting*, inategemea *underlying geology*, huko chini ambako hatuoni. Ndiyo maana wakati mwingine unaweza ukachimba usipate maji na ndiyo maana wanasema wanaweka watafiti kutafuta maji. Sasa unapotafuta unaweza ukapata, unaweza usipate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *consultant* au yule anayefanya *drilling* kwa ajili ya *prospecting*, asipopata huwezi kusema halipi pesa, nilitaka niliweke vizuri hili, maana kazi yake amefanya. Labda tu hoja hapa ingekuwa hivi, tunapofanya *prospecting* ya maji, tunapokuta maji

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

hayakupatikana, huwezi kusema huyu mtaalam, huyu Waziri ameleta hasara, tutafute *fallback position* kwamba pale ambapo hatukupata maji ya *ground* tubadilisha kutafuta *sources* nyingine. Suala la kwamba yalitafutwa maji yakakosekana, wameleta hasara, mimi sidhani kama ni hoja ya msingi kwa sababu *ground water*, hata wewe mwenyewe nenda kachimbe, tofauti na unavyoanza kujenga nyumba yako kwenda juu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hukusaidia. Kwa sababu hoja hapa, mtu anapewa shilingi milioni mia mbili akatafute maji, maji hayapatikani, hujui anachimba, hachimbi; sisi tume-*experience* hata hapa ilala vilevile, pesa hizi za *World Bank*. Hoja ya msingi, amezungumza Waziri vizuri tu, sasa hivi atakayetafuta maji ndiye achimbe maji, akikosa maji halipwi. Sasa wewe umetuchanganya kabisa humu ndani, Mheshimiwa Waziri. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru sana michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Mimi narudi palepale kwa Mheshimiwa Sakaya. Mheshimiwa Sakaya kumbe alikuwa analenga eneo *specific* na katika eneo hili *specific*, hili eneo kabisa la Urambo, tunajua kwa uhakika sasa kwamba Mkoa wa Tabora kwenye maeneo mengi hakuna maji huko chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa pale hivi sasa tuna timu ya wataalam inafanya kazi ya *ku-design* mradi wa kutoa maji kwenye mto Ugala kuleta Urambo kwa sababu hakuna *possibility* ya kupata maji huko chini ya kukidhi mahitaji ya maji wa Urambo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, unaendelea.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ukishindwa kufanya jambo hili kwa sababu hali haiwezekaniki unatafuta mbadala...

**MWENYEKITI:** *Plan B*.

**WAZIRI WA MAJI:** Sisi tumetafuta mbadala, tutaleta maji Urambo na Kaliua kutoka mto Ugala.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya kaa kwanza. Waziri amekubali, eneo la Tabora lina tatizo kubwa sana la maji pamoja na maeneo mengine kama vile Ubungo. Upungufu ambao tunaona na tunaomba yasirudie tena, kama ilishafahamika eneo hili lina matatizo ya maji kulikuwa hakuna sababu ya kupeleka pesa kuchimba maji ambayo hayapo, hakuna sababu. (*Makofi*)

Sasa mimi nafikiri kubaliana naye, *plan B* ndiyo hiyo na wewe ukiwa Mbunge wa pale na Mama Margaret Sitta mjaribu kulifuatilia sasa kuhakikisha hiyo *plan B works* na wananchi wanapata maji, nakuomba hivyo. Kwa sababu ukitaka twende kwenye hatua zingine, hoja yako ni ya msingi, ni *valid*, inaweza ikafaa halafu isiwe na tija. Leo wamepewa *eighty billion*, kwa hiyo, wewe kamata hizo shilingi *eighty billion*, hakikisha anakusaidia. Mheshimiwa Sakaya. (*Makofi*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke kumbukumbu vizuri, mwishoni nitakubaliana na hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba ni *specific*, nilitoa Urambo kama mfano, siyo *specific* na ndiyo maana umeona Mheshimiwa Mbunge wa Nkenge

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

kasimama kasema kati ya vijiji 10 ni kijiji kimoja tu ndicho kimetoa maji. Kwa hiyo, suala ni *global*, ni nchi nzima na siyo Urambo tu, nilisema Urambo kama mfano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa nafikiri kwamba ndiyo maana tunao wataalam wa Jiolojia, anapopelekwa mtaalam kwenda kufanya uchunguzi wa maji, tunaamini anaweza kugundua kama maji yapo. Anapokuja na taarifa kwamba maji yapo, yasipopatikana, nataka nijue hatua gani zimechukuliwa kwa wale watu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *plan B*, ameshaniambia kwamba kuna *alternative* kwa upande wa Kaliua lakini siyo kwa upande wa Kaliua tu ila na Urambo na kwenye Majimbo mengine ambayo yana shida kama hii, kwamba tunapata maji kutoka mto Ugala, japo pia *speed* yake naona ni kidogo sana lakini napenda kujua kwa nini hazungumzi kuhusu ni hatua gani zinachukuliwa kwa wale wataalam waliobobea, waliosomea, waliolipwa na maji wanasema yapo halafu hayapo? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya, tulikubaliana unamrudishia shilingi yake baada ya kupata maelezo, ni kweli huko Urambo kuna matatizo. Hiyo hoja yako pili sasa haikuwepo katika hoja yako ya shilingi lakini ni *valid*.

Mheshimiwa Waziri, hoja iliyopo hapa ni kwamba *value for money* hazifanyi kazi huko mnakopeleka watu. Inawezekana kuna mtindo vilevile watu wanapewa pesa, ni *deal* tu, kachimbe, rudi hapa tugawane, *I am sorry* sielekei huko huko lakini ni *perception* ya watu ni hiyo, kwa hiyo, tunaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Medeye.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilichangia hoja hii wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na katika mchango wangu wa maandishi leo hii nilielezea haya yafuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilisema kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ambayo ndiyo Jimbo langu, wakazi wake wamekuwa kama wafinyanzi ambao hutengeneza vyombo wasivyovitumia. Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ndiyo chanzo cha maji yanayotumika Jijini Arusha, Monduli na Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi hatuna maji. Tunaambiwa yale yanayokwenda Longido tutagawiwa kidogo, yanayokwenda Arusha tutagawiwa kidogo, yanayokwenda Monduli tutagawiwa kidogo, kwa hiyo sisi tunapewa makombo yale wakati sisi ndiyo tunaotunza vyanzo vya maji, tusingetunza vyanzo vya maji, hayo maji yanayokwenda Wilaya nyingine yasingekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia hotuba ya Ofisi ya Rais, nilisema ugawaji wa rasilimali za Taifa hauzingatii uwiano wa maendeleo katika nchi hii na katika sekta ya maji iko hivyo hivyo. Nilimuomba Waziri atueleze ni mkakati gani uliopo wa kuwezesha wananchi wanaoishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ambao utawafanya nao wapate maji na kuondoa kabisa kero ya maji. Kwa mfano, kuna mradi unaotekelezwa katika Jiji la Arusha ambao utanufaisha Kata mbili, Kata ya Engutoto pamoja na Kata ya Mwoshono. Kata ya Mwoshono ilikuwa sehemu ya Wilaya yetu, baadaye ikahamishiwa Arusha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Natarajia kutoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Umechelewa.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Ole-Medeye kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba vyanzo muhimu vya maji kwa Mji wa Arusha, Mji wa Monduli, viko kwenye Wilaya ya Arusha. Pale ambapo inawezekana kuwapelekea maji kama kisima hicho cha Sombetini, Ngurtoto na kule Ngaramtoni, watapatiwa maji wala hakuna tatizo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Arusha itaendelea kupatiwa maji kwa wananchi wanaokaa katika eneo hilo kama Wilaya nyingine yoyote hapa Tanzania. Hakuna mtu anayeweza kuibagua na mimi nadhani hata Mamlaka ya Arusha wanapenda kila inapowezekana wawapatie maji wananchi wa Wilaya kila ambapo wanachimba maji katika vyanzo vipya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri muambie lini, mpe imani lini.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivyo vyanzo alivyosema ni vingi lakini kile chanzo ambacho ni cha Sombetini tutawapatia maji mwaka huu.

**MWENYEKITI:** Haya nakushukuru. Mheshimiwa Kirigini.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri wazi sina nia ya kuondoka na shilingi ya Mheshimiwa Waziri bali naomba niipongeze sana Serikali na Wizara kwa ujumla kwa kuwa sikivu, kwa kusikiliza kilio chetu kwa yale yaliyotokea kwenye Bwawa la Mwanjolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuiomba Serikali, kwa zile pesa ambazo zimekwishapatikana kiasi cha shilingi bilioni 80, niombe sasa na yule Mkandarasi ameshatimuliwa, yule Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa wa Serikali akabidhiwe kazi ile mara moja. Aidha, sisi Halmashauri ya Wilaya ya Meatu wakiongozwa na mimi Mkuu wao wa Wilaya, tusimamie kwa karibu ili tuhakikishe ndani ya mwaka mmoja, wananchi wa vijiji vya Mwanjolo na Jinamo wanapta maji safi na salama. Naomba hiyo *commitment* kutoka kwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri *commitment*.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia niliwahakikishia kwamba baada ya miezi mitatu tutampata mkandarasi lakini pia mkandarasi mwenyewe ndiye huyohuyo Wakala wa Visima. Kwa hiyo, nakubaliana naye na nawaahidi kwamba ndani ya miezi mitatu, mkandarasi atakuwa amepatikana lakini pia tutajenga ndani ya miezi mingine mitatu. Kwa hiyo, tutajitahidi na fedha tulizopata kuona kwamba adha ya maji na hiyo kero ya bwawa kwa muda mrefu tunaitatua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami sina nia ya kuchukua shilingi ya mshahara wa Waziri lakini nataka kupata maelezo kidogo. Kwanza, nampongeza Waziri kwa mradi mkubwa wa maji unaotekelezwa pale Kigoma Mjini. Wakati naandika maoni yangu nilisema mradi ule utakuwa mkubwa na utakuwa na maji mengi sana ambayo ukiangalia *population* ya Kigoma angalau kwa miaka 10 ijayo hawawezi kuyatumia yote. Niliomba maji



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

yale sasa waingize Kata mbili za Jimbo la Kigoma Kaskazini hasa Kata ya Mwandiga pamoja na Kata ya Bitale ambayo kwa kweli wamekuwa na shida kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri kama nilivyomuandikia anipe hiyo *commitment*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, *commitment*.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hizi mbili za Mwandiga na ile nyingine, tumezitungumzia kwa muda mrefu na tumezitungumza kati yetu na Mheshimiwa Mbunge lakini pia tumezitungumza na Mamlaka ya Maji ya Kigoma. Kata hizo zitapewa maji kutoka kwenye mradi uliopo sasa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Serikali kwa ujumla na iwapo sitaridhika na maelezo nitaomba kuondoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninacho kitabu cha Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Tumaini iliyorejea ambapo pamoja na mambo mengine kina hotuba ya Rais Bungeni ya tarehe 30 Desemba, 2005 ya kulifungua Bunge. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya mwaka 2005, alisema yafuatayo kuhusu maji.

"Tatizo la maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania mjini na vijijini, ndiyo kero *number one*. Serikali za awamu zote zimefanya jitihada kubwa kukabiliana na tatizo hilo. Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia kulikabili tatizo hili kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Ni makusudio yangu kuwa tuwe na mpango kabambe wa maji kwa nchi nzima, mpango ambao utajumuisha mkakati na mbinu mpya za kutekeleza kwa kasi. Aidha, tutakamilisha miradi mikubwa ya ukarabati na upanuzi wa maji safi na maji taka Dar es Salaam na ule wa kupeleka maji vijijini." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kauli ya Rais ya mwaka 2005 ambayo ukomo wake wa utekelezaji kimsingi ilikuwa ni mwaka 2010. Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba Serikali hii itatengeneza mpango kabambe wa maji nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza kuhusu programu ya vijiji kumikumi kwenye kila Halmashauri yaani Halmashauri hata kama ina vijiji mia, hata kama ina vijiji 120, tunazungumzia miaka 50 baada ya uhuru, maji katika vijiji kumi. Kwa Dar es Salaam mpango maalum wa maji wa toka wakati huo utekelezaji haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba ufafanuzi kutoka kwa Wizara. Kwa kuwa maji ni maisha, maji ni maendeleo, je, Wizara iko tayari sasa ili kutekeleza ahadi hii ambayo mpaka ilipofika mwaka 2010 ilikuwa haijatekelezwa ili kutekeleza ahadi hii, ichomoe hiyo mipango yote mingine, programu ya vijiji kumi ichanganywe, programu sijui ya *Quick Win*, zichanganywe, mpango maalum wa maji Dar es Salaam, ilete hapa Bungeni mpango kabambe wa maji nchi nzima, Bunge lipitishie Azimio la Utekelezaji wa Mpango huo ili utengewe fedha za kutosha kuhakikisha tunamaliza tatizo la maji kwa Watanzania. (*Makofi*)

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, ahsante. Una hoja ya msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu, *commitment* na mpango.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza hapa na mimi nimuombe sana Mheshimiwa Mnyika kwamba mipango ni jambo moja, utekelezaji nao una vikwazo vyake ikiwemo changamoto ya upatikanaji wa fedha. Tunayo nia ya dhati tumeeleza na hata hapa nimeeleza namna gani miradi hii mitatu mikubwa itakamilika, mradi wa Ruvu Chini kufikia Julai au Agosti utakuwa umekamilika na tutapata maji ya kutosho. Kuna Ruvu Juu, tumeeleza utakamilika mwezi Septemba mwakani na ule wa visima vya Mpera na Kimbiji. Yote hii ni mipango na nia ya dhati ya Serikali kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Sasa nilikuwa namuomba atuelewe kwamba tunayo nia hiyo ya dhati na huo ndio mpango hasa na hasa hiyo BRN ni pamoja na kuona tunatatua tatizo la maji Mkoa wa Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, mpango ndiyo huo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kuondoa shilingi si kwa sababu nina tatizo na Mheshimiwa Naibu Waziri na majibu yake ila nina tatizo na Serikali kwa ujumla wake. Ni vizuri Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu akanisikiliza na Wizara ya Fedha pia nao wakanisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiamua kutengeneza mpango kabambe kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliliahidi Bunge, maana yake ni kwamba taifa litafanya maji kuwa *number one*. Tukiamua kufanya hivyo, tutaondokana na tatizo la sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge, siyo maneno yangu, Kamati ya Bunge inasema, kwa bajeti ile tuliyoipitisha kwa nyongeza.

"Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu liazimie kuitaka Serikali iwe imetoa fedha zote za ndani za miradi ya maendeleo shilingi bilioni 226.1 ambazo hazijatolewa hadi sasa. Shilingi bilioni 127.2 kutoka kwenye vyanzo vya nyongeza na shilingi bilioni 98.9 kutoka kwenye vyanzo vya fedha zilizopangwa ifikapo tarehe 31, 2014".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumamosi tuliomba mwongozo wa Waziri Mkuu leo ndiyo dhadi imetekelezwa ya shilingi bilioni 80. Kwa hiyo maana yake ni nini? Kwenye bajeti ya mwaka jana peke yake ya fedha za maendeleo kwenye miradi ya maji shilingi bilioni 146.1 hazijatolewa tuko mwezi Juni, siku chache mwaka wa fedha unaokusudiwa kuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya hili ni nini? Hata hizi pesa tunazotaka kupitisha sasa ambazo Mheshimiwa Waziri amezingumzia, kimsingi pesa za mwaka huu mpya sasa hazitapatikana. Sasa ili tuwasaidie ninyi, Serikali kwa ujumla wake isimame hapa, Kaimu Waziri Mkuu asimame hapa aseme kwamba Serikali sasa inakwenda kulifikiria tatizo la maji kama jambo la dharura linalohitaji mpango maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri Mkuu aliweza kusimama hapa wakati wa bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini miaka kadhaa iliyopita, tukasema ukatengenezwe mpango wa dharura wa umeme na tukatenga pesa za mpango wa dharura wa umeme, ni kwa nini hatuoni udharura wa tatizo la maji ambapo maji ni maisha, maji ni uhai wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo hili lijadiliwe ili Serikali hii itakiwe kwenda kutengeneza mpango maalum. Mwaka 2009, kulipotokea mdororo wa uchumi duniani, Bunge hili likapitisha Azimio la Bunge la matrilioni ya pesa, siyo bilioni, trilioni 1.7 kwa ajili ya kunusuru

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

uchumi wa nchi. Sasa kama tunaweza kupitisha pesa nyingi namna hiyo ni kwa nini hatutaki kupitisha pesa za kunusuru maisha ya wananchi kutokana na matatizo makubwa ya maji? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Serikali hii itakiwe kuja na mpango maalum wa maji nchi nzima ili sasa tuondokane na tatizo hili. Jambo hili lijadiliwe na Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Sanga, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, wewe utasema mwisho, Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Shekifu, Mheshimiwa Kiwanga na Mheshimiwa Rebecca. Mheshimiwa Pauline Gekul anza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa John Mnyika kwa asilimia 100 kwa sababu zifuatazo. Pamoja na tatizo la Wizara kutokupeleka fedha na Serikali kwa ujumla kuipuuza Wizara hii lakini bado kuna tatizo la kibajeti katika Wizara hii. Nitoe mfano, ukiangalia hata bajeti ya mwaka huu, ukienda kwenye fedha za maendeleo utaona ni fedha za mafunzo, kuwezeshana, posho na *per diem*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wabunge wenzetu wa upande wa pili ambao ni wengi tusilalamike kuhusu suala la maji. Mimi binafsi siungi mkono kabisa Serikali kuongeza fedha. Nishauri hii bajeti ifumuliwe upya kwa sababu nimepitia randama ya Mheshimiwa Waziri na nilikuwa ninaiangalia kwa muda mrefu hapa yaani bajeti ya Wizara hii pamoja na kwamba Serikali haipeleki pesa lakini hata uandishi wa randama yao ni mbovu sijawahi kuona, fedha zote ni za posho. Zile za maendeleo kwenye kitabu cha nne, ni fedha za posho, za mafunzo na safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisima kimoja kinaanzia shilingi milioni 15 mpaka shilingi milioni 25 au shilingi milioni 30. Mimi katika Halmashauri yangu ya Babati, Mheshimiwa Waziri umetenga shilingi milioni 183 lakini kuna mafunzo shilingi milioni 500, kuna mafunzo shilingi bilioni 1.0. Randama hii imejaa uchafu, naomba ifumuliwe upya, Kamati ya Bajeti ikae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iache kutenga fedha kwenye Wizara hii, Waziri awajibike, ifumuliwe bajeti hii fedha zitapatikana hapa hata baadaye kama tutaongeza zitakuwa chache sana. Hatuwezi kupitisha bajeti hii kwenye kitabu cha pili cha matumizi ya kawaida, mafunzo, posho, *per diem* kwenye maendeleo kitabu cha nne, posho, mafunzo, visima havipo, maji hakuna, Babati wananitengea shilingi milioni 183.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika ili bajeti hii iangaliwe upya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa John Mnyika, ya mpango kabambe wa maji kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kama tunataka kunusuru maisha ya Watanzania na hali ilivyo sasa na jinsi ambavyo Mheshimiwa Mnyika alivyoeleza kwamba Wizara hii bado

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

haipewi nafasi inayostahili. Mpaka sasa hivi ikiwa jumla ya shilingi bilioni 146 fedha za miradi ya maendeleo hazijapatikana hili ni tatizo kubwa. Hata maelezo ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2005 alivyoahidi akasema atakuwa tayari kuona kwamba suala la maji linapewa kkpambebe na linakuwa ni jambo la kwanza kabisa lakini hakuna utekelezaji wa aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba mpango wa Ruvu Chini kwa Dar es Salaam utakamilika Agosti 2014 na ule wa Ruvu Juu ni Septemba, 2015. Sasa hata kama huo mpango wa Ruvu Juu ni Septemba 2015 na jinsi mchakato unavyoendelea bado tatizo linakuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa John John Mnyika bajeti hii ifumuliwe upya tuone kwamba suala hili sasa tunaweza kuliweka katika hali nzuri. Hatujaingia katika *subvote* nyingine, ukiangalia maji, vitafunwa na viburudisho kuanzia *subvote* 1002 mpaka 1003 ni mara dufu au mara nane, ni unywaji tu wa maji ya chupa kwenye *subvote*, tutakwenda muda si mrefu ikiwa utanipa nafasi. Ni unywaji tu wa maji ya chupa kwenye *subvote* zote kutoka milioni tano mpaka 48, kutoka tisa mpaka 24, utaangalia. Hili ni tatizo kwani watu wanajipangia unywaji wao wa maji safi ya chupa lakini watu hawana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa John John Mnyika na nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage!

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Uchangiaji wa wenzangu waliotangulia unanipa shida. Hoja ya Baba John ni kwamba tuna tatizo la maji, tuainishe miradi ya maji tuamue kwa nguvu tuimalize, hiyo ndiyo hoja, wanaokula vitumbua hiyo haituhusu, waache kula vitumbua wale mihogo, hoja ni kwamba tutambue tatizo la maji, tutafute vyanzo kama tulivyofanya kwenye mambo mengine ili tuweze kumaliza tatizo. Kama ndiyo hivyo Baba, mimi nakuunga mkono, unajua siwezi kukataa kukuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ndiyo hivyo sasa tunawahisha ajenda ya Mfuko wa Maji, tukubaliane wote hapa tuanzishe Mfuko wa Maji. Ningekuwa na muda ningekueleza falsafa ya India, Falsafa ya India walipotaka kuleta maendeleo waliamua akina mama na akina baba kutafuta dhahabu zote. Akina mama wa India walikuwa wanafunga hata dhahabu kwenye kiuno wakazikusanya wakazifunga pamoja wakaziweka benki wakapata fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuamue wote kama tunaweka kodi kwenye simu, kwenye mafuta au hata kwenye bia tutengeneze mfuko. Nadhani Baba nimekuunga mkono kwenye hoja yako tuamue hilo. Kwa hiyo, nadhani Waziri usiwe na tatizo, tukubaliane Mfuko uanze, weka *charge* kwenye simu, kwenye *petrol* na kadhalika ili tumaliza tatizo la maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimwia Shekifu!

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kukubaliana na Mjumbe aliyekaa sasa. Tatizo la maji ni zito na kama ni zito ni vizuri wote tukubaliana kwa nia njema tu tutoe tamko kwa sababu tatizo ni kubwa. Mimi napendekeza kama ilivyopendekezwa hebu tuandae Mfuko ambao utatusaidia kuliondoa tatizo hili, wala tusiogope kusema ukweli. *(Makofi)*

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba zipo *programs* ambazo zimeanza lakini hazijanikiwa. Kwa mfano, *Water Sector Development Program* ipo lakini haijafanikiwa, ndiyo hii ya *World Bank*. Sasa hebu tuingie tena tutafute njia nyingine na njia ya uhakika ni kuunda utaratibu kama ule wa mamlaka kama *REA* au *TANROAD*, zitafutwe fedha zipelekwe huko ili tupate maji, tutajibu hoja muhimu sana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMANI S. JAFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi pia sipo mbali na wenzangu kwa sababu ukiangalia tatizo la maji hasa mimi kwangu Kisarawe ni muathirika mkubwa sana wa tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ni kwamba tunakubaliana katika hili kwamba tuna kila sababu kama Wabunge tujipange kwa pamoja na Serikali tuangalie jinsi gani hii mradi mikubwa tuweze kuitekeleza kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji katika nchi yetu. Nasema hivyo kwa sababu bila maji hakuna jambo lolote linaloweza kufanyika. Leo hii kuna watu hata uchumi unashuka hawashughuliki na suala la uchumi bali wanashughulika na suala la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi hapa nina imani kubwa kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Mnyika kwamba Kaimu Waziri Mkuu yupo hapa na bahati nzuri yeye ni mzoefu sana wa sekta ya maji, naamini kwamba kauli yake inaweza kutusaidia sana kutuonyesha wapi tunakwenda na katika hili mimi naamini hatuna mashaka. Mheshimiwa Mark Mwandosya atatusaidia sana kututoa hapa tulipo lakini jambo la msingi ni tufanye vipi kutatua tatizo la maji katika nchi yetu ya Tanzania, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiwanga!

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami moja kwa moja naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika kwamba kuna umuhimu sana wa kuangalia suala la maji hasa katika kuvipatia maji vijiji vyote nchini Tanzania na kuna ahadi mbalimbali zilitolewa kwamba ikifika miaka kama hii kina mama tunahamasishwa kwamba tutapata maji mita 400 lakini leo ukiangalia ni ndoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natolea mfano Wilaya ya Kilombero, kule maji ni maafa lakini maji siyo matumizi na kama maji ni uhai basi kinyume chake ni kifo. Kwa hiyo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu wanaimba kwamba maji ni uhai, kwa kuwa maji hakuna sasa hivi wanahamasisha vifo na wanaoteseka nchini kuhusu maji ni akina mama, akina mama kuna tarehe maalum lazima upate maji ya kutosha ili uwe msafi. Akina mama wanapojifungua hospitalini ni lazima wapata maji ya kutosha. Ukiangalia leo vijiji karibu vyote kwenye Zahanati hakuna maji. Kwa hiyo, wanaoteseka na maji ndani ya nchi yetu ni akina mama, baba anaweza akakaa hata siku tatu hajaoga lakini mama je, utakaa hata siku tatu katika zile siku maalum hujaoga, kuna baba atakusogelea ndani ya nyumba? Kwa hiyo, maji ni uhai na maji ni hali tete sana hasa kwa jicho la kijinsia kwa wanawake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya Mnyika kwamba ni muhimu sana tukaanzisha Mfuko Maalum wa maji ili uangalie maji katika maeneo yote, kulikokuwa na miamba chini, kulikokuwa na mito, bahari au maziwa tuweke maji. Mbona kwenye nchi za

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Ulaya ambako kumezungukwa na bahari tupu maji ya chumvi wenzetu hawana shida ya maji?  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda Singapore, unaambiwa ukinywa maji ukienda kujisaidia wao ndiyo wanafurahi, maji machafu wanayageuza kuwa maji safi ya kunywa na salama lakini kwa nini Tanzania tufike huko wakati tuna mito, mabonde na maziwa? Kwa hiyo, kuna haja ya kuanzisha Mfuko Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunga mkono hoja hii nataka tu Kamati yako niipeleke ukurasa wa 100 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, inahusu Mfuko wa Maji. Tayari Bunge lako lilishamaliza biashara hii ya kuanzisha Mfuko wa Maji kupitia Sheria Na.12 ya mwaka 2009 na ndiyo maana Waziri anasema hivi, maandalizi ya kuwezesha Mfuko kuanza kazi yamekamilika na kwa mwaka 2013/2014, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 100 kama kianzio (*seed money*) kwa ajili ya Mfuko. Serikali itaendelea kuutunisha mfuko huo kwa kubaini vyanzo vingine vya mapato ikiwa ni pamoja na ada na tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndiyo tungeamua kama tunataka kwenda sasa kwa hoja hii ya maji ambayo ni muhimu, tulisimamie vizuri sasa kwamba tunaishauri Serikali tutafute vyanzo vingine vya kuweza kutunisha Mfuko huu na tulitolee uamuzi lakini Mfuko upo. (Makofi)  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kutoa taarifa hiyo, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwigulu una lolote la kuongeza au ndiyo hilohilo?

**MBUNGE FULANI:** Bado.

**MWENYEKITI:** Mimi ndiye ninayepanga majina. Mheshimiwa Mwigulu Mchemba!  
(Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme hoja iliyopo mezani ni hoja ya msingi sana na hakuna ubishi hapa Tanzania hakuna mtu ambaye haoni kama hilo ni tatizo na ni vema tukakubaliana kwenye mambo mawili au matatu hivi. La kwanza, hali ya hewa imebadilika sana nchini kwetu. Kwa hiyo, kwenye hili tunapotamka kwamba tunatakiwa tufanye jambo hili ni jambo ambalo la lazima na tunatakiwa kufanya kwa muda huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa kuhusu fedha za Mfuko, ni jambo ambalo sisi kama Wizara tutaangalia kwenye vyanzo kwa sababu kama *seed money* tayari ilishawekwa na utaratibu huo ulishawekwa, kwa hiyo, ni jambo la kibunge tu tutakapokuwa tunajadili kuhusu *Finance Bill* tuangalie namna ya *ku-ring fence* kama tulivyosema sehemu nyingine kubainisha baadhi ya vyanzo vyenyewe viende moja kwa moja kwenye Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tunalolipata kuhusu maji kama utakumbuka kwenye bajeti iliyopita ilikuwa ni pale tulipokuwa tunatumia fedha nyingi zaidi kwenye miradi ya maji zinazotokana na vyanzo vya nje ya nchi. Utakumbuka bajeti ya mwaka jana, Bunge liliamuru Serikali ijadili upya ili ibainishe vyanzo vya ndani ambavyo vitakwenda kwenye miradi ya maji

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

kwa sababu bajeti ya Wizara ya mwaka jana vyanzo vingi vilikuwa vinatokana na fedha za nje. Kwa hiyo, kwa upande wetu kama Wizara hatuna tatizo na Mfuko na mimi mwenyewe ni mdau mkubwa wa maji, mimi ni mtoto wa mfugaji, nimebeba maji kwa bega zaidi ya kilomita 18. Kwa hiyo, tutakalofanya sisi Wizara tutaleta mapendekezo vyanzo gani tunaweza tukaanza navyo ambavyo vitakuwa na mfumo sawa na vile vya *Road Fund* ambavyo kwenye kila kitu kinachotumika unajua hiki kinakwenda kwenye barabara, kwenye kila kitu kinachotumika unasema hiki kinakwenda kwenye REA. Tuwe pia na kwenye kila kitu kinachotumika kuwe na tozo ambayo inakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa Maji na naamini hilo linaweza kututoa hatua moja kwenda nyingine na kukamilisha vitu vingine ambavyo ni vya kisheria vitakuwa bado havijakamilika katika kuanza kutekeleza Mfuko rasmi wa Maji ili kuweza kuondokana na tatizo hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa majibu mazuri, Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu!

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA (KAIMU WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikiliza kwa makini sana yale yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge na kweli ni hoja ya msingi. Maji ni uhai na ni tatizo namba moja nchini na lazima Serikali ionekane inalipa umuhimu namba moja kama inavyotoa kwa sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimuuliza mwanachi wa kijijini kama umeme ndiyo namba moja au ni maji, atakuambia maji. Kwa hiyo, ni lazima vilevile Serikali iweke nguvu katika kutatua tatizo hili ambalo ni tatizo namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, yote yaliyozungumzwa ni kweli Mfuko wa Maji umeanzishwa lakini umeanzishwa kisheria lakini siyo kwa sheria maalum. Kwa maana hiyo ningependa kutoa uthibitisho kwa niaba ya Serikali kwamba tutaleta Bungeni Muswada wa sheria mahsusi kwa ajili ya kuanzisha rasmi Mfuko wa Maji, kisheria! Tukifanya hivyo basi masuala yote ya kwamba vyanzo hivi, vyanzo hivi maana yake ni kwamba tuta-ring fence hata huo Mfuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimalizie pia kwa suala la jumla ambao limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na hili suala la kupatikana maji chini ya ardhi, niseme tu inafanana sana na uchimbaji wa mafuta. Tangu mwaka 1950, tumekuwa tukitafuta mafuta nchi hii na vimechimbwa visima zaidi ya 70 na bado hatujapata mafuta na ni patapotea kwa sababu jiolojia na angani ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, tutaendelea na jitihada na ndiyo maana nasema kuongezea elimu au ujuzi wa watu ni kitu muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka kuzungumza hiki lakini sanasana ni kusisitiza kwamba Mfuko wa Maji utaundwa kisheria na tutaleta Muswada hapa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mapema iwezekanavyo kabla mwaka huu haujaisha tunaweza tukapata?

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA (KAIMU WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kabla ya Bunge halijafunjwa yaani mwaka kesho. Ahsante sana!

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana! Mheshimiwa Mnyika!

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Kaimu Waziri Mkuu kwa *commitment* ya kwamba Serikali italeti Muswada na nasema jambo hili lichukuliwe na Serikali kwa uzito kwa sababu wakati wa Hoja Binafsi ya Maji niliyowasilisha na hata katika majumuisho ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri ya mwaka jana, hili suala la Mfuko wa Maji, kuanzisha TANWATER na mambo yote haya, kauli zilizotolewa wakati ule zilikuwa zinafanana na kauli hizi na wananchi wanazidi kupata shida ya maji. Kwa hiyo, hii *commitment* ya sasa iwe ni *commitment* kweli ambayo itakwenda kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba Serikali imejibu kipande kidogo sana cha hoja kwa sababu hoja ilikuwa Mheshimiwa Rais aliliahidi Bunge tarehe 30 Desemba, 2005 kwamba nchi itakuwa na mpango kabambe wa maji kwa nchi nzima. Kwa hiyo, kuwa na Mfuko wa Maji ni kipengele kidogo sana yaani kipande tu cha mpango kabambe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano ili niweze kueleweka, sasa hivi tunapitisha bajeti ya ujenzi wa bomba la maji kutoka Mlandizi mpaka Kimara pamoja na chanzo cha maji pale na Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia kuhusu Ruvu. Kama umeamua kuwa maji ni dharura, utaamua lile bomba kwa pesa ulizozipata za mkopo wa India badala ya kusubiri mpaka Septemba 2015 na kitabu cha Waziri kwenye randama inaonesha ni mpaka mwaka 2017 ndiyo bomba likamilike, utaweka mpango wa kwamba maji ni dharura, Mkandarasi aanze kujenga Mlandizi aanzie na Kimara ili bomba likamilike. Kama Serikali kwa sababu ya udharura wa umeme inasema inajenga kwa kipindi kifupi bomba kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam kwa ajili ya gesi kwa muda mfupi sana, ni kwa nini bomba la maji lichukue muda mrefu zaidi? Ukikosa umeme unaweza kutumia kibitari, ukikosa maji huwezi kunywa bia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachokiomba kwa Serikali, nataka kurudisha shilingi kwa hawa Mawaziri kama nitapata *commitment* ya kwamba ukiondoa masuala ya Mfuko, maji sasa itakuwa *number one* kama alivyosema Rais kwamba Serikali nzima inakaa inaharakisha miradi ikamilike kwa haraka, tukisubiri Muswada peke yake Muswada utakuja huko baadaye na Mfuko wa Maji utakuja huko baadaye wananchi wana shida ya maji hivi sasa wanataka hatua za haraka za kuhakikisha maji yanapatikana. Naomba *commitment* tu kwamba pamoja na suala la Mfuko Serikali sasa itashughulikia maji kama *number one* kwenye utekelezaji wa mikakati ili kuharakisha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ili niweze kurudisha hii shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika tumekuelewa vizuri, kaa basi! Tumekuelewa vizuri sana hoja yako na Kaimu Waziri Mkuu ameeleza vizuri sana na hii sheria itakapokuja na wewe utaendelea kuongeza. Hii hoja ya kusema ni lini, agizo la Rais haliwezi kupingwa na Waziri yeyote humu ndani na agizo hilo la Rais lilisemwa ndani ya Bunge hili ...

**MBUNGE FULANI:** Tokea mwaka 2005.

**MWENYEKITI:** Na sisi tunakuunga mkono kuwa agizo la Rais lisipingwe wala lisicheleweshwe. Mheshimiwa Waziri, *commitment* juu ya agizo la Rais!

**MBUNGE FULANI:** Tokea mwaka 2005!

**MWENYEKITI:** Wewe sema ndiyo mzee utatekeleza, utakosa kazi! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Toka mwaka 2005 leo 2014?



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu haina tatizo kuanzisha Mfuko wa Maji, huo ndiyo ambao ulikuwa kwenye hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi ambayo tayari inatekelezwa kwa mfano, mradi wa kutoa maji Ruvu Darajani kupeleka Dar es Salaam mkandarasi tayari ameingia mkataba na Serikali yuko kazini, hatuwezi kuweka mkandarasi mwingine katikati au kuanzisha mradi mwingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupeleka maji lita 192 milioni kwa siku Dar es Salaam siyo kama kukamua machungwa ya *juice* na kumpa mtu *glass* ya juice, ni kazi ambayo inataka muda, umakini na lazima ifanywe kwa umakini ili maji yaende Dar es Salaam...

**MBUNGE FULANI:** Miaka 50 ya uhuru bado tu?

**WAZIRI WA MAJI:** Kazi hiyo inafanywa sasa na itakwisha Septemba, 2015 na siyo 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri jibu lilikuwa ni dogo tu, agizo la Rais tumeshaanza kulitekeleza, sasa hivi maji lita 200 Dar es Salaam na tunaendelea kulitekeleza, kwa hiyo, nakubaliana na wewe na tunaheshimu maagizo, *that was simple like that!*

Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu!

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA (KAIMU WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tumekubaliana na tunajua kwamba maji ni muhimu na ni uhai, maji ni *number one* na kwa maana hiyo hata katika sekta zilizowekwa katika Matokeo Makubwa Sasa au *Big Results Now* maji ni mojawapo. Kwa hiyo, utekelezaji wa miradi yote unafuatiliwa haraka sana na ni mkataba kati ya Rais na Waziri wa Maji. Kwa hiyo, asipofanya hivyo atakosa kazi yaani ni kitu muhimu sana na ndiyo maana Serikali imekiweka katika *Big Results Now*. Kwa hiyo, tunakubaliana na wewe kabisa. Tunamshauri Waziri wa Maji kwa sababu ya umuhimu wa maji labda kila anapopata nafasi katika kila Bunge awe anatoa Kauli ya Serikali kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa program wa sekta ya maji, hii itamfanya kila mtu ajue kwamba tunakwenda mbele. Kwa hiyo tunakuomba Mheshimiwa Mnyika uturudishie shilingi halafu tuendeleo na kazi, ahsante.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *commitment* hiyo ya Kaimu Waziri Mkuu kwamba Serikali itakuwa inatoa kauli kuhusu maendeleo ya utekelezaji kwenye kila Mkutano wa Bunge, naomba nirudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)  
Kif. 1002 - Finance and Accounts.....Tshs.1,400,788,200/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)  
Kif. 1003 - Policy and Planning.....Tshs.3,542,008,600/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline, Mheshimiwa Paresso, Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Betty Machangu, unaondoka basi nenda. Mheshimiwa Pauline. (Kicheko)

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nipate ufafanuzi katika *total* ya kifungu hiki kwa ujumla wake kwenye kitabu cha matumizi ni Sh.3,542,008,600/= lakini ukienda kwenye randama ni Sh.2,519,000,000/= tofauti ya zaidi ya shilingi bilioni moja isiyokuwa na maelezo. Maana yake ni nini? Maana yake tunapitisha kwenye hiki kitabu Sh.3,000,000,000/= lakini kwenye randama ndio unapata maelezo ya kila hela zinatumiwa ni Sh.2,000,000,000/=. Kwa maana hiyo basi kwenye kitabu hiki cha matumizi (*Volume II*) shilingi bilioni moja imezidi isiyokuwa na maelezo. Maana kwenye randama haijajelezwa hizi shilingi bilioni ni za nini, naomba tu ufafanuzi wa kina, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi *one billion* haionekani kwenye kitabu.

**WAZIRI WA MAJI:** Ni kifungu kipi?

**MWENYEKITI:** 1003 - *Policy and Planning* 3,542,000,000/=, ukurasa wa 306. *Total* ni shilingi bilioni tatu kwenye randama shilingi bilioni 2.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna tofauti, nafikiri ni *typing error* lakini ya kwenye kitabu ndio sahihi zaidi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda hajaelewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri hebu jibu tena vizuri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, iliyoko kwenye kitabu, hapa *total* ni Sh.3,542,000,000/= lakini kwenye randama kuna Sh.2,000,000,000 na kwamba kuna tofauti ya shilingi bilioni moja, hiyo tofauti yake ni mishahara ya Chuo cha Maji.

**MWENYEKITI:** Ndiyo ishawekwa hiyo, Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Hebu subiri. Mheshimiwa Pauline hukutoa shilingi, maelezo uliyoyataka ni hayo, *it ends there*.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** (*Aliongelea nje ya kipaza sauti*)

**MWENYEKITI:** Ndio nasema ulitaka maelezo ameshakujibu wewe hukutoa shilingi huna nafasi tena ya kuendeleza hoja yako, inakufa hapohapo. Unayo sasa nafasi ya kuhoji ukamwambia mwingine na mwingine naye hawezi tena akahoji hoja yako hiyo, Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko *subvote* 1003 - *Policy and Planning* yaani Sera na Mipango, niko katika kasma 220800 - *Training Domestic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata kigugumizi na wasiwasi juu ya mafunzo ya ndani ya nchi kwa watumishi wa Kitengo cha Sera na Mipango kuhusiana na ongezeko la fedha kutoka Sh.9,200,000/= mwaka 2013/2014 na kwa mwaka huu ni Sh.75,450,000/=. Ongezeko hili katika kasma hii ya mafunzo ya ndani na juu ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri katika ufafanuzi wake haikuwekwa wazi kwamba kutakuwa na ongezeko la watumishi wangapi.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata wasiwasi juu ya ongezeko kubwa la fedha hizi katika mafunzo ya ndani zaidi ya Sh.65,000,000/= kwa mafunzo ya ndani kwa watumishi wa Kitengo hiki cha Sera na Mipango. Naomba ufafanuzi wa kina juu ya ongezeko hili kubwa la fedha katika kasma hii.

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hilo analolisema Mheshimiwa Mbunge ni kwa ajili ya kujenga uwezo wa watumishi 15 wa Idara ya Maji ambao watapata mafunzo juu ya maandiko ya miradi na uchambuzi wa miradi ya maji na hapa tumeshakubaliana kwamba tunahitaji wafanye maandiko mbalimbali kuangalia miradi ya maji. Kwa hiyo, hii ndiyo hela kwa ajili ya mafunzo ya watumishi hao 15.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kupata ufafanuzi, kwa kuwa randama ya Wizara hii haijaonyesha kasma mbalimbali lakini kuna kazi ambazo zinajirudia na zimetengewa fedha. Mfano kuandaa bajeti ya Wizara ya Mwaka na Mpango Kazi imetengewa Sh.152, 750,000/=.

**MWENYEKITI:** Kifungu kipi?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, randama yao...

**MWENYEKITI:** *No, no, no!* Humu kwenye *Volume II*, inasemaje?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Subvote 1003, Sera na Mipango.

**MWENYEKITI:** *Yes! Policy and Planning*, kasma ipi?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Nataka niende kwenye randama kwa sababu randama yao haijaonyesha kasma tofauti na randama za Wizara zingine zote.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mujibu wa randama madhumuni ya shughuli namba mbili, inaonyesha kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Ukija kwenye mchanganuo sasa kuna kazi ambazo zinajirudia, tunataka kupata maelezo. Mfano kuandaa bajeti ya mwaka na mpango kazi imetengwa Sh.152,000,000/=, kuandaa mpango kazi wa Wizara zimetengwa Sh.126,500,000/=, halafu kuandaa hotuba ya bajeti ya Wizara imetengwa Sh.167,000,000/=. Kingine inasema kuratibu na kuandaa ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Kamati za Bunge zimetengwa Sh.30,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna kazi zimejirudia lakini kuna shughuli zingine ambazo tunaona haina tija sana ni bora wangepeleka kuchimba visima kuliko fedha nyingi zinatengwa kwa shughuli zilizoainishwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Lakini kweli Mheshimiwa Waziri, hii randama yako imekaa vibaya sana, inamchanganya kila mtu humu ndani. Hata Meza sasa mnaipa taabu hapa, haya jibu. (*Makofi*)

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kifungu kwenye kitabu cha Hazina tuna maelezo yake. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge ange-specify specific kifungu katika kitabu cha Hazina tunayo maelezo.

**MBUNGE FULANI:** Randama.

**WAZIRI WA MAJI:** Tunayo maelezo very detailed.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, maelezo unayo wewe kwenye kitabu cha Hazina, kwenye randama hapa mezani vilevile hakuna maelezo. (Makofi)

**WAZIRI WA MAJI:** Hiyo section ni ipi maana katika hiki kitabu juu...

**MWENYEKITI:** Fungua randama ukurasa wa 68, madhumuni namba mbili.

**WAZIRI WA MAJI:** Iko kwenye kifungu 1003, Sera na Mipango, *what exactly is it?* Ni kasma ipi kwa sababu tuna maelezo kwa kila kasma. Tunayo maelezo ya kila kifungu kama ilivyowekwa kwenye kitabu cha Hazina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo Mheshimiwa AG aongee.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hii tunajadili kitabu hiki cha pili na mahesabu ambayo sasa hivi yanatuongoza ni haya ambayo yako kwenye kitabu hiki *Volume II*.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Yamekosewa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sio kama yamekosewa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa AG anazungumza na mimi halafu na nyie mtazungumza na mimi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nashauri *definitely* za Mawaziri wanatakiwa pia kuzifahamu zile randama vizuri *at fingertips*. Hata hivyo, *figures* zinazoongoza Kamati hii sasa hivi ni hizi ambazo zipo kwenye kitabu hiki, sio randama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG, nakushukuru lakini kama ulivyosema Mawaziri hizi randama muwe nazo katika *fingertips*. Hoja hapa ni za msingi sababu matumizi ya hapa yanakuwa *justified* kwenye hizi randama. Nakubaliana na Mheshimiwa AG lakini vilevile lazima tujue na hii kitu lazima muwe nayo na ndiyo ina *spell out* mambo yote ambayo yanatakiwa matumizi. Mheshimiwa Jafo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo, maelezo baadaye nitakupeni mie.

**MHE. SELEMANI S. JAFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja yangu iko katika kasma namba 270600 - *Current Grant To Non-Financial Public Units – (Agencies)* ambayo hapa kuna jumla ya Sh.2,075,437,000/=

**MWENYEKITI:** Sema tena hicho kifungu?

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. SELEMANI S. JAFU:** Ni kasma ndogo ya 270600 - *Current Grant to Non-Financial Public Units – (Agencies)* ambayo ina shilingi bilioni mbili na kadhaa.

**MWENYEKITI:** Okay.

**MHE. SELEMANI S. JAFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu inasimama kwamba mimi ninavyoelewa ni kwamba fedha hii zinakwenda katika hizi *agencies especially* DAWASA. Sasa ofisi ya Waziri wa Maji inayo *concern* kubwa ya mradi wa maji pale Kisarawe Kimani ambao hata kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaelezea ni jinsi gani *iron content* ilivyokuwa kubwa mpaka asilimia 14. Hali ile hivi sasa imesababisha watu wa Mji wa Kisarawe leo hii hawana maji karibuni wiki ya pili hivi sasa kwa sababu madini ya chuma ni ya kiwango kikubwa zaidi zile bomba zimelika, bomba ya chuma inakatika. Kwa hiyo, hali imekuwa mbaya zaidi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka mliyoniipa naongeza nusu saa.

**MHE. SELEMANI S. JAFU:** Sasa kutokana na kiwango cha madini ya chuma kuwa kikubwa zaidi, tulipeleka *special request* pale Wizarani ili yale maji wayafanyie *aeration process*. Sasa nilitaka kujua kwamba fedha hii itakwenda kusaidia mradi wa maji Kisarawe ili wananchi wa Kisarawe ambao sasa hivi wana wiki ya pili hawana maji waweze kusaidiwa katika changamoto hiyo inayowakabili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ni kwa ajili ya kuwezesha Chuo cha Maji na *DDCA* kujiendesha. Ongezeko linatokana na mahitaji ya chakula na mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wapya 520 watakaodahiliwa mwaka 2014/2015 katika Chuo cha Maji pamoja na mishahara ya watumishi wapya 26.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kuna baadhi ya vifungu watu wameshazungumzia lakini na mimi nitasema kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachia suala la randama, nataka kwenda kwenye kifungu 221400 - *Hospitality Supplies and Services* yaani kwa maana vitafunwa, chai na vitu vingi tu ambavyo vime-raise kutoka Sh.5,000,000/= mpaka Sh.48,000,000/=. Wizaru hii tumekuwa tukiilalamikia kwamba haina fedha lakini fedha nyingi kwenye matumizi ya kulakula na nini yamekuwa yakipanda, maana hii ukiangalia *percentage* yake imepanda nafikiri mara 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ukweli kwamba ukipitia randama ya Serikali haelezi kitu chochote, kila kitu imeweka katika ujumla. Hii tafsiri yake ni nini? Wanasema, *if you can't convince them confuse them*. Kwa hiyo, Wizaru ya Maji imeamua kutu-confuse tu ili mradi Wizaru yao ipite na kinachokwenda kutokea hapa ni kwamba wanasubiri tu *guillotine* ipite na kwa sababu mnajua kuna mambo ya msingi kama yale ya Momba ambayo nimekuwa nikiyazungumza muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungependa kupata ufafanuzi hao watu wana uwezo gani wa kula chai na nini kutoka Sh.5,000,000/= mwaka jana mpaka Sh.8,000,000/= mwaka huu. Tunajali chai kuliko maendeleo.

**Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa bei na pia fedha za kifungu hiki mwaka 2013/2014 zilitengwa kimakosa katika kifungu cha *other operating expenses* lakini kwa mwaka 2014/2015 fedha zimerejeshwa katika kifungu sahihi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 - *Government Communication*  
Unit.....Tshs. 369,108,000/=

Kif. 1005 - *Legal Service Unit* .....Tshs. 464,518,900/=

Kif. 1006 - *Procurement Management*  
Unit.....Tshs. 886,505,800/=

Kif. 1007 - *Management Information*  
System.....Tshs. 462,845,500/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1008 - *Internal Audit Unit*.....Tshs. 641,372,400/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid, Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Paresso na Mheshimiwa Sanga.

**MHE RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko katika *subitem 221000 – Travel in Country*

**MWENYEKITI:** Ngapi?

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** *Subvote 221000 - Travel In Country.*

**MWENYEKITI:** *Travel in Country Sh.229,000,000/=*

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Ndiyo. Nimepata na mshangao kidogo kwa ongezeko kubwa la fedha la Kitengo hiki cha Ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana walitengewa Sh.30,600,000/= lakini mwaka huu ni Sh.229,000,000/= hili ni ongezeko mara saba ya bajeti iliyopita mwaka jana. Sasa nataka kujua safari hizi ni safari gani, safari za kukodi ndege ya *Jet* au helikopta au kitu gani na kwenda wapi? Naomba maelezo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri maelezo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ongezeko hili ni kukiwezesha Kitengo hiki cha Ukaguzi wa Ndani kukagua miradi mingi ya maji nchi nzima, kwa sababu miradi ya maji inayotekelezwa imeongezeka sana na tunayo miradi mingi mingine ambayo inakuwa na matatizo kama ule wa Longido. Kwa hiyo, hii ndiyo maana ya ongezeko hili.

**MWENYEKITI:** Hilo ndio jibu sahihi, very good. Mheshimiwa Sanga.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 221000 lakini tayari kimeshaulizwa na mimi nilitaka niulize hivyo kwa sababu fedha hapa mwaka jana zilikuwa chache na mwaka huu ni nyingi na Makambako pale wakati anajibu hajajibu ni mikakati gani ya Serikali ambayo imejipanga juu ya kutatua tatizo la Makambako.

**MWENYEKITI:** Hoja imeshapita, Mheshimiwa Silinde. (Kicheko)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nilikuwa na hoja hiyo hiyo, lakini ningeweka tu *question* moja tu samahani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba nimefanya jumla ya fedha zote za Wizara ya Maji, *Travel In Country* ina bajeti ya Sh.1,893,000,000/= kwenye vipengele vyote nimejumlisha mimi hapa, hiyo ndiyo bajeti yake. Sasa watueleze Wizara hii watakuwa mnasafiri sana mwaka huu wa fedha kuliko kitu kingine? Miradi yenyewe haikamiliki na *feasibility* zao ambazo wameweka *zero zero*, hamna kitu chochote cha maana kinachofanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri mjibu vitengo mbalimbali, visima vingi, miradi mingi. (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kama Wizara kama alivyosema mwenyewe kuna vitengo mbalimbali. Kwa hiyo, kila Kitengo kina majukumu yake lakini hapa kikubwa si kukaa ofisini lazima kwenda kutembelea miradi mbalimbali na kuona namna gani inatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Pareso. Mheshimiwa Pareso yeye amesharudisha majeshi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Water Resource*

*Management*.....Tshs. 6,292,645,800/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwaiposa, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Pareso na Mheshimiwa Christina.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi lakini pamoja na kutambua umuhimu wa kifungu hiki mimi *concern* yangu iko kwenye kifungu namba 221000 – *Travel – In - Country*. Naona pale kwa mwaka huu fedha zimepanda kwa 90% kutoka milioni kumi na sita mpaka kwenye milioni mia moja na sitini na tano na laki tano. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kujua kwamba pamoja na matatizo mengi tuliyo nayo katika Jimbo la Ukonga, visima vimeachwa havijamalizika, ni kwa nini sasa tunatenga fedha nyingi kiasi hiki kwa wafanyakazi kusafiri badala ya *ku-invest* kwenye visima ambavyo havijamalizika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ndiyo yaleyale.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi ya maji lakini fedha hizi ni kwa ajili ya usimamizi wa miradi ya ujenzi wa mabwawa nane na ujenzi wa ofisi za mabonde sita zitakazoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2014/2015.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye kifungu hicho cha 229900. Kuna ongezeko kubwa sana la ajabu hapa kutoka shilingi laki tano, mwaka jana shilingi milioni kumi, mwaka huu shilingi milioni mia tatu na kumi na laki tano. Tungependa kujua kwamba hizo *other expenses* ni kitu gani ambacho kimepandisha fedha kwenda kiasi kikubwa hivyo na wakati tunataka wananchi wakapate maji vijijini, hela haziendi huko zinakwenda kwenye *other expenses* ambazo hizo ni kazi za ofisi. Tunaomba maelezo ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka hii ya karibuni tumekuwa tunadaiwa kila mwaka na wafanyakazi wa Wizara shilingi bilioni mbili na laki nane. Kwa hiyo, fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kupunguza madai hayo ya wafanyakazi katika Idara hii ya Mipango na Idara zingine zimetenga fedha pia kwa ajili ya kuwalipa madeni wafanyakazi ambao hawakulipwa siku za nyuma.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nilikuwa nataka maelezo katika fungu hilo hilo ambalo Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba ongezeko la hizi fedha, *other operating expenses* kutoka milioni kumi za mwaka jana mpaka milioni milioni mia tatu na kumi za mwaka huu ni kwa ajili ya kulipa madeni. Mheshimiwa Waziri haoni kwamba wamechukua kiasi kikubwa sana kwenda kulipa madeni ya wafanyakazi wakati pesa hii wangeweza kulipa kidogokidogo na zikaelekezwa kwenye tatizo kubwa la maji kama vile kuchimba visima?

**MWENYEKITI:** Jamani ni wafanyakazi wangapi mnakuja kuwalilia humu kuwa hawalipwi hela zao, Serikali inawalipa mnakasirika, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu kama mkiangalia bajeti za Wizara hii, Wizara ilikuwa inapewa OC kidogo sana, ilikuwa inapewa OC ya 3.9 bilioni. Madeni ya umeme peke yake ya kulipia miji ya Daraja B na C pamoja na miradi ya Taifa ni shilingi bilioni tatu na laki nane. Kwa hiyo, OC ya Wizara ilikuwa inatoshwa kulipa umeme peke yake, kwa hiyo, wafanyakazi wengi walikuwa hawalipwi stahili zao. Sasa fedha za OC zimetolewa zinazolingana na matumizi halisi ni vizuri tualipe wafanyakazi stahili zao, wao ndiyo wanafanya kazi hizi.

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana wanachimba visima maji hayatoki kwa sababu ya hasira, Mheshimiwa Mwijage. (Kicheko)

**MHE. CHARLES J.P MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, niko kasma 220800, katika hizi shughuli za *water resource management*. Katika kifungu hiki wametenga shilingi milioni themanini na moja na katika *water resource management* ndiyo unakuta tuna matatizo, nyie huku Wizarani mnakosa *linkage* na watu wa Wilayani ambao wanatekeleza. Mimi nilitaka kujua kama hizi shilingi milioni themanini na moja, mmetenga kiasi cha kuweza kuwapatia *training* wale watendaji wa kwenye Halmashauri hasa Wilaya ya Muleba ili wapate ufahamu zaidi kwenye mambo ya *water resource management*?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya gharama za mafunzo kwa jumuiya za watumia maji na watumia maji kumi na nane katika mabonde yote nchini. Ongezeko linatokana na kuongezeka kwa idadi za jumuiya za watumia maji zilizopangwa kufikiwa katika mafunzo kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na utunzaji wa rasilimali za maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso, haya ameridhika?



**Nakala ya Mtandao (Online Document)**

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.2002 - Central Stores.....Tshs.390,076,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Kibona.

**MHE. MASOUD ABDLLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko katika *subvote* 2002, *Central Stores*, niko katika *item 227100 - Rental Expenses*. Ukiangalia fedha hizi za kodi la pango ambazo zilikuwa zimetengwa mwaka 2013/14 ilikuwa ni shilingi milioni moja lakini mwaka huu wa fedha 2014/2015, fedha ambazo zimetengwa ni shilingi milioni kumi na nne na laki nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua ongezeko la mara kumi na nne kutoka fedha za mwaka jana ambayo imepelekea kuwa shilingi milioni kumi na nne na laki nne, kwanza mwaka jana mlakodi nini hata mara hii ikawapelekea mkaongeza fedha mara kumi na nne pointi nne kufikia shilingi milioni kumi na nne pointi nne. Mlakodi nini mwaka jana mara hii mkapata sababu za kuongeza fedha kutoka milioni moja mpaka milioni kumi na nne na laki nne? Naomba maelezo ya kina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya kuhudumia maghala mapya ya kuhifadhia vifaa vya maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kibona.

**MHE. ALIKO K. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *item 410700 - Feasibility Studies, Project Preparation and Design*. Ukiangalia vifungu vyote au kasma zote tulizoanza nazo mwaka jana zilitengewa pesa ya upembuzi lakini nimeshindwa kuelewa ningependa kupata ufafanuzi, ni mambo gani hayo ambayo kuanzia *accounts, auditing* kila mahali kulikuwa na *Feasibility Studies, Project Preparation and Design* lakini mwaka huu zote hazipo na wakati huohuo tuna haja ya kuwa na watu wa namna hii ili waweze kutufanyia *design* ya miradi yetu mbalimbali ambayo inakwama katika Halmashauri zetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kuwa mwaka huu haikutengwa fedha ni kwamba kazi zilizokuwa zimepangwa zimekamilika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.2300 - Water Laboratory.....Tshs.2,026,594,100/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa na Mheshimiwa Silinde.

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIBU JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati hivi vifungu vinaongezeka kwa ongezeko kubwa sana.

**MWENYEKITI:** Kipi?

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIBU JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 2300, kifungu 210500 - *Personal Allowance In Kind*.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MWENYEKITI:** Okay.

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIBU JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati imeongezeka kutoka shilingi milioni nane laki sita na arobaini kufika shilingi milioni sitini na tano, ongezeko la asilimia mia sita sitini na moja. Ni vizuri tueleze katika maabara za maji, ni nini kipya kilichotendeka, hizo *personal allowance in kind* zimeongezeka namna gani? Ni vizuri kupata ufafanuzi ili watu tusishtuke kwamba kumetengwa fedha za mambo maalum.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili ni ongezeko la Wakurugenzi Wasaidizi wapya watatu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka ufafanuzi katika kifungu 290700 - *Contingencies Non- Emergency*, hizi ni gharama ambazo Serikali wanakuwa ni kama vile hawazifahamu ndiyo maana wanaweka katika hiki kifungu. Sasa unaposema *Non-Emergency* maana yake ni kitu ambacho unakijua kipo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia randama nzima au hii bajeti yao yote katika Idara nyingi hiki kifungu ni kipya na kina kina gharama zaidi ya milioni mia tano ukizijumlisha moja moja. Sasa tueleze hizo *non-emergency* msizozijua hizo mlizozijazia fedha ni nini mpaka mkakianzisha hiki kifungu kipya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka jana hakukuwa na fedha katika kifungu hiki na sasa kuna shilingi milioni hamsini na tano. Fedha hizi ni kwa ajili ya kulipia madeni ya watumishi na wazabuni.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Urban Water Supply and*

*Sewerage*.....Tshs. 6,280,558,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko, Mheshimiwa Pareso, Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Mwaiposa na Mheshimiwa Shekifu. Mheshimiwa Pareso.

**MHE. CECILIA D. PARESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwenye kasma 220200 - *Utilities Supplies and Services*, imetengwa shilingi bilioni tatu na milioni mia tisa. Ukisoma randama imefafanuliwa kwamba ni kuwezesha uendeshaji wa miradi ya Kitaifa na Mamlaka za Maji za Daraja B na C kwa kugharamia bili za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kupata ufafanuzi, Sera ya Maji inaeleza kwamba watumia maji au wanaopata huduma watalipia maji yale ili miradi mbalimbali iweze kujiendesha ikiwemo kulipia bili za umeme. Sasa kwa nini tena hapa imetengwa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya gharama hizohizo za umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, miji yetu iko kwenye daraja A, B na C. Ie ya daraja A inajilipia umeme, inajilipia uendeshaji kwa maana ya kununua dawa, vitu vya mitambo, kulipia umeme pamoja na mishahara ya wafanyakazi. Katika daraja B kama mji wa Bukoba, Kigoma, Sumbawanga, miji hii hata ingefanyaje labda ipandishe bei ya maji iwe juu

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

sana ya wenzao wote haiwezi kulipia bili za maji. Kwa hiyo, zile ziko katika daraja B na Serikali inawalipia umeme. Pamoja na miradi kama ule wa KASHUWASA unaoleta maji kutoka Ziwa Victoria kuja Shinyanga, fedha wanazopata hawawezi kulipia ule umeme ni lazima mzigo ubebwe na Serikali na miradi hiyo iko pamoja na mradi wa Mugango -Kyabakari, mradi wa Maswa, mradi wa Wanging'ombe, mradi wa Makonde, miradi hiyo ni lazima isaidiwe kulipia umeme na Serikali. Kila mwaka bei ya umeme ni shilingi bilioni tatu na milioni mia tisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Umependeza leo. (Kicheko)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Nakushukuru sana kwa kunipa hiyo *compliment*. Kasma ndogo 229900 - *Other Operating Expenses*, kwa mwaka 2012/2013 kulikuwa hakuna kitu chochote kilichotengwa, mwaka 2013/2014 walitenga shilingi milioni tano lakini mwaka huu kwa maana ya mwaka 2014/2015 wametenga shilingi milioni mia mbili arobaini na nane na laki tano. Nataka kujua ongezeko kubwa la zaidi ya shilingi milioni mia mbili arobaini na tatu na laki tano ni kwa ajili ya nini kwenye hiyo kasma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya kulipia madeni ya watumishi na wazabuni na ongezeko hili ni kwa ajili ya kuendelea kupunguza madeni hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya. Ahsante, Mheshimiwa Mwaiposa.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu alichokuwa ameulizia Mheshimiwa Matiko.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekifu.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Kimeulizwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Tunaingia kwenye *guillotine*

Kif.4001 - *Rural Water Supply*.....Tshs.2,812,567,500/=

Kif.4002 - *Water Sector Program*

*Coordination Unit*.....Tshs.396,758,000/=

Kif.5002 - *Water Development and*

*Management Inst* .....Tshs.227,493,800/=

Kif.6001 - *Drilling and Dam*

*Construction Agency* .....Tshs.759,429,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **Fungu 49 - Wizara ya Maji**

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Kif.1001 – Administration and  
HR Management.....Tshs.10,537,000,000/=

Kif.1003 - Policy and  
Planning .....Tshs.16,979,050,000/=

Kif.2001 - Water Resources Assesment  
& Exploration .....Tshs. 49,874,700,000/=

Kif.2003 - Water Laboratory .....Tshs. 7,842,834,000/=

Kif.3001 Urban Water  
Supply and Sewerage.....Tshs.207,663,868,000/=

Kif.4001 - Rural Water Supply.....Tshs. 197,109,580,000/=

(Bunge lilirudia)

### **T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imejadili Taarifa ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2014/2015 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Bajeti imepita lakini nachukua nafasi kukushukuru sana Kaimu Waziri Mkuu, Mheshimiwa *Attorney General* kwa namna mlivyo-*intervene* katika bajeti hii na kuweza kutoa busara na hoja ambazo zimeweza kuisaidia Serikali. Vilevile niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu kwa kazi nzuri na wataalam wenu. Tunaomba lakini *next time* hizi randama zenu ziwe *in order*, zinaleta *confusion* kwa Wabunge na hatupendi sana *confusion* kama hizo. (Makofi)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Assumpter.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niombe mwongozo maana naona kama kuna vitu sijaelewa. Natumia Kanuni ya 68(7), nadhani kinaeleweka ili nisipoteze wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetokea kama kuchanganyikiwa kidogo kwa utaratibu unaoendeshwa sasa hivi namna ya kutupanga ili tuweze kuchangia. Kwa mfano, zile Wizara tatu ambazo zimepita nilikuwa nimeomba kuchangia na zilizobaki mimi sina nafasi. Kwa maana nyingine zile nilizochagua kama zimepita kama *priority* kwangu itakuwa siwezi kuchangia hapo baadaye.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonishangaza mtu amechangia hapohapo unampa tena katika kushika kifungu akiwa wa kwanza ambapo *at least* ingekuwa inatolewa nafasi kwa wale ambao hawajachangia basi wapate nafasi katika kushika hivi vifungu. Matokeo yake sisi tunabaki, mimi nimepata hapa *message* mwaka huu imekuwaje maana watu hawaelewi, mtu unasikika huwa unachangia lakini sasa hivi nimechangia mara mbili na pale nilipotakiwa kuchangia sijaweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu nipe maelezo maana tumefika mahali kubembeleza mtu, unamfuata kwenye kiti nipange, nipange na matokeo yake hakupangi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Assumpter, masuala ya kuchangia ndani ya Bunge ni masuala ya Chama kinachohusika na wewe ukiwa ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, inabidi wewe ukae na viongozi wako wa Chama cha Mapinduzi wakuweke kwenye orodha ya kuchangia. Meza hapa haihusiki na kupanga jina la mtu, haihusiki kumkataa mtu na wala haihusiki kumpendelea mtu.

Leo kuna Wabunge wengi wamekwenda kuzika Kigoma, nimewapa Wabunge wengi sana nafasi zaidi ya tisa kufidia wale ambao hawakuwepo na Mheshimiwa Assumpter wewe mwenyewe Bungeni hukuwepo hapa asubuhi, umeingia jioni na wakati umeingia muda wa kuchangia umekwisha. Tunakwenda na muda, kwa hiyo bahati mbaya basi omba Mungu na wewe ni Mchungaji leo usali vizuri kesho inawezekana ukaingia. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.21 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 3 Juni 2014, Saa Tatu Asubuhi)*